**SHERIA YA KUFUTA SHERIA YA MWENENDO WA JINAI NAM. 7 YA 2004 NA KUTUNGA SHERIA MPYA YA MWENENDO WA JINAI NA KUWEKA UTARATIBU BORA WA UPELELEZI WA MAKOSA YA JINAI NA USIKILIZAJI WA KESI ZA JINAI NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO.**

---

## MPANGILIO WA VIFUNGU

**VIFUNGU** **MAELEZO**

### SEHEMU YA KWANZA
### MASHARTI YA AWALI


1. Jina fupi na kuanza kutumika.
2. Ufafanuzi.
3. Usikilizaji wa mashtaka kwa makosa yaliyo chini ya Sheria ya Adhabu na sheria nyengine.


### SEHEMU YA PILI
### UWEZO WA MAHAKAMA


4. Makosa chini ya Sheria ya Adhabu.
5. Makosa chini ya sheria nyengine.
6. Adhabu zinazoweza kutolewa na Mahakama Kuu.
7. Adhabu ambazo Hakimu wa Mahakama ya Mkoa anaweza kutoa.
8. Adhabu ambazo Hakimu wa Mahakama ya Wilaya anaweza kutoa.
9. Adhabu ambazo Mahakama ya Mwanzo inaweza kutoa.
10. Kusimamisha adhabu ya kifungo.
11. Mahakama za chini zinaweza kuwapeleka watu waliotiwa hatiani kwenda mahakama za juu yake kwa ajili ya kupewa adhabu.


### SEHEMU YA TATU
### MASHARTI YA JUMLA KUHUSU KUKAMATA, KUTOROKA NA KUKAMATA TENA

**Kukamata**


12. Kukamata, vipi kunafanyika.
13. Ushughulikiaji wa mtu aliyekamatwa.

14. Upekuzi wa pahala alipoingia mtu anayetafutwa ili akamatwe.
15. Uwezo wa kuvunja ili kutoka nje ya nyumba au pahala kwa madhumuni ya kujiokoa.
16. Kutokuwepo kizuizi kisicho cha lazima.
17. Upekuzi wa watu waliokamatwa.
18. Uwezo wa Afisa wa Polisi kuzuia na kupekua vyombo, watu katika mazingira fulani.
19. Namna ya kuwapekua wanawake.
20. Uwezo wa kuchukua silaha za hatari.

**Kukamata bila ya hati**

21. Ukamataji unaofanywa na Afisa wa Polisi bila ya hati.
22. Notisi ya kufika mbele ya Afisa wa Polisi.
23. Tangazo kwa mtu anayetoroka.
24. Ukamataji wa mali ya mtu aliyetangazwa.
25. Kurejesha mali iliyokamatwa.
26. Ukamataji wa wazururaji na majambazi sugu.
27. Ukamataji bila hati unaofanywa na Afisa Mdogo wa Polisi.
28. Kukataa kutoa jina na kutaja makaazi.
29. Kuwashughulikia watu waliokamatwa na afisa polisi.
30. Ukamataji unaofanywa na watu binafsi.
31. Kumshughulikia mtu aliyeokamatwa na mtu binafsi.
32. Mtu aliyekamatwa hatawekwa ndani zaidi ya saa ishirini na nne.
33. Polisi kutoa taarifa ya ukamataji.
34. Mtu aliyekamatwa kujulishwa sababu za kukamatwa na haki ya kukaa kimya.
35. Wajibu wa kutoa taarifa ya ukamataji.
36. Mipaka katika kumhoji mtu.
37. Wakati gani mtu asichukuliwe kuwekwa kizuizini.
38. Muda unaoruhusiwa kwa ajili ya kumhoji mtu.
39. Pale ambapo upelelezi chini ya ulinzi hauwezi kukamilika ndani ya saa nne.
40. Jinsi ya kuwatendea watu walio kizuizini.
41. Wajibu maalum wakati wa kuwahoji watoto.
42. Kumbukumbu za mahojiano.
43. Maelezo ya mtuhumiwa.
44. Uwezo wa kuchukua alama za vidole, picha za watuhumiwa.

45. Gwaride la utambuzi.

46. Kuwatambua mawakili.

47. Uchunguzi wa daktari tiba kwa mtuhumiwa kufuatia maombi ya Afisa wa Polisi.

48. Uchunguzi wa muathirika wa jinai au mshtakiwa.


**Ukamataji kwa amri ya Hakimu**


49. Kosa lililotendwa mbele ya Hakimu.

50. Ukamataji unaofanywa na Hakimu.


**Kutoroka na kukamata tena**


51. Kumkamata tena mtu aliyetoroka.

52. Kuwafuata wakosaji katika eneo la mamlaka nyengine.

53. Matumizi ya masharti ya vifungu vya 14 na 15.

54. Msaada kwa Hakimu au Afisa wa Polisi.


## SEHEMU YA NNE
## KUZUIA MAKOSA

**Dhamana kwa ajili ya kutunza amani au kuwa na tabia njema**


55. Dhamana kwa ajili ya kutunza amani au kuwa na tabia njema kwa ujumla.

56. Uwezo wa Hakimu mwengine.

57. Dhamana kwa ajili ya tabia njema kutoka kwa watu wanaosambaza mambo ya uchochezi.

58. Dhamana kwa ajili ya tabia njema kutoka kwa watuhumiwa.

59. Dhamana kwa ajili ya tabia njema kwa watu wenye tabia ya kutenda makosa.

60. Utoaji wa amri.

61. Utaratibu kuhusu mtu aliyepo mahakamani.

62. Utaratibu kuhusu mtu asiyekuwepo mahakamani.

63. Nakala ya amri itaambatana na wito au hati.

64. Uwezo wa kusamehe uhudhuriaji binafsi.

65. Uchunguzi kuhusu ukweli wa taarifa.

66. Amri ya kuweka dhamana.

67. Kuachiwa huru watu ambao dhidi yao taarifa zilitolewa.

**Mwenendo katika kesi zote baada ya amri ya kuweka dhamana**

68. Kuanza kwa kipindi ambacho dhamana inatakiwa.
69. Maudhui na ukiukaji wa dhamana.
70. Uwezo wa kuwakataa wadhamini.
71. Utaratibu unaohusiana na mtu kushindwa kuweka dhamana.
72. Kuachiwa huru mtu aliyefungwa kwa kushindwa kuweka dhamana.
73. Uwezo wa Mahakama Kuu kufuta dhamana.
74. Kuondoa jukumu la wadhamini.

**Hatua za uzuiaji wa Polisi**

75. Polisi kuzuia kosa analoweza kukamatwa mtu bila ya hati.
76. Taarifa ya mpango wa kutenda kosa.
77. Kukamata kwa ajili ya kuzuia kosa.
78. Uzuiaji wa uharibifu wa mali ya umma.

**SEHEMU YA TANO**
**MASHARTI YANAYOHUSIANA NA UPELELEZI WOTE WA JINAI**

**Pahala pa uchunguzi au usikilizaji kesi**

79. Upelelezi wa kosa.
80. Mamlaka ya jumla ya Mahakama za Zanzibar.
81. Mshitakiwa kupelekwa katika Wilaya ambapo kosa limetendwa.
82. Kuondoshwa mshtakiwa chini ya hati.
83. Mamlaka ya Mahakama Kuu.
84. Pahala na tarehe ya vikao vya Mahakama Kuu.
85. Pahala pa kawaida pa uchunguzi na usikilizaji kesi.
86. Usikilizaji wa kesi katika pahala kosa lilipotendwa au athari zilipojitokeza.
87. Usikilizaji wa kesi pale kosa moja limeungana na kosa jengine.
88. Usikilizaji wa kesi pale sehemu iliyotendwa kosa haijulikani.
89. Usikilizaji wa kesi pale kosa limetendwa kwenye safari.
90. Kosa lililotendwa kwa barua.
91. Pahala pa kusikiliza makosa yanayosikilizwa pamoja.
92. Mahakama Kuu kuamua katika mazingira ya shaka.
93. Mahakama zitakuwa za wazi.

**Uhamisho wa kesi**


94. Uhamisho wa kesi ikiwa kosa limetendwa nje ya eneo la mamlaka.

95. Uhamishaji wa kesi baina ya Mahakimu.

96. Utaratibu kuhusu uhamishaji wa kesi unaofanywa na Hakimu.

97. Mahakama Kuu kubadilisha pahala pa kusikiliza kesi

98. Utaratibu wa kuwezesha kutumika mamlaka ya Mahakama Kuu chini ya kifungu cha 97.


**Udhibiti wa Mkurugenzi wa Mashtaka katika Mwenendo wa Mashauri ya Jinai**


99. Mkurugenzi wa Mashtaka.

100. Jina la kesi za jinai.

101. Hati ya kufuta mashtaka.


**Uendeshaji wa mashtaka**


102. Uwezo wa waendesha mashtaka wa Serikali.

103. Uondoshaji wa kesi katika mahakama za chini.


**SEHEMU YA SITA**
**UFUNGUAJI WA KESI**

**Kuwasilisha malalamiko**


104. Malalamiko na hati rasmi ya shtaka.

105. Utoaji wa wito au hati.

106. Kuondosha malalamiko.


**SEHEMU YA SABA**
**HATI ZA KUWALAZIMISHA WASHTAKIWA KUFIKA MAHAKAMANI**

**Wito**


107. Aina na maudhui ya wito.

108. Uwasilishaji wa wito.

109. Uwasilishaji wa wito pale mtu anayeitwa hawezi kupatikana.

110. Utaratibu pale wito hauwezi kuwasilishwa kama ilivyoelezwa kabla.

111. Uwasilishaji wito kwa mtumishi wa Serikali.
112. Uwasilishaji wito kwenye kampuni.
113. Uwasilishaji wito nje ya mipaka ya mamlaka ya mahakama.
114. Uthibitisho wa uwasilishaji wito.

**Hati ya ukamataji**

115. Hati ya ukamataji kwa kukataa wito, au baada ya kutolewa wito.
116. Aina, maudhui na muda wa hati ya ukamataji.
117. Uwezo wa kuelekeza kutolewa kwa dhamana.
118. Hati za ukamataji kwao zitaelekezwa.
119. Hati za ukamataji zinaweza kuelekezwa kwa mmiliki wa ardhi.
120. Utekelezaji wa hati ya ukamataji iliyoelekezwa kwa Afisa wa Polisi.
121. Kutoa taarifa ya yaliyomo katika hati za ukamataji.
122. Mtu aliyekamatwa ataletwa mbele ya Mahakama.
123. Pahala ambapo hati ya ukamataji inaweza kutekelezwa.
124. Utekelezaji wa hati ya ukamataji nje ya eneo la mipaka ya mamlaka.
125. Utaratibu katika hali ya utekelezaji wa hati ya ukamataji nje ya eneo la mipaka ya mamlaka.
126. Utaratibu wa ukamataji wa mtu nje ya eneo la mamlaka.
127. Upungufu katika hati ya ukamataji.

**Masharti mbalimbali kuhusiana na Hati.**

128. Uwezo wa kuchukua ahadi ya dhamana kwa ajili ya kufika mahakamani.
129. Ukamataji kwa kukiuka ahadi ya dhamana.
130. Uwezo wa kuamuru kufika kwa mwanafunzi aliyepo Chuo cha Mafunzo.
131. Matumizi ya masharti yanayohusu wito na hati za ukamataji.

**Hati za upekuzi**

132. Wito wa kuwasilisha nyaraka au kitu chengine.
133. Utaratibu kuhusu barua na ujumbe wa simu.
134. Utaratibu kuhusu hesabu za benki.
135. Upekuzi, uchukuaji wa taarifa za kompyuta na vifaa.
136. Kumsaidia polisi na afisa aliyeidhinishwa.
137. Rekodi za kuingia kwa ajili ya kuchukua taarifa.

138. Uwasilishaji wa taarifa.
139. Kuweka bayana taarifa zilizohifadhiwa.
140. Kuhifadhi taarifa.
141. Upelelezi wa mawasiliano ya kielektroniki.
142. Upelelezi wa usafirishaji wa taarifa.
143. Usiri na mipaka ya dhima.
144. Tafsiri.
145. Uwezo wa kutoa hati ya upekuzi.
146. Upekuzi unaofanywa na afisa wa polisi.
147. Wajibu wa watu kuruhusu upekuzi.
148. Masharti ya utekelezaji wa hati ya upekuzi.
149. Uzuiaji wa mali iliyochukuliwa.
150. Masharti yanayotumika kwa hati ya upekuzi.

**Masharti kuhusu Dhamana**

151. Uwezo wa jumla wa kutoa dhamana.
152. Pale dhamana inapoweza kutolewa kwa makosa yasiyo na dhamana.
153. Ahadi ya dhamana.
154. Kuachiwa kutoka kizuizini watu waliochukuliwa dhamana.
155. Uwekaji wa fedha au mali badala ya ahadi ya dhamana.
156. Uwezo wa kuamrisha dhamana inayotosheleza.
157. Uwezo wa kukataa wadhamini.
158. Kuondoa dhima kwa wadhamini.
159. Kifo cha mdhamini.
160. Uwezo wa kumpeleka kizuizini mtu anayetoroka.
161. Kuondolewa ahadi ya dhamana.
162. Rufaa na mapitio ya amri.
163. Kutoza kiwango kinachodaiwa kuhusiana na ahadi ya dhamana.

**Mashtaka na Taarifa ya Mashtaka kwa Mahakama Kuu**

164. Maudhui ya shtaka.
165. Kuunganisha mashtaka au makosa katika hati rasmi ya mashtaka au katika taarifa ya mashtaka.

166. Kuunganisha washtakiwa wawili au zaidi katika hati moja rasmi ya mashtaka au katika taarifa ya mashtaka.

## Kanuni za kutengeneza hati za mashtaka na taarifa za mashtaka.

167. Kanuni za kutengeneza hati za mashtaka na taarifa za mashtaka.

## Hatia ya Awali au Kuachiwa Huru

168. Watu hawatoshtakiwa mara mbili kwa kosa hilo hilo.
169. Mtu anaweza kushtakiwa tena kwa kosa jengine.
170. Matokeo yaliyojitokeza au mahakama ya awali kutokuwa na mamlaka.
171. Utaratibu wa kuthibitisha hatia ya awali.

## Usikilizaji wa Kesi kwa Haraka na Umalizaji wa Kesi

172. Usikilizaji wa awali kuamua mambo ambayo hayabishaniwi.

## Kulazimisha Mahudhurio ya Mashahidi

173. Wito kwa shahidi.
174 Hati ya ukamataji kwa shahidi asiyetii wito.
175. Hati ya ukamataji kwa shahidi mara ya kwanza.
176. Namna ya kumshughulikia shahidi atakapokamatwa.
177. Uwezo wa kuamrisha uletwaji wa mwanafunzi wa Chuo cha Mafunzo kama shahidi.
178. Adhabu kwa kutokuhudhuria kama shahidi.

## Kuwahoji Mashahidi

179. Uwezo wa mahakama kuhoji na kuhoji tena.
180. Ushahidi utatolewa kwa kiapo.
181. Mashahidi wakaidi.
182. Ushahidi wa mume au mke wa mshtakiwa.
183. Hatua maalum kwa mashahidi wenye mazingira magumu au mashahidi wanaotishwa.

## Kutoa Maelekezo kwa ajili ya Kuwahoji Mashahidi

184. Utoaji wa maelekezo kwa ajili ya kuwahoji mashahidi.
185. Wahusika wa kesi wanaweza kuwahoji mashahidi.

186. Uwezo wa hakimu kuomba kutolewa maelekezo ya kuchukua ushahidi.
187. Marejesho ya maelekezo ya kuchukua ushahidi.
188. Kuakhirisha kesi kusubiri marejesho ya maelekezo ya kuchukua ushahidi.

**Ushahidi kwa Ajili ya Utetezi**

189. Kufaa kwa mshtakiwa na kufaa kwa mume au mke kutoa ushahidi.
190. Pale mshtakiwa anapokusudia kutegemea utetezi wa kutokuwepo kwenye eneo la tukio.
191. Utaratibu pale mshtakiwa ni shahidi pekee anayeitwa.
192. Haki ya kujibu.

**Utaratibu katika Kesi zinazohusu Mshtakiwa kutokuwa na Uwezo wa Akili au Uwezo Mwengine**

193. Uchunguzi kuhusu hali ya akili ya mshtakiwa.
194. Utaratibu pale mtu anapothibitishwa kuwa anaweza kujitetea.
195. Kuanza tena usikilizaji wa kesi au uchunguzi.
196. Utetezi wa kutokuwa na akili timamu.
197. Utaratibu pale mshtakiwa hafahamu mwenendo wa kesi.

**Haki ya Mshtakiwa Kupata Utetezi**

198. Haki ya mshtakiwa kupata utetezi.
199. Msaada wa kisheria kwa mshtakiwa kwa gharama za Serikali katika baadhi ya kesi.

**SEHEMU YA NANE**
**UTARATIBU WA KUCHUKUA NA KUREKODI USHAHIDI KATIKA UCHUNGUZI NA USIKILIZAJI WA KESI**

**Masharti ya Jumla**

200. Ushahidi utachukuliwa mbele ya mshtakiwa.

**Mahakama za Chini**

201. Namna ya kurekodi ushahidi mbele ya Hakimu.
202. Tafsiri ya ushahidi kwa mshtakiwa au Wakili wake.
203. Maelezo kuhusu muonekano wa shahidi.
204. Ushahidi utakaorekodiwa sehemu ya ushahidi huo na Hakimu mmoja na sehemu nyengine na Hakimu mwengine.

**Mahakama Kuu**

205. Kumbukumbu za ushahidi katika Mahakama kuu.

## SEHEMU YA TISA
## UTARATIBU KATIKA USIKILIZAJI KESI MBELE YA MAHAKAMA ZA CHINI

**Masharti yanayohusiana na Usikilizaji na Uamuzi wa Kesi**

206. Kutokuhudhuria kwa mlalamikaji.
207. Kufika kwa wahusika wote wa kesi.
208. Kuondosha malalamiko.
209. Kuakhirisha.
210. Kuanza usikilizaji wa kesi kwa makosa yenye dhamana.
211. Kutokuhudhuria kwa wahusika wa kesi baada ya kuakhirishwa.
212. Gharama za uakhirishaji.
213. Kumwita mshtakiwa kujibu shtaka.
214. Utaratibu kwa jawabu la "kutokuwa na hatia".
215. Kumuachia mshtakiwa anapokuwa hana kesi ya kujibu.
216. Utetezi.
217. Ushahidi katika majibu.
218. Ufunguaji na ufungaji wa kesi kwa upande wa mashtaka na upande wa utetezi.
219. Tofauti baina ya hati ya mashtaka na ushahidi na marekebisho ya hati ya mashtaka.
220. Uamuzi.
221. Kuandika hatia au amri.
222. Amri ya kufuta shtaka itazuia utaratibu zaidi.

**Ukomo wa Muda na Udhuru Kuhusiana na usikilizaji wa Kesi mbele ya Mahakama za Chini**

223. Ukomo wa muda kwa ajili ya usikilizaji wa kesi moja kwa moja.
224. Utaratibu katika kesi ya kosa linalothibitika halifai kusikilizwa kwa utaratibu wa usikilizaji kesi moja kwa moja.

## SEHEMU YA KUMI
## UTARATIBU KATIKA USIKILIZAJI WA KESI MBELE YA MAHAKAMA KUU

225. Ufanyaji kazi wa Mahakama Kuu katika mamlaka yake ya jinai.
226. Mashtaka kuendeshwa na Mkurugenzi wa Mashtaka.
227. Upande wa Mashtaka kutoa rekodi za ushahidi.

### Namna ya Usikilizaji Kesi

228. Usikilizaji kesi utakuwa pamoja na washauri wa mahakama watatu.

### Orodha ya Washauri wa Mahakama

229. Utayarishaji wa Orodha.
230. Wajibu wa kuhudumu kama washauri.
231. Kutoruhusiwa kuhudumu kama washauri wa mahakama.
232. Uchapishaji wa orodha.
233. Mapitio ya orodha.
234. Washauri wa mahakama kula kiapo.

### Mahudhurio ya Washauri wa Mahakama

235. Kuwaita washauri wa mahakama.
236. Aina ya wito.
237. Dharura kwa kutohudhuria.
238. Orodha ya washauri wa mahakama wanaohudhuria.
239. Adhabu kwa kutohudhuria.

### Kusomewa shtaka

240. Kujibu taarifa ya shtaka.
241. Marekebisho ya taarifa ya shtaka, usikilizaji wa kesi tofauti na uakhirishaji wa usikilizaji wa kesi.
242. Kuondoshwa kwa taarifa ya shtaka.
243. Utaratibu katika hatia za awali.
244. Mapatano ya kukubali kosa.

245. Matokeo ya mapatano ya kukubali kosa.
246. Taarifa ya makubaliano kwa mahakama.
247. Utaratibu unaofanana kwa Mahakama ya Mkoa.
248. Matokeo ya kutokukubali kosa.
249. Kujibu kuwa alishaachiliwa huru na alishatiwa hatiani.
250. Kukataa kujibu.
251. Utaratibu wa kukubali kosa.
252. Utaratibu unaohusiana na kujibu "siyo mkosa".
253. Uwezo wa kupeleka mbele au kuakhirisha mwenendo wa kesi.

**Uteuzi wa Washauri wa Mahakama**

254. Uteuzi wa Washauri wa Mahakama.
255. Kutokuwepo kwa Mshauri wa Mahakama.
256. Mshauri wa mahakama kuhudhuria katika vikao vilivyoakhirishwa.

**Maswali kutoka kwa Washauri wa Mahakama**

257. Uwezo wa washauri wa mahakama kuuliza maswali.

**Kesi ya Upande wa Mashtaka**

258. Kuanza usikilizaji wa kesi kwa upande wa mashtaka.
259. Mashahidi wa upande wa mashtaka.
260. Kutokufika kwa wahusika wa kesi baada ya kuakhirishwa.
261. Shahidi anaweza kutoa ushahidi kwa njia ya kielektroniki.
262. Mahojiano kinzani kwa mashahidi.
263. Ufungaji wa kesi kwa upande wa mashtaka.

**Kesi kwa Upande wa Utetezi**

264. Kuanza kwa kesi kwa ajili ya utetezi.
265. Mashahidi kwa ajili ya utetezi.
266. Majibu ya mwendesha mashtaka.
267. Pale mshtakiwa hatoi ushahidi wowote.

### Ufungaji wa Usikilizaji Kesi

268. Utoaji wa maoni ya washauri wa mahakama.

### Utoaji wa Adhabu

269. Kumuita mshtakiwa.
270. Hoja ya kuzuia hukumu.
271. Adhabu.
272. Uwezo wa kuzuia uamuzi.
273. Pingamizi zilizosawazishwa na uamuzi wa Mahakama.
274. Ushahidi kwa ajili ya kufikia adhabu inayofaa.

## SEHEMU YA KUMI NA MOJA
## HATIA NA HUKUMU

### Kutiwa hatiani kwa makosa ambayo siyo yaliyoshtakiwa nayo mshtakiwa

275. Iwapo kosa limethibitishwa linajumuishwa na kosa lililoshtakiwa.
276. Mtu anayeshtakiwa kwa kosa lolote anaweza kutiwa hatiani kwa kujaribu kutenda kosa.
277. Mwanamke anayeshtakiwa kwa kosa la kuua kwa makusudi mtoto wake anaweza kutiwa hatiani kwa kosa la kuua mtoto mchanga.
278. Mtu anayeshtakiwa kwa kosa la kuharibu mtoto anaweza kutiwa hatiani kwa kosa dogo.
279. Mtu anayeshtakiwa kwa kosa la kuua kwa makusudi au kuua mtoto mchanga au kuua mtoto aliyekuwa hajazaliwa anaweza kutiwa hatiani kwa kosa la kuficha kuzaa.
280. Uwezo wa kutia hatiani kwa kosa la uzembe au uendeshaji wa hatari katika usikilizaji wa kesi kwa kuua bila ya kukusudia.
281. Mtu anayeshtakiwa kwa kosa la kubaka anaweza kutiwa hatiani kwa kosa lolote chini ya masharti ya Sheria ya Adhabu.
282. Mtu anayeshtakiwa kwa kosa la kuingilia maharimu anaweza kutiwa hatiani kwa kosa la kuingilia bila ya halali.
283. Mtu anayeshtakiwa kwa kosa la kunajisi mtoto wa kiume anaweza kutiwa hatiani kwa kosa chini ya masharti mengine ya Sheria ya Adhabu.
284. Mtu anayeshtakiwa kwa kosa la kuvunja nyumba usiku anaweza kutiwa hatiani kwa kosa linalofanana na hilo.

285. Mtu anayeshtakiwa kwa kosa la kuiba anaweza kutiwa hatiani kwa kosa la kupokea mali ya wizi au kupata mali kwa njia ya kujisingizia.

286. Hukumu mbadala katika mashtaka ya kupatikana na mali inayotuhumiwa kuwa imepatikana kwa njia ya rushwa.

287. Mtu anayeshtakiwa kwa kujipatia mali kwa njia ya kujisingizia anaweza kutiwa hatiani kwa kosa la kuiba.

288. Tafsiri ya vifungu vya 275 hadi 287.

**Hukumu**

289. Utaratibu wa kutoa Hukumu.

290. Yaliyomo kwenye hukumu.

291. Haki ya mshtakiwa kupatiwa nakala ya hukumu.

**SEHEMU YA KUMI NA MBILI**
**ADHABU NA UTEKELEZAJI WAKE**

**Aina Tofauti za Adhabu**

292. Aina tofauti za adhabu.

**Adhabu ya kifo**

293. Adhabu ya kifo.

294. Utaratibu pale mwanamke aliyetiwa hatiani kwa kosa lenye adhabu ya kifo anapodai kuwa yeye ni mja mzito.

295. Rufaa ya uamuzi kwamba mwanamke siyo mja mzito.

296. Mshtakiwa kujulishwa haki ya kukata rufaa.

297. Uthibitisho kwa ajili ya kuweka kizuizini.

298. Kumbukumbu na taarifa kupelekwa kwa Rais.

**Adhabu ya Kifungo**

299. Kifungo.

300. Hati kwa adhabu ya kifungo.

301. Kutumika kizuizi cha polisi kwa ajili ya kifungo kidogo.

302. Adhabu kuchanganywa isipokuwa pale itakapoamuliwa vyenginevyo.

303. Adhabu katika hali ya hatia kwa makosa tofauti katika usikilizaji mmoja wa kesi.

304. Adhabu kwa mkosaji ambaye tayari ameshaadhibiwa kwa kosa jengine.

305. Wanafunzi wanaotoroka kutumikia kifungo kilichokuwa hakijamaliza pale anapokamatwa.

306. Kufutwa kwa adhabu ya viboko.

**Faini**

307. Faini badala ya au ziada ya kifungo.

308. Uwezo wa Mahakama.

309. Kutaifisha.

**Gharama**

310. Uwezo wa kutoza gharama dhidi ya mshtakiwa au mwendesha mashtaka binafsi.

311. Haki ya rufaa kutokana na amri ya gharama.

312. Kurejesha gharama.

**Fidia**

313. Mahakama inaweza kuamuru fidia.

314. Fidia katika kesi za makosa ya kingono.

315. Uwezo wa kuagiza ulipwaji wa gharama au fidia kutoka katika faini.

316. Uainishaji na upatikanaji wa fidia.

**Utekelezaji wa Amri kwa ajili ya Malipo ya Faini, Gharama, au Fidia kwa kukamata Mali**

317. Hati kwa ajili ya kutoza faini.

318. Pingamizi kwa ukamataji mali.

319. Kasoro au kukosekana muundo katika mwenendo wa kesi hakuwezi kubatilisha ukamataji.

**Kifungo Kwa Kushindwa Kulipa Faini, Gharama au Fidia**

320. Kifungo kwa kushindwa kulipa faini.

321. Uakhirishaji wa adhabu ya kifungo kwa kushindwa kulipa faini.

322. Kupelekwa Chuo cha Mafunzo kwa kushindikana ukamataji mali.

323. Kupelekwa Chuo cha Mafunzo badala ya ukamataji mali.

324. Kiwango cha kifungo kwa kushindwa kulipa faini.

325. Malipo yote baada ya mtu kupelekwa Chuo cha Mafunzo.

326. Sehemu ya malipo baada ya kupelekwa Chuo cha Mafunzo.

**Dhamana kwa Ajili ya Kutunza Amani au Kufika kwa ajili ya Hukumu**

327. Dhamana kwa ajili ya kutunza amani.

328. Dhamana kwa ajili ya kufika kupokea hukumu.

329. Masharti yanayotumika kwa, na ahadi ya dhamana chini ya vifungu vya 327 na 328.

**Kuachiwa Mkosaji Bila ya Kutiwa Hatiani au Kuwekwa kwenye Uangalizi**

330. Kuachiwa mkosaji bila ya kutiwa hatiani au kuwekwa kwenye uangalizi.

**Usimamizi**

331. Uwezo wa kumuweka mtu kwenye usimamizi.

332. Masharti yanayoweza kuwekwa kwa mtu anayewekwa kwenye usimamizi.

333. Kosa la kushindwa kutekeleza masharti yaliyowekwa kwa mtu aliyepo kwenye usimamizi.

**Hati na Amri**

334. Nani anaweza kutoa hati.

335. Marekebisho ya makosa na kasoro.

## SEHEMU YA KUMI NA TATU
## KUREJESHA MALI

**Mali Aliyokutwa nayo Mshtakiwa**

336. Mali aliyokutwa nayo mshtakiwa.

**Kurejeshwa Mali Iliyoibiwa**

337. Mali iliyoibiwa.

## SEHEMU YA KUMI NA NNE
## RUFAA KWA UJUMLA

338. Tafsiri.

339. Haki za asili za rufaa.

340. Kukata rufaa Mahakama Kuu.

341. Kukata rufaa Mahakama ya Hakimu wa Mkoa.

342. Kukata rufaa Mahakama ya Hakimu wa Wilaya.

343. Kukatwa rufaa na Mkurugenzi wa Mashtaka.

344. Kukata rufaa endapo mtu ameachiwa huru.

345. Notisi ya nia ya kukata rufaa.

346. Ukomo.

347. Ombi la rufaa.

348. Muomba rufaa katika Chuo cha Mafunzo.

349. Ukataaji wa rufaa mara moja.

350. Taarifa ya muda, pahala na usikilizaji.

351. Uwezo wa Mahakama inayosikiliza Rufaa.

352. Amri ya Mahakama inayosikiliza Rufaa itathibitishwa kwa mahakama ya chini.

353. Kupewa dhamana muomba rufaa na kuwa kizuizini kusubiri rufaa.

354. Uwezo wa kuchukua ushahidi wa ziada.

355. Idadi ya majaji katika rufaa.

356. Kuondoshwa kwa rufaa.

357. Rufaa katika Mahakama ya Rufaa.

358. Kupewa dhamana kusubiri rufaa katika Mahakama ya Rufaa.

**Mapitio**

359. Uwezo wa Mahakama Kuu kuita kumbukumbu.

360. Uwezo wa Mahakimu kuita kumbukumbu kwa mahakama ya chini.

361. Uwezo wa Mahakama Kuu katika mapitio.

362. Uwezo wa Mahakama katika kuwasikiliza wahusika wa kesi.

363. Idadi ya Majaji katika mapitio.

364. Amri ya mapitio itathibitishwa na Mahakama ya chini.

**Kupeleka Kesi Mahakama Kuu**

365. Kupeleka kesi Mahakama Kuu.

366. Kuimaliza kesi kwa mujibu wa uamuzi wa Mahakama Kuu.

367. Uwezo wa kuirejesha kesi katika Mahakama ya chini.

368. Idadi ya majaji kwa kesi iliyopelekwa Mahakama Kuu.

**Rufaa Kutoka Mahakama Kuu**

369. Rufaa kwa Mahakama ya Rufaa kuhusiana na hatia iliyopatikana katika Mahakama Kuu.

## SEHEMU YA KUMI NA TANO
## UPELELEZI WA VIFO VYA GHAFLA NA UCHUNGUZI WA VIFO

### Jukumu la Kutoa Taarifa ya Uhalifu au Ajali au Kifo katika Mazingira Fulani

370. Wajibu wa kutoa taarifa ya uhalifu.

371. Wajibu wa kutoa taarifa kuhusu kukutwa maiti.

### Upelelezi Kuhusiana na Vifo vya Ghafla

372. Upelelezi na taarifa ya polisi.

### Uchunguzi wa Vifo

373. Wajibu wa kumjulisha Jaji Mkuu.

374. Uchunguzi wa kifo unaofanywa na Hakimu.

## SEHEMU YA KUMI NA SITA
## MAELEKEZO YA HABEAS CORPUS NA AMRI NYENGINE ZA KIPEKEE

### Maelekezo ya Aina ya Habeas Corpus

375. Uwezo wa kutoa maelekezo ya aina ya habeas corpus.

376. Uwezo wa kutoa baadhi ya amri.

377. Uwezo wa kutunga kanuni.

## SEHEMU YA KUMI NA SABA
## MWENENDO WA KESI USIOFUATA UTARATIBU

378. Mwenendo wa kesi pahala pasipo sahihi.

379. Kupokelewa au kukataliwa ushahidi kimakosa.

380. Kuacha kula kiapo.

381. Kuacha na makosa katika mwenendo wa kesi.

## SEHEMU YA KUMI NA NANE
## MENGINEYO

382. Watu ambao viapo vinaweza kuapwa mbele yao.

383. Hatimkato za mwenendo wa kesi.

384. Kumbukumbu za kielektroniki.
385. Haki ya kupata nakala za mwenendo wa kesi.
386. Fomu zitakazotumika.
387. Gharama za washauri wa Mahakama na mashahidi.
388. Kanuni za jumla.
389. Marekebisho ya Sheria ya Mahakama za Mahakimu.
390. Kufuta Sheria ya Mwenendo wa Jinai, Nam. 7 ya 2004.
391. Masharti ya Mpito.

JADWELI

**SHERIA NAMBA 7 YA 2018**

**NIMESAINI**

**{DR. ALI MOHAMED SHEIN}**
**RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI**
**WA BARAZA LA MAPINDUZI**

21 Machi **, 2018**

# SHERIA YA KUFUTA SHERIA YA MWENENDO WA JINAI NAM. 7 YA 2004 NA KUTUNGA SHERIA MPYA YA MWENENDO WA JINAI NA KUWEKA UTARATIBU BORA WA UPELELEZI WA MAKOSA YA JINAI NA USIKILIZAJI WA KESI ZA JINAI NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO.

---

**IMETUNGWA** na Baraza la Wawakilishi Zanzibar.

## SEHEMU YA KWANZA
## MASHARTI YA UTANGULIZI

Jina fupi na kuanza kutumika.

**1.** Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Mwenendo wa Jinai, 2018 na itaanza kutumika baada ya kuwekwa saini na Rais.

Ufafanuzi.

**2.** Katika Sheria hii, isipokuwa kama maelezo yanahitaji vyenginevyo:

"kosa lenye dhamana" maana yake ni kosa ambalo mshtakiwa anaweza kupewa dhamana na Mahakama yoyote au mkuu wa kituo cha polisi kama ilivyoelezwa chini ya kifungu 151(1) cha Sheria hii;

"kosa analoweza kukamatwa mtu bila ya hati" maana yake ni kosa ambalo afisa wa polisi anaweza, kwa mujibu wa Jadweli ya Kwanza la Sheria hii au chini ya sheria yoyote ambayo kwa wakati huo inatumika, kukamata bila ya hati;

"mtoto" maana yake ni mtu aliye chini ya umri wa miaka 18;

"malalamiko" maana yake ni tuhuma zilizotolewa kwa mdomo au kwa maandishi mbele ya hakimu kwa lengo la kuchukua hatua chini ya Sheria hii;

"mlalamikaji" katika uendeshaji mashtaka binafsi maana yake ni mwendesha mashtaka binafsi au mtu anayepeleka malalamiko mbele ya Mahkama, katika mashtaka yote ya umma maana yake mtu anayewasilisha kesi mbele ya Mahakama kwa niaba ya Serikali;

"Mkurugenzi wa Mashtaka ya Jinai" maana yake ni mtu mwenye dhamana ya kuendesha mashtaka ya jinai aliyeteuliwa kwa mujibu wa masharti ya Katiba ya Zanzibar, 1984 na pale inapofaa itajumuisha wakili wa Serikali, mwendesha mashtaka wa umma au mtu mwengine yeyote anayeendesha mashtaka chini ya maelekezo ya Mkurugenzi wa Mashtaka;

"upelelezi" unajumuisha nyenendo zote chini ya Sheria hii kwa ajili ya ukusanyaji wa ushahidi zinazofanywa na afisa wa polisi au na mtu mwengine yeyote, asiyekuwa hakimu, ambaye amepewa mamlaka hayo na hakimu au na Mkurugenzi wa Mashtaka au chini ya sheria yoyote kwa ajili hiyo;

"Hakimu" ina maana iliyopewa na Sheria ya Mahakama za Mahakimu;

"uchunguzi wa kitabibu" unajumuisha upimaji au uchunguzi wa pumzi, damu, mabaka ya damu, mbegu za kiume, sampuli (katika kesi za kujamiiana), mate, jasho, sampuli za nywele, takataka za kucha za vidole kwa ajili ya uchunguzi wa vinasaba (DNA) na upimaji mwengine au uchunguzi ambao daktari aliyesajiliwa ataona ni muhimu katika kesi husika;

"afisa wa utabibu" maana yake ni daktari yeyote aliyeajiriwa na Serikali aliyesajiliwa chini ya masharti ya Sheria ya Madaktari na Madaktari wa Meno;

"daktari" maana yake ni daktari aliyesajiliwa chini ya Sheria ya Madaktari na Madaktari wa Meno;

"kosa lisilo na dhamana" maana yake ni kosa lililoainishwa chini ya kifungu cha 151(1) cha Sheria hii, ambalo dhamana inaweza kutolewa na Jaji Mkuu tu chini ya kifungu cha 151(4) cha Sheria hii;

"kosa asiloweza kukamatwa mtu bila ya hati ya kukamata" maana yake ni kosa ambalo afisa wa polisi hawezi kumkamata mtu bila ya hati ya kukamata;

"kosa" maana yake ni kutenda au kuacha kutenda kunakoadhibiwa na sheria yoyote inayotumika kwa wakati huo;

"mkuu wa kituo cha polisi" inajumuisha afisa yeyote mkubwa kwa cheo kuliko mkuu wa kituo cha polisi na pia inajumuisha, pale ambapo mkuu wa kituo hayupo katika kituo au hawezi kutokana na maradhi au sababu nyengine kutekeleza majukumu yake, afisa wa polisi aliyepo kwenye kituo ambaye anafuatia kwa cheo baada ya mkuu huyo wa kituo na yuko juu ya cheo cha koplo, au, pale ambapo Kamishna wa Polisi anaelekeza hivyo, afisa mwengine yeyote wa polisi aliyopo;

"makubaliano ya kukubali kosa" maana yake ni utaratibu ulioelezwa ndani ya Sheria hii kufikia makubaliano ya kukubali kosa;

"afisa wa polisi" inajumuisha mtendaji yeyote wa jeshi la polisi;

"kituo cha polisi" maana yake ni kituo kidogo au pahala palipoteuliwa na Kamishna wa Polisi kuwa kituo cha polisi, na inajumuisha eneo lolote linaloangaliwa na kituo hicho;

"Idara Maalum" maana yake ni idara ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iliyoanzishwa kwa mujibu wa kifungu cha 121 cha Katiba ya Zanzibar, 1984;

"Dola" kuhusiana na Mahakama za Zanzibar maana yake ni Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar;

"mahakama ya chini" maana yake ni mahakama yoyote iliyo chini ya Mahakama Kuu isiyokuwa Mahakama ya Kadhi;

"usikilizaji wa kesi moja kwa moja" maana yake ni usikilizaji wa kesi unaofanywa na mahakama ya chini kwa mujibu wa Sehemu ya Tisa ya Sheria hii.

Usikilizaji wa mashtaka kwa makosa yaliyo chini ya Sheria ya Adhabu na sheria nyengine.

**3.**-(1) Makosa yote chini ya Sheria ya Adhabu yatapelelezwa, yatachunguzwa, yatasikilizwa na kushughulikiwa kwa mujibu wa masharti yaliyomo katika Sheria hii.

(2) Makosa yote chini ya sheria nyengine yoyote yatapelelezwa, yatachunguzwa, yatasikilizwa, na vyenginevyo yatashughulikiwa kwa mujibu wa masharti hayo hayo, hata hivyo yatashughulikiwa kwa hali nyengine iwapo imeelezwa katika sheria yoyote inayotumika kwa wakati huo namna inayosimamia utaratibu au pahala pa uchunguzi, usikilizwaji au vyenginevyo ushughulikiaji wa makosa hayo.

(3) Bila ya kujali kitu chochote kilichomo katika Sheria hii, Mahakama Kuu inaweza, bila ya kuathiri masharti ya sheria yoyote inayotumika Zanzibar kwa wakati huo, katika kutekeleza mamlaka yake ya jinai kuhusu jambo au kitu chochote ambapo

utaratibu ulioelezwa katika Sheria hii hautumiki, kutekeleza mamlaka hayo kwa mujibu wa utaratibu kama unavyoelezwa na Mahakama za Nchi za Jumuiya ya Madola.

(4) Bila ya kuathiri ujumla wa masharti ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki, hakuna chochote katika Sheria hii kitakachochukuliwa kuathiri utaratibu wowote au uzoefu ambao unaweza kuelezwa katika mambo ya kijinai chini ya masharti ya:

(a) Sheria inayohusiana na kuwaweka wahalifu katika majaribio;

(b) Sheria ya Watoto Nam. 6 ya 2011;

(c) amri yoyote inayohusiana na Mahakama za Mahakimu inayotolewa na Jaji Mkuu wa Zanzibar chini ya Sheria ya Mahakama za Mahakimu; au

(d) kanuni zozote zilizotengenezwa au zinazochukuliwa kuwa zimetengenezwa chini ya sheria yoyote katika hizo zilizotajwa.

## SEHEMU YA PILI
## UWEZO WA MAHAKAMA

Makosa chini ya Sheria ya Adhabu.

**4.**-(1) Kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii, kosa lolote chini ya Sheria ya Adhabu linaweza kusikilizwa na Mahakama Kuu au Mahakama yoyote ya chini kama ilivyoainishwa chini ya Jadweli la Kwanza la Sheria hii.

(2) Mamlaka ya mahakama ya chini inayoongozwa na Hakimu wa Mkoa itakuwa na mamlaka ya ziada na itajumuisha usikilizaji wa makosa yaliyopo chini ya vifungu vifuatavyo vya Sheria ya Adhabu, yaani, vifungu 108, 115, 133, 134, 143, 279, 281, 319, 339, 340 na 341.

(3) Isipokuwa katika mazingira ya kiwango cha chini kabisa cha adhabu kama ilivyoelezwa katika sheria yoyote ambayo kwa wakati huo inatumika kwa ajili ya kusikiliza kesi hiyo mbele ya Mahakama, Mahakama ya Hakimu wa Mkoa haitokuwa na mamlaka ya kutoa adhabu ya kifungo kinachozidi miaka kumi na nne isipokuwa pale ambapo mahakama hiyo imepewa mamlaka ya ziada kwa mujibu wa Sheria ya Mahakama za Mahakimu.

Makosa chini ya sheria nyengine.

**5.**-(1) Kosa lolote chini ya sheria yoyote isiyokuwa Sheria ya Adhabu, pale ambapo mahakama yoyote imetajwa kwa ajili hiyo katika sheria hiyo, litasikilizwa na mahakama hiyo.

(2) Pale ambapo hakuna mahakama iliyotajwa, linaweza, kwa kuzingatia masharti mengine ya Sheria hii, kusikilizwa na Mahakama Kuu, au na mahakama yoyote ya chini ambayo kosa hilo limeainishwa katika Jadweli la Kwanza kuwa litasikilizwa.

Adhabu zinazoweza kutolewa na Mahakama Kuu.

**6.** Mahakama Kuu inaweza kutoa adhabu yoyote au kutoa amri nyengine yoyote inayoruhusiwa na sheria.

Adhabu ambazo Hakimu wa Mahakama ya Mkoa anaweza kutoa.

**7.** Mahakama ya Hakimu wa Mkoa inaweza, katika kesi ambazo adhabu hizo zinaruhusiwa na sheria, kutoa adhabu zifuatazo:

(a) kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka kumi na nne;

(b) faini isiyozidi Shilingi Milioni Kumi na Nne; au

(c) kutumikia jamii kwa kipindi kisichozidi miezi kumi na mbili kwa mujibu wa Kanuni zilizotungwa na Jaji Mkuu.

Adhabu ambazo Hakimu wa Mahakama ya Wilaya anaweza kutoa.

**8.** Mahakama ya Hakimu wa Wilaya inaweza, katika kesi ambazo adhabu hizo zinaruhusiwa na sheria, kutoa adhabu zifuatazo:

(a) kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka saba;

(b) faini isiyozidi Shilingi Milioni Saba; au

(c) kutumikia jamii kwa kipindi kisichozidi miezi sita kwa mujibu wa Kanuni zilizotungwa na Jaji Mkuu.

Adhabu ambazo Mahakama ya Mwanzo inaweza kutoa.

**9**. Mahakama ya Mwanzo inaweza, katika kesi ambazo adhabu hizo zinaruhusiwa na sheria, kutoa adhabu zifuatazo:

(a) kifungo kwa kipindi kisichozidi mwaka mmoja;

(b) faini isiyozidi Shilingi Milioni Moja; au

(c) kutumikia jamii kwa kipindi kisichozidi miezi miwili kwa mujibu wa Kanuni zilizotungwa na Jaji Mkuu.

Kusimamisha adhabu ya kifungo.

**10.**-(1) Isipokuwa kama maelezo yanahitaji vyenginevyo, mahakama yoyote ambayo inatoa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka mitatu kwa kosa lolote, inaweza kuamrisha kwamba adhabu hiyo haitaanza kutekelezwa hadi pale katika kipindi kilichoainishwa na mahakama hiyo mkosaji huyo atakapotenda kosa jengine, ama kosa hilo linaadhibiwa kwa kifungo, faini au adhabu zote mbili.

(2) Pale ambapo mkosaji ametiwa hatiani kwa kosa katika kipindi kilichoainishwa cha usimamishwaji wa adhabu, adhabu kwa kosa la kwanza alilotiwa hatiani chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, itaanza kutekelezwa.

(3) Adhabu iliyotolewa kwa kosa lililofuata itatekelezwa baada ya kutekelezwa kwa adhabu iliyotolewa kwa kosa la kwanza.

Mahakama za chini zinaweza kuwapeleka watu waliotiwa hatiani kwenda mahakama za juu yake kwa ajili ya kupewa adhabu.

**11.**-(1) Pale ambapo chini ya masharti ya Sheria hii, mahakama ya chini imemtia hatiani mtu yeyote kwa kosa, baadae, ikiwa kwa kupata taarifa juu ya tabia na historia ya mtu huyo au juu ya mazingira na kuenea kwa kosa hilo mahakama ikawa na maoni kwamba kwa mazingira hayo adhabu kubwa itapaswa kutolewa kwa kosa hilo kuliko ile ambayo mahakama hiyo ina uwezo wa kutoa, mahakama inaweza, badala ya kumshughulikia mtu huyo kwa namna yoyote, itampeleka mkosaji huyo katika hifadhi ya mahakama ya juu kwa ajili ya kupewa adhabu kwa mujibu wa masharti ya kifungu hiki.

(2) Endapo mtu aliyetiwa hatiani ikiwa amepelekwa katika mahakama ya juu kwa ajili ya kupewa adhabu chini ya masharti ya kifungu hiki, mahakama hiyo ya juu itachunguza mazingira ya kesi hiyo na ama itarudisha kesi hiyo katika mahakama iliyomleta mkosaji, au itamshughulikia mkosaji katika namna yoyote ambayo mkosaji huyo angeweza kushughulikiwa na mahakama ya juu ikiwa mkosaji huyo angetiwa hatiani na mahakama hiyo ya juu kwa kosa husika.

(3) Ikiwa chini ya masharti ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki, mahakama ya juu inairejesha kesi hiyo kwa ajili ya adhabu katika mahakama iliyomleta mkosaji, masharti ya Sheria hii kuhusiana na mapitio, uthibitishaji wa adhabu hiyo na rufaa dhidi ya hatia au adhabu yatatumika kama yanavyotumika kwa ajili ya kesi nyengine yoyote inayosikilizwa na mahakama ya chini.

(4) Ikiwa mahakama ya juu inatoa adhabu kwa mtu aliyetiwa hatiani, masharti ya Sheria hii kuhusiana na rufaa dhidi ya hatia tu yatatumika kama yanavyotumika kwa kesi nyengine yoyote iliyosikilizwa na mahakama ya chini.

(5) Ikiwa mahakama ya juu inatoa adhabu kwa mtu aliyetiwa hatiani, mtu huyo anaweza kukata rufaa dhidi ya adhabu kwa mahakama ya juu zaidi kuliko mahakama ya juu iliyompa adhabu katika utaratibu ule ule kama kwamba mtu huyo ametiwa hatiani na mahakama ya juu, na masharti ya Sheria hii yanayohusiana na rufaa dhidi ya adhabu iliyotolewa na mahakama ya juu yatatumika ipasavyo katika mahakama inayosikiliza rufaa.

(6) Mahakama ya juu inaweza, kwa uwezo wake, kuakhirisha uchunguzi wake chini ya masharti ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki, mpaka utakapomalizika muda wa kuwasilisha taarifa ya kukata rufaa dhidi ya hatia, na ikiwa taarifa hiyo imeshawasilishwa mbele ya mahakama ya juu itaanza uchunguzi huo, mahakama ya juu inaweza, kwa uwezo wake, kuakhirisha uchunguzi huo hadi uamuzi wa mwisho wa rufaa hiyo au rufaa zinazofuata au kwa kipindi kifupi zaidi kama mahakama itavyoona inafaa.

(7) Endapo mtu ambaye amepelekwa katika mahakama ya juu kwa ajili ya kupewa adhabu, kwa mujibu wa masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, yuko kizuizini na amewasilisha taarifa ya kukata rufaa dhidi ya kutiwa kwakwe hatiani, mahakama ya juu au mahakama ya chini ambayo imemtia hatiani mtu huyo inaweza, kwa sababu zitakazowekwa kwenye kumbukumbu na mahakama kwa maandishi, kutoa dhamana kwa kuwa na wadhamini au bila ya wadhamini kwa ajili ya kusubiri usikilizaji wa rufaa hiyo.

(8) Masharti ya kifungu hiki yatatafsiriwa kwa ajili ya kuiwezesha mahakama ya juu katika kuishughulikia kesi yoyote iliyopo mbele yake kutumia uwezo wake wa mapitio kwa namna ile ambayo kama kwamba kumbukumbu za mwenendo wa kesi chini ya kifungu hicho zimeshawasilishwa kwa mahakama ya juu kwa ajili ya kutoa amri.

(9) Kwa madhumuni ya kifungu hiki, maneno "mahakama ya juu" maana yake ni mahakama ya juu zaidi kimamlaka inayofuata baada tu ya mahakama ambayo imemtia hatiani.

## SEHEMU YA TATU
## MASHARTI YA JUMLA KUHUSU KUKAMATA, KUTOROKA NA KUKAMATA TENA

### Kukamata

Kukamata, vipi kunafanyika.

**12.-**(1) Katika kukamata afisa wa polisi au mtu mwengine anayefanya ukamataji atamshika kikamilifu au atauzuia mwili wa mtu anayetaka kukamatwa, isipokuwa kama atajisalimisha mwenyewe kwa maneno au vitendo.

(2) Ikiwa mtu huyo atakaidi kwa nguvu juhudi za kumkamata, au atajaribu kukwepa kukamatwa, afisa huyo wa polisi au mtu mwengine anaweza kutumia njia zote za lazima kufanikisha ukamataji.

Ushughulikiaji wa mtu aliyekamatwa.

**13.-**(1) Mtu aliyekamatwa hatotendewa jambo lolote dhidi ya heshima ya utu wake wala hatodhalilishwa kimwili au kimaadili.

(2) Mtu aliyekamatwa atakuwa na haki ya kuipa taarifa familia yake, au taasisi ambayo yeye anahusika nayo, na kuwasiliana nayo kuhusu kukamatwa huko.

(3) Endapo mtu aliyekamatwa ni mtoto, au mwenye ugonjwa wa akili, au maradhi yoyote, katika namna ambayo kwamba mtu huyo hawezi kuwasiliana na familia yake, au taasisi ambayo mtu huyo anahusika nayo, Polisi, Mwendesha Mashtaka au Mahakama, kwa jitihada zake yenyewe, itaijulisha familia au taasisi husika.

(4) Mtu aliyekamatwa atakuwa na haki ya kupata kiasi cha kutosha cha chakula, mavazi na vifaa vyengine vya kawaida, kwa gharama zake mwenyewe, kwa mujibu wa masharti yanayohusiana na usalama na utulivu wa jamii.

(5) Mtu aliyekamatwa atakuwa na haki wakati wote kuwasiliana au kukutana na wakili aliyemchagua yeye mwenyewe wakati yupo chini ya kizuizi cha polisi au wakati wa mahojiano na hatohamishwa, au kupelekwa pahala pengine isipokuwa kutokana na amri au maelekezo ya Mkurugenzi wa Mashtaka au mahakama kama itakavyokuwa.

Upekuzi wa pahala alipoingia mtu anayetafutwa ili akamatwe.

**14.**-(1) Endapo mtu yeyote anaitekeleza hati ya ukamataji, au afisa yeyote wa polisi mwenye mamlaka ya kukamata, ana sababu ya kuamini kwamba mtu anayetaka kukamatwa ameingia ndani au yumo ndani ya pahala popote, mtu anayeishi ndani humo au mwenye dhamana ya pahala hapo atawajibika, atakapotakiwa na mtu anayetekeleza hati ya ukamataji au afisa wa polisi mwenye mamlaka ya kukamata, kumruhusu bila pingamizi kuingia ndani humo na kumuwezesha kwa njia zote zitakazowezekana kufanya upekuzi ndani humo.

(2) Endapo uingiaji katika pahala hapo hauwezi kupatikana chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, itakuwa halali kwa njia yoyote kwa mtu anayetekeleza hati ya ukamataji, na katika hali yoyote ambayo hati ingeweza kutolewa, lakini haiwezi kupatikana bila ya kuwezesha mtu anayetaka kukamatwa kupata fursa ya kutoroka, kwa afisa wa polisi, kuingia pahala hapo na kufanya upekuzi ndani humo, na, kwa ajili ya kuwezesha kuingia ndani ya pahala hapo, kuvunja mlango wa nje au wa ndani au dirisha lolote la nyumba yoyote au pahala, ama pa mtu huyo anayetaka kukamatwa au pa mtu mwengine yoyote au vyenginevyo kuwezesha kuingia ndani ya nyumba au pahala, ikiwa baada ya kutoa taarifa ya mamlaka yake na makusudio yake, na kutaka kuruhusiwa kuingia ndani hakuweza vyenginevyo kupata ruhusa.

(3) Ikiwa pahala popote hapo ni fleti inayokaliwa na mwanamke, asiyekuwa mtu anayetaka kukamatwa, ambaye, kwa mujibu wa desturi, hatakiwi kuonekana hadharani, mtu huyo au afisa wa polisi, kabla ya kuingia ndani ya fleti hiyo, atatoa taarifa kwa mwanamke huyo kwamba yuko huru kuondoka na atampa fursa muafaka ya kuweza kuondoka, na baadae anaweza kuvunja fleti hiyo na kuingia.

(4) Endapo mwanamke ndiye anayetakiwa kukamatwa, isipokuwa kama mazingira yanahitaji vyenginevyo au isipokuwa kama afisa wa polisi ni mwanamke, kujisalimisha kwake chini ya ulinzi kwa taarifa ya mdomo kutachukuliwa kuwa amejisalimisha na afisa wa polisi hatougusa mwili wa mwanamke huyo kwa ajili ya kumkamata.

(5) Hakuna chochote kitakachohalalisha utumiaji wa nguvu ya ziada kuliko inayostahiki katika mazingira maalum ambayo katika mazingira hayo nguvu hiyo

imetumika au ni ya lazima kwa ajili ya ukamataji wa mkosaji, au inayokusudiwa au inayoweza kupelekea kusababisha kifo au madhara makubwa ya mwili kwa mkosaji.

(6) Ukamataji hautofanywa isipokuwa kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii na, isipokuwa katika mazingira maalum, mtoto au mwanamke hatokamatwa baada ya kuchwa kwa jua au kabla ya kuchomoza jua.

(7) Endapo mazingira hayo maalum yapo kama ilivyotajwa katika kifungu kidogo cha (6) cha kifungu hiki, afisa wa polisi, kwa kuandaa taarifa ya maandishi, atapata kwanza ruhusa ya mahakama ambayo ndani ya eneo lake kosa limetendeka au ukamataji utafanyika.

(8) Kwa mujibu wa Sheria hii, ukamataji wowote wa mtoto unaofanywa ni lazima ufuate masharti ya Sheria ya Watoto.

Uwezo wa kuvunja ili kutoka nje ya nyumba au pahala kwa madhumuni ya kujiokoa.

**15.** Afisa wa polisi au mtu mwengine aliyeidhinishwa kufanya ukamataji anaweza kuvunja ili atoke nje ya nyumba yoyote au pahala kwa ajili ya kujiokoa yeye mwenyewe au mtu mwengine yeyote ambaye, aliingia kihalali kwa madhumuni ya kufanya ukamataji, akafungiwa ndani yake.

Kutokuwepo kizuizi kisicho cha lazima.

**16.** Mtu aliyekamatwa hatowekwa kwenye kizuizi kikubwa zaidi ya kile cha lazima kuzuia asitoroke.

Upekuzi wa watu waliokamatwa.

**17.** Wakati wowote ambapo mtu amekamatwa:

(a) na afisa wa polisi chini ya hati ambayo hairuhusu kupewa dhamana, au chini ya hati inayoruhusu kupewa dhamana lakini mtu aliyekamatwa akashindwa kuweka dhamana; au

(b) bila ya hati, au amekamatwa na mtu binafsi chini ya hati, na mtu aliyekamatwa hawezi kisheria kupewa dhamana au akashindwa kuweka dhamana,

afisa wa polisi aliyefanya ukamataji au, pale ukamataji unapofanywa na mtu binafsi, afisa wa polisi aliyekabidhiwa mtu huyo aliyekamatwa anaweza kumpekua mtu huyo na kuweka katika sehemu salama vitu vyote vilivyoorodheshwa na kusajiliwa, isipokuwa vitu muhimu vya kuvaa alivyokutwa navyo, na kumpatia nakala mtu huyo aliyekamatwa.

Uwezo wa afisa wa polisi kuzuia na kupekua vyombo, watu katika mazingira fulani.

**18.** Afisa wa polisi anaweza kusimamisha, kupekuwa na kuzuia chombo chochote cha majini, boti, ndege au chombo cha nchi kavu ambapo ndani au juu ya chombo hicho ana sababu ya kutuhumu kwamba kitu chochote kilichoibiwa au kilichopatikana bila

halali kinaweza kukutwa, au mtu ambaye kuna sababu za msingi za kutuhumiwa ana katika umiliki wake au anasafirisha kwa namna yoyote kitu chochote kilichoibiwa au kilichopatikana bila halali, na anaweza kukichukua kitu chochote hicho.

Namna ya kuwapekua wanawake

**19.** Wakati wowote ikiwa ni lazima kuwezesha mwanamke kupekuliwa, upekuzi utafanywa na afisa mwengine wa polisi mwanamke au mtumishi wa umma mwanamke kwa kuzingatia kikamilifu heshima yake.

Uwezo wa kuchukua silaha za hatari.

**20.** Afisa au mtu mwengine anayefanya ukamataji wowote anaweza kuchukua kutoka kwa mtu aliyekamatwa silaha ya hatari yoyote ambayo anayo mtu huyo, na atawasilisha silaha zote hizo alizozichukua mbele ya mahakama au mbele ya afisa, mahakama ambayo au afisa ambaye mtu aliyefanya ukamataji anatakiwa kisheria kumpeleka mtu huyo aliyekamatwa.

**Kukamata bila ya hati**

Ukamataji unaofanywa na afisa wa polisi bila ya hati.

**21.**-(1) Afisa wa polisi anaweza, bila ya amri kutoka kwa hakimu na bila ya hati, kukamata:

(a) mtu ambaye anatenda, mbele ya afisa wa polisi, kosa analoweza kukamatwa mtu bila ya hati;

(b) mtu ambaye dhidi yake malalamiko ya msingi yamewasilishwa au taarifa za kuaminika zimepokelewa au zipo tuhuma za msingi kwamba mtu ametenda kosa au anahusika katika kosa analoweza kukamatwa mtu bila ya hati;

(c) mtu ambaye anamtuhumu kwa sababu za msingi kuwa amehusika katika tendo lolote lililotendwa pahala popote nje ya Zanzibar ambalo, kama lingetendwa Zanzibar, lingeadhibiwa kama kosa, na kwa tendo hilo mtu huyo chini ya sheria inayohusu ubadilishanaji wahalifu, angepaswa kukamatwa na kuwekwa kizuizini Zanzibar;

(d) mtu ambaye ana katika umiliki wake bila ya sababu ya msingi, jukumu la kuthibitisha sababu hiyo lipo juu ya mtu huyo, kifaa chochote cha kuvunjia nyumba;

(e) mtu yeyote aliyetiwa hatiani na kuachiwa anatenda kosa la kuvunja sharti lolote lililoainishwa katika kifungu cha 328 cha Sheria hii au Kanuni yoyote iliyotengenezwa chini yake;

(f) mtu ambaye kwa ajili yake ana sababu za msingi za kuamini kwamba hati ya kumkamata ilikwishatolewa.

(2) Kwa madhumuni ya masharti ya aya ya (a) na (b) ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, mtu hatokamatwa kwa kosa analoweza kukamatwa mtu bila ya hati linaloadhibiwa kwa adhabu ya kifungo kilicho chini ya miaka saba isipokuwa:

(a) afisa wa polisi ana sababu ya kuamini kwa msingi wa malalamiko hayo, taarifa au tuhuma kwamba mtu huyo ametenda kosa hilo; au

(b) afisa wa polisi anaridhika kwamba kukamatwa mtu huyo ni lazima kwa ajili ya kumzuia mtu huyo kutenda kosa jengine lolote au kusababisha ushahidi wa kosa kupotea au kwa ajili ya upelelezi unaofaa wa kosa hilo.

(3) Afisa wa polisi, katika namna yoyote ambapo ukamataji wa mtu hauhitajiki chini ya kifungu hiki, ataweka kumbukumbu kwa maandishi ya sababu za kutokufanya ukamataji.

(4) Kwa mujibu wa masharti ya kifungu cha 24 cha Sheria hii, mtu asiyehusika katika kosa asiloweza kukamatwa mtu bila ya hati au dhidi ya mtu ambaye malalamiko yametolewa dhidi yake au taarifa za kuaminika zimepokelewa au zipo tuhuma za msingi za kuhusika kwake huko, hatokamatwa isipokuwa chini ya hati iliyotolewa na mahakama yenye mamlaka.

Notisi ya kufika mbele ya afisa wa polisi.

**22.**-(1) Endapo kesi itakuwa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu cha 21 cha Sheria hii, afisa wa polisi, badala ya kumkamata mtu husika, atatoa notisi kwa mtu huyo kumtaka kufika mbele ya polisi aliyetoa notisi au kufika sehemu nyengine kama ilivyoainishwa katika notisi kushirikiana na polisi katika upelelezi wa kosa lililotajwa katika kifungu kidogo cha (1) cha kifungu cha 21 cha Sheria hii.

(2) Pale notisi hiyo itakapotolewa kwa mtu, itakuwa ni jukumu la mtu huyo kufuata maelekezo ya notisi hiyo iliyotolewa.

(3) Pale mtu anatekeleza na anaendelea kutekeleza notisi hiyo, mtu huyo hatokamatwa kuhusiana na kosa lililotajwa katika notisi hiyo, isipokuwa kwa sababu zitakazorikodiwa, polisi ataona kwamba mtu huyo anapaswa kukamatwa.

(4) Endapo mtu huyo, wakati wowote, anashindwa kufuata masharti ya notisi au hayuko tayari kujitambulisha yeye mwenyewe, polisi anaweza, kwa mujibu wa amri zilizotolewa na mahakama yenye mamlaka kwa ajili hiyo, kumkamata mtu huyo kwa kosa lililotajwa katika notisi.

Tangazo kwa mtu anayetoroka.

**23.**-(1) Iwapo mahakama yoyote ina sababu za kuamini, ama baada ya kuchukua ushahidi au bila ya kuchukua ushahidi, kwamba mtu yeyote ambaye dhidi yake hati

imeshatolewa na mahakama hiyo ametoroka au anajificha yeye mwenyewe ili kwamba hati hiyo isiweze kutekelezwa, mahakama itachapisha tangazo la maandishi linalomtaka mtu huyo kufika pahala palipoainishwa na wakati ulioainishwa si chini ya siku thelathini kuanzia tarehe ya kuchapishwa kwa tangazo hilo.

(2) Tangazo litachapishwa kama ifuatavyo:

(a) tangazo litasomwa hadharani pahala pa wazi katika mji, kijiji au mtaa katika au karibu na pahala ambapo mtu huyo kwa kawaida anaishi;

(b) tangazo litabandikwa kwenye sehemu ya wazi ya nyumba au pahala pengine ambapo mtu huyo kikawaida anaishi au sehemu ya wazi katika mji, kijiji au mtaa; na

(c) nakala ya tangazo hilo itabandikwa kwenye sehemu ya wazi mahakamani.

(3) Maelezo ya maandishi ya mahakama iliyotoa tangazo yanayoeleza kwamba tangazo limechapishwa kwa kufuata taratibu zote katika siku iliyoainishwa itakuwa ni ushahidi tosha kwamba matakwa ya kifungu hiki yametimizwa na kwamba tangazo limechapishwa katika siku hiyo.

Ukamataji wa mali ya mtu aliyetangazwa.

**24.**-(1) Mahakama iliyotoa tangazo chini ya kifungu cha 23 cha Sheria hii, inaweza wakati wowote kuamrisha kukamatwa kwa mali yoyote inayohamishika au isiyohamishika au zote kwa pamoja zinazomilikiwa na mtu huyo aliyetangazwa.

(2) Amri hiyo itaidhinisha ukamataji wa mali yoyote inayomilikiwa na mtu huyo ndani ya eneo la mipaka ya mamlaka ya mahakama ambayo imetoa tangazo hilo, na itaidhinisha ukamataji wa mali yoyote ya mtu huyo nje ya eneo la mipaka ya mamlaka ya mahakama pale itakapoidhinishwa na hakimu ambaye ndani ya eneo la mipaka ya mahakama yake mali hiyo ipo.

(3) Ikiwa mali iliyoamriwa kukamatwa inajumuisha madeni au mali nyengine inayohamishika ukamataji utafanywa:

(a) kwa kutwaa;

(b) kwa kuteua mpokeaji mali;

(c) kwa kutoa amri ya maandishi inayokataza kumpa mali hiyo mtu aliyetangazwa au mtu yeyote kwa niaba ya mtu huyo aliyetangazwa, au

(d) kwa njia zote au mbili zozote kati ya njia hizo kama mahakama itakavyoona inafaa.

(4) Ikiwa mali iliyoamriwa kukamatwa ni mali isiyohamishika, ukamataji chini ya kifungu hiki utakuwa kwa kupitia kwa Mkurugenzi wa Ardhi na Usajili; na baada ya kupokea amri ya kukamata Mkurugenzi huyo au afisa yeyote aliyeidhinishwa kwa niaba yake atatekeleza hayo:

(a) kwa kuchukua na kuweka mikononi mwake;

(b) kwa kuteua mpokeaji mali;

(c) kwa kutoa amri ya maandishi inayokataza ulipaji wa malipo ya kodi au upokeaji wa mali kwa mtu aliyetangazwa au kwa mtu yeyote kwa niaba ya mtu huyo aliyetangazwa; au

(d) kwa njia zote au mbili zozote kati ya njia hizo kama atakavyoona inafaa.

(5) Ukamataji huo wa ardhi yoyote inayomilikiwa kwa hati ya umiliki hautoanza kuwa na nguvu za kisheria mpaka amri ya ukamataji itakaposajiliwa ipasavyo chini ya sheria ya usajili.

(6) Mamlaka, wajibu na dhima ya mpokeaji mali aliyeteuliwa chini ya kifugu hiki zitakuwa sawa na zile za mpokeaji mali aliyeteuliwa chini ya Kanuni za mahakama zinazotumika kwa wakati huo.

(7) Ikiwa mtu aliyetangazwa hakufika ndani ya wakati ulioainishwa katika tangazo, mali itakuwa katika uangalizi wa Serikali, lakini haitauzwa mpaka itakapomalizika miezi sita kuanzia tarehe ya ukamataji isipokuwa kama kimaumbile mali hiyo inaweza kuharibika haraka, au mahakama inaona kwamba kuuzwa kwa mali hiyo itakuwa ni kwa manufaa ya mmiliki, katika hali yoyote kati ya hizo mahakama inaweza kuwezesha kuuzwa kwa mali hiyo wakati wowote itakapoona inafaa.

(8) Mtu mwengine asiyekuwa mtu aliyetangazwa anaweza kufika mbele ya mahakama iliyotoa amri ya ukamataji na kudai, kueleza maslahi yake au umiliki wake katika mali hiyo, mali hiyo au sehemu yoyote ya mali hiyo iliyokamatwa au iliyoamriwa kukamatwa ikizingatiwa kwamba dai hilo liwe limefanywa ndani ya miezi mitatu kutoka siku iliyotolewa amri ya kukamatwa.

(9) Mahakama itarikodi dai hilo lililodaiwa na itawezesha dai hilo kupelekwa kwa muendesha mashtaka wa Serikali pamoja na notisi inayomtaka ahudhurie mbele ya mahakama katika siku na wakati ulioelezwa katika notisi hiyo kwa ajili ya kuonesha sababu kwa nini mali hiyo, ikiwa itakamatwa, isiachiwe, au kwa nini amri ya ukamataji isifutwe kwa kiasi ambacho kinahusisha mali hiyo inayodaiwa.

(10) Wakati wa kusikiliza mahakama itaendelea kuchunguza ukweli na haki ya dai lililodaiwa na kuchukua ushahidi huo kama itakavyolazimu.

(11) Uchunguzi huo utafanywa, kama itakavyowezekana, katika utaratibu utakaoelezwa baadae ndani ya Sheria hii kuhusu uendeshaji wa kesi za moja kwa moja mbele ya mahakimu.

(12) Mahakama, iwapo itaridhika na ukweli na haki kuhusu dai lililoletwa, itaelekeza mali hiyo iachiwe au amri hiyo ifutwe, au ikiwa itaridhika kama ilivyoelezwa kuhusu sehemu tu ya dai lililoletwa itaelekeza sehemu hiyo kuachiwa au sehemu ya amri hiyo inayohusu sehemu ya dai lililoletwa ifutwe.

Kurejesha mali iliyokamatwa.

**25.** Ikiwa ndani ya miaka miwili kutoka tarehe ya ukamataji, mtu yeyote ambaye mali yake ipo au imekuwepo katika uangalizi wa Serikali chini ya kifungu cha 24, cha Sheria hii, amefika kwa hiari yake au amekamatwa na ameletwa mbele ya mahakama ambayo kwa amri ya mahakama hiyo mali ilikamatwa na akathibitisha kwa kuiridhisha mahakama kwamba hakutoroka, au kujificha kwa ajili ya kuepuka kutekelezwa kwa hati, na kwamba hakuwa na taarifa ya tangazo hilo kumuwezesha kuhudhuria ndani ya wakati ulioanishwa ndani yake, mali au, ikiwa mali hiyo imeshauzwa, mapato halisi ya mauzo hayo au, ikiwa sehemu tu ya mali hiyo imeshauzwa, mapato halisi ya mauzo hayo na kilichobaki kwenye mali, baada ya kulipa gharama zilizoingiwa kutokana na kukamatwa, atarejeshewa mwenyewe.

Ukamataji wa wazururaji na majambazi sugu.

**26.** Mkuu wa kituo cha polisi anaweza kwa njia kama hiyo kukamata au kuwezesha kukamatwa:

(a) mtu yeyote atakayekutwa anachukua tahadhari ya kujificha ndani ya mipaka ya kazi ya kituo hicho katika mazingira yanayowezesha kuamini kwamba anachukua tahadhari hizo akiwa na nia ya kutenda kosa analoweza kukamatwa mtu bila ya hati;

(b) mtu yeyote ndani ya mipaka ya kituo ambaye hana njia za wazi za kipato zinazomuwezesha kuishi au ambaye hawezi kutoa maelezo yanayojitosheleza kuhusu yeye mwenyewe;

(c) mtu yeyote ambaye kwa sifa ni jambazi sugu, mvunjaji nyumba au mwizi au mzoefu wa kupokea vitu vilivyoibiwa akijua kuwa vimeibiwa, au ambaye kwa sifa anafanya uporaji kwa nguvu au katika kufanya uporaji kwa nguvu anawaweka au anajaribu kuwaweka watu katika hali ya kuogopa kudhuriwa.

Ukamataji bila hati unaofanywa na afisa mdogo wa polisi.

**27.** Wakati mkuu wa kituo cha polisi anapomtaka afisa wa polisi aliye chini yake kumkamata bila ya hati mtu ambaye kisheria anaweza kukamatwa bila ya hati chini ya masharti ya kifungu cha 21 cha Sheria hii, iwapo kosa halijatendeka mbele ya afisa huyo wa polisi aliyeamriwa kukamata, mkuu wa kituo atatoa kwa afisa aliyemtaka

kufanya ukamataji amri ya maandishi inayoainisha mtu anayetakiwa kukamatwa na kosa au sababu nyengine inayotaka ukamataji ufanyike.

Kukataa kutoa jina na kutaja makaazi.

**28.**-(1) Wakati mtu yeyote akiwa mbele ya afisa wa polisi amctenda au ametuhumiwa kutenda kosa asiloweza kukamatwa mtu bila ya hati anakataa baada ya kutakiwa na afisa huyo kutaja jina lake au makaazi yake, au anataja jina au makaazi ambayo afisa huyo ana sababu za msingi za kuamini kuwa ni uongo, anaweza kukamatwa na afisa huyo ili kwamba jina lake na makaazi yake yaweze kuhakikiwa.

(2) Wakati jina na makaazi halisi ya mtu huyo yamehakikiwa ataachiwa baada ya kutekeleza masharti ya dhamana, akiwa na wadhamini au bila ya kuwa na wadhamini, kufika mbele ya hakimu ikiwa atahitajika kufanya hivyo.

(3) Ikiwa mtu huyo siyo mkaazi wa Zanzibar dhamana italazimika kuchukuliwa na mdhamini au wadhamini ambao ni wakaazi wa Zanzibar.

(4) Ikiwa jina na makaazi halisi ya mtu huyo hayatahakikiwa ndani ya saa ishirini na nne kuanzia muda wa kukamatwa, au kama atashindwa kutekeleza masharti ya dhamana au, iwapo itahitajika kufanya hivyo, kuwaleta wadhamini wanaotosheleza, atapelekwa mara moja kwa hakimu mwenye mamlaka aliye karibu.

Kuwashughulikia watu waliokamatwa na afisa polisi.

**29.** Afisa wa polisi anayefanya ukamataji bila hati, bila ya kuchelewa na kwa kuzingatia masharti yaliyomo ndani ya Sheria hii kuhusu utoaji wa dhamana, atalazimika kumchukua au kumpeleka mtu huyo aliyekamatwa mbele ya hakimu mwenye mamlaka ya kusikiliza kesi hiyo, au mbele ya mkuu wa kituo cha polisi.

Ukamataji unaofanywa na watu binafsi.

**30.**-(1) Mtu yeyote binafsi anaweza kumkamata mtu yeyote ambaye akiwa mbele yake anatenda kosa analoweza kukamatwa bila ya hati, au ambaye ana sababu za kumtuhumu kuwa ameshatenda kosa.

(2) Watu wanaokutwa wanatenda kosa lolote linalohusisha uharibifu wa mali wanaweza kukamatwa bila ya hati na mmiliki wa mali hiyo au wafanyakazi wake au watu walioidhinishwa na mmiliki wa mali.

Kumshughulikia mtu aliyekamatwa na mtu binafsi.

**31.**-(1) Mtu yeyote binafsi anayemkamata mtu mwengine yeyote bila ya hati atalazimika, bila ya kuchelewa, kumkabidhi mtu huyo aliyekamatwa kwa afisa wa polisi, au kama hakuna afisa wa polisi atampeleka mtu huyo kwenye kituo cha polisi kilicho karibu.

(2) Iwapo kuna sababu za kuamini kwamba mtu huyo yupo chini ya masharti ya kifungu cha 27 cha Sheria hii, afisa polisi atamkamata tena mtu huyo.

(3) Ikiwa kuna sababu za kuamini kuwa ametenda kosa asiloweza kukamatwa mtu bila ya hati, na anakataa baada ya kutakiwa na afisa wa polisi kutaja jina lake au

makaazi, au anataja jina au makaazi ambayo afisa huyo ana sababu za kuamini kuwa ni uongo, atashughulikiwa chini ya masharti ya kifungu cha 28 cha Sheria hii, ikiwa hakuna sababu za kutosha kuamini kuwa ametenda kosa lolote ataachiwa mara moja.

Mtu aliyekamatwa hatawekwa ndani zaidi ya saa ishirini na nne.

**32.** Mtu aliyekamatwa bila ya hati hatowekwa kizuizini kwa kipindi kirefu zaidi ya kile cha kawaida na kipindi hicho, kama hakuna amri ya hakimu, hakitozidi saa ishirini na nne, ukitoa siku za mapumziko ambazo mahakama haifanyi kazi.

Polisi kutoa taarifa ya ukamataji.

**33.** Wakuu wa vituo vya polisi watatoa taarifa kwa hakimu aliye karibu kuhusu kesi za watu wote waliokamatwa bila ya hati ndani ya mipaka ya kazi ya vituo vyao husika, ama watu hao wamepewa dhamana au hawajapewa dhamana.

Mtu aliyekamatwa kujulishwa sababu za kukamatwa na haki ya kukaa kimya.

**34.-**(1) Afisa wa polisi au mtu mwengine anayemkamata mtu bila ya hati atalazimika mara moja:

(a) kujitambulisha yeye mwenyewe kwa ukamilifu kwa mtu anayetakiwa kukamatwa; na

(b) kumjulisha mtu anayekamatwa taarifa kamili juu ya kosa ambalo kwa kosa hilo anakamatwa;

(2) Afisa wa polisi atamjulisha mtu anayekamatwa kwamba ana haki ya kukaa kimya lakini iwapo ataamua kuzungumza, basi chochote atakachokisema kinaweza kutumiwa dhidi yake mahakamani.

(3) Mtu aliyekamatwa atajulishwa pia haki yake ya kuwa na wakili au rafiki mwengine wakati wa mahojiano.

(4) Iwapo afisa wa polisi anamkamata bila ya hati mtu yeyote asiyekuwa yule anayetuhumiwa kwa kosa lisilo na dhamana, atamjulisha mtu huyo aliyekamatwa kwamba ana haki ya kuachiwa kwa dhamana na kwamba afisa huyo wa polisi, pale inapowezekana, anaweza kusaidia kupatikanwa wadhamini kwa niaba yake.

Wajibu wa kutoa taarifa ya ukamataji.

**35.-**(1) Afisa wa polisi au mtu mwengine anayefanya ukamataji chini ya Sheria hii, atalazimika mara moja kutoa taarifa ya ukamataji huo na sehemu ambayo mtu aliyekamatwa anashikiliwa kwa jamaa zake wowote, marafiki zake au watu wengine wowote kama watakavyotajwa na mtu aliyekamatwa kwa madhumuni ya kuwapa taarifa hiyo.

(2) Kumbukumbu za taarifa kuhusiana na nani aliyepewa taarifa ya kukamatwa kwa mtu huyo zitawekwa katika daftari litakalowekwa katika kituo cha polisi katika utaratibu utakaowekwa kwa ajili hiyo na afisa aliyefanya ukamataji.

(3) Kumbukumbu zitashuhudiwa na kusainiwa na angalau shahidi mmoja, ambaye ni mtu wa familia ya mtu aliyekamatwa au mwanajamii wa sehemu ambayo ukamataji wa mtu huyo umefanyika.

(4) Mahakama itajiridhisha kwamba matakwa ya kifungu kidogo cha (1), (2) na (3) vya kifungu hiki, yametekelezwa kuhusiana na mtu huyo aliyekamatwa.

Mipaka katika kumhoji mtu.

**36.**-(1) Pale ambapo mtu yupo, au amekuwepo, kizuizini kuhusiana na kosa, afisa wa polisi anaweza:

(a) kumuuliza mtu huyo maswali; au

(b) kuchukuwa hatua nyengine za kiupelelezi,

kuhusiana na upelelezi wa kosa hilo, katika kipindi kinachoruhusiwa katika kumuhoji mtu na siyo vyenginevyo.

(2) Masharti ya Sheria hii yanayohusiana na muda unaoruhusiwa kumhoji mtu hayatachukuliwa:

(a) kuhalalisha kumshikilia mtu chini ya kizuizi katika kipindi chochote ambapo kipindi hicho kingekuwa, isipokuwa kwa masharti hayo, kinyume na sheria kumshikilia chini ya kizuizi; au

(b) kuidhinisha uulizwaji wa maswali yoyote au uchukuliwaji wa hatua nyengine za upelelezi kuhusiana na mtu huyo katika kipindi ambapo kipindi hicho kingekuwa, isipokuwa kwa masharti hayo, kinyume na sheria kumshikilia chini ya kizuizi.

(3) Maelezo ya mwanamke ambaye dhidi yake kosa la kubaka, kubaka kwa kikundi, au kujaribu kubaka linadaiwa kuwa limetendwa au limejaribu kutendwa yatarekodiwa, kwa kadiri iwezekanavyo, na afisa wa polisi mwanamke.

Wakati gani mtu asichukuliwe kuwekwa kizuizini.

**37.** Afisa wa polisi hatamuweka kizuizini kuhusiana na kosa lolote mtu ambaye alikuwa awali chini ya kizuizi kuhusiana na kosa hilo:

(a) isipokuwa kama anafanya hivyo kutokana na mambo ambayo yamejulikana na afisa wa polisi msimamizi wa upelelezi wa kosa hilo baada tu ya mtu huyo alipoacha kuwa chini ya kizuizi; na

(b) isipokuwa kama muda wa kutosha umepita tangu mtu huyo alipoacha kuwa chini ya kizuizi.

Muda unaoruhusiwa kwa ajili ya kumhoji mtu.

**38.** Kwa madhumuni ya Sheria hii, muda unaoruhusiwa kwa ajili ya kumuhoji mtu ambaye yupo kizuizini kuhusiana na kosa utakuwa:

(a) kwa kuzingatia aya ya (b) ya kifungu hiki, muda wa msingi unaoruhusiwa kumuhoji mtu, yaani, ni muda wa saa nne kuanzia muda alipowekwa chini ya kizuizi kuhusiana na kosa hilo;

(b) kiwa muda wa msingi unaoruhusiwa kwa ajili ya kumhoji mtu umeongezwa chini ya kifungu cha 39 cha Sheria hii, muda wa msingi utakuwa kama hivyo ulivyoongezwa.

katika kuhesabu muda unaoruhusiwa kwa ajili ya kumuhoji mtu ambaye yupo kizuizini kuhusiana na kosa, muda unaohitajika kuwasiliana na mwanasheria, au kuwasiliana na mtu ambaye mtuhumiwa anataka azungumze naye au awepo wakati wa mahojiano, au muda ambao mtu aliyopo kizuizini anautumia kwa ajili ya kusubiri kuwasili kwa mtu yeyote kati ya waliotajwa awali hautahesabiwa.

Pale ambapo upelelezi chini ya ulinzi hauwezi kukamilika ndani ya saa nne.

**39.**-(1) Pale mtu anapokuwa chini ya ulinzi halali kuhusiana na kosa katika muda wa msingi unaoruhusiwa kwa ajili ya kumhoji mtu, lakini bado hajashitakiwa kwa kosa, na inaonekana kwa afisa wa polisi msimamizi wa upelelezi wa kosa hilo, kwa sababu ya msingi, kwamba ni muhimu kuwa mtu huyo ahojiwe zaidi, anaweza:

(a) kuongeza muda wa kuhoji kwa kipindi kisichozidi saa nane, na atamuarifu mtu anayehusika ipasavyo; au

(b) ama kabla ya kumalizika kwa muda wa awali au muda ule ulioongezwa, kufanya maombi kwa hakimu kwa ajili ya kuongeza zaidi muda huo.

(2) Afisa wa polisi hatalazimika kuongeza bila sababu za msingi au bila ya sababu za maana muda wa msingi unaoruhusiwa kwa ajili ya kumuhoji mtu, lakini mtu yeyote ambaye muda wake wa kuhojiwa umeongezwa kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (1) (a) cha kifungu hiki, anaweza kupeleka maombi ya kudai malipo au fidia dhidi ya uongezwaji wa muda uliofanywa bila ya sababu ya msingi au maana, jukumu la kuthibitisha litakuwa juu yake.

(3) Pale hakimu ambaye maombi yameletwa mbele yake na afisa wa polisi chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, baada ya kumpa mtu huyo, au wakili anayemuwakilisha kwa niaba yake, fursa ya kuwasilisha utetezi kuhusiana na maombi hayo, ameridhika kwamba:

(a) mtu huyo yupo katika kizuizi halali;

(b) upelelezi wa kosa hilo unaofanywa na afisa wa polisi umekuwa ukifanywa na unaendelea kufanywa kwa haraka iwezekanavyo; na

(c) itakuwa ni sahihi, katika mazingira yote kuongeza muda husika,

hakimu anaweza kuongeza muda huo kwa muda huo wa ziada kama atakavyoona inafaa.

Jinsi ya kuwatendea watu walio kizuizini.

**40.**-(1) Mtu yeyote, wakati akiwa kizuizini, atatendewa kwa mujibu wa ubinaadamu pamoja na kuheshimiwa utu wake.

(2) Mtu yeyote, akiwa kizuizini, hatatendewa vitendo vya ukatili, vitendo vilivyo kinyume na ubinadamu au vitendo vya kumdhalilisha.

(3) Pale mtu aliye kizuizini:

(a) anamuomba afisa wa polisi kupatiwa matibabu, ushauri au msaada kuhusiana na ugonjwa au jeraha; au

(b) anaonekana na afisa wa polisi kuwa anahitaji matibabu, ushauri au msaada kuhusiana na ugonjwa au jeraha,

afisa wa polisi atalazimika mara moja kuchukuwa hatua zinazofaa ambazo ni muhimu kuhakikisha kwamba mtu huyo anapatiwa matibabu, ushauri au msaada.

Wajibu maalum wakati wa kuwahoji watoto.

**41.**-(1) Afisa wa polisi msimamizi wa upelelezi wa kosa ambalo kuhusiana na kosa hilo mtoto amewekwa kizuizini atalazimika mara moja, baada ya mtoto kuwekwa kizuizini, kuwezesha mzazi au mlezi wa mtoto huyo kuarifiwa kwamba mtoto wake huyo yupo kizuizini na kuarifiwa kosa ambalo kwa kosa hilo yuko kizuizini.

(2) Utaratibu wa kuwahoji watoto utakuwa kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Watoto kuhusiana na watoto wanaokinzana na sheria.

Kumbukumbu za mahojiano.

**42.**-(1) Afisa yeyote wa polisi ambaye anamuhoji mtu kwa madhumuni ya kujua kama mtu huyo ametenda kosa atawezesha mahojiano hayo kurekodiwa.

(2) Ikiwa mshtakiwa atadai, kumbukumbu za mahojiano hayo chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, zitarekodiwa ama kwa njia ya sauti au kwa njia ya picha za video au kwa chombo chochote cha kielektroniki, kama itakavyokuwa.

Maelezo ya mtuhumiwa.

**43.**-(1) Pale mtu aliye kizuizini anamuarifu afisa wa polisi kuwa anapenda kuandika maelezo, afisa huyo wa polisi atalazimika kumuonya juu ya athari ya maelezo hayo

na iwapo mtu huyo bado anapenda kuandika maelezo, afisa huyo wa polisi atampatia vifaa vya kuandikia kwa ajili ya kuandika maelezo hayo.

(2) Afisa wa polisi atamtaka mtu aliye kizuizini kusaini maelezo hayo, na ikiwa maelezo hayo ni zaidi ya kurasa moja, mtuhumiwa huyo ataamriwa kusaini katika kila ukurasa.

Uwezo wa kuchukua alama za vidole au picha, za watuhumiwa.

**44.** Mkuu wa kituo cha polisi au afisa wa polisi anayepeleleza kosa anaweza kuchukua au kuwezesha kuchukuliwa vipimo au alama za mikono, vidole, nyayo, au vidole vya miguu, au rekodi za sauti au, picha ya, au sampuli za maandishi ya mkono ya mtu ambaye anashitakiwa kwa kosa, ama mtu huyo yupo kwenye kizuizi halali cha polisi au vyenginevyo pale vipimo hivyo, alama, rekodi, picha au sampuli, kama itakavyokuwa inaaminika kwa sababu za msingi kuwa ni muhimu kwa ajili ya utambuzi wa mtu huyo kuhusiana na, au kwa ajili ya kupata ushahidi kuhusu utendaji wa kosa ambalo limepelekea yeye kuwekwa kizuizini au kushtakiwa.

Gwaride la utambuzi.

**45.**-(1) Mkuu wa kituo cha polisi au afisa yeyote wa polisi anayepeleleza kosa anaweza kuendesha gwaride la utambuzi kwa madhumuni ya kuhakikisha kama shahidi anaweza kumtambua mtu anayetuhumiwa kutenda kosa.

(2) Afisa wa polisi atahakikisha kwamba gwaride la utambuzi linaendeshwa katika hali ambayo mtuhumiwa hatoweza kulalamika baadae kuwa halikuendeshwa kwa haki, vyenginevyo thamani ya utambuzi huo kama ushahidi itashuka kwa kiwango kikubwa.

(3) Mkuu wa kituo au afisa yeyote wa polisi anayepeleleza kosa anaweza kumtaka mtu yeyote ambaye ushiriki wake ni muhimu katika upelelezi wa kosa kuhudhuria na kushiriki katika gwaride la utambuzi.

(4) Mtu ambaye anatakiwa chini ya kifungu kidogo cha (3) cha kifungu hiki, kuhudhuria na kushiriki katika gwaride la utambuzi hatokuwa na haki ya kukataa au kupinga kuhudhuria na kushiriki katika gwaride la utambuzi.

(5) Mtu yeyote ambaye bila ya sababu ya msingi, au anakataa bila ya sababu kuhudhuria na kushiriki katika gwaride la utambuzi atakuwa ni mkosa na atapewa adhabu atakapotiwa hatiani kwa kutozwa faini isiyozidi Shilingi Laki Tano au kifungo kwa kipindi kisichozidi miezi sita au adhabu zote mbili faini na kifungo.

Kuwatambua mawakili.

**46.** Wakili aliyesajiliwa na Mahakama Kuu chini ya masharti ya sheria ya mawakili, atakuwa na haki chini ya Sheria hii kumuwakilisha na kumtetea au kumshauri mtu anayetuhumiwa au anayeshitakiwa kwa kosa lolote, na polisi, mamlaka za Chuo cha Mafunzo, hospitali na taasisi nyengine za Serikali zitawajibika kuwapatia mawakili wa utetezi fursa ya kuonana na watuhumiwa na msaada utakaofanikisha kazi yao ya kuwatetea au kuwashauri watuhumiwa waliopo chini ya hifadhi yao au mamlaka yao.

Uchunguzi wa daktari tiba kwa mtuhumiwa kufuatia maombi ya afisa wa polisi.

**47.**-(1) Wakati mtu anakamatwa kwa kutenda kosa lenye hali fulani na inadaiwa kuwa ametenda kosa hilo chini ya mazingira ambayo kuna sababu za msingi kuamini kwamba, uchunguzi wa mwili wake utapelekea kupatikana ushahidi wa kutenda kosa, itakuwa ni halali kwa daktari tiba aliyesajiliwa baada ya kuombwa na afisa wa polisi mwenye cheo si chini ya Msaidizi Mkaguzi, na kwa mtu yeyote anayetenda kwa nia njema kwa maelekezo yake kufanya uchunguzi huo wa mtu aliyekamatwa kama itakavyolazimika ili kuhakikisha ukweli ambao unawezesha kupatikana ushahidi huo, na kutumia nguvu kama itakavyolazimika kwa madhumuni hayo.

(2) Pale ambapo mtu mwanamke anatakiwa achunguzwe chini ya kifungu hiki, uchunguzi utafanywa tu na au chini ya usimamizi wa daktari tiba mwanamke aliyesajiliwa.

Uchunguzi wa muathirika wa jinai au mshtakiwa.

**48.**-(1) Pale ambapo kuna sababu za msingi za kuamini kwamba uchunguzi wa muathirika wa jinai na, au mshtakiwa utawezesha kupatikana ushahidi kuhusu kutenda makosa, daktari tiba aliyesajiliwa atamchunguza muathirika wa jinai na, au mshtakiwa na kutayarisha, bila ya kuchelewa, ripoti ya uchunguzi inayoeleza taarifa zifuatazo:

(a) jina na anuani ya muathirika wa jinai au mshtakiwa na mtu aliyemleta huyo muathirika wa jinai au huyo mshtakiwa;

(b) umri wa muathirika wa jinai na, au mshtakiwa;

(c) alama za jeraha, kama zipo, katika mwili wa muathirika wa jinai au mshtakiwa;

(d) maelezo ya vitu vilivyochukuliwa kutoka katika mwili wa muathirika wa jinai au mshtakiwa;

(e) hali ya jumla ya akili na idhini ya muathirika wa jinai kuhusu kufanyiwa uchunguzi huo;

(f) taarifa nyenginezo muhimu kwa ukamilifu;

(g) sababu za kila hitimisho alilofikia mchunguzi huyo; na

(h) maelezo ya muda halisi wa kuanza na kumalizika kwa uchunguzi huo.

(2) Daktari tiba aliyesajiliwa atapeleka nakala ya taarifa ya uchunguzi kwa afisa mpelelezi, muathirika wa jinai na mtu aliyekamatwa au mtu mwengine yeyote aliyeteuliwa na muathirika wa jinai au mshtakiwa.

### Ukamataji kwa amri ya hakimu

Kosa lililotendwa mbele ya hakimu.

**49.** Pale ambapo kosa linatendwa mbele ya hakimu ndani ya mipaka ya eneo la mamlaka yake anaweza yeye mwenyewe kumkamata au kumuamrisha mtu kumkamata mkosaji, na anaweza hapo, bila ya kuathiri masharti ya Sheria hii kuhusu dhamana, kumpeleka mkosaji kizuizini.

Ukamataji unaofanywa na hakimu.

**50.** Hakimu anaweza wakati wowote kumkamata au kuelekeza kukamatwa mbele yake, ndani ya mipaka ya eneo la mamlaka yake, mtu ambaye hakimu huyo ana mamlaka wakati huo na katika mazingira ambayo anaweza kutoa hati ya kukamatwa.

### Kutoroka na kukamata tena

Kumkamata tena mtu aliyetoroka.

**51.** Ikiwa mtu aliyopo katika kizuizi halali anatoroka au anaokolewa, mtu huyo mwenye dhamana ya kizuizi hicho ambaye kutoka katika kizuizi chake mtu ametoroka au ameokolewa anaweza mara moja kumfuata na kumkamata mtu aliyetoroka katika sehemu yoyote ndani ya Zanzibar.

Kuwafuata wakosaji katika eneo la mamlaka nyengine.

**52.** Afisa wa polisi anaweza, kwa madhumuni ya kutekeleza hati ya ukamataji dhidi ya mtu ambaye yeye ameidhinishwa kumkamata chini ya hati hiyo, kumfuata mtu huyo katika sehemu yoyote ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Matumizi ya masharti ya vifungu vya 14 na 15.

**53.** Masharti ya vifungu vya 14 na 15 vya Sheria hii, yatatumika katika ukamataji chini ya kifungu cha 51 cha Sheria hii, ijapokuwa mtu anayefanya ukamataji huo hafanyi ukamataji huo kwa hati na siyo afisa wa polisi mwenye mamlaka ya kukamata.

Msaada kwa hakimu au afisa wa polisi.

**54.** Mtu analazimika kumsaidia hakimu au afisa wa polisi ambaye hakika anahitaji msaada wake:

(a) katika kumchukua au kuzuia utorokaji wa mtu mwengine yeyote ambaye hakimu huyo au afisa wa polisi ameidhinishwa kumkamata;

(b) katika kuzuia au kudhibiti uvunjaji wa amani, au katika kuzuia madhara yoyote yanayojaribiwa kufanywa katika reli yoyote, barabara ya umma, mifereji, njia za simu au mali ya umma.

## SEHEMU YA NNE
## KUZUIA MAKOSA

### Dhamana kwa ajili ya kutunza amani na kuwa na tabia njema

Dhamana kwa ajili ya kutunza amani au kuwa na tabia njema kwa ujumla.

**55.**-(1) Hakimu mwenye dhamana ya kuendesha mahakama ya chini, baada ya kupata malalamiko ya mtu, anaweza, katika namna itakayoelezwa humu baadaye, kumtaka mtu alete sababu kwa nini asiamrishwe kuweka dhamana, akiwa na wadhamini au bila ya wadhamini, kutunza amani au kuwa na tabia njema kwa kipindi hicho, kisichozidi miaka miwili, kama hakimu huyo anavyoona inafaa.

(2) Mwenendo wa kesi hautoanza chini ya kifungu hiki isipokuwa ama mtu ambaye dhidi yake malalamiko yametolewa yupo ndani ya eneo la mipaka ya mamlaka ya hakimu huyo au pahala ambapo jambo husika limetokea pako ndani ya eneo la mipaka ya mamlaka ya hakimu huyo.

Uwezo wa Hakimu mwengine.

**56.**-(1) Pale hakimu yeyote asiye na mamlaka ya kuendesha kesi chini ya kifungu cha 55 cha Sheria hii, anapewa taarifa kwamba mtu anaelekea kutenda kosa la uvunjifu wa amani au kuvuruga utulivu wa jamii, au kufanya kitendo chochote kiovu ambacho kinaweza kupelekea uvunjifu wa amani au kuvuruga utulivu wa jamii, na kwamba uvunjifu huo wa amani au uvurugaji huo hauwezi kuzuiwa vyenginevyo isipokuwa kwa kumuweka kizuizini mtu huyo, hakimu huyo anaweza, baada ya kurekodi sababu zake, kutoa hati ya kukamatwa kwake, ikiwa mtu huyo bado hayupo kizuizini au hayupo mbele ya mahakama, na atampeleka mtu huyo mbele ya hakimu mwenye dhamana ya kushughulikia kesi hiyo, na nakala ya sababu zake.

(2) Hakimu ambaye mbele yake mtu huyo amepelekwa chini ya kifungu hiki anaweza kwa uwezo wake kumuweka kizuizini mtu huyo hadi kukamilika kwa uchunguzi utakaoelezwa katika Sheria hii baadaye.

Dhamana kwa ajili ya tabia njema kutoka kwa watu wanaosambaza mambo ya uchochezi.

**57.** Wakati wowote hakimu mwenye dhamana ya kuendesha mahakama ya chini akiwa na taarifa kwamba ndani ya eneo la mipaka ya mamlaka yake yupo mtu ambaye, ndani ya mipaka hiyo au nje ya mipaka hiyo, ama kwa mdomo au kwa maandishi au kwa namna nyengine yoyote, anasambaza, au anajaribu kusambaza, au kwa namna nyengine anasaidia usambazaji wa:

(a) jambo lolote la uchochezi, yaani, jambo lolote ambalo uchapishaji wa jambo hilo unaadhibiwa chini ya Sheria ya Usajili wa Mawakala wa Habari, Magazeti na Vitabu; au

(b) jambo lolote linalomuhusu Jaji ambalo ni kashfa ya kimaandishi chini ya Sheria Nam. 5 ya 1988,

hakimu huyo anaweza, katika namna iliyoelezwa katika Sheria hii, kumtaka mtu huyo aoneshe sababu za kwa nini asiamriwe kuweka dhamana akiwa na wadhamini au bila ya wadhamini kwa ajili ya kuwa na tabia njema kwa kipindi hicho, kisichozidi mwaka mmoja, kama hakimu anavyoona inafaa.

Dhamana kwa ajili ya tabia njema kutoka kwa watuhumiwa.

**58.** Wakati wowote hakimu mwenye dhamana ya kuendesha mahakama ya chini akipewa taarifa kwa kiapo kwamba mtu anachukua tahadhari ya kujificha ndani ya eneo la mipaka ya mamlaka ya hakimu huyo, na kwamba kuna sababu ya kuamini kwamba mtu huyo anachukua tahadhari kwa nia ya kutenda kosa, hakimu huyo anaweza, katika namna itakayoelezwa humu baadaye, kumtaka mtu huyo kuonesha sababu kwa nini asiamriwe kuweka dhamana, akiwa na wadhamini, kwa ajili ya tabia yake njema kwa kipindi ambacho, hakitozidi mwaka mmoja, kama hakimu anavyoona inafaa.

Dhamana kwa ajili ya tabia njema kwa watu wenye tabia ya kutenda makosa.

**59.** Wakati wowote hakimu mwenye dhamana ya kuendesha mahakama ya chini akipewa taarifa kwa kiapo kwamba mtu yeyote anachukua tahadhari kujificha ndani ya eneo la mipaka ya mamlaka ya hakimu huyo:

(a) kwa tabia zake mtu huyo ni jambazi, mvunjaji wa nyumba au mwizi;

(b) kwa tabia zake mtu huyo ni mpokeaji wa mali ya wizi, huku akijua kwamba mali hiyo imeibiwa;

(c) kwa tabia zake anawalinda au anawahifadhi wezi, au anasaidia katika ufichaji au uuzaji wa mali ya wizi;

(d) kwa tabia zake anatenda au anajaribu kutenda, au anasaidia au anawezesha utendaji wa kosa lolote linaloadhibiwa chini ya Sehemu ya Ishirini na Nane, Thelathini na Moja au Thelathini na Tatu za Sheria ya Adhabu zinazohusiana na kujisingizia, makosa ya kusababisha madhara kwa mali, na makosa yanayohusiana na sarafu na noti;

(e) kwa tabia zake anatenda au anajaribu kutenda, au anasaidia au anawezesha utendaji wa makosa yanayohusiana na uvunjifu wa amani; au

(f) amehamanika na ni mtu wa hatari ambaye kuwa kwake huru bila ya dhamana ni hatari kwa jamii,

hakimu huyo anaweza, katika namna itakayoelezwa humu baadaye, kumtaka mtu huyo kuonesha sababu kwa nini asiamriwe kuweka dhamana, akiwa na wadhamini, kwa ajili ya tabia yake njema kwa kipindi hicho, kisichozidi miaka mitatu, kama hakimu huyo anavyoona inafaa.

Utoaji wa amri.

**60.** Pale ambapo hakimu anachukua hatua chini ya kifungu cha 55, 57, 58 au 59 cha Sheria hii, anapoona ni lazima kumtaka mtu yeyote aoneshe sababu chini ya kifungu hicho, atatoa amri kwa maandishi inayoeleza:

(a) maudhui ya malalamiko au taarifa iliyopokelewa;

(b) kiwango cha dhamana kitakachowekwa;

(c) muda ambao dhamana hiyo itakuwa na nguvu za kisheria; na

(d) idadi, sifa na aina ya wadhamini, kama wapo, na kama wanahitajika.

Utaratibu kuhusu mtu aliyepo mahakamani.

**61.** Ikiwa mtu ambaye kuhusiana na yeye amri hiyo imetolewa yupo mahakamani, mtu huyo atasomewa amri hiyo au, iwapo mtu huyo atapenda, maudhui ya amri hiyo yatafafanuliwa kwake.

Utaratibu kuhusu mtu asiyekuwepo mahakamani.

**62.-**(1) Iwapo mtu huyo hayupo mahakamani, hakimu atatoa wito kumtaka mtu huyo kufika mahakamani, au, endapo mtu huyo yupo kizuizini, atatoa hati inayomuelekeza afisa ambaye mtu huyo yupo kwenye kizuizi chake kumleta mtu huyo mbele ya mahakama.

(2) Wakati wowote itapoonekana na hakimu huyo kutokana na ripoti ya afisa wa polisi au taarifa nyengine kwamba kuna sababu ya kuogopa kutendeka kwa uvunjifu wa amani, na kwamba uvunjifu huo wa amani hauwezi kuzuiwa vyenginevyo isipokuwa kwa ukamataji wa mara moja wa mtu huyo, hakimu huyo anaweza wakati wowote kutoa hati kwa ajili ya kukamatwa kwake.

(3) Maudhui ya ripoti au taarifa iliyotajwa katika kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki, yatarikodiwa na hakimu huyo.

Nakala ya amri itaambatana na wito au hati.

**63.** Kila wito au hati inayotolewa chini ya kifungu cha 62 cha Sheria hii, itaambatana na nakala ya amri iliyotolewa chini ya kifungu cha 60 cha Sheria hii, na nakala hiyo itapelekwa na afisa anayepeleka wito au anayetekeleza hati kwa mtu anayepelekewa wito huo au mtu anayetakiwa akamatwe chini ya amri hiyo.

Uwezo wa kusamehe uhudhuriaji binafsi.

**64.** Hakimu anaweza, endapo kutakuwa na sababu za msingi, kusamehe uhudhuriaji binafsi wa mtu yeyote aliyeitwa kwa ajili ya kuonesha sababu kwanini mtu huyo asiamriwe kuweka dhamana kwa ajili ya kutunza amani, na anaweza kumruhusu mtu huyo awakilishwe na wakili.

Uchunguzi kuhusu ukweli wa taarifa.

**65.-**(1) Wakati amri chini ya kifungu cha 60 cha Sheria hii, imeshasomwa au imeshaelezwa chini ya kifungu cha 61 cha Sheria hii, kwa mtu aliyepo mahakamani, au wakati mtu yeyote anahudhuria au analetwa mbele ya hakimu kwa kufuata au

kwa kutekeleza wito au hati iliyotolewa chini ya kifungu cha 62 cha Sheria hii, hakimu ataendelea kuchunguza ukweli wa lalamiko hilo au taarifa hiyo ambayo hatua imeshachukuliwa, na kuchukua ushahidi wa ziada kama itavyoonekana inafaa.

(2) Uchunguzi huo utafanywa, kwa karibu itakavyowezekana, kwa namna itakavyoelezwa humu baadae kwa ajili ya usikilizaji wa kesi na uwekaji kumbukumbu za ushahidi katika usikilizaji kesi mbele ya mahakama za chini.

(3) Kwa madhumuni ya kifungu hiki, ukweli kwamba mtu anapaswa kushughulikiwa kwa mujibu wa masharti ya kifungu cha 59 cha Sheria hii, unaweza kuthibitishwa kwa ushahidi wa mwenendo wa kawaida wa mtu huyo unaojulikana na jamii au vyenginevyo.

(4) Endapo watu wawili au zaidi wamehusishwa kwa pamoja katika jambo linalochunguzwa, wanaweza kushughulikiwa kwa uchunguzi wa pamoja au katika uchunguzi tofauti kama hakimu atavyoona inafaa.

Amri ya kuweka dhamana.

**66.**-(1) Endapo baada ya uchunguzi huo imethibitika kwamba ni muhimu kwa ajili ya utunzaji wa amani au kuendeleza tabia njema, kama hali itakavyokuwa, kwamba mtu ambaye uchunguzi umefanywa kwa ajili yake atalazimika kuweka dhamana, akiwa na wadhamini au bila ya wadhamini, hakimu atatoa amri ipasavyo, ikizingatiwa kwamba:

(a) mtu hatoamrishwa kuweka dhamana ya namna tofauti kutoka, au ya kiwango kikubwa kuliko, au kwa ajili ya kipindi kirefu zaidi kuliko, kile kilichoainishwa katika amri iliyotolewa chini ya kifungu cha 60 cha Sheria hii;

(b) kiwango cha kila dhamana kitawekwa kwa kuzingatia ipasavyo mazingira ya kesi husika na hakitokuwa kikubwa sana; na

(c) wakati mtu ambaye uchunguzi umefanywa kwa ajili yake ni mtoto, dhamana itatolewa tu na wadhamini wake.

(2) Mtu aliyeamriwa kuweka dhamana kwa ajili ya kutunza amani au kwa ajili ya kuwa na tabia njema chini ya kifungu hiki anaweza kukata rufaa Mahakama Kuu, na masharti ya Sehemu ya Kumi na Nne ya Sheria hii kuhusiana na rufaa, yatatumika kwa kila rufaa hiyo.

Kuachiwa huru watu ambao dhidi yao taarifa zilitolewa.

**67.** Ikiwa baada ya uchunguzi chini ya kifungu cha 65 cha Sheria hii haikuthibitika kwamba ni lazima kwa ajili ya kutunza amani au kuendeleza tabia njema, kama hali itakavyokuwa, kwamba mtu ambaye uchunguzi umefanywa kwa ajili yake atalazimika kuweka dhamana, hakimu ataingiza katika kumbukumbu kuwa hakuna ulazima huo, na, ikiwa mtu huyo yupo kizuizini kwa madhumuni tu ya uchunguzi huo, atamuachia kutoka kizuizini, au, ikiwa mtu huyo hayupo kizuizini atamuachia huru.

**Mwenendo katika kesi zote baada ya amri ya kuweka dhamana**

Kuanza kwa kipindi ambacho dhamana inatakiwa.

**68.**-(1) Ikiwa mtu ambaye kwake yeye amri ya dhamana imetolewa chini ya kifungu cha 60 na kifungu cha 66 cha Sheria hii, wakati amri hiyo inatolewa, ameadhibiwa au anatumikia adhabu ya kifungo, kipindi ambacho dhamana inatakiwa kitaanza baada ya kumalizika adhabu hiyo.

(2) Katika kesi nyengine kipindi hicho kitaanza toka tarehe ya kutolewa amri hiyo isipokuwa hakimu, kwa sababu ya msingi, ataweka tarehe ya baadae.

Maudhui na ukiukaji wa dhamana.

**69.** Dhamana itakayowekwa na mtu yeyote huyo itamlazimisha yeye kutunza amani au kuwa na tabia njema, kama hali itakavyokuwa, na katika kuwa na tabia njema kutenda au kujaribu kutenda au kusaidia, kuwezesha, kushauri au kuwezesha kutenda kosa linaloadhibiwa kwa kifungo, popote linapoweza kutendwa, itakuwa ni ukiukaji wa dhamana.

Uwezo wa kuwakataa wadhamini.

**70.** Hakimu anaweza kumkataa mdhamini aliyeletwa chini ya kifungu chochote kati ya vifungu vilivyotangulia kwa msingi kwamba, kwa sababu zitakazorekodiwa na hakimu, mdhamini huyo ni mtu asiyefaa.

Utaratibu unaohusiana na mtu kushindwa kuweka dhamana.

**71.**-(1) Ikiwa mtu ameamriwa kuweka dhamana kama ilivyoelezwa hakuweka dhamana hiyo katika tarehe au kabla ya tarehe ambayo kipindi kwa ajili ya dhamana hiyo inayotakiwa kutolewa kitaanza, atalazimika, isipokuwa katika mazingira yaliyotajwa katika kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki, kupelekwa Chuo cha Mafunzo, au, ikiwa tayari yupo Chuo cha Mafunzo, atalazimika kuzuiliwa katika chuo hicho mpaka kipindi hicho kitakapomalizika au mpaka ndani ya kipindi hicho atakapoweka dhamana mahakamani au kwa hakimu aliyetoa amri hiyo inayomtaka kuweka dhamana hiyo.

(2) Pale mtu huyo ameshaamriwa na hakimu kuweka dhamana kwa kipindi kinachozidi mwaka mmoja, hakimu huyo, iwapo mtu huyo hakuweka dhamana hiyo kama ilivyoelezwa, atalazimika kutoa hati inayoelekeza yeye awekwe kizuizini katika Chuo cha Mafunzo ikisubiriwa amri za Mahakama Kuu, na mwenendo wa kesi utapelekwa haraka itakavyowezekana mbele ya mahakama hiyo.

(3) Mahakama Kuu, baada ya kupitia mwenendo huo na kutaka kutoka kwa hakimu taarifa nyengine za ziada au ushahidi ambao inaona unafaa au wa lazima, na baada ya kumpa mtu husika fursa ya kutosha ya kusikilizwa, inaweza kutoa amri hiyo katika kesi hiyo kama inavyoona inafaa.

(4) Kipindi hicho, kama kipo, ambacho mtu yeyote amewekwa kizuizini kwa kushindwa kuweka dhamana hakitozidi miaka mitatu.

(5) Endapo dhamana imepelekwa kwa afisa dhamana wa Chuo Cha Mafunzo, atalipeleka mara moja jambo hilo mahakamani au kwa hakimu ambaye alitoa amri na atalazimika kusubiri amri za mahakama hiyo au hakimu huyo.

Kuachiwa huru mtu aliyefungwa kwa kushindwa kuweka dhamana.

**72.** Wakati wowote hakimu mwenye dhamana ya kuendesha kesi katika mahakama ya chini ana maoni kwamba mtu yeyote aliyefungwa kwa kushindwa kuweka dhamana anaweza kuachiwa huru bila ya madhara kwa jamii, hakimu huyo atatoa mara moja ripoti ya kesi kwa ajili ya kupata amri za Makahama Kuu, na Mahakama Kuu inaweza, kama inaona inafaa, kutoa amri mtu huyo kuachiwa huru.

Uwezo wa Mahakama Kuu kufuta dhamana.

**73.** Mahakama Kuu inaweza wakati wowote, kwa sababu za msingi zitakazorekodiwa kwa maandishi, kufuta dhamana yoyote kwa ajili ya kutunza amani au kuwa na tabia njema iliyowekwa chini ya kifungu chochote kati ya vifungu vilivyotangulia kwa amri ya mahakama yoyote.

Kuondoa jukumu la wadhamini.

**74.**-(1) Mdhamini yeyote aliyeweka dhamana kwa ajili ya mtu mwengine kutunza amani au kuwa na tabia njema anaweza wakati wowote kuomba kwa hakimu mwenye dhamana ya kuendesha mahakama ya chini kufuta dhamana yoyote iliyowekwa chini ya kifungu chochote miongoni mwa vifungu vilivyotangulia ndani ya eneo la mipaka ya mamlaka yake.

(2) Kufuatia maombi yaliyofanywa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, hakimu atatoa wito wake au hati, kama anavyoona inafaa, kumtaka mtu aliyedhaminiwa kufika au kuletwa mbele yake.

(3) Pale mtu **huyo** anapohudhuria au kuletwa mbele ya hakimu, hakimu huyo atafuta dhamana na atamuamrisha mtu huyo kuweka, kwa sehemu ya muda uliobaki wa masharti ya dhamana hiyo, dhamana mpya ya aina ile ile kama ile dhamana ya mwanzo.

(4) Amri hiyo chini ya kifungu kidogo cha (3) cha kifungu hiki, kwa madhumuni ya vifungu vya 69, 70, 71 na 72 vya Sheria hii, itahesabika kuwa ni amri iliyotolewa chini ya kifungu cha 66 cha Sheria hii.

**Hatua za uzuiaji wa Polisi**

Polisi kuzuia kosa analoweza kukamatwa mtu bila ya hati.

**75.** Afisa wa polisi anaweza kuingilia kwa madhumuni ya kuzuia, na kwa kadiri ya uwezo wake wote atazuia, kutendeka kwa kosa lolote analoweza kukamatwa mtu bila ya hati.

Taarifa ya mpango wa kutenda kosa.

**76.** Afisa wa polisi anayepokea taarifa ya mpango wa kutenda kosa lolote analoweza kukamatwa mtu bila ya hati atatoa taarifa hiyo kwa afisa wa polisi ambaye ni mkubwa wake, na kwa afisa mwengine yeyote ambaye jukumu lake ni kuzuia au kutambua kutendeka kwa kosa lolote kama hilo.

Kukamata kwa ajili ya kuzuia kosa.

**77.** Afisa wa polisi anayejua mpango wa kutenda kosa lolote analoweza kukamatwa mtu bila ya hati anaweza kumkata, bila ya amri kutoka kwa hakimu na bila ya hati, mtu anayepanga mpango huo, ikiwa itabainika kwa afisa huyo kwamba utendekaji wa kosa hilo hauwezi kuzuiwa vyenginevyo.

Uzuiaji wa uharibifu wa mali ya umma.

**78.** Afisa wa polisi anaweza, kwa mamlaka yake mwenyewe, kuingilia kwa ajili ya kuzuia uharibifu wowote unaojaribiwa kufanywa mbele yake kwa mali yoyote ya umma, inayoweza kuhamishika au isiyohamishika, au kuondosha au kuharibu alama yoyote ya umma au boya au alama nyengine yoyote inayotumika kwa ajili ya usafiri.

## SEHEMU YA TANO
## MASHARTI YANAYOHUSIANA NA UPELELEZI WOTE WA JINAI

### Pahala pa uchunguzi au usikilizaji kesi

Upelelezi wa kosa.

**79.**-(1) Upelelezi wa kosa lililotendwa chini ya sheria yoyote utafanywa na yeyote ya wafuatao:

(a) polisi kama sheria haijataja mpelelezi mahsusi wa kosa hilo;

(b) afisa yoyote aliyeidhinishwa chini ya sheria yoyote kufanya upelelezi kuhusiana na kosa maalum;

(c) mtu yeyote aliyeidhinishwa na Mkurugenzi wa Mashtaka; au

(d) mtu aliyeidhinishwa na hakimu.

(2) Ushahidi uliokusanywa katika upelelezi wowote uliotajwa chini ya aya ya (a) mpaka (d) katika kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, utaweza kutumika katika usikilizaji kesi yoyote mbele ya Mahakama yoyote.

Mamlaka ya jumla ya mahakama za Zanzibar.

**80.** Mahakama ina mamlaka ya kuwezesha kuletwa mbele yake mtu yeyote ambaye yupo katika eneo la mipaka ya mamlaka yake na anashitakiwa kwa kosa lililotendwa ndani ya Zanzibar au kosa ambalo kwa mujibu wa sheria linaweza kushughulikiwa kama kwamba limetendwa ndani ya Zanzibar, na kumshughulikia mshitakiwa kwa mujibu wa mamlaka yake.

Mshitakiwa kupelekwa katika Wilaya ambapo kosa limetendwa.

**81.** Pale ambapo mtu anashitakiwa kwa kutenda kosa ndani ya Zanzibar ametoroka au ameondoka kutoka katika Wilaya ambayo kosa limetendwa na akapatikana ndani ya Wilaya nyengine, Mahakama ambayo ndani ya mipaka ya mamlaka yake mtu huyo amepatikana itawezesha mtu huyo kuletwa mbele yake, isipokuwa kama imeidhinishwa kuendelea na kesi hiyo, itampeleka mtu huyo katika kizuizi cha Mahakama ambayo ndani ya mipaka ya mamlaka yake kosa hilo limedaiwa kutendwa, au kumtaka mtu huyo kuweka dhamana kwa ajili ya kujisalimisha kwake katika mahakama hiyo kujibu shtaka na kushughulikiwa kwa mujibu wa sheria.

Kuondoshwa mshtakiwa chini ya hati.

**82.**-(1) Pale ambapo mtu anatakiwa kupelekwa kizuizini kwa mujibu wa kifungu cha 81 cha Sheria hii, hati itatolewa na mahakama ambayo ndani ya mipaka ya mamlaka yake mtu huyo amepatikana, na hati hiyo itakuwa ni mamlaka tosha kwa mtu yeyote ambaye hati hiyo imeelekezwa kwake kumpokea na kumuweka kizuizini mtu aliyetajwa katika hati hiyo na kumchukua na kumpeleka mtu huyo mahakamani ndani ya Wilaya ambayo kosa lilitendwa au kosa linaweza kuchunguzwa au kusikilizwa.

(2) Mtu ambaye hati imeelekezwa kwake atatekeleza hati hiyo kwa mujibu wa masharti ya hati hiyo bila ya kuchelewa.

Mamlaka ya Mahakama Kuu.

**83.** Mahakama Kuu inaweza kuchunguza na kusikiliza kosa lolote kwa mujibu wa mipaka yake katika pahala popote ambapo ina mamlaka ya kufanya vikao.

Pahala na tarehe ya vikao vya Mahakama Kuu.

**84.**-(1) Kwa ajili ya utekelezaji wa mamlaka yake ya jinai, Mahakama Kuu itafanya vikao katika pahala na katika siku kama Jaji Mkuu atakavyoelekeza.

(2) Mrajis wa Mahakama Kuu kwa kawaida atatoa notisi kabla vikao hivyo vyote.

Pahala pa kawaida pa uchunguzi na usikilizaji kesi.

**85.** Kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 83 cha Sheria hii na mamlaka ya kuhamisha kesi yaliyowekwa na vifungu vya 95 na 97 vya Sheria hii, kosa kwa kawaida litachunguzwa au kusikilizwa na mahakama ndani ya eneo la mipaka ya mamlaka yake lilipotendwa.

Usikilizaji wa kesi katika pahala kosa lilipotendwa au athari zilipojitokeza.

**86.** Wakati mtu anashtakiwa kwa kutenda kosa lolote kwa sababu ya kitu chochote ambacho kilichotendwa au kwa athari yoyote iliyojitokeza, kosa hilo linaweza kuchunguzwa au kusikilizwa na Mahakama ambayo ndani ya eneo la mipaka ya mamlaka yake kitu chochote hicho kimetendwa au athari yoyote ile imejitokeza.

Usikilizaji wa kesi pale kosa moja limeungana na kosa jengine.

**87.** Wakati ambapo kitendo ni kosa kwa sababu ya uhusiano wake na kitendo chengine chochote ambacho nacho pia ni kosa au ambacho kingekuwa ni kosa kama mtendaji angeweza kutenda kosa, shtaka la kosa lililotajwa mwanzo linaweza kuchunguzwa au kusikilizwa na mahakama ambayo ndani ya eneo la mipaka ya mamlaka yake tendo lolote kati ya hayo limetendwa.

Usikilizaji wa kesi pale sehemu iliyotendwa kosa haijulikani.

**88.** Pale ambapo haijulikani katika eneo lipi miongoni mwa maeneo kosa limetendwa; au pale sehemu ya kosa imetendwa katika eneo moja na sehemu ya kosa imetendwa katika sehemu nyengine au pale kosa ni la kuendelea, na linaendelea kutendwa katika sehemu zaidi ya moja; au pale kosa linapojumuisha matendo mbali mbali yaliyotendwa katika maeneo tofauti, linaweza kuchunguzwa au kusikilizwa na Mahakama yenye mamlaka katika yoyote miongoni mwa maeneo hayo.

Usikilizaji wa kesi pale kosa limetendwa kwenye safari.

**89.** Kosa lililotendwa wakati mkosaji yupo katika safari ya nchi kavu au safari ya majini linaweza kuchunguzwa au kusikilizwa na Mahakama kupitia au ndani ya eneo la mipaka ya mamlaka ya Mahakama ambayo mkosaji au mtu aliyetendewa kosa amepita au kitu kinachohusiana na kosa lililotendwa kimepita wakati wa safari ya nchi kavu au safari ya majini.

Kosa lililotendwa kwa barua.

**90.** Kosa ambalo linajumuisha kuhadaa linaweza, ikiwa udanganyifu umefanywa kwa njia ya barua au ujumbe wa simu, kuchunguzwa au kusikilizwa na mahakama yoyote ambayo ndani ya eneo la mipaka ya mamlaka yake barua hizo au ujumbe huo umetumwa au kupokelewa; na kosa lolote la kuhadaa na kosa la kushawishi bila ya uaminifu kupeleka mali linaweza kuchunguzwa au kusikilizwa na Mahakama ambayo ndani ya eneo la mipaka ya mamlaka yake mali ilipelekwa na mtu aliyehadaiwa au ilipokelewa na mshtakiwa.

Pahala pa kusikiliza makosa yanayo-sikilizwa pamoja.

**91.** Endapo:

(a) makosa yaliyotendwa na mtu yeyote ni yale ambayo kwamba mtu anaweza kushtakiwa kwa pamoja, na kusikilizwa katika shauri moja, kila moja ya kosa hilo kwa mujibu wa masharti ya kifungu cha 165 cha sheria hii; au

(b) kosa au makosa yametendwa na watu mbali mbali ni yale ambayo kwamba yanaweza kushtakiwa na kusikilizwa kwa pamoja kwa mujibu wa masharti ya kifungu cha 166 cha Sheria hii,

makosa hayo yanaweza kuchunguzwa au kusikilizwa na Mahakama yoyote yenye mamlaka ya kuchunguza au kusikiliza kosa lolote miongoni mwa makosa hayo.

Mahakama Kuu kuamua katika mazingira ya shaka.

**92.**-(1) Wakati wowote inapojitokeza shaka yoyote kuhusu Mahakama ambayo kosa linaweza kuchunguzwa au kusikilizwa, mahakama yoyote inayokuwa na shaka hiyo

inaweza, katika uwezo wake, kutoa taarifa ya mazingira hayo kwa Mahakama Kuu, na Mahakama Kuu itaamua katika mahakama ipi kosa hilo litachunguzwa au kusikilizwa.

(2) Uamuzi wowote huo wa Mahakama Kuu utakuwa ni wa mwisho, isipokuwa kwamba mshtakiwa ataruhusika kuonesha kwamba hakuna mahakama katika Zanzibar yenye mamlaka katika kesi hiyo.

Mahakama zitakuwa za wazi.

**93.**-(1) Pahala ambapo mahakama ya jinai itafanya shughuli zake kwa madhumuni ya kuchunguza au kusikiliza kosa lolote itachukuliwa kuwa ni mahakama ya wazi katika mahakama hiyo watu kwa ujumla wanaruhusiwa, kwa kiasi ambacho mahakama hiyo itakuwa na uwezo wa kuwaingiza watu hao bila ya shida.

(2) Jaji au hakimu anayeongoza mahakama anaweza, ikiwa anaona inafaa, kuamuru katika hatua yoyote ya uchunguzi au usikilizaji wa kesi yoyote mahsusi kwamba watu kwa ujumla au mtu yeyote mahsusi asiruhusiwe au asiwepo au asibakie katika chumba au jengo linalotumiwa na mahakama.

(3) Bila ya kujali kitu chochote kilichomo katika kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, uchunguzi na usikilizaji wa kesi ya kubaka, kubaka kwa kikundi, kujaribu kubaka, kunajisi watoto wa kiume, au kunajisi watu wenye ulemavu wa akili utaendeshwa katika faragha.

(4) Jaji au hakimu anayeongoza mahakama anaweza, ikiwa anaona inafaa, au kwa maombi yatakayofanywa na yeyote kati ya wahusika wa kesi, kumruhusu mtu yeyote mahsusi kuhudhuria, au kuwepo au kubakia katika chumba au jengo linalotumiwa na mahakama.

(5) Mtu yeyote hatotoa nakala au hatochapisha jambo lolote la mwenendo wowote wa shauri lililosikilizwa chini ya kifungu kidogo cha (3) cha kifungu hiki, isipokuwa kwa ruhusa iliyotolewa awali na mahakama.

**Uhamisho wa kesi**

Uhamisho wa kesi ikiwa kosa limetendwa nje ya eneo la mamlaka.

**94.**-(1) Iwapo baada ya kusikiliza malalamiko yoyote itaonekana kwamba chanzo cha malalamiko kimetokea nje ya eneo la mipaka ya mamlaka ya mahakama ambayo malalamiko hayo yamepelekwa mbele yake, mahakama hiyo, baada ya kuridhika kwamba haina mamlaka, itaelekeza kesi hiyo kuhamishwa kwenda kwenye mahakama yenye mamalaka ambapo chanzo cha malalamiko kimetokea.

(2) Iwapo mtuhumiwa yupo kizuizini na mahakama inayoelekeza uhamisho huo inaona inafaa kwamba kizuizi hicho kiendelee, au ikiwa hayupo kizuizini, kwamba awekwe katika kizuizi hicho, mahakama itaelekeza mkosaji apelekwe na afisa wa polisi mbele ya mahakama yenye mamlaka ambapo chanzo au malalamiko yalitokea, na itatoa

hati kwa ajili ya madhumuni hayo kwa afisa huyo, na itampa mtu huyo malalamiko na ahadi ya dhamana, kama ipo, iliyochukuliwa na Mahakama hiyo, ili ipelekwe kwenye mahakama ambayo mbele yake mtuhumiwa atapelekwa na malalamiko hayo na ahadi hiyo ya dhamana, kama ipo, itachukuliwa kwa madhumuni yote na malengo kama kwamba yamechukuliwa na Mahakama hiyo iliyotajwa mwisho atakayopelekwa mtu huyo.

(3) Iwapo mtuhumiwa hayupo kizuizini au hakuwekwa kwenye hifadhi kama ilivyoelezwa awali, Mahakama itamuarifu mtu huyo kwamba imeshaelekeza uhamisho wa kesi hiyo kama ilivyoelezwa, na baada ya hapo masharti ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki, yanayohusiana na uhamishaji na uhalali wa nyaraka katika kesi hiyo yatatumika.

Uhamishaji wa kesi baina ya mahakimu.

**95.** Hakimu mwenye dhamana anayeendesha Mahakama ya chini anaweza:

(a) kuhamisha kesi yoyote ambayo ameitambua kwa ajili ya uchunguzi au usikilizaji kwa hakimu yeyote anayeendesha Mahakama ya chini mwenye mamlaka ya kuchunguza au kusikiliza kesi hiyo ndani ya eneo la mipaka ya mamlaka ya Mahakama hiyo ya chini; na

(b) kuelekeza au kuiwezesha Mahakama yoyote ya chini ambayo imeshaitambua kesi yoyote, na ama ushahidi umeshachukuliwa katika kesi hiyo au haujachukuliwa, kuhamisha kesi hiyo kwa uchunguzi au usikilizaji kwake yeye mwenyewe au kwa mahakama nyengine yoyote iliyoainishwa ndani ya eneo la mipaka ya mamlaka ya Mahakama yake ambayo ina mamlaka ya kumsikiliza mtuhumiwa au kumpeleka kwa ajili ya kusikilizwa, na Mahakama hiyo inaweza kuimaliza kesi hiyo ipasavyo.

Utaratibu kuhusu uhamishaji wa kesi unaofanywa na hakimu.

**96.** Iwapo wakati wa uchunguzi au usikilizaji wa kesi mbele ya hakimu ushahidi unaonesha dhana ya kuwa kesi hiyo inapaswa kusikizwa au kupelekwa kwa ajili ya kusikilizwa na hakimu mwengine, atasimamisha mwenendo wa kesi na ataipeleka kesi hiyo pamoja na muhtasari wa taarifa kwa hakimu mwenye dhamana ya kuendesha mahakama ya chini, mwenye mamlaka ya kuelekeza uhamishaji wa kesi chini ya kifungu cha 95 cha Sheria hii.

Mahakama Kuu kubadilisha pahala pa kusikiliza kesi

**97.** Wakati wowote itakapoonekana na Mahakama Kuu:

(a) kwamba uchunguzi au usikilizaji wa kesi kwa haki hautakuwepo katika mahakama yoyote ya jinai ya chini yake;

(b) kwamba suala fulani la kisheria lenye ugumu usio wa kawaida linaweza kujitokeza;

(c) kwamba mazingira ya pahala ambapo katika pahala hapo au karibu na pahala hapo kosa lolote lilitendwa patahitajika kwa ajili ya uchunguzi wa kutosheleza au usikilizaji wa kosa hilo;

(d) kwamba amri chini ya kifungu hiki itakuwa ni kwa manufaa ya wahusika wa kesi au mashahidi; au

(e) kwamba amri hiyo ni kwa kuharakisha utendaji wa haki au inahitajika kwa sharti lolote la Sheria hii; inaweza kuamuru:

(i) kosa lolote lichunguzwe au lisikilizwe na mahakama yoyote isiyo na mamlaka chini ya vifungu vilivyotangulia vya Sehemu hii lakini kwa namna nyengine ina mamlaka ya kuchunguza au kusikiliza kosa hilo;

(ii) kesi yoyote mahsusi ya jinai au aina ya kesi ihamishwe kutoka kwenye mahakama ya jinai ya chini ya mamlaka yake kwenda kwenye mahakama nyengine yoyote ya jinai yenye mamlaka sawa au yenye mamlaka makubwa zaidi; au

(iii) mtuhumiwa apelekwe mbele yake kwa ajili ya kusikilizwa.

Utaratibu wa kuwezesha kutumika mamlaka ya Mahakama Kuu chini ya kifungu cha 97.

**98.**-(1) Mahakama Kuu inaweza kuchukua hatua kutokana na taarifa ya mahakama ya chini au kwa maombi ya muhusika mwenye maslahi katika kesi au kwa maamuzi ya mahakama yenyewe.

(2) Utekelezaji wa mamlaka yaliyotolewa chini ya kifungu cha 97 cha Sheria hii, utafanywa kwa njia ya maombi ambayo yataungwa mkono na hati ya kiapo, isipokuwa tu pale muombaji ni Mkurugenzi wa Mashtaka.

(3) Mtuhumiwa anayefanya maombi hayo atatoa kwa Mkurugenzi wa Mashtaka taarifa ya maandishi kuhusu ombi hilo, pamoja na nakala ya sababu ya kwa nini ombi hilo limefanywa; na hakuna amri itakayotolewa kuhusu misingi ya ombi hilo isipokuwa angalau saa ishirini na nne ziwe zimeshapita baina ya kutolewa kwa taarifa hiyo na kusikilizwa kwa ombi hilo.

(4) Endapo mtuhumiwa amefanya ombi hilo, Mahakama Kuu inaweza kumuelekeza mtu huyo kuweka dhamana, akiwa na wadhamini au bila ya wadhamini, kwa sharti kwamba, akitiwa hatiani, atalipa gharama za mwendesha mashtaka.

## Udhibiti wa Mkurugenzi wa Mashtaka katika Mwenendo wa Mashauri ya Jinai

Mkurugenzi wa Mashtaka.

**99.**-(1) Kutakuwa na Mkurugenzi wa Mashtaka ambaye atakuwa ni afisa wa umma katika Serikali ambaye uteuzi na mamlaka yake yatakuwa kama yalivyoelezwa katika Katiba.

(2) Mkurugenzi wa Mashtaka amepewa haki za uendeshaji wa mashtaka yote ya jinai na makosa yote yaliyotendwa ndani ya Zanzibar na pale inapofaa, nje ya Zanzibar.

(3) Mkurugenzi wa Mashtaka anaweza kuchukua kesi yoyote ya jinai katika hatua yoyote ya mwenendo na baadae kesi hiyo itakuwa chini ya udhibiti wa Mkurugenzi wa Mashtaka kama kwamba alikuwa mlalamikaji au mwendesha mashtaka halisi.

Jina la kesi za Jinai.

**100.**-(1) Kesi yoyote ya jinai na kila rufaa ya jinai itakuwa kwa jina la Mkurugenzi wa Mashtaka dhidi ya mshtakiwa au watu au mpinga rufaa kama hali itakavyokuwa.

(2) Endapo mwendesha mashtaka ni mtu binafsi, jina lake pia litaonekana katika jina la mwenendo wa kesi kama mwendesha mashtaka.

Hati ya kufuta mashtaka.

**101.**-(1) Katika kesi yoyote ya jinai ama iliyofunguliwa na Mkurugenzi wa Mashtaka au afisa mwengine yeyote au mtu na katika hatua yoyote ya kesi hiyo kabla ya kutolewa hukumu, Mkurugenzi wa Mashtaka anaweza kupeleka hati ya kufuta kesi, ama kwa kueleza mahakamani au kwa kuiarifu mahakama kwa maandishi kwamba Mkurugenzi wa Mashtaka anakusudia kwamba mwenendo wa shauri usiendelee, na hapo mshtakiwa ataachiwa mara moja kuhusiana na shtaka hilo ambalo kwa kosa hilo hati ya kufuta mashtaka imepelekwa, na ikiwa alishapelekwa Chuo cha Mafunzo atatolewa, au ikiwa yupo katika ahadi ya dhamana basi ahadi hiyo itafutwa; lakini kuachiwa huko kwa mshtakiwa hakutakuwa kizuizi kwa mashtaka yoyote ya baadaye dhidi yake kuhusu tuhuma hizo hizo.

(2) Ikiwa mshtakiwa hayupo mbele ya mahakama wakati hati hiyo ya kufuta mashtaka inawasilishwa, mrajis au karani wa mahakama hiyo atawezesha mara moja kutolewa taarifa ya maandishi kuhusu hati hiyo ya kufuta kesi kupelekwa kwa muangalizi wa Chuo cha Mafunzo ambacho mshtakiwa anazuiliwa, na pia, kwa mshtakiwa na wadhamini wake endapo alikuwa amepewa dhamana.

## Uendeshaji wa mashtaka

Uwezo wa waendesha mashtaka wa Serikali.

**102.** Mwendesha mashtaka wa Serikali anaweza kwenda na kuongea bila idhini yoyote ya maandishi mbele ya mahakama yoyote ambayo katika mahakama hiyo kesi yoyote anayoisimamia ipo katika uchunguzi, kusikilizwa au rufaa; na ikiwa mtu yeyote binafsi amemuajiri wakili kwa ajili ya kuendesha mashtaka katika kesi hiyo yoyote

mwendesha mashtaka wa Serikali anaweza kuendesha mashtaka, na wakili huyo aliyeajiriwa na ataendesha mashtaka kwa kufuata maelekezo ya wakili huyo wa Serikali.

Uondoshaji wa kesi katika mahakama za chini.

**103.** Katika usikilizaji wa kesi yoyote mbele ya mahakama ya chini mwendesha mashtaka wa Serikali yeyote anaweza, kwa idhini ya mahakama au kwa maelekezo ya Mkurugenzi wa Mashtaka, wakati wowote kabla ya hukumu kusomwa, kuondoa kesi kutoka katika mashtaka ya mtu yeyote; na kutokana na kuiondoa huko:

(a) iwapo uondoshwaji umefanywa kabla mshtakiwa hajaitwa kuwasilisha utetezi wake, ataachiwa huru, lakini kuachiwa huko huru kwa mshtakiwa hakutokuwa ni kuzuizi kwa mashtaka ya baadaye kuhusiana na tuhuma hizo hizo;

(b) iwapo uondoshwaji umefanywa baada ya mshtakiwa kuitwa kuwasilisha utetezi wake, ataachiwa huru na hana hatia.

## SEHEMU YA SITA
## UFUNGUAJI WA KESI

### Kuwasilisha malalamiko

Malalamiko na hati rasmi ya shtaka.

**104.**-(1) Kesi inaweza kufunguliwa ama kwa kuwasilisha malalamiko au kwa kumleta mbele ya hakimu mtu aliyekamatwa bila ya hati.

(2) Mtu yeyote anayeamini kwa sababu ya msingi na ya kuaminika kwamba kosa limetendwa na mtu yeyote anaweza kuwasilisha malalamiko kuhusu kosa hilo kwa hakimu mwenye mamlaka.

(3) Malalamiko yanaweza kuwasilishwa kwa mdomo au kwa maandishi, lakini, ikiwa yamewasilishwa kwa mdomo, yatatakiwa kuandikwa na hakimu, na, katika hali yoyote, yatasainiwa na mlalamikaji na hakimu huyo.

(4) Hakimu, baada ya kupokea malalamiko yoyote hayo, atatayarisha au atawezesha kutayarishwa na atasaini hati rasmi ya shtaka inayojumuisha maelezo ya kosa au makosa ambapo kosa au makosa hayo mtuhumiwa anashtakiwa.

(5) Kwa kuzingatia kifungu kidogo cha (4) cha kifungu hiki, hakimu anaweza kumtaka mwendesha mashtaka wa Serikali kuendesha kesi hiyo dhidi ya mshtakiwa au kwa sababu zitakazorekodiwa kwa maandishi, na bila ya kuathiri uwezo wa Mkurugenzi wa Mashtaka chini ya kifungu cha 56A (3) (b) na (c) cha Katiba ya Zanzibar, anaweza kumruhusu mlalamikaji au wakili wake aendeshe kesi hiyo dhidi ya mshtakiwa.

(6) Wakati mshtakiwa ambaye amekamatwa bila ya hati ameletwa mbele ya hakimu, hati rasmi ya shtaka, ikijumuisha maelezo ya kosa au makosa ambapo kosa

au makosa hayo mtuhumiwa anashtakiwa, itasainiwa na itawasilishwa na mwendesha mashtaka wa Serikali anayeleta shtaka.

Utoaji wa wito au hati.

**105.**-(1) Baada ya kupokea malalamiko na baada ya kusaini hati ya shtaka kwa mujibu wa masharti ya kifungu cha 104 cha Sheria hii, hakimu anaweza kwa uwezo wake kutoa ama wito au hati kumtaka mshtakiwa kuhudhuria mbele ya mahakama ya chini yenye mamlaka ya kuchunguza au kusikiliza kosa linalotuhumiwa kwamba limetendwa.

(2) Hati haitatolewa kwa mara ya kwanza isipokuwa malalamiko yawe yamefanywa kwa kiapo ama na mlalamikaji au shahidi au mashahidi.

(3) Uhalali wa mwenendo wa shauri uliofanywa kwa mujibu wa malalamiko au shtaka hautoathiriwa ama na kasoro yoyote kwenye malalamiko au kwenye shtaka au kwa ukweli kwamba wito au hati ilitolewa bila ya malalamiko au shtaka.

(4) Wito wowote au hati inaweza kutolewa na kutekelezwa baina ya saa za kuchomoza jua na kuzama kwa jua katika siku yoyote ya wiki ikijumuisha siku ya mapumziko, lakini mahakama inaweza kwa hati, kumuidhinisha afisa wa polisi au mtu mwengine ambaye wito au hati hiyo imepelekwa kwake kwa ajili ya kuitekeleza saa yoyote.

Kuondosha malalamiko.

**106.** Ikiwa, baada ya kuyatafakari maelezo ya kiapo, kama yapo, ya mlalamikaji na au ya mashahidi na matokeo ya uchunguzi au upelelezi, kama yapo, hakimu anaona kwamba hakuna sababu ya msingi kwa ajili ya kuendelea, hakimu atayaondosha malalamiko, na katika kila kesi kama hiyo hakimu kwa ufupi atarekodi sababu zake za kufanya hivyo.

## SEHEMU YA SABA
## HATI ZA KUWALAZIMISHA WASHTAKIWA KUFIKA MAHAKAMANI

### Wito

Aina na maudhui ya wito.

**107.**-(1) Wito unaotolewa na mahakama chini ya Sheria hii utakuwa kwa maandishi, katika nakala mbili, utasainiwa na kuwekwa muhuri na hakimu anayeongoza mahakama hiyo au afisa mwengine kama ambavyo Mahakama Kuu mara kwa mara, kwa kupitia kanuni, itaelekeza.

(2) Wito utaelekezwa kwa mtu anayeitwa na utamtaka yeye kufika katika wakati na pahala patakapoteuliwa mbele ya mahakama yenye mamlaka ya kuchunguza na kushughulikia lalamiko au shtaka hilo.

(3) Wito utaeleza kwa ufupi kosa ambalo mtu ambaye dhidi yake wito umetolewa anashtakiwa nalo na maelezo ya kosa hilo.

Uwasilishaji wa wito.

**108.-**(1) Wito utawasilishwa na afisa wa polisi, afisa wa mahakama iliyotoa wito huo, au na mtu mwengine huyo kama mahakama itakavyoelekeza na, ikiwa itawezekana, utawasilishwa kwa mtu mwenyewe binafsi anayeitwa kwa kuupeleka au kumpatia yeye moja ya nakala za wito.

(2) Mtu ambaye amepelekewa wito huo atawajibika, akitakiwa kufanya hivyo na afisa aliyewasilisha wito huo, kusaini upokeaji wa wito huo sehemu ya nyuma ya nakala nyengine.

Uwasilishaji wa wito pale mtu anayeitwa hawezi kupatikana.

**109.** Pale mtu anayeitwa, kwa kutumia jitihada muafaka, hawezi kupatikana, wito unaweza kuwasilishwa kwa kuacha nakala moja kwa ajili yake kwa mtu mzima wa familia yake au kwa mfanyakazi wake anayeishi naye au kwa muajiri wake au kwa Sheha; na mtu anayeachiwa wito huo atawajibika, akitakiwa kufanya hivyo na afisa aliyewasilisha wito huo, kusaini upokeaji wa wito huo sehemu ya nyuma ya nakala nyengine.

Utaratibu pale wito hauwezi kuwasilishwa kama ilivyoelezwa kabla.

**110.** Iwapo uwasilishaji wito kwa namna iliyoelezwa na vifungu vya 108 na 109 vya Sheria hii, hauwezi kutekelezwa kwa kutumia juhudi muafaka, afisa anayewasilisha wito atabandika moja ya nakala za wito katika sehemu yoyote ya wazi ya nyumba au makaazi ambayo mtu anayeitwa kwa kawaida anaishi, na baada ya hapo wito huo utachukuliwa kuwa umewasilishwa ipasavyo.

Uwasilishaji wito kwa mtumishi wa Serikali.

**111.** Endapo mtu aliyeitwa yupo kwenye utumishi wa Idara yoyote ya Serikali, mahakama inayotoa wito italazimika kikawaida kuupeleka wito huo katika nakala mbili kwa mkuu wa Idara ambayo mtu huyo ameajiriwa, na mkuu huyo baadaye atawezesha wito huo kuwasilishwa kwa namna iliyoelezwa na kifungu cha 108 cha Sheria hii na ataurejesha wito huo mahakamani chini ya saini yake ukiwa pamoja na uthibitisho unaotakiwa na kifungu hicho, saini hiyo itakuwa ni ushahidi wa uwasilishaji wa wito huo.

Uwasilishaji wito kwenye Kampuni.

**112.-**(1) Uwasilishaji wito kwenye kampuni iliyosajiliwa au taasisi nyengine inayojitegemea unaweza kufanywa kwa kuwasilisha wito huo kwa katibu, meneja wa kampuni husika au afisa mwengine mkuu wa kampuni hiyo katika ofisi iliyosajiliwa ya kampuni hiyo au taasisi hiyo inayojitegemea au kwa barua iliyosajiliwa iliyopelekwa kwa afisa mtendaji mkuu wa kampuni ndani ya Zanzibar.

(2) Katika uwasilishaji kwa njia ya barua iliyosajiliwa, uwasilishwaji utachukuliwa kuwa umefanyika pale ambapo barua ingekuwa imefika katika njia ya kawaida ya posta.

Uwasilishaji wito nje ya mipaka ya mamlaka ya mahakama.

**113.** Pale mahakama inapenda kwamba wito iliyoutowa uwasilishwe pahala popote nje ya eneo la mipaka ya mamlaka yake, itapeleka wito huo katika nakala mbili kwa

hakimu ambaye ndani ya eneo la mipaka ya mamlaka yake mtu anayeitwa anaishi au yupo, kwa ajili ya kuwasilishiwa wito huo hapo.

Uthibitisho wa uwasilishaji wito.

**114.**-(1) Endapo afisa ambaye amewasilisha wito hayupo katika usikilizaji wa kesi, na katika kesi yoyote ambapo wito uliotolewa na mahakama umewasilishwa nje ya eneo la mipaka ya mamlaka ya mahakama hiyo, hati ya kiapo inayodaiwa kufanywa mbele ya hakimu kwamba wito huo umeshawasilishwa, na nakala moja ya wito huo inayodaiwa kuthibitishwa kwa namna iliyoelezwa kabla na mtu ambaye wito huo uliwasilishwa au ulipelekwa au kwake yeye wito huo uliachwa, itakubalika katika ushahidi, na maelezo yaliyoelezwa katika hati hiyo ya kiapo yatachukuliwa kuwa ni sahihi isipokuwa na hadi pale itakapothibitishwa vyenginevyo.

(2) Hati ya kiapo iliyotajwa katika kifungu hiki inaweza kuambatanishwa na nakala ya wito na kurudishwa mahakamani.

**Hati ya ukamataji**

Hati ya ukamataji kwa kukataa wito au baada ya kutolewa wito.

**115.**-(1) Mahakama itamwita mshtakiwa kwa njia ya wito.

(2) Ikiwa mshtakiwa hakufika katika muda na pahala palipotajwa ndani ya wito aliopewa, Mahakama inaweza kutoa hati ya kumkamata na kuwezesha yeye kuletwa mbele ya mahakama hiyo.

(3) Bila ya kujali kutolewa kwa wito, hati ya ukamataji inaweza kutolewa wakati wowote kabla au baada ya muda uliotajwa kwenye wito kwa ajili ya kufika mshtakiwa mahakamani.

(4) Hati ya ukamataji haitatolewa chini ya kifungu kidogo cha (2) au (3) cha kifungu hiki, isipokuwa kama malalamiko au shtaka limeletwa kwa njia ya kiapo.

Aina, maudhui na muda wa hati ya ukamataji.

**116.**-(1) Hati ya ukamataji itakuwa chini ya usimamizi wa Jaji au Hakimu anayetoa hati hiyo na itakuwa na muhuri wa Mahakama.

(2) Hati ya ukamataji itaeleza kwa ufupi kosa ambalo mtu ambaye dhidi yake hati hiyo imetolewa anashtakiwa nalo na maelezo ya kosa hilo na itamtaja au vyenginevyo itamuelezea mtu huyo, na itaamuru mtu au watu ambao hati hiyo imeelekezwa kwao kumkamata mtu ambaye dhidi yake hati hiyo imetolewa na kumleta mtu huyo mbele ya mahakama iliyotoa hati hiyo, au mbele ya mahakama nyengine yenye mamlaka katika kesi hiyo kujibu shtaka lililotajwa katika hati hiyo na itaendelea kumshughulikia kwa mujibu wa sheria.

(3) Hati hiyo ya ukamataji itaendelea kuwa na nguvu za kisheria hadi pale itakapotekelezwa au hadi pale itakapositishwa na mahakama ambayo imetoa hati hiyo.

Uwezo wa kuelekeza kutolewa kwa dhamana.

**117.-**(1) Mahakama inayotoa hati kwa ajili ya ukamataji wa mtu kuhusiana na kosa lisilokuwa kosa la kuua kwa makusudi, uhaini, usafirishaji wa dawa za kulevya, unyang'anyi wa kutumia silaha, kukutwa na silaha, kosa linalohusiana na kiwango kikubwa cha dawa za kulevya, kubaka, kosa la kuingilia kinyume na maumbile, kumnajisi mtoto wa kiume, kubaka kwa kikundi au kumuingilia maharimu, inaweza kwa uwezo wake kuelekeza kwa kuthibitisha kwenye hati ya ukamataji kwamba, ikiwa mtu huyo ameweka dhamana kwa wadhamini wenye kuaminika kuwa atahudhuria mahakamani katika muda ulioainishwa na baadae hadi itakavyoelekezwa vyenginevyo na mahakama hiyo, afisa ambaye hati ya ukamataji imeelekezwa kwake atapokea dhamana hiyo na atamuachia mtu huyo kutoka kizuizini.

(2) Uthibitisho huo utaeleza:

(a) idadi ya wadhamini;

(b) kiwango ambacho wadhamini na mtuhumiwa ambaye kwa ajili ya kukamatwa kwake hati ya ukamataji imetolewa watawajibika kuahidi kukilipa; na

(c) muda ambao mtuhumiwa anatakiwa kufika mbele ya mahakama.

(3) Wakati wowote dhamana itakapochukuliwa chini ya kifungu hiki afisa ambaye hati ya ukamataji imeelekezwa kwake ataiwasilisha hati ya ahadi ya dhamana mahakamani.

Hati za ukamataji kwao zitaelekezwa.

**118.-**(1) Hati ya ukamataji inaweza kuelekezwa kwa afisa wa polisi mmoja au zaidi, au kwa afisa mmoja wa polisi au kwa maafisa wengine wote wa polisi wa eneo ambalo mahakama ina mamlaka, au kwa ujumla kwa maafisa wote wa polisi wa eneo hilo, lakini mahakama yoyote iliyotoa hati hiyo inaweza, ikiwa utekelezaji wake wa haraka ni muhimu, na hakuna afisa yoyote wa polisi anaepatikana kwa haraka, kuelekeza hati hiyo kwa mtu mwengine yeyote au watu, na mtu huyo au watu hao wataitekeleza hati hiyo.

(2) Pale hati inaelekezwa kwa maafisa wengi au watu zaidi ya mmoja, inaweza kutekelezwa na wote au na mmoja au zaidi ya mmoja.

Hati za ukamataji zinaweza kuelekezwa kwa mmiliki wa ardhi.

**119.-**(1) Hakimu mwenye dhamana ya kuendesha mahakama ya chini anaweza kuelekeza hati ya ukamataji kwa mmiliki yoyote wa ardhi, mkulima, au meneja wa ardhi ndani ya eneo la mipaka ya mamlaka yake kwa ajili ya kumkamata mtu yeyote aliyetiwa hatiani aliyekimbia, au mtu ambaye ametuhumiwa kwa kosa analoweza kukamatwa mtu bila ya hati na anakwepa kukamatwa.

(2) Mmiliki huyo wa ardhi, mkulima au meneja atathibitisha kwa maandishi upokeaji wa hati hiyo na ataitekeleza ikiwa mtu ambaye hati hiyo imetolewa kwa ajili

yake yumo au anaingia katika ardhi yake au shamba lake au ardhi hiyo ipo chini ya usimamizi wake.

(3) Pale ambapo mtu dhidi yake hati ya ukamataji imetolewa amekamatwa, atakabidhiwa pamoja na hati ya ukamataji kwa afisa wa polisi aliye karibu yake, ambaye atawezesha kupelekwa mbele ya hakimu mwenye mamlaka, isipokuwa kama dhamana itatolewa chini ya kifungu cha 117 cha Sheria hii.

Utekelezaji wa hati ya ukamataji iliyoelekezwa kwa afisa wa polisi.

**120.** Hati ya ukamataji iliyoelekezwa kwa afisa wa polisi inaweza pia kutekelezwa na afisa wa polisi mwengine yeyote ambaye jina lake limeidhinishwa kwenye hati ya ukamataji na afisa wa polisi ambaye hati hiyo imewasilishwa kwake au imeidhinishwa.

Kutoa taarifa ya yaliyomo katika hati za ukamataji.

**121.** Afisa wa polisi au mtu mwengine anayetekeleza hati ya ukamataji atampa taarifa ya yaliyomo kwenye hati hiyo mtu anayetaka kukamatwa, na itakapohitajika kufanya hivyo, atamuonesha mtu huyo hati ya ukamataji.

Mtu aliyekamatwa ataletwa mbele ya mahakama.

**122.** Afisa wa polisi au mtu mwengine anayetekeleza hati ya ukamataji, kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 117 cha Sheria hii kuhusu dhamana, bila ya kuchelewa, atampeleka mtu aliyekamatwa mbele ya Mahakama ambayo yeye mkamataji kisheria anatakiwa kumpeleka mtu huyo.

Pahala ambapo hati ya ukamataji inaweza kutekelezwa.

**123.** Hati ya ukamataji inaweza kutekelezwa pahala popote ndani ya Zanzibar.

Utekelezaji wa hati ya ukamataji nje ya eneo la mipaka ya mamlaka.

**124.**-(1) Pale ambapo hati ya ukamataji inatakiwa kutekelezwa nje ya eneo la mipaka ya mamlaka ya mahakama iliyotoa hati hiyo, mahakama hiyo inaweza, badala ya kuielekeza hati hiyo kwa afisa wa polisi, itaipeleka hati hiyo kwa njia ya posta au vyenginevyo kwa hakimu yeyote aliyepo ndani ya eneo la mipaka ya mamlaka ambayo hati hiyo inatakiwa kutekelezwa.

(2) Hakimu ambaye hati hiyo ya ukamataji ilitumwa kwake atathibitisha kwa kuweka jina lake katika hati hiyo na, kama itakavyowezekana, atawezesha hati hiyo kutekelezwa ndani ya eneo la mipaka ya mamlaka yake katika namna iliyoelezwa kabla.

Utaratibu katika hali ya utekelezaji wa hati ya ukamataji nje ya eneo la mipaka ya mamlaka.

**125.**-(1) Pale ambapo hati ya ukamataji imeelekezwa kwa afisa wa polisi inatakiwa kutekelezwa nje ya eneo la mipaka ya mamlaka ya mahakama iliyotoa hati hiyo, ataichukua kwa ajili ya kuthibitishwa na hakimu ndani ya eneo la mipaka ya mamlaka ambayo inatakiwa kutekelezwa.

(2) Hakimu huyo atathibitisha kwa kuweka jina lake kwenye hati hiyo, na uthibitisho huo utatosheleza kuwa ni ruhusa tosha kwa afisa wa polisi ambaye hati hiyo ya ukamataji imeelekezwa kwake kuitekeleza hati hiyo ndani ya eneo la mipaka hiyo, na maafisa wa polisi wa eneo hilo, itakapohitajika, watamsaidia afisa huyo katika utekelezaji wa hati hiyo ya ukamataji.

(3) Pale ambapo kuna sababu ya kuamini kwamba uchelewaji wa kupatikana uthibitisho wa hakimu ndani ya eneo la mipaka ya mamlaka ambayo hati ya ukamataji inatakiwa kutekelezwa utazuia utekelezaji huo, afisa wa polisi ambaye hati hiyo imeelekezwa kwake anaweza kutekeleza hati hiyo bila ya uthibitisho huo pahala popote nje ya eneo la mipaka ya mamlaka ya mahakama iliyotoa hati hiyo.

Utaratibu wa ukamataji wa mtu nje ya eneo la mamlaka.

**126.**-(1) Wakati hati ya ukamataji inatekelezwa nje ya eneo la mipaka ya mamlaka ya mahakama ambayo ilitoa hati hiyo, mtu aliyekamatwa, isipokuwa pale mahakama iliyotoa hati ya ukamataji ipo ndani ya maili ishirini kutoka sehemu aliyokamatwa, au ipo karibu kuliko hakimu ambaye ndani ya eneo la mipaka ya mamlaka ya hakimu huyo ukamataji umefanyika, au isipokuwa dhamana imechukuliwa chini ya kifungu cha 117 cha Sheria hii, atapelekwa mbele ya hakimu ambaye yupo ndani ya eneo la mipaka ya mamlaka ambayo ukamataji umefanyika.

(2) Hakimu, ikiwa mtu aliyekamatwa ataonekana kuwa ni mtu aliyekusudiwa na mahakama iliyotoa hati hiyo, ataelekeza utolewaji wake kutoka kizuizini ili kupelekwa kwenye mahakama hiyo iliyotoa hati ya ukamataji.

(3) Ikiwa mtu huyo amekamatwa kwa kosa ambalo sio la kuua kwa makusudi, uhaini, usafirishaji dawa za kulevya, unyang'anyi wa kutumia silaha, kupatikana na silaha, kosa linalohusiana na kiwango kikubwa cha dawa za kulevya, kubaka, kuingilia kinyume na maumbile, kunajisi mtoto wa kiume, kubaka kwa kikundi au kuingilia maharimu, na yupo tayari na anataka kuweka dhamana kama hakimu huyo atakavyoridhika au ikiwa maelekezo yameshaidhinishwa chini ya kifungu cha 117 cha Sheria hii, katika hati hiyo ya ukamataji na mtu huyo yupo tayari na anataka kuweka dhamana inayotakiwa na maelekezo hayo, Hakimu huyo atatoa dhamana hiyo, kama itakavyokuwa, na ataiwasilisha hati ya ahadi ya dhamana kwa mahakama ambayo ilitoa hati ya ukamataji.

(4) Hakuna chochote katika kifungu hiki kitakachochukuliwa kumzuia afisa wa polisi kutoa dhamana chini ya kifungu cha 117 cha Sheria hii.

Upungufu katika hati ya ukamataji.

**127.**-(1) Upungufu au kasoro katika maudhui au muundo wa hati ya ukamataji, na tofauti yoyote baina ya hati ya ukamataji na malalamiko ya maandishi au taarifa, au baina ya yoyote kati ya hivyo na ushahidi uliowasilishwa na upande wa mashtaka katika uchunguzi wowote au usikilizaji wa kesi, hautoathiri uhalali wa mwenendo wowote wa shauri au yatakayofuata baada ya usikilizaji wa kesi.

(2) Ikiwa tofatuti yoyote hiyo inaonekana na mahakama kwamba mshtakiwa amedanganywa au amepotoshwa, Mahakama hiyo inaweza, kutokana na maombi ya mshtakiwa, kuakhirisha usikilizaji wa kesi hadi tarehe ya baadae, na kwa wakati huo itamuweka mahabusu mshtakiwa au itampa dhamana.

**Masharti mbalimbali kuhusiana na Hati.**

Uwezo wa kuchukua ahadi ya dhamana kwa ajili ya kufika mahakamani.

**128.** Endapo mtu kwa ajili ya kufika kwake Mahakamani au kukamatwa kwake, hakimu anayeongoza mahakama yoyote mwenye mamlaka ya kutoa wito au hati ya ukamataji yupo katika mahakama hiyo, hakimu huyo anaweza kumtaka mtu huyo kuweka ahadi ya dhamana, akiwa na wadhamini au bila ya wadhamini, kwa ajili ya kufika kwake katika mahakama hiyo.

Ukamataji kwa kukiuka ahadi ya dhamana.

**129.** Wakati mtu ambaye anawajibika kwa ahadi ya dhamana aliyoiweka chini ya Sheria hii kufika mbele ya Mahakama na hakufika, Hakimu anayeongoza mahakama hiyo anaweza kutoa hati inayoelekeza kwamba mtu huyo akamatwe na aletwe mbele yake.

Uwezo wa kuamuru kufika kwa mwanafunzi aliyepo Chuo cha Mafunzo.

**130.**-(1) Endapo mtu kwa ajili ya kufika kwake mahakamani au kukamatwa kwake, mahakama ina mamlaka ya kutoa wito au hati ya ukamataji yupo kizuizini katika Chuo cha Mafunzo chochote kilichopo kwenye eneo la mipaka ya mamlaka ya Mahakama hiyo, Mahakama inaweza kutoa amri kwa afisa dhamana wa Chuo hicho cha Mafunzo kumtaka afisa huyo kumpeleka mwanafunzi huyo katika kizuizi kinachofaa, kwa wakati utakaotajwa katika amri hiyo, mbele ya mahakama hiyo.

(2) Afisa huyo mwenye dhamana, atakapopokea amri hiyo, atatekeleza kwa mujibu wa masharti ya amri hiyo, na atampa hifadhi salama mwanafunzi huyo wakati ambapo hatokuwepo kwenye Chuo cha Mafunzo kwa ajili ya utekelezaji ulioelezwa awali.

Matumizi ya masharti yanayohusu wito na hati za ukamataji.

**131.** Masharti yaliyomo katika Sehemu hii kuhusu wito na hati, na utoaji wake, upelekwaji na utekelezaji, kwa kadiri itakavyokuwa, yatatumika kwa kila wito na kila hati ya ukamataji iliyotolewa chini ya Sheria hii, au katika sheria nyengine yoyote ikiwa masharti hayo hayendi kinyume na masharti ya hizo sheria nyengine.

**Hati za upekuzi**

Wito wa kuwasilisha nyaraka au kitu chengine.

**132.**-(1) Wakati wowote Mkurugenzi wa Mashtaka au mahakama yoyote yenye mamlaka itakapoona kwamba uwasilishaji wa nyaraka yoyote au kitu chengine ni muhimu au unahitajika kwa madhumuni ya upelelezi wowote, uchunguzi, usikilizaji wa kesi, au mwenendo mwengine wa kesi chini ya Sheria hii, Mkurugenzi wa Mashtaka au mahakama hiyo inaweza kutoa amri ya maandishi au wito kwa mtu ambaye katika umiliki wake au mamlaka yake waraka huo au kitu kinaaminika kuwepo, kumtaka mtu

huyo kufika na kuwasilisha waraka au kitu hicho katika wakati na pahala palipotajwa katika wito, au kuwasilisha waraka au kitu hicho kwa afisa wa polisi au afisa mwengine aliyetajwa katika amri ya maandishi au wito.

(2) Mtu anayetakiwa chini ya kifungu hiki kwa ajili tu ya kuwasilisha waraka au kitu chengine atachukuliwa kuwa ametekeleza amri au wito iwapo mtu huyo atawezesha waraka huo au kitu hicho kuwasilishwa badala ya kufika yeye mwenyewe kuwasilisha waraka au kitu hicho.

(3) Hakuna chochote katika kifungu hiki kitakachochukuliwa:

(a) kuathiri masharti ya Sheria ya Ushahidi yanayohusiana na mambo ya Serikali au mawasiliano rasmi; au

(b) kutumika katika barua, postikadi, ujumbe wa simu au waraka mwengine au kifurushi chochote au kitu kilichopo katika hifadhi ya mamlaka ya posta au simu.

Utaratibu kuhusu barua na ujumbe wa simu.

**133.** Ikiwa waraka wowote, kifurushi, ankara au kitu kilichopo katika hifadhi ya mamlaka ya posta, simu au ujumbe wa simu, kwa maoni ya Hakimu wa Mkoa, kitu hicho kinatakiwa kwa madhumuni ya upelelezi, uchunguzi au mwenendo mwengine wa kesi chini ya Sheria hii, Hakimu huyo anaweza kuitaka mamlaka ya posta, simu au ujumbe wa simu, kama itakavyokuwa, kuwasilisha waraka, kifurushi, ankara au kitu kwa mtu huyo kama hakimu atavyoelekeza.

Utaratibu kuhusu hesabu za benki.

**134.** Wakati wowote Mkurugenzi wa Mashtaka anapoona ni muhimu kwamba hesabu ya benki au muamala wowote mwengine wa kifedha kufanyiwa uchunguzi kuhusiana na uhalifu wowote unaotuhumiwa kuwa umetendwa, Mkurugenzi wa Mashtaka anaweza, kwa amri ya maandishi, kumuidhinisha afisa wa polisi wa cheo kisicho chini ya mkaguzi msaidizi au mtu mwengine yeyote kufanya uchunguzi wa hesabu hiyo au muamala wa kifedha uliotajwa na anaweza kuiamrisha benki kuzuia kwa muda uendeshaji wa hesabu hiyo kusubiri upelelezi huo.

Upekuzi, uchukuaji wa taarifa za kompyuta na vifaa.

**135.**-(1) Ikiwa hakimu ameridhika kwa msingi wa taarifa ya kiapo kwamba kuna sababu za msingi kutuhumu kwamba kunaweza kuwepo katika pahala kitu au taarifa za kompyuta:

(a) zinazoweza kuwa ni muhimu kwa ushahidi katika kuthibitisha kosa; au

(b) kwamba zimepatikana na mtu zikiwa ni matokeo ya kosa,

hakimu anaweza kutoa hati inayomuidhinisha polisi au mtu yeyote aliyeidhinishwa kuingia pahala hapo kufanya upekuzi na kuchukua kitu au taarifa za kompyuta.

(2) Katika kifungu hiki, "kitu" kinajumuisha:

(a) mfumo wa kompyuta au sehemu ya mfumo wa kompyuta; na

(b) kifaa cha kuhifadhia taarifa za kompyuta.

Kumsaidia polisi na afisa aliyeidhinishwa.

**136.**-(1) Mtu yeyote ambaye ana katika milki yake au udhibiti wake kifaa cha kuhifadhia taarifa za kompyuta au mfumo wa komyuta ambao unafanyiwa upekuzi chini ya kifungu cha 135 cha Sheria hii ni lazima aruhusu, na amsaidie ikihitajika, mtu anayefanya upekuzi:

(a) kupata na kutumia mfumo wa kompyuta au kifaa cha kuhifadhia taarifa za kompyuta ili kufanya upekuzi wowote wa taarifa zinazopatikana kwenye mfumo wa kompyuta au kwenye kifaa cha kuhifadhia taarifa za kompyuta;

(b) kupata na kunakili taarifa hizo za kompyuta;

(c) kutumia kifaa kwa ajili ya kunakili; na

(d) kupata matokeo yanayofahamika kutoka katika mfumo wa kompyuta katika utaratibu wa maandishi ya kawaida ambayo yanaweza kusomwa na mtu.

(2) Mtu yeyote anayeshindwa bila ya sababu ya msingi au inayokubalika kumruhusu au kumsaidia mtu anayefanya upekuzi huo atakuwa ni mkosa na atatozwa faini isiyozidi Shilingi Milioni Moja au atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi mwaka mmoja au adhabu zote mbili faini na kifungo.

(3) Katika kifungu hiki, "kusaidia" kunajumuisha utoaji wa maneno ya siri, funguo za kuficha taarifa na taarifa nyengine muhimu kwa ajili ya kuingia kwenye kompyuta au mfumo wa kompyuta.

Rekodi za kuingia kwa ajili ya kuchukua taarifa.

**137.**-(1) Ikiwa mfumo wa kompyuta au taarifa ya kompyuta imetolewa au imefanywa isipatikane, kufuatia upekuzi au uchukuaji chini ya kifungu cha 135 cha Sheria hii, mtu ambaye alifanya upekuzi huo, wakati wa upekuzi au mara tu kama itakavyowezekana baada ya upekuzi huo, atalazimika:

(a) kutengeneza orodha ya kile kilichochukuliwa au kilichofanywa kisipatikane, pamoja na tarehe na wakati wa kuchukuliwa; au

(b) kutoa nakala ya orodha hiyo kwa:

(i) mkaazi wa jengo; na

(ii) mtu mwenye udhibiti wa mfumo wa kompyuta.

(2) Kwa kuzingatia kifungu kidogo cha (3)cha kifungu hiki, kwa maombi, afisa wa polisi au mtu aliyeidhinishwa atalazimika:

(a) kumruhusu mtu ambaye alikuwa na hifadhi au udhibiti wa mfumo wa kompyuta, au mtu anayefanya kazi kwa niaba yao kupata na kunakili taarifa za kompyuta katika mfumo huo wa kompyuta; au

(b) kumpa mtu huyo nakala au taarifa ya kompyuta.

(3) Afisa wa polisi au mtu mwengine aliyeidhinishwa anaweza kukataa kutoa ruhusa ya kuingia au kutoa nakala ikiwa mtu huyo ana sababu za msingi za kuamini kwamba kutoa ruhusa ya kuingia, au kutoa nakala:

(a) kungekuwa ni kosa la jinai; au

(b) kungeathiri:

(i) upelelezi unaohusiana na upekuzi huo uliokuwa unafanyika; au

(ii) upelelezi mwengine unaoendelea; au

(iii) mwenendo wowote wa kijinai ambao bado haujakamilika au unaweza kufanywa kuhusiana na mmoja kati ya upelelezi huo.

Uwasilishaji wa taarifa.

**138.** Ikiwa Mkurugenzi wa Mashtaka anaridhika kwamba taarifa za kompyuta zilizoainishwa au zilizochapishwa au taarifa nyengine, kimsingi zinahitajika kwa madhumuni ya upelelezi wa jinai au mwenendo wa kijinai, anaweza kuamuru kwa maandishi kwamba:

(a) mtu mwenye udhibiti wa mfumo wa kompyuta kutoa, kutoka katika mfumo ulioanishwa, taarifa za kompyuta au machapisho au kitu chengine kinachoeleweka kinachotokana na taarifa hizo; na

(b) mtoa huduma ya mtandao au mtoa huduma nyengine kutoa taarifa kuhusu watu ambao waliojisajili au vyenginevyo wanaotumia huduma hiyo.

Kuweka bayana taarifa zilizohifadhiwa.

**139.** Ikiwa Mkurugenzi wa Mashtaka anaridhika kwamba taarifa zilizoainishwa zimehifadhiwa katika mfumo wa kompyuta kimsingi zinahitajika kwa madhumuni ya upelelezi wa jinai au mwenendo wa kijinai, Mkurugenzi wa Mashtaka anaweza kwa

amri ya maandishi kuelekeza kwamba mtu mwenye dhamana ya mfumo wa kompyuta kuweka bayana mienendo ya uhakika ya taarifa kuhusu mawasiliano yaliyoainishwa ili kutambua:

(a) mtoaji wa huduma; na

(b) njia ambayo mawsiliano hayo yalipitia.

Kuhifadhi taarifa.

**140.**-(1) Ikiwa afisa wa polisi anaridhika kwamba:

(a) taarifa zilizohifadhiwa katika mfumo wa kompyuta kimsingi zinahitajika kwa madhumuni ya upelelezi wa jinai; na

(b) kuna hatari kwamba taarifa hizo zinaweza kuharibiwa au kufanywa zisipatikane,

afisa wa polisi au mtu mwengine aliyeidhinishwa anaweza, kwa notisi ya maandishi iliyotolewa kwa mtu mwenye udhibiti wa mfumo wa kompyuta, kumtaka mtu huyo kuhakikisha kwamba taarifa zilizoainishwa katika notisi hiyo zinahifadhiwa kwa kipindi hadi siku saba kama itakavyoainishwa katika notisi hiyo.

(2) Kipindi kilichotajwa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, kinaweza kuongezwa ikiwa Jaji au Hakimu ataidhinisha kuongezwa kwa kipindi cha ziada kilichoainishwa katika amri.

Upelelezi wa mawasiliano ya kielektroniki.

**141.** Ikiwa Jaji au Hakimu anaridhika kwa msingi wa hati ya kiapo kwamba kuna sababu za msingi kutuhumu kwamba maudhui ya mawasiliano ya kielektroniki kimsingi yanahitajika kwa madhumuni ya upelelezi wa jinai, Jaji au Hakimu:

(a) atatoa amri kwa mtoa huduma ya mtandao ambaye huduma yake inapatikana kupitia matumizi ya njia za kiufundi kukusanya au kurekodi au kuruhusu au kuzisaidia mamlaka husika pamoja na ukusanyaji au kurekodi maudhui ya taarifa zinazohusiana na mawasiliano yaliyosafirishwa kwa njia ya mfumo wa kompyuta; au

(b) atamuidhinisha afisa wa polisi kukusanya au kurekodi taarifa hizo kwa kutumia njia za kiufundi.

Upelelezi wa usafirishaji wa taarifa.

**142.**-(1) Ikiwa afisa wa polisi anaridhika kwamba usafirishaji wa taarifa zinazohusiana na mawasiliano yaliyoainishwa kimsingi zinahitajika kwa madhumuni ya upelelezi wa jinai, afisa wa polisi huyo anaweza, kwa notisi ya maandishi aliyopewa mtu mwenye udhibiti wa taarifa hizo, kumtaka mtu huyo:

(a) kukusanya au kurekodi taarifa za usafirishaji zinazohusiana na mawasiliano yaliyoainishwa katika kipindi kilichoainishwa; na

(b) kumruhusu na kumsaidia afisa wa polisi aliyeainishwa kukusanya au kurekodi taarifa hizo.

(2) Ikiwa hakimu anaridhika kwa msingi wa hati ya kiapo kwamba kuna sababu za msingi kutuhumu kwamba taarifa za usafirishaji kimsingi zinahitajika kwa madhumuni ya upelelezi wa jinai, hakimu huyo anaweza kumuidhinisha afisa wa polisi kukusanya au kurekodi taarifa za usafirishaji zinazohusiana na mawasiliano yaliyoainishwa katika kipindi kilichoainishwa kupitia matumizi ya njia za kiufundi.

Usiri na mipaka ya dhima.

**143.**-(1) Mtoa huduma ya mtandao ambaye bila ya mamlaka halali anaweka bayana:

(a) ukweli kwamba amri chini ya vifungu vya 135, 136, 137, 138, 139, 140 na 142 vya Sheria hii imetolewa; au

(b) chochote kilichofanywa chini ya amri hiyo; au

(c) taarifa yoyote iliyokusanywa au iliyorekodiwa chini ya amri hiyo,

anatenda kosa na, atakapotiwa hatiani, atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi mwaka mmoja, au atatozwa faini isiyozidi Shilingi Milioni Moja, au adhabu zote mbili.

(2) Mtoa huduma ya mtandao au mtoa huduma mwengine yeyote hatokuwa na dhima chini ya sheria ya madai au jinai kwa ajili ya kuweka bayana taarifa yoyote au mawasiliano mengine ambayo ameweka bayana chini ya Sheria hii.

Tafsiri.

**144.** Maneno na masharti yaliyotumika katika vifungu 136 mpaka 143 vya Sheria hii, yatapewa tafsiri ile ile iliyotolewa kwa maneno hayo chini ya Sheria ya Adhabu.

Uwezo wa kutoa hati ya upekuzi.

**145.**-(1) Endapo inathibitika kwa kiapo mbele ya mahakama kwamba kiuhakika au kwa mujibu wa tuhuma za msingi kuhusiana na kitu chochote, kwa au kuhusiana na kitu hicho kosa limetendwa au kitu chochote ambacho ni muhimu kwa madhumuni ya upelelezi wa kosa lolote kipo katika jengo lolote, chombo, chombo cha uchukuzi, boksi, kontena au pahala, mahakama inaweza kwa hati, inayoitwa "hati ya upekuzi", kumuidhinisha afisa wa polisi au mtu mwengine atakayetajwa ndani ya hati hiyo kufanya upekuzi wa jengo hilo, chombo, chombo cha uchukuzi, boksi, kontena au pahala ambapo patatajwa au pataelezwa katika hati kwa ajili ya kitu hicho chochote na, ikiwa kitu chochote kinachotafutwa kwa njia ya upekuzi huo kitaonekana, akichukuwe na akipeleke mbele ya mahakama iliyotoa hati hiyo au mahakama nyengine kukishughulikia kwa mujibu wa sheria.

(2) Kwa kuzingatia kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, maudhui muhimu na muundo wa hati ya upekuzi utakuwa kama ulivyoelezwa katika Jadweli la Sita la Sheria hii.

Upekuzi unaofanywa na afisa wa polisi.

**146.**-(1) Ikiwa mkuu wa kituo cha polisi anaridhika kwamba kuna sababu za msingi za kutuhumu kwamba kuna katika jengo lolote, chombo, chombo cha uchukuzi, boksi, kontena au pahala:

(a) kitu chochote kuhusiana na kitu hicho kosa lolote limetendwa;

(b) kitu chochote kuhusiana na kitu hicho kuna sababu za msingi kuamini kwamba kitapelekea kupatikana ushahidi katika utendaji wa kosa lolote;

(c) kitu chochote kuhusiana na kitu hicho kuna sababu za msingi za kuamini kwamba kimekusudiwa kutumika kwa madhumuni ya kutenda kosa lolote, na afisa huyo anaridhika kwamba ucheleweshaji wowote utapelekea kuondosha au kuharibu kitu hicho, au utahatarisha maisha au mali,

anaweza kupekua au kutoa idhini ya maandishi kwa afisa yeyote wa polisi aliye chini ya polisi huyo kupekua jengo, chombo, chombo cha uchukuzi, boksi, kontena, au pahala, kama hali itakavyokuwa.

(2) Wakati idhini yoyote iliyotajwa katika kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, inapotolewa, afisa wa polisi anayehusika, haraka iwezekanavyo atatoa taarifa kwa hakimu ya utoaji wa idhini hiyo, sababu zilizopelekea kutolewa kwa idhini hiyo, na matokeo ya upekuzi wowote uliofanywa chini ya idhini hiyo.

(3) Endapo kitu chochote kimechukuliwa kwa mujibu wa uwezo ulioelezwa na kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, afisa anayechukua kitu hicho atatoa risiti inayotambua uchukuaji wa kitu hicho ikiwa na saini ya mmiliki wa jengo hilo, na saini za mashahidi walioshuhudia upekuzi huo.

(4) Mkuu wa kituo cha polisi, akiwa amepewa uwezo wa kisheria kutoa amri, kuidhinisha au kufanya upekuzi kwa mtu yeyote, pahala, jengo, chombo, chombo cha uchukuzi au kontena, bila ya sababu ya maana na bila ya kuwa na sababu ya msingi ya kufanya hivyo, anaamuru, anaidhinisha au anafanya upekuzi huo, atakuwa ni mkosa na atatozwa faini isiyopungua Shilingi Milioni Moja au kifungo kwa kipindi kisichozidi mwaka mmoja au vyote viwili kwa pamoja.

(5) Mashtaka dhidi ya mtu yeyote chini ya kifungu kidogo cha (4) cha kifungu hiki, hayataanzishwa isipokuwa kwa idhini ya maandishi ya Mkurugenzi wa Mashtaka.

Wajibu wa watu kuruhusu upekuzi.

**147.**-(1) Wakati wowote jengo lolote au pahala pengine panapohitajika kupekuliwa pamefungwa, mtu yeyote anayeishi humo ndani au akiwa msimamizi wa jengo hilo au pahala hapo, anapotakiwa na afisa wa polisi au mtu mwengine anayetekeleza hati ya upekuzi au aliyepewa idhini ya maandishi, na atakapowasilisha hati hiyo au idhini hiyo ya maandishi, atamruhusu mtu huyo kuingia ndani humo bila ya vikwazo na kutoka ndani humo na kumpa msaada wote unaohitajika kwa ajili ya kufanya upekuzi ndani humo.

(2) Ikiwa kuingia ndani au kutoka nje ya jengo hilo au pahala pengine hakukuwezekana, afisa wa polisi au mtu mwengine anayetekeleza hati ya upekuzi au mtu mwenye idhini ya maandishi, anaweza kuendelea katika namna iliyoelezwa na kifungu cha 14 au 15 cha Sheria hii.

(3) Endapo mtu yupo katika au karibu na jengo hilo au pahala hapo kimsingi anatuhumiwa kuficha katika mwili wake kitu chochote ambacho upekuzi unafanywa kukitafuta, mtu huyo anaweza kupekuliwa.

(4) Ikiwa mtu huyo ni mwanamke, masharti ya kifungu cha 19 cha Sheria hii yatazingatiwa.

Masharti ya utekelezaji wa hati ya upekuzi.

**148.**-(1) Kabla ya kufanya upekuzi chini ya kifungu cha 145, 146 au 147 cha Sheria hii, afisa au mtu mwengine anayetaka kuanza kupekua, atawaita wakaazi wawili au zaidi wenye kuheshimika wa eneo hilo ambapo jengo hilo lipo au pahala pengine panapotaka kupekuliwa wahudhurie na kushuhudia upekuzi huo, na anaweza kutoa amri ya maandishi kwa mashahidi hao au kwa yeyote miongoni mwao kufanya hivyo.

(2) Upekuzi utafanywa mbele yao, na orodha ya vitu vyote vilivyochukuliwa katika upekuzi huo na pahala ambapo kila kimojawapo kimekutwa itatayarishwa na afisa huyo au mtu mwengine na kusainiwa na mashahidi hao; lakini mtu aliyeshuhudia upekuzi chini ya kifungu hiki hatotakiwa kufika mahakamani kama shahidi wa upekuzi huo isipokuwa kama ameitwa rasmi na mahakama.

(3) Mkaazi wa jengo au pahala pengine palipopekuliwa, au mtu mwengine kwa niaba yake, kama yupo, ataruhusiwa kuhudhuria wakati wa upekuzi, na nakala ya orodha iliyotayarishwa chini ya kifungu hiki, iliyosainiwa na mashahidi hao, atapewa mkaazi huyo au mtu mwengine endapo ataomba.

(4) Pale mtu anapopekuliwa chini ya masharti ya kifungu kidogo cha (3) cha kifungu cha 147 cha Sheria hii, orodha ya vitu vyote vilivyochukuliwa itatayarishwa, na nakala ya orodha hiyo atapewa mtu huyo endapo ataomba.

(5) Mtu yeyote ambaye bila ya sababu ya msingi anakataa au anadharau kuhudhuria na kushuhudia upekuzi chini ya kifungu hiki wakati anapotakiwa kufanya hivyo kwa amri ya maandishi iliyopelekwa au iliyowasilishwa kwa mtu huyo,

atachukuliwa kuwa ametenda kosa la kutokutii amri halali linaloadhibiwa chini ya kifungu cha 99 cha Sheria ya Adhabu.

(6) Hati ya upekuzi inaweza kutolewa katika siku yoyote, ikijumuisha siku ya mapumziko, na inaweza kutekelezwa siku yoyote, ikijumuisha siku ya mapumziko, baina ya saa za kuchomoza kwa jua na kuzama kwa jua, lakini mahakama inaweza, kwa hati hiyo, kwa uwezo wake, kumuidhinisha afisa wa polisi au mtu mwengine ambaye hati hiyo imeelekezwa kwake kuitekeleza hati hiyo saa yoyote.

Uzuiaji wa mali iliyochukuliwa.

**149.**-(1) Wakati kitu chochote hicho kinachukuliwa na kinapelekwa mbele ya mahakama, kinaweza kuzuiliwa hadi pale itakapomalizika kesi au upelelezi, uangalizi unaostahiki utachukuliwa kwa ajili ya uhifadhi wake.

(2) Ikiwa rufaa yoyote inafunguliwa, Mahakama inaweza kuamrisha kitu hicho kiendelee kuzuiwa kwa madhumuni ya rufaa hiyo.

(3) Ikiwa hakuna rufaa iliyofunguliwa, au hakuna mtu aliyepelekwa Mahakamani kwa ajili ya kesi hiyo, Mahakama itaelekeza kitu hicho kirejeshwe kwa mtu ambaye kutoka kwa mtu huyo kitu hicho kilichukuliwa, isipokuwa kama Mahakama inaona inafaa au inaruhusiwa au inatakiwa kwa mujibu wa Sheria kukishughulikia kitu hicho vyenginevyo.

Masharti yanayotumika kwa hati ya upekuzi.

**150.** Masharti ya vifungu vya 116 (1) na (3), 118, 120, 123, 124 na 125 vya Sheria hii, kama itakavyowezekana, yatatumika kwa hati zote za upekuzi zinazotolewa chini ya kifungu cha 145 cha Sheria hii.

### Masharti kuhusu Dhamana

Uwezo wa jumla wa kutoa dhamana.

**151.**-(1) Pale mtu yeyote, asiyekuwa mtu anayeshtakiwa kwa kuua kwa kukusudia, uhaini, unyang'anyi wa kutumia silaha, kukutwa na silaha, kusafirisha dawa za kulevya, kosa linalohusu kiwango kikubwa cha dawa za kulevya, kubaka, kuingilia kinyume na maumbile, kunajisi mtoto wa kiume, kubaka kwa kikundi au kuingilia maharimu, anakamatwa au anawekwa kizuizini bila ya hati ya ukamataji na mkuu wa kituo cha polisi, au anafika au analetwa mbele ya mahakama, na yuko tayari wakati wowote wakati yupo kwenye hifadhi ya afisa huyo au katika hatua yoyote ya mwenendo wa shauri mbele ya mahakama hiyo kuweka dhamana, mtu huyo anaweza kupewa dhamana.

(2) Mkuu huyo wa kituo cha polisi au mahakama, badala ya kuchukua dhamana kutoka kwa mtu huyo inaweza, kumuachia mtu huyo atakapotekeleza ahadi ya dhamana bila ya wadhamini kwa ajili ya kuhudhuria kwake kama itakavyoelezwa baadae.

(3) Kiwango cha dhamana kitapangwa kwa kuzingatia mazingira ya kesi husika na hakitokuwa kikubwa sana.

(4) Bila ya kujali chochote kilichomo katika kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Jaji Mkuu anaweza katika kesi yoyote kuelekeza kwamba mtu yeyote apewe dhamana.

(5) Mahakama Kuu inaweza, katika kesi ya makosa yenye dhamana, kuelekeza kwamba mtu yeyote apewe dhamana au kwamba masharti ya dhamana yaliyowekwa na mahakama ya chini au polisi yapunguzwe.

(6) Endapo mtu ameshindwa kutekeleza masharti ya ahadi ya dhamana kuhusu muda na pahala pa kuhudhuria, mahakama inaweza kukataa kumuachia mtu huyo kwa dhamana kwa mara nyengine baadae katika kesi hiyo ambapo yeye atafika mbele ya mahakama au ataletwa kwenye kizuizi, na kukataa huko kokote kutakuwa bila ya kuathiri mamlaka ya mahakama kumuita mtu yeyote anayewajibika na ahadi hiyo kulipa adhabu inayotokana na ahadi hiyo.

(7) Ukiukaji wa ahadi ya dhamana ya polisi unaweza kutiliwa nguvu za kisheria mahakamani kwa kutumia masharti ya Sheria hii.

Pale dhamana inapoweza kutolewa kwa makosa yasiyo na dhamana.

**152.**-(1) Usikilizaji wa kesi ambayo mtu anashtakiwa kwa kosa lisilo na dhamana lazima uanze ndani ya miezi sita kutoka tarehe mtu huyo anayeshtakiwa alipokamatwa.

(2) Kama kesi haitaanza kusikilizwa ndani ya kipindi cha miezi sita kilichotajwa, mshtakiwa atapewa dhamana isipokuwa kama mahakama, kwa sababu zitakazorekodiwa kwa maandishi, itaelekeza vyenginevyo.

(3) Ikiwa, wakati wowote baada ya kumalizika kwa usikilizaji wa kesi ya mtu anayeshtakiwa kwa kosa lisilo na dhamana na kabla ya hukumu kutolewa, mahakama inaona kwamba kuna sababu za msingi za kuamini kwamba mshtakiwa si mkosa wa kosa hilo, itamuachia mshtakiwa huyo, ikiwa mshtakiwa huyo yupo kizuizini, atakapotekeleza ahadi ya dhamana bila ya wadhamini kwa ajili ya kufika mahakamani kusikiliza hukumu itakayotolewa.

(4) Mahakama ambayo imemuachia mtu kwa dhamana chini ya kifungu kidogo cha (2) au (3) cha kifungu hiki, inaweza, ikiwa itaona ni muhimu kufanya hivyo, kuelekeza kwamba mtu huyo akamatwe na apelekwe kizuizini.

Ahadi ya dhamana.

**153.** Kabla ya mtu hajaachiwa kwa dhamana au kwa ahadi ya dhamana yake mwenyewe, ahadi ya dhamana kwa ajili ya kiasi fulani kama mahakama au afisa wa polisi kama itakavyokuwa itaona au ataona inafaa, itawekwa na mtu huyo, na, pale atakapoachiwa kwa dhamana, kwa mdhamini mmoja au zaidi, kwa masharti kwamba mtu huyo atahudhuria katika muda na pahala palipotajwa katika ahadi ya dhamana na ataendelea kuhudhuria hivyo hadi pale itakapoelekezwa vyenginevyo na mahakama au afisa wa polisi, kama itakavyokuwa.

Kuachiwa kutoka kizuizini watu walio-chukuliwa dhamana.

**154.**-(1) Mara baada ya ahadi ya dhamana kutekelezwa, mtu ambaye amechukuliwa dhamana ataachiwa, na endapo mtu huyo yupo Chuo cha Mafunzo mahakama iliyompa dhamana itatoa amri ya kuachiwa mtu huyo kwa afisa mwenye dhamana wa Chuo cha Mafunzo, na afisa huyo atakapopokea amri hiyo atamuachia mtu huyo.

(2) Hakuna chochote katika kifungu hiki au kifungu cha 152 cha Sheria hii, kitakachochukuliwa kuwa kinaelekeza kuachiwa kwa mtu yeyote anayewajibika kuwekwa kizuizini kwa jambo jengine lisilokuwa lile ambalo linalohusu ahadi ya dhamana iliyotekelezwa.

Uwekaji wa fedha au mali badala ya ahadi ya dhamana.

**155.** Endapo mtu anatakiwa na mahakama au afisa kutekeleza ahadi ya dhamana, akiwa na wadhamini au bila wadhamini, mahakama hiyo au ofisa anaweza, isipokuwa katika mazingira ya ahadi ya dhamana ya kuwa na tabia njema, kumruhusu mtu huyo kuweka kiwango cha fedha kwa kiasi ambacho kama mahakama au afisa anaweza kukipanga badala ya kutekeleza ahadi hiyo ya dhamana, na anaweza kumruhusu mtu huyo kuweka mali yoyote.

Uwezo wa kuamrisha dhamana in-ayotosheleza.

**156.** Ikiwa, kwa makosa, udanganyifu au vyenginevyo, wadhamini wasiotosheleza wamekubaliwa, au wadhamini hao baadae wamekuwa hawatoshelezi, mahakama inaweza kutoa hati ya ukamataji ikielekeza kwamba mtu aliyeachiwa kwa dhamana aletwe mbele yake na inaweza kumuamuru mtu huyo kutafuta wadhamini wa kutosheleza, na akishindwa kufanya hivyo inaweza kumpeleka mtu huyo Chuo cha Mafunzo.

Uwezo wa kukataa wadhamini.

**157.** Mahakama inaweza kukataa kumkubali mdhamini yeyote kwa sababu zitakazorekodiwa, kwa msingi kwamba, mdhamini huyo ni mtu asiyefaa.

Kuondoa dhima kwa wadhamini.

**158.**-(1) Wote au yeyote miongoni mwa wadhamini kwa ajili ya kufika au kuhudhuria mahakamani mtu aliyepewa dhamana anaweza, wakati wowote, kuomba kwa hakimu kuondoa ahadi ya dhamana ama yote au kwa kiasi kile kinachomhusu muombaji au waombaji.

(2) Baada ya ombi hilo kufanywa, hakimu atatoa hati yake ya ukamataji inayoelekeza kwamba mtu huyo aliyeachiwa aletwe mbele yake.

(3) Atakapofika mtu huyo kufuatia hati ya ukamataji, au kwa kujisalimisha yeye mwenyewe, hakimu ataelekeza ahadi ya dhamana kuondolewa ama yote au kwa kiwango kinachomhusu muombaji au waombaji, na atamuita mtu huyo kutafuta wadhamini wengine wanaotosheleza, na ikiwa mtu huyo atashindwa kufanya hivyo anaweza kumpeleka Chuo cha Mafunzo.

Kifo cha mdhamini.

**159.** Pale ambapo mdhamini aliyeweka ahadi ya dhamana amefariki kabla ahadi hiyo haijatekelezwa, mali zake zitaondolewa kutoka katika dhima kuhusiana na ahadi hiyo

ya dhamana, lakini mtu aliyewekewa dhamana anaweza kuhitajika kutafuta mdhamini mpya.

Uwezo wa kumpeleka kizuizini mtu anayetoroka.

**160.** Ikiwa itaonekana na mahakama yoyote, kwa taarifa iliyotolewa kwa kiapo, kwamba mtu yeyote anayewajibika kwa ahadi ya dhamana anataka kuondoka Zanzibar, mahakama inaweza kuwezesha mtu huyo akamatwe na inaweza kumpeleka mtu huyo Chuo cha Mafunzo hadi pale mwisho wa usikilizaji wa kesi, isipokuwa kama mahakama inaona inafaa kumpa dhamana mtu huyo baada ya kuwekwa ahadi ya ziada ya dhamana.

Kuondolewa ahadi ya dhamana.

**161.**-(1) Wakati wowote itakapothibitika kwa kuridhika kwa mahakama ambayo ahadi ya dhamana chini ya Sheria hii imewekwa, au pale ahadi ya dhamana imewekwa kwa afisa wa polisi kwa ajili ya kufika mbele ya mahakama, kwamba kwa kuridhika kwa mahakama hiyo, kwamba ahadi hiyo ya dhamana imeshaondolewa, mahakama itarikodi sababu za uthibitisho huo, na inaweza kumwita mtu yeyote anaewajibika kwa ahadi hiyo ya dhamana kulipa adhabu inayotokana na ahadi ya dhamana hiyo, au kuonesha sababu kwanini isilipwe.

(2) Ikiwa sababu za msingi hazikuoneshwa na adhabu haijalipwa, mahakama inaweza kuendelea kuchukua adhabu hiyo kwa kutoa hati kwa ajili ya kukamata na kuuza mali inayohamishika au isiyohamishika inayomilikiwa na mtu huyo.

(3) Hati hiyo inaweza kutekelezwa ndani ya eneo la mipaka ya mamlaka ya mahakama hiyo ambayo imetoa hati hiyo; na itaidhinisha ukamataji na uuzaji wa mali inayohamishika inayomilikiwa na mtu huyo nje ya mipaka hiyo, itakapothibitishwa na hakimu yeyote aliyopo ndani ya eneo la mipaka ya mamlaka ya mahakama ambayo mali hiyo inapatikana.

(4) Iwapo adhabu hiyo haijalipwa na haiwezi kuchukuliwa kwa ukamataji huo na uuzaji huo, mtu anayewajibika atalazimika kwa amri ya mahakama ambayo ilitoa hati hiyo, kutumikia adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miezi sita.

(5) Mahakama inaweza, kwa uwezo wake, kurudisha sehemu yoyote ya adhabu hiyo iliyotajwa na kulazimisha sehemu tu ya malipo.

(6) Wakati mtu ambaye ameweka dhamana anatiwa hatiani kwa kosa ambalo utendwaji wa kosa hilo unapelekea uvunjaji wa masharti ya ahadi yake ya dhamana nakala iliyothibitishwa ya hukumu ya mahakama ambayo mtu huyo ilimtia hatiani kwa kosa hilo inaweza kutumika kama ushahidi katika mwenendo wa kesi dhidi ya mdhamini au wadhamini, na, ikiwa nakala hiyo iliyothibitishwa imetumika hivyo, mahakama itachukulia kwamba hilo limetendwa na mtu huyo isipokuwa kama itathibitika vyenginevyo.

Rufaa na mapitio ya amri.

**162.** Amri zote zilizotolewa chini ya kifungu cha 161 cha Sheria hii na hakimu yeyote zitakatiwa rufaa na zinaweza kufanyiwa mapitio na Mahakama Kuu.

Kutoza kiwango kinachodaiwa kuhusiana na ahadi ya dhamana.

**163.** Mahakama Kuu inaweza kumuelekeza hakimu yeyote kutoza kiwango kinachodaiwa kuhusiana na ahadi ya dhamana ya kufika na kuhudhuria Mahakama Kuu.

## Mashtaka na Taarifa ya Mashtaka kwa Mahakama Kuu

Maudhui ya shtaka.

**164.**-(1) Shtaka chini ya Sheria hii litaeleza kosa ambalo mshtakiwa anashtakiwa nalo pamoja na maelezo mafupi ya kosa hilo.

(2) Ikiwa sheria iliyounda kosa hilo imelipa kosa hilo jina lolote maalum, kosa hilo linaweza kuelezwa katika shtaka kwa jina hilo tu.

(3) Ikiwa sheria iliyounda kosa hilo haijatoa jina lolote maalum kwa kosa hilo, kiasi cha kutosha cha maana ya kosa hilo lazima kielezwe ili kumpa mshtakiwa taarifa ya jambo ambalo anashtakiwa nalo.

(4) Shtaka litaeleza sheria na kifungu cha sheria ambapo dhidi ya sheria hiyo na dhidi ya kifungu hicho kosa linasemekana limetendwa.

(5) Shtaka litaandikwa katika lugha ya mahakama.

(6) Ikiwa mshtakiwa, awali ameshawahi kutiwa hatiani, anawajibika, kwa sababu ya kutiwa huko hatiani kabla, kupewa adhabu kubwa zaidi, au kupewa adhabu ya aina tofauti kwa kosa linalofuata, na inakusudiwa kuthibitisha hatia hiyo ya awali kwa madhumuni ya kuathiri adhabu hiyo ambayo mahakama inaweza kuona inafaa kutoa kwa shtaka linalofuata, ukweli, tarehe na pahala pa hatia ya awali pataelezwa katika shtaka hilo; na ikiwa maelezo hayo hayakuingizwa, mahakama inaweza kuyaongeza wakati wowote kabla adhabu haijatolewa.

Kuunganisha mashtaka au makosa katika hati rasmi ya mashtaka au katika taarifa ya mashtaka.

**165.**-(1) Mashtaka kwa makosa yoyote yanaweza kuunganishwa pamoja katika hati moja rasmi ya mashtaka au katika taarifa ya mashtaka ikiwa mashtaka yote yanajengeka kutokana na mambo hayo hayo au aina au sehemu ya mfuatano wa makosa ya aina moja au aina zinazofanana.

(2) Pale zaidi ya kosa moja linashtakiwa katika hati rasmi ya mashtaka au katika taarifa ya mashtaka, maelezo ya kila kosa linaloshtakiwa yatawekwa katika shtaka tofauti lililomo katika hati rasmi ya mashtaka au katika aya tofauti, inayoitwa kosa, katika taarifa ya mashtaka.

(3) Pale, kabla ya kusikilizwa kwa kesi, au katika hatua yoyote ya usikilizaji wa kesi, mahakama inaona kwamba mtu anayeshtakiwa anaweza kukwazika katika utetezi wake kwa sababu ya kushtakiwa kwa kosa zaidi ya moja katika hati hiyo moja rasmi au katika taarifa ya mashtaka, au kwamba kwa sababu nyengine yoyote inafaa kuelekeza kwamba mtu huyo ashtakiwe tofauti kwa kosa moja lolote au kwa makosa hayo zaidi ya moja mahakama inaweza kuamuru usikilizaji tofauti wa shtaka moja au mashtaka hayo zaidi ya moja au makosa.

Kuunganisha washtakiwa wawili au zaidi katika hati moja rasmi ya mashtaka au katika taarifa ya mashtaka.

**166.** Watu wafuatao wanaweza kuunganishwa katika hati moja rasmi ya mashtaka au katika taarifa ya mashtaka na wanaweza kusikilizwa kwa pamoja:

(a) watu wanaoshtakiwa kwa kosa moja hilo hilo lililotendwa katika muamala huo huo mmoja;

(b) watu wanaoshtakiwa kwa kosa na watu wanaoshtakiwa kusaidia, au wanaoshtakiwa kwa kujaribu kutenda kosa hilo;

(c) watu wanaoshtakiwa kwa makosa zaidi ya moja ya aina hiyo moja, yaani ni kusema kwamba, makosa yanayoadhibiwa kwa kiwango hicho hicho cha adhabu chini ya kifungu hicho hicho cha Sheria ya Adhabu au sheria nyengine yoyote, yaliyotendwa na wao kwa pamoja ndani ya kipindi cha miezi kumi na mbili;

(d) watu wanaoshtakiwa kwa makosa tofauti katika muamala mmoja huo huo;

(e) watu wanaoshtakiwa kwa kosa, ambalo linalohusiana na wizi, makosa yanayohusiana na kuiba, unyang'anyi, uporaji, kuvunja nyumba usiku, kuvunja nyumba mchana na makosa yanayofanana nayo, na kujisingizia, na watu wanaoshtakiwa kupokea au kubakia na mali, umiliki wake unatuhumiwa umehaulishwa na kosa lolote hilo lililotendwa na watu waliotajwa awali, au kwa kusaidia au kwa kujaribu kutenda kosa lolote hilo lililotajwa mwisho; na

(f) watu wanaoshtakiwa kwa kosa lolote linalohusiana na sarafu bandia, na watu wanaoshtakiwa kwa kosa jengine lolote linalohusiana na sarafu hiyo hiyo, au kwa kusaidia au kwa kujaribu kutenda kosa hilo lolote.

## Kanuni za kutengeneza hati za mashtaka na taarifa za mashtaka

Kanuni za kutengeneza hati za mashtaka na taarifa za mashtaka.

**167.**-(1) Kanuni chini ya kifungu hiki zitatumika kwa hati zote za mashtaka na taarifa za mashtaka na, bila ya kujali kanuni yoyote ya sheria au mazoea, hati ya mashtaka au taarifa ya mashtaka, kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii, haitaweza kupingwa kuhusu muundo wake au yaliyomo kwenye hati hiyo ikiwa imetengenezwa kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii.

(2) Ufuatao utakuwa ni utaratibu ambao katika utaratibu huo makosa yatashtakiwa:

(a) shtaka au kosa litaanza kwa maelezo ya kosa linaloshtakiwa, yanayoitwa maelezo ya kosa;

(b) maelezo ya kosa yataelezea kosa kwa ufupi katika lugha ya kawaida, yatakayoepuka kwa kadiri iwezekanavyo matumizi ya lugha ya kiufundi, na siyo lazima kuelezea viini vyote muhimu vya kosa, na ikiwa kosa linaloshtakiwa limeundwa na sheria, maelezo yatajumuisha marejeo ya kifungu cha sheria iliyotengeneza kosa;

(c) baada ya maelezo ya kosa, maelezo ya kosa hilo yataelezwa katika lugha ya kawaida, ambapo matumizi ya lugha ya kiufundi hayatakuwa ya lazima;

(d) endapo kanuni yoyote ya sheria au sheria imeweka mipaka ya maelezo ya kosa ambayo yanahitajika kutolewa katika shtaka au taarifa ya shtaka, hakuna chochote katika aya hii kitakachohitaji maelezo yoyote ya ziada kutolewa kuliko hayo yanayohitajika;

(e) fomu zilizoainishwa katika Jadweli la Pili la Sheria hii au fomu zinazowiyana na hizo kwa kiasi kikubwa kitakachowezekana zitatumika katika mazingira ambayo fomu hizo zinaweza kutumika; na katika mazingira mengine fomu zenye athari kama hizo au zinazowiana na hizo kwa kiasi kikubwa kitakachowezekana zitatumika, maelezo ya kosa na taarifa za kosa zitatofautishwa kwa mujibu wa mazingira ya kila kesi;

(f) endapo hati rasmi ya mashtaka au taarifa ya mashtaka inajumuisha zaidi ya shtaka moja au kosa moja, mashtaka hayo au makosa hayo yatapewa nambari zinazofuatana.

(3) Yafuatayo ni masharti yanayohusiana na makosa yaliyomo katika sheria:

(a) endapo sheria inayotengeneza kosa inaeleza kosa ni kutokutenda tendo lolote mojawapo miongoni mwa matendo tofauti katika njia mbadala, au kutenda au kuacha kutenda tendo lolote katika mojawapo ya miongoni mwa namna tofauti, au pamoja na kusudio moja lolote miongoni mwa makusudio tofauti, au inaeleza sehemu yoyote ya kosa katika njia mbadala, matendo, kuacha kutenda, namna au makusudio, au mambo mengine yaliyoelezwa katika njia mbadala katika sheria, yanaweza kuelezwa katika njia mbadala katika shtaka au kosa linaloshtaki kosa hilo;

(b) haitakuwa lazima, katika shtaka lolote au kosa linaloshtaki kosa lililoundwa kwa sheria, kuikanusha dharura yoyote au msamaha au kigezo kuhusiana na utumikaji wa sheria inayounda kosa hilo.

(4) Maelezo ya mali yatakuwa katika namna ifuatayo:

(a) maelezo ya mali katika shtaka au taarifa ya shtaka yatakuwa katika lugha ya kawaida, na kiasi cha kuonesha kwa uwazi mali iliyokusudiwa, na, ikiwa mali imeelezewa kwa namna hiyo, haitakuwa lazima, isipokuwa endapo itahitajika kwa madhumuni ya kuelezea kosa linalotegemea umiliki maalum wa mali yoyote au thamani maalum ya mali, kutaja jina la mmiliki wa mali hiyo au thamani ya mali.

(b) endapo mali inamilikiwa na mtu zaidi ya mmoja, na wamiliki wa mali wanatajwa katika hati ya shtaka au taarifa ya shtaka, itatosha kuelezea mali kama inamilikiwa na mmoja miongoni mwa watu hao kwa jina pamoja na wengine, na ikiwa watu wanaomiliki mali hiyo ni jumuiya ya watu wenye jina la pamoja, kama vile kampuni ya pamoja ya wenye hisa, au "wakaazi", "wadhamini", au "makamishna", au "klabu" au jina hilo jengine, itatosha kutumia jina la pamoja bila ya kumtaja mtu yeyote;

(c) mali inayomilikiwa na au iliyotolewa kwa ajili ya matumizi ya taasisi ya umma, huduma au idara inaweza kuelezwa kama ni mali ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar;

(d) sarafu na noti za kibenki zinaweza kuelezwa kama ni fedha; na tuhuma yoyote kuhusu fedha, kwa kiasi kinachohusiana na maelezo ya mali, zitasimama kwa uthibitisho wa kiasi chochote cha sarafu au sarafu ya benki yoyote au noti, ijapokuwa aina mahsusi ya sarafu ambazo zimefanya jumla ya kiasi hicho, au maumbile mahsusi ya noti au sarafu hiyo, hayatathibitishwa; na katika kesi za wizi au za

udanganyifu kwa kujifananisha kwa uongo, kwa uthibitisho kwamba mshtakiwa bila ya uaminifu ametumia au amejipatia sarafu au sarafu ya benki au noti, au sehemu yoyote ya thamani yake sarafu hiyo au noti hiyo, ijapokuwa sarafu hiyo au sarafu ya benki au noti inaweza kuwa ilitolewa kwa mtu huyo ili kwamba sehemu ya thamani yake irejeshwe kwa mtu aliyetoa vitu hivyo au kwa mtu mwengine yeyote na sehemu hiyo itakuwa imerejeshwa ipasavyo;

(e) endapo mtu anashtakiwa kwa kosa lolote chini ya kifungu cha 261, 262, 263 au 264 cha Sheria ya Adhabu, ambacho kinahusika na wizi unaofanywa na watu katika utumishi wa umma, makarani, watumishi, wakurugenzi au maafisa wa kampuni, wakala na wenye hati ya uwakala, itatosha kuainisha kiwango cha jumla ambacho kuhusiana na kiwango hicho inadaiwa kosa limetendwa na tarehe ambazo baina ya tarehe hizo kosa linadaiwa limetendwa, bila ya kuainisha vitu mahsusi au tarehe halisi.

(5) Maelezo au wadhifa, katika hati ya mashtaka au taarifa ya mashtaka, ya mshtakiwa, au mtu mwengine yeyote ambaye ametajwa katika hati hiyo utakuwa kwa namna ambayo inatosha kumtambua mtu huyo, bila ya ulazima wa kueleza jina lake sahihi, au pahala anapoishi, mtindo, kiwango, au kazi na kama jina lake halijulikani, au kwa sababu nyengine yoyote, haiwezekani kutoa maelezo hayo au wadhifa huo, maelezo hayo au wadhifa huo utatolewa kama itakavyowezekana katika mazingira hayo, au mtu huyo anaweza kuelezewa kama "mtu asiyejulikana".

(6) Pale ambapo ni lazima kutaja waraka wowote au hati yoyote katika shtaka au taarifa ya shtaka, itatosha kuelezea waraka au hati hiyo kwa jina lolote au wadhifa ambao kwa kawaida waraka huo au wadhifa huo unajulikana, au kwa makusudio hayo, bila ya kuwasilisha nakala yoyote ya waraka huo au hati hiyo.

(7) Kwa kuzingatia masharti mengine yoyote ya kifungu hiki, itatosha kuelezea pahala popote, wakati, kitu, jambo, kitendo au kuacha kutenda kitendo chochote ambacho ni muhimu kukitaja katika hati ya shtaka au taarifa ya shtaka katika lugha ya kawaida katika namna ambayo inaweza kuonesha kwa uwazi unaokubalika pahala hapo, wakati, kitu, jambo, kitendo au kuacha kutenda kulikotajwa.

(8) Haitokuwa lazima katika kueleza nia yoyote ya kudanganya, kuhadaa au kudhuru kuelezea nia ya kumdanganya, kumhadaa au kumdhuru mtu yeyote mahsusi, pale sheria inayounda kosa haikufanya nia ya kumdanganya, kumhadaa au kumdhuru mtu mahsusi kuwa kiini cha lazima cha kosa.

(9) Nambari na ufupisho wa maneno unaweza kutumika kwa ajili ya kuelezea kitu chochote ambacho kikawaida kinaelezewa hivyo.

## Hatia ya Awali au Kuachiwa Huru

Watu hawa-toshtakiwa mara mbili kwa kosa hilo hilo.

**168.** Mtu ambaye alishashtakiwa mara moja katika mahakama yenye mamlaka kwa kosa na akatiwa hatiani au akaachiwa huru kwa kosa hilo, wakati hatia hiyo au kuachiwa huru huko hakujabadilishwa au kuwekwa kando, hatowajibika kushtakiwa tena kwa mambo hayo hayo kwa kosa hilo hilo.

Mtu anaweza kushtakiwa tena kwa kosa jengine.

**169.** Mtu aliyetiwa hatiani au aliyeachiwa huru kwa kosa lolote anaweza baadae kushtakiwa kwa kosa jengine lolote ambalo angeweza kushtakiwa katika kesi iliyopita chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu cha 165 cha Sheria hii.

Matokeo yaliyojitokeza au mahakama ya awali kutokuwa na mamlaka.

**170.**-(1) Mtu aliyetiwa hatiani au aliyeachiwa huru kwa kitendo chochote kilichosababisha matokeo ambayo pamoja na kitendo hicho yanaunda kosa jengine tofauti na lile alilowahi kutiwa hatiani au kuachiwa huru, anaweza baadae kushtakiwa kwa kosa hilo lililotajwa mwisho, ikiwa matokeo hayo yalikuwa hayajatokea au yalikuwa hayajulikani na Mahakama kuwa yametokea wakati alipoachiwa huru au alipotiwa hatiani.

(2) Mtu aliyetiwa hatiani au aliyeachiwa huru kwa kosa linaloundwa na vitendo vyovyote anaweza, bila ya kujali kutiwa hatiani huko au kuachiwa huru huko, baadae kushtakiwa kwa kosa jengine lolote linaloundwa na vitendo hivyo hivyo ambavyo anaweza kuwa amevitenda, ikiwa mahakama ambayo imesikiliza kesi ya mtu huyo mara ya kwanza haikuwa na mamlaka kusikiliza kesi hiyo ambayo mtu huyo anashtakiwa baadae.

Utaratibu wa kuthibitisha hatia ya awali.

**171.**-(1) Katika uchunguzi wowote, usikilizaji wa kesi au mwenendo mwengine chini ya Sheria hii, hatia ya awali inaweza kuthibitishwa, pamoja na utaratibu mwengine wowote ulioelezwa na sheria nyengine yoyote inayotumika kwa wakati huo:

(a) kwa sehemu tu ya maelezo yaliyothibitishwa, na afisa mwenye dhamana ya uhifadhi wa kumbukumbu za mahakama ambayo ilimtia hatiani mtu huyo, kuwa nakala ya adhabu au amri; au

(b) kwa hati iliyosainiwa na afisa dhamana wa Chuo cha Mafunzo ambacho adhabu hiyo au sehemu ya adhabu hiyo ilitekelezwa, au kwa kuwasilisha hati ya kupelekwa Chuo cha Mafunzo ambapo chini ya hati hiyo adhabu ilitumikiwa,

pamoja na, katika kila kesi hizo, ushahidi kwa ajili ya utambulisho wa mshtakiwa pamoja na utambulisho wa mtu huyo aliyetiwa hatiani.

(2) Hati katika muundo ulioelezwa na Jaji Mkuu iliyotolewa na afisa aliyeteuliwa na Kamishna wa Polisi kwa ajili hiyo, ambaye atakuwa amelinganisha alama za vidole vya mshtakiwa pamoja na alama za vidole za mtu aliyetiwa hatiani awali, itakuwa ni ushahidi wa awali wa mambo yote yaliyomo ndani humo ikiwa unawasilishwa na mtu ambaye alichukua alama za vidole za mshtakiwa.

(3) Hatia ya awali ya pahala popote nje ya Zanzibar inaweza kuthibitishwa kwa kuwasilisha hati inayodaiwa kutolewa na afisa wa polisi wa nchi ambayo hatia ya awali ilipatikana, ikijumuisha nakala ya adhabu au amri na alama za vidole, au picha za alama za vidole za mtu huyo aliyetiwa hatiani, pamoja na ushahidi kwamba alama hizo za vidole za mtu huyo aliyetiwa hatiani ndio zile za mshtakiwa.

(4) Hati hiyo kama ilivyoelezwa awali itakuwa ni ushahidi wa awali wa mambo yote yaliyoelezwa ndani humo bila ya uthibitisho kwamba afisa huyo anayedaiwa kusaini kwa hakika alisaini hati hiyo na alikuwa na mamlaka ya kufanya hivyo.

## Usikilizaji wa Kesi kwa Haraka na Umalizaji wa Kesi

Usikilizaji wa awali kuamua mambo ambayo hayabishaniwi.

**172.**-(1) Bila ya kujali masharti ya kifungu cha 214 (1) cha Sheria hii, ikiwa mshtakiwa ambaye anawakilishwa kisheria anakataa kosa, mahakama haraka iwezekanavyo itafanya usikilizaji wa awali katika mahakama ya wazi mbele ya mshtakiwa na wakili wake na mbele ya mwendesha mashtaka wa Serikali kwa ajili ya kuzingatia mambo ambayo hayabishaniwi baina ya wahusika wa kesi na ambayo yatasaidia uendeshaji wa kesi kwa njia ya haki na ya haraka.

(2) Katika kuamua mambo hayo ambayo hayabishaniwi mahakama inaweza kuwauliza maswali wahusika katika kesi kama itakavyoona inafaa na majibu yanaweza kutolewa bila ya kiapo au uthibitisho.

(3) Wakati wa kuhitimisha usikilizaji wa awali uliofanywa chini ya kifungu hiki, mahakama itaandaa randama ya mambo yaliyokubaliwa na randama hiyo itasomwa na itafafanuliwa kwa mshtakiwa katika lugha ambayo anaifahamu, itasainiwa na mshtakiwa na wakili wake na muendesha mashtaka wa Serikali na baadae itahifadhiwa katika jalada.

(4) Jambo lolote au waraka wowote uliopokelewa au uliokubaliwa, ama jambo hilo au waraka huo umetajwa katika muhtasari wa ushahidi au haujatajwa, katika randama iliyohifadhiwa kwenye jalada chini ya kifungu hiki, litachukuliwa au utachukuliwa kuwa umethibitishwa ipasavyo isipokuwa kwamba ikiwa, wakati wa usikilizaji mahakama itaona kwamba, maslahi ya haki yanahitaji hivyo, mahakama inaweza kuelekeza kwamba jambo lolote au waraka wowote uliopokelewa au kukubaliwa katika randama iliyohifadhiwa kwenye jalada chini ya kifungu hiki ithibitishwe rasmi.

(5) Pale ambapo inawezekana mshtakiwa atashtakiwa mara moja baada ya usikilizaji wa awali na ikiwa kesi itaahirishwa kutokana na kutokuwepo shahidi au kutokana na sababu nyengine yoyote, hakuna chochote katika kifungu hiki kitakachotafsiriwa kuwa kinamtaka Jaji huyo au hakimu huyo aliyefanya usikilizaji wa awali chini ya kifungu hiki kuongoza usikilizaji wa kesi hiyo.

(6) Jaji Mkuu anaweza kwa amri itakayochapishwa katika Gazeti la Serikali kutengeneza kanuni kwa ajili ya utekelezaji mzuri wa makusudio ya kifungu hiki na bila ya kuathiri maelezo ya jumla yaliyotangulia, kanuni hizo zinaweza kueleza:

(a) ucheleweshaji wa kuwaita mashahidi mpaka itakapoamuliwa ama wanahitajika kutoa ushahidi katika kesi au hawahitajiki; au

(b) utoaji wa notisi kwa shahidi inayowatahadharisha mashahidi kwamba wanaweza wakatakiwa kufika mahakamani kutoa ushahidi katika kesi.

(7) Katika kifungu hiki, utaratibu au njia inakusudia kuharakisha usikilizaji na umalizaji wa mwenendo wa mashauri ya jinai.

**Kulazimisha Mahudhurio ya Mashahidi**

Wito kwa shahidi.

**173.**-(1) Ikiwa itaonekana kwamba ushahidi muhimu unaweza kutolewa na au upo mikononi mwa mtu yeyote ambaye hatohudhuria kwa hiyari yake kutoa ushahidi au hatouleta kwa hiyari yake ushahidi huo, itakuwa ni halali kwa mahakama yenye uwezo wa kutambua kesi yoyote ya jinai au jambo kutoa wito kwa mtu huyo kumtaka ahudhurie mbele ya mahakama hiyo au kumtaka mtu huyo kuleta na kuwasilisha katika mahakama hiyo kwa ajili ya ushahidi nyaraka zote na vitu vyengine vya aina yoyote ile vilivyo mikononi mwake au kwenye mamlaka yake ambavyo vinaweza kuainishwa au vyenginevyo kuelezewa ipasavyo katika wito.

(2) Hakuna kitu chochote katika kifungu hiki kitakachochukuliwa kuathiri masharti ya Sheria ya Ushahidi yanayohusika na ushahidi kuhusu mambo ya Serikali au mawasiliano rasmi.

Hati ya ukamataji kwa shahidi asiyetii wito.

**174.** Iwapo, bila ya sababu ya msingi, shahidi hajafika mahakamani baada ya kupata wito, mahakama, kwa ushahidi unaoonesha kuwa wito ulipelekwa ipasavyo na kwa wakati muafaka kabla, inaweza kutoa hati ya ukamataji kumleta shahidi huyo mbele ya mahakama katika wakati na pahala patakapoainishwa ndani ya hati hiyo.

Hati ya ukamataji kwa shahidi mara ya kwanza.

**175.** Ikiwa mahakama itaridhika kwa ushahidi uliotolewa kwa njia ya kiapo kwamba mtu huyo hatofika hadi alazimishwe kufanya hivyo, inaweza mara moja kutoa hati ya kumkamata na kumleta shahidi huyo mbele ya mahakama katika wakati na pahala patakapoainishwa ndani ya hati hiyo.

Namna ya kumshughulikia shahidi atakapokamatwa.

**176.** Pale shahidi anakamatwa chini ya hati ya ukamataji mahakama inaweza, atakapoweka dhamana kwa ahadi ya dhamana kwa kuiridhisha mahakama kwa ajili ya kufika kwake katika usikilizaji wa kesi, kuamuru mtu huyo aachiwe kutoka kizuizini, au atakaposhindwa kuweka dhamana hiyo, kuamuru mtu huyo kuwekwa kizuizini kwa ajili ya kuletwa katika usikilizaji huo wa kesi.

Uwezo wa kuamrisha uletwaji wa mwanafunzi wa Chuo cha Mafunzo kama shahidi.

**177.**-(1) Mahakama inayotaka kumhoji kama shahidi, katika kesi yoyote iliyopo mbele yake, mtu yeyote aliyezuiliwa katika Chuo cha Mafunzo chochote ndani ya eneo la mipaka ya mamlaka ya mahakama inaweza kutoa amri kwa afisa mwenye dhamana wa Chuo cha Mafunzo hicho kumtaka afisa huyo kumleta mwanafunzi huyo katika hifadhi inayofaa, katika wakati utakaotajwa ndani ya amri hiyo, mbele ya mahakama kwa ajili ya kumhoji.

(2) Afisa huyo mwenye dhamana, atakapopokea amri hiyo, atatekeleza kama ilivyo kwa mujibu wa amri hiyo na atampatia mwanafunzi huyo hifadhi salama wakati hayupo Chuo cha Mafunzo kwa madhumuni yaliyoelezwa.

Adhabu kwa kutokuhudhuria kama shahidi.

**178.**-(1) Mtu aliyeitwa kufika kama shahidi ambaye, bila ya sababu ya msingi, anashindwa kufika kama alivyotakiwa na wito, au ambaye, ameshafika, anaondoka bila ya kupata ruhusa ya mahakama, au anashindwa kufika baada ya mahakama kuakhirisha baada ya kuamrishwa kuhudhuria, atatozwa faini isiyozidi Shilingi Laki Tano.

(2) Faini hiyo itatozwa kwa kukamata na kuuza mali yoyote inayohamishika inayomilikiwa na shahidi huyo ndani ya eneo la mipaka ya mamlaka ya mahakama hiyo.

(3) Ikishindikana kupatikana faini hiyo kwa njia ya ukamataji na kuuza shahidi anaweza, kwa amri ya mahakama, kufungwa kama mfungwa wa madai kwa kipindi cha siku kumi na tano isipokuwa kama faini hiyo inalipwa kabla ya kumalizika kwa kipindi hicho kilichotajwa.

(4) Kwa sababu za msingi zitakazotolewa, Mahakama Kuu inaweza kurudisha au kupunguza faini yoyote iliyotozwa chini ya kifungu hiki na mahakama ya chini.

**Kuwahoji Mashahidi**

Uwezo wa mahakama kuhoji na kuhoji tena.

**179.** Mahakama inaweza, katika hatua yoyote ya uchunguzi wowote, usikilizaji kesi au mwenendo wowote wa kesi chini ya Sheria hii kumwita mtu yeyote kama shahidi, au inaweza kumwita tena na kumuhoji tena mtu yeyote aliyekwisha kuhojiwa; na mahakama itamuhoji au itamwita tena na kumhoji tena mtu huyo yeyote ikiwa ushahidi wake unaonekana kuwa ni muhimu katika kufikia uamuzi wa haki wa kesi hiyo.

Ushahidi utatolewa kwa kiapo.

**180.**-(1) Shahidi katika shauri lolote la jinai au jambo atahojiwa kwa kiapo au uthibitisho, na mahakama ambayo mbele yake shahidi yeyote atafika itakuwa na uwezo kamili na mamlaka kusimamia kiapo cha kawaida au uthibitisho.

(2) Mahakama inaweza, katika wakati wowote itakapoona inafaa na kwa haraka na kwa sababu zitakazorikodiwa katika mwenendo wa shauri, kuchukua bila ya kiapo ushahidi wa mtu atakayetamka kwamba kula kiapo chochote kwa mujibu wa imani yake ya dini haifai, au ambaye kwa sababu ya umri mdogo au kwa kuwa hana dini, kwa maoni ya mahakama, hapaswi kuruhusiwa kutoa ushahidi kwa kiapo; ukweli wa kuwa ushahidi umechukuliwa bila ya kiapo pia utarekodiwa kwenye mwenendo wa kesi.

Mashahidi wakaidi.

**181.**-(1) Wakati wowote mtu, anayefika mahakamani kwa kutii wito au kwa sababu ya hati ya ukamataji, au akiwa yupo mahakamani na akatakiwa kwa mdomo na mahakama kutoa ushahidi:

(a) anakataa kuapishwa;

(b) ameapishwa, anakataa kujibu swali lolote analoulizwa;

(c) anakataa au anapuuza kuwasilisha waraka wowote au kitu ambacho ametakiwa kukiwasilisha; au

(d) anakataa kusaini maelezo yake ya ushahidi, bila katika mazingira hayo yoyote, kutoa sababu ya msingi ya kukataa huko au kupuuza huko,

mahakama inaweza kuakhirisha kesi hiyo kwa kipindi kisichozidi siku nane, na inaweza katika kipindi hicho kumpeleka mtu huyo Chuo cha Mafunzo, isipokuwa kama atakubali haraka kufanya kile alichotakiwa kukifanya.

(2) Ikiwa mtu huyo, baada ya kuletwa mbele ya mahakama wakati au kabla ya kuakhirishwa usikilizaji huo wa kesi, kwa mara nyengine anakataa kufanya kile alichotakiwa kukifanya, mahakama inaweza, kama inaona inafaa, kwa mara nyengine kuakhirisha kesi na kumpeleka mtu huyo Chuo cha Mafunzo kwa kipindi kama kile, na vile vile tena kila baada ya muda mpaka mtu huyo akubali kufanya kile anachotakiwa kukifanya.

(3) Hakuna sharti lolote lililomo katika kifungu hiki litakaloathiri uwajibikaji wa mtu huyo yeyote kwa adhabu nyengine yoyote au mwenendo wa shauri kwa kukataa au kwa kupuuza kufanya kile alichotakiwa kukifanya, au litakaloizuia mahakama kuimaliza kesi hiyo katika wakati huo kwa mujibu wa ushahidi mwengine wowote unaofaa uliowasilishwa mbele yake.

Ushahidi wa mume au mke wa mshtakiwa.

**182.** Katika uchunguzi wowote au usikilizaji wa kesi mke au mume wa mtu anayeshtakiwa atafaa kuwa shahidi wa upande wa mashtaka au utetezi bila ya ridhaa ya mke au mume huyo.

Hatua maalum kwa mashahidi wenye mazingira magumu au mashahidi wanaotishwa.

**183.**-(1) Mhusika katika kesi, anayehusiana na shahidi, atatoa notisi kwa mahakama kwamba anakusudia kutumia hatua maalum zinazohusiana na mashahidi wenye mazingira magumu au mashahidi wanaotishwa.

(2) Mahakama, baada ya kupewa notisi chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, itahakikisha kwamba matayarisho husika yanafanywa katika sehemu ambayo mahakama inaona kwamba mwenendo wa shauri utaendeshwa hapo.

## Kutoa Maelekezo kwa ajili ya Kuwahoji Mashahidi

Utoaji wa maelekezo kwa ajili ya kuwahoji mashahidi.

**184.**-(1) Wakati wowote katika mwenendo wowote wa kesi chini ya Sheria hii, Mahakama Kuu au hakimu mwenye dhamana ya kuongoza mahakama ya chini anaridhika kwamba mahojiano ya shahidi ni muhimu kwa ajili ya kufikia haki, na kwamba mahudhurio ya shahidi huyo hayawezekani bila ya kuwepo ucheleweshaji, gharama au usumbufu ambao, katika mazingira hayo ya kesi, ingekuwa siyo busara, mahakama au hakimu anaweza kutoa maelekezo kwa hakimu mwengine yeyote ambaye ndani ya eneo la mipaka ya mamlaka yake shahidi huyo anaishi, kuchukua ushahidi wa shahidi huyo.

(2) Hakimu ambaye kwake yeye maelekezo yametolewa atakwenda katika pahala ambapo shahidi huyo yupo au atamwita shahidi huyo mbele yake, na atachukua ushahidi wake katika namna ile ile, na anaweza kwa madhumuni hayo kutumia mamlaka yale yale, kama katika usikilizaji wa kesi hiyo.

Wahusika wa kesi wanaweza kuwahoji mashahidi.

**185.**-(1) Wahusika wa mwenendo wa kesi yoyote chini ya Sheria hii, ambapo maelekezo ya kuchukua ushahidi yametolewa wanaweza kupeleka maswali yoyote kwa maandishi ambayo Mahakama au Hakimu aliyeelekeza kuchukuliwa ushahidi anaweza kuona yanafaa katika shauri hilo, na Hakimu ambaye amepewa maelekezo ya kuchukua ushahidi atamuhoji shahidi kuhusiana na maswali hayo yaliyoletwa.

(2) Mhusika huyo yeyote anaweza kufika mbele ya Hakimu huyo kwa kutumia Wakili wake, au ikiwa hayupo kizuizini, atafika yeye mwenyewe binafsi, na anaweza kumhoji shahidi huyo, kufanya mahojiano kinzani na kumhoji tena, kama hali itakavyokuwa.

Uwezo wa hakimu kuomba kutolewa maelekezo ya kuchukua ushahidi.

**186.** Wakati wowote katika mwenendo wowote wa kesi chini ya Sheria hii mbele ya Hakimu yeyote, inaonekana kwamba maelekezo ya kuchukua ushahidi yanapaswa kutolewa kwa ajili ya kumhoji shahidi ambaye ushahidi wake ni muhimu kwa ajili ya kufikia haki, na kwamba mahudhurio ya shahidi huyo hayawezekani bila ya kuwepo ucheleweshaji, gharama au usumbufu ambao, katika mazingira hayo ya kesi, ingekuwa siyo busara, Hakimu huyo ataomba katika Mahakama Kuu, akieleza sababu za ombi hilo; na Mahakama Kuu ama itatoa maelekezo ya kuchukuliwa ushahidi kwa namna iliyoelezwa kabla au italikataa ombi hilo.

Marejesho ya maelekezo ya kuchukua ushahidi.

**187.**-(1) Baada ya maelekezo ya kuchukua ushahidi yaliyotolewa chini ya kifungu cha 184 au 186 cha Sheria hii kuwa yametekelezwa ipasavyo yatarejeshwa, pamoja na maelezo ya ushahidi wa shahidi aliyehojiwa kwa maelekezo hayo, katika Mahakama Kuu, au kwa Hakimu wa Mkoa, kama hali itakavyokuwa, na maelekezo hayo ya kuchukua ushahidi, marejesho yake, na maelezo ya shahidi yatakuwa wazi katika kipindi chote muafaka kwa ajili ya ukaguzi wa wahusika wa kesi, na yanaweza, kwa kuzingatia dharura zinazokubalika, kusomwa katika ushahidi kwenye kesi na mhusika yeyote wa kesi, na yatakuwa ni sehemu ya kumbukumbu za kesi.

(2) Maelezo ya shahidi yaliyochukuliwa kwa utaratibu huo, ikiwa yatatosheleza masharti yaliyoainishwa katika kifungu cha 36 cha Sheria ya Ushahidi, yanaweza pia kupokelewa katika ushahidi katika hatua yoyote ya baadae ya kesi hiyo mbele ya mahakama nyengine.

Kuakhirisha kesi kusubiri marejesho ya maelekezo ya kuchukua ushahidi.

**188.** Katika kesi yoyote ambayo maelekezo ya kuchukua ushahidi yametolewa chini ya kifungu cha 184 au 186 cha Sheria hii, mwenendo wa shauri unaweza kuakhirishwa kwa muda utakaoainishwa kwa kiasi cha kutosha kwa ajili ya utekelezaji wa maelekezo na marejesho ya maelekezo ya kuchukua ushahidi.

## Ushahidi kwa Ajili ya Utetezi

Kufaa kwa mshtakiwa na kufaa kwa mume au mke kutoa ushahidi.

**189.** Mtu anayeshtakiwa kwa kosa lolote, na mke au mume, kama hali itakavyokuwa, wa mtu huyo anayeshtakiwa, atakuwa anafaa kuwa shahidi kwa ajili ya utetezi katika kila hatua ya mwenendo wa shauri, ama mtu huyo anayeshtakiwa anashtakiwa peke yake au anashtakiwa pamoja na mtu mwengine yeyote, ikiwa itakuwa kama ifuatavyo:

(a) mtu huyo anayeshtakiwa hatoitwa kama shahidi kwa mujibu wa kifungu hiki isipokuwa kwa ombi lake yeye mwenyewe;

(b) kushindwa kwa mtu anayeshtakiwa kwa kosa, au kwa mke au mume, kama hali itakavyokuwa, wa mtu huyo anayeshtakiwa, kutoa ushahidi hakutokuwa jambo ambalo upande wa mashtaka unaweza kutoa maoni;

(c) mke au mume wa mtu anayeshtakiwa, ispokuwa kama ilivyoelezwa kabla, hatoitwa kama shahidi isipokuwa kwa ombi la mtu huyo anayeshtakiwa;

(d) hakuna chochote katika kifungu hiki kitakachomfanya mume alazimike kuweka bayana mawasiliano yoyote yaliyofanywa kwake yeye na mke wake wakati wa ndoa, au mke alazimike kuweka bayana mawasiliano yoyote yaliyofanywa kwake na mume wake wakati wa ndoa;

(e) mtu anayeshtakiwa na akawa shahidi kwa mujibu wa kifungu hiki anaweza kuulizwa swali lolote katika mahojiano kinzani bila ya kujali kwamba swali hilo litapelekea yeye kuhusishwa na kosa analoshtakiwa nalo;

(f) mtu anayeshtakiwa na akaitwa kama shahidi kwa mujibu wa kifungu hiki hatoulizwa, na ikiwa ataulizwa hatotakiwa kujibu, swali lolote linalopelekea kuonesha kwamba ameshatenda kosa au ameshatiwa hatiani, au ameshashtakiwa kwa kosa lolote lisilokuwa hilo ambalo wakati huo anashtakiwa nalo, au ni mwenye tabia mbaya, isipokuwa:

(i) uthibitisho kwamba mtu huyo ametenda kosa au amekwishatiwa hatiani kwa kosa hilo jengine ni ushahidi unaokubalika kuonesha kwamba mtu huyo ni mkosa wa kosa ambalo wakati huo anashtakiwa nalo;

(ii) yeye mwenyewe binafsi au kwa kupitia wakili wake aliwauliza maswali mashahidi wa upande wa mashtaka kwa dhamira ya kuonesha kuwa yeye ana tabia nzuri, au ametoa ushahidi wa tabia yake nzuri, au uhalisia au matendo ya utetezi yanahusisha tuhuma kuhusu tabia ya mlalamikaji au mashahidi wa upande wa mashtaka; au

(iii) ametoa ushahidi dhidi ya mtu mwengine yeyote anayeshtakiwa pamoja naye kwa kosa hilo hilo;

(g) mtu anayeitwa kama shahidi kwa mujibu wa kifungu hiki, isipokuwa kama ataamrishwa vyenginevyo na mahakama, atatoa ushahidi wake kutoka kwenye kizimba cha shahidi au pahala pengine ambapo mashahidi wengine wametoa ushahidi wao;

(h) hakuna chochote katika kifungu hiki kitakachoathiri haki ya mtu anayeshtakiwa kutoa maelezo bila ya kula kiapo.

Pale mshtakiwa anapokusudia kutegemea utetezi wa kutokuwepo kwenye eneo la tukio.

**190.**-(1) Endapo mshtakiwa anakusudia kutegemea ushahidi wa kutokuwepo kwenye eneo la tukio katika utetezi wake atatoa notisi kwa mahakama na kwa mwendesha mashtaka kuhusu nia yake ya kutegemea ushahidi huo kabla ya kusikilizwa kwa kesi.

(2) Endapo mshtakiwa hatatoa notisi kuhusu nia yake ya kutegemea ushahidi wa kutokuwepo kwenye eneo la tukio katika utetezi wake kabla ya usikilizwaji wa kesi, atawasilisha kwa upande wa mashtaka maelezo mahsusi ya ushahidi wa kutokuwepo kwenye eneo la tukio wakati wowote kabla ya upande wa mashtaka haujafunga ushahidi wake.

(3) Ikiwa mshtakiwa anatoa utetezi wa ushahidi wa kutokuwepo eneo la tukio bila ya kuwasilisha awali mahakamani au kwa mwendesha mashtaka maelezo mahsusi ya utetezi wa ushahidi wa kutokuwepo eneo la tukio kwa mujibu wa kifungu hiki, mahakama inaweza kwa uwezo wake kutoupa uzito wa aina yoyote utetezi huo.

Utaratibu pale mshtakiwa ni shahidi pekee anayeitwa.

**191.** Pale shahidi pekee wa maelezo ya kesi anayeitwa na upande wa utetezi ni mtu anayeshtakiwa, ataitwa kama shahidi mara tu baada ya kufungwa ushahidi wa upande wa mashtaka.

Haki ya kujibu.

**192.**-(1) katika mazingira ambapo haki ya kujibu inategemea suala la ama ushahidi umeletwa kwa ajili ya utetezi, ukweli kwamba mtu anayeshtakiwa ameitwa kama shahidi haututoa kwa upande wa mashtaka haki ya kujibu.

(2) Mkurugenzi wa Mashtaka au wakili wa Serikali wakati anapofika mahakamani yeye mwenyewe kama wakili wa upande wa mashtaka katika kesi zote atakuwa na haki ya kujibu.

## Utaratibu katika Kesi zinazohusu Mshtakiwa kutokuwa na Uwezo wa Akili au Uwezo Mwengine

Uchunguzi kuhusu hali ya akili ya mshtakiwa.

**193.**-(1) Pale wakati wa usikilizaji kesi, mahakama ina sababu za kuamini kwamba mshtakiwa hana akili timamu na matokeo yake hawezi kujitetea, itachunguza jambo hilo la kutokuwa na akili timamu.

(2) Ikiwa mahakama ina maoni kwamba mshtakiwa hana akili timamu na matokeo yake hawezi kujitetea, itaakhirisha kuendelea zaidi na kesi hiyo.

(3) Ikiwa kesi ni moja miongoni mwa zile amabazo mahakama inaweza kutoa dhamana, mahakama inaweza kumuachia mshtakiwa baada ya kuwekwa dhamana inayotosha kwamba mtu huyo atapewa uangalizi unaofaa na atazuiwa kufanya madhara kwake mwenyewe au kwa mtu mwengine yeyote, na kwa kufika kwake mbele ya mahakama au mbele ya afisa kama mahakama itakavyomteua kwa niaba yake.

(4) Ikiwa kesi ni moja miongoni mwa zile ambazo mahakama haiwezi kutoa dhamana au ikiwa dhamana inayotosha haijatolewa, mahakama itaamuru mshtakiwa awekwe kwenye hifadhi salama katika pahala ambapo na kwa namna ambayo kama itakavyoona inafaa na itahamisha rekodi za mahakama au nakala zilizothibitishwa za rekodi hizo kwa Mwenyekiti wa Bodi ya Afya ya Akili kwa ajili ya mazingatio ya Bodi.

(5) Baada ya kuzingatia rekodi za mahakama na baada ya kufanya uchunguzi wake yenyewe kuhusu jambo hilo, Bodi itaishauri mahakama juu ya uamuzi unaofaa kuchukuliwa na mahakama inaweza kumzuia au vyenginevyo kumshughulikia mshtakiwa kama itakavyoona inafaa mpaka wakati huo ambapo mahakama itaamuru mshtakiwa aletwe tena mbele yake katika namna iliyoelezwa na vifungu 194 na 195 vya Sheria hii.

Utaratibu pale mtu anapothibitishwa kuwa anaweza kujitetea.

**194.**-(1) Ikiwa mtu amezuiwa katika hospitali ya akili au pahala pengine pa hifadhi chini ya kifungu cha 193 cha Sheria hii anagundulika na daktari mwenye dhamana wa hospitali hiyo au pahala kuwa anaweza kujitetea, daktari huyo atapeleka mara moja hati inayoeleza hayo kwa Mkurugenzi wa Mashtaka.

(2) Mkurugenzi wa Mashtaka baadae ataiarifu mahakama ambayo ilirekodi kilichogundulika dhidi ya mtu huyo ama ni nia ya Mkurugenzi wa Mashtaka kwamba mwenendo wa shauri dhidi ya mtu huyo uendelee au vyenginevyo.

(3) Endapo ataona mwenendo wa kesi uendelee mahakama hiyo itaamuru kuondolewa mtu huyo kutoka pahala ambapo anazuiwa na itawezesha mtu huyo kuletwa katika kizuizi mbele yake kwa namna iliyoelezwa na kifungu cha 195 cha Sheria hii; vyenginevyo, mahakama haraka iwezekanavyo itatoa amri kwa ajili ya kuachiwa mara moja mtu huyo kutoka katika kizuizi.

Kuanza tena usikilizaji wa kesi au uchunguzi.

**195.**-(1) Wakati wowote ambapo usikilizaji wa kesi yoyote umeakhirishwa chini ya kifungu cha 193 cha Sheria hii, mahakama inaweza wakati wowote, kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 194 cha Sheria hii, kuanza tena usikilizaji wa kesi na kumtaka mshtakiwa kufika au kuletwa mbele ya mahakama hiyo, pale iwapo mahakama itamuona mtu huyo kuwa anaweza kujitetea, usikilizaji wa kesi utaendelea, au utaanza upya, kama mahakama itakavyoona inafaa.

(2) Ikiwa mahakama itaona mshtakiwa kuwa bado hawezi kujitetea mwenyewe, itafanya kama kwamba mshtakiwa ameletwa mbele yake kwa mara ya kwanza.

(3) Hati yoyote aliyopewa Mkurugenzi wa Mashtaka chini ya kifungu cha 194 cha Sheria hii inaweza kutolewa katika ushahidi katika mwenendo wa shauri chini ya kifungu hiki bila ya kuhitaji uthibitisho wa ziada isipokuwa kama itathibitika kwamba daktari anaedaiwa kusaini hati hiyo kwa hakika hakusaini hati hiyo.

Utetezi wa kutokuwa na akili timamu.

**196.**-(1) Endapo kutenda au kuacha kutenda kunashtakiwa dhidi ya mtu yeyote kama ni kosa na inatolewa kwenye ushahidi katika usikilizaji wa kesi ya mtu huyo kwa kosa hilo kwamba mtu huyo alikuwa hana akili timamu, kiasi cha kutokuwajibika kwa vitendo vyake hivyo wakati pale kitendo kilipotendwa au kuacha kutenda kumefanyika, baadae, ikiwa itaonekana na mahakama ambayo mbele yake mtu huyo kesi yake inasikilizwa kwamba alitenda kitendo au aliacha kutenda kunakoshtakiwa lakini alikuwa hana akili timamu kama ilivyoelezwa awali wakati pale alipotenda au alipoacha kutenda, mahakama itatoa uamuzi maalum kwamba mshtakiwa alikuwa ni mkosa wa kitendo au kuacha kutenda kunakoshtakiwa lakini alikuwa hana akili timamu kama ilivyoelezwa awali wakati alipotenda kitendo au alipoacha kutenda.

(2) Pale uamuzi huo maalum unapotolewa, mahakama itatoa taarifa ya kesi hiyo kwa ajili ya kupata amri ya Rais, na kwa wakati huo itaamuru mshtakiwa awekwe kwenye hifadhi kama mtu aliyetiwa hatiani asiyekuwa na akili timamu katika pahala ambapo na katika namna ambayo kama mahakama itakavyoelekeza.

(3) Rais anaweza kuamuru mtu huyo azuiwe katika hospitali ya akili, Chuo cha Mafunzo au pahala pengine panapofaa pa hifadhi salama.

(4) Muangalizi wa hospitali ya akili, Chuo cha Mafunzo au pahala pengine ambapo mtu yeyote aliyetiwa hatiani asiyekuwa na akili timamu anazuiwa kwa amri ya Rais chini ya kifungu kidogo cha (3) cha kifungu hiki, atatayarisha taarifa kwa Katibu Mkuu Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuhusu hali, historia na mazingira ya kila mtu huyo aliyetiwa hatiani asiyekuwa na akili timamu baada ya kumalizika kwa kipindi cha miaka mitatu tokea tarehe ya amri ya Rais na baada ya hapo baada ya kumalizika kwa vipindi vya miaka miwili kutoka tarehe ya taarifa ya mwisho.

(5) Baada ya kuzingatia taarifa hiyo yoyote Rais anaweza kuamuru kwamba mtu aliyetiwa hatiani asiye na akili timamu aachiwe ama moja kwa moja au kwa masharti yanayohusu kipindi cha kuachiwa huko na vyenginevyo kama Rais atakavyoweza kuamuru.

(6) Bila ya kujali masharti ya vifungu vidogo vya (4) na (5) vya kifungu hiki, Kamishna wa Chuo cha Mafunzo au Mkurugenzi wa Huduma za Tiba anaweza, wakati wowote baada ya mtu aliyetiwa hatiani asiyekuwa na akili timamu kuwa amezuiwa katika pahala popote kwa amri ya Rais, kutayarisha taarifa maalum kwa Katibu Mkuu Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuhusu hali, mazingira na historia ya mtu huyo aliyetiwa hatiani asiyekuwa na akili timamu, na Rais, baada ya kuzingatia taarifa hiyo yoyote, anaweza kuamuru kwamba mtu aliyetiwa hatiani asiyekuwa na akili timamu aachiwe huru ama moja kwa moja au kwa masharti yanayohusu kipindi cha kuachiwa huko na vyenginevyo kama Rais atakavyoweza kuamuru.

(7) Rais anaweza wakati wowote kuamuru kwamba mtu aliyetiwa hatiani asiye na akili timamu ahamishwe kutoka katika hospitali ya akili kupelekwa Chuo cha Mafunzo, au kutoka Chuo cha Mafunzo kupelekwa hospitali ya akili, au kutoka pahala popote ambapo mtu huyo anazuiliwa kupelekwa ama Chuo cha Mafunzo au hospitali ya akili.

Utaratibu pale mshtakiwa hafahamu mwenendo wa kesi.

**197.** Ikiwa mshtakiwa, ingawa siyo mgonjwa wa akili, hawezi kufahamu mwenendo wa kesi, mahakama inaweza kuendelea na usikilizaji wa kesi; na, katika mazingira ambayo Mahakama hiyo siyo Mahakama Kuu iwapo usikilizaji wa kesi hiyo utapelekea katika hatia, mwenendo wa kesi utapelekwa Mahakama Kuu pamoja na taarifa ya mazingira hayo, na Mahakama Kuu itatoa kutokana na mazingira hayo amri kama itakavyoona inafaa.

**Haki ya Mshtakiwa Kupata Utetezi**

Haki ya mshtakiwa kupata utetezi.

**198.** Ikiwa hakuna sharti lolote katika Sheria nyengine yoyote kinyume na Sheria hii, mtu anayeshtakiwa mbele ya mahakama yoyote ya jinai, au dhidi yake mwenendo wa kesi umeanzishwa chini ya Sheria hii, katika Mahakama yoyote hiyo atakuwa na haki ya kutetewa na Wakili.

Msaada wa kisheria kwa mshtakiwa kwa gharama za Serikali katika baadhi ya kesi.

**199.** Endapo katika usikilizaji wa kesi yoyote inayohusisha adhabu ya kifo, mshtakiwa hawakilishwi na wakili, na pale inapoonekana na Mahakama Kuu kwamba mshtakiwa hana uwezo wa kutosha kuajiri Wakili, Mahakama inaweza kumteua Wakili kwa ajili ya utetezi wake kwa gharama za Serikali.

## SEHEMU YA NANE
## UTARATIBU WA KUCHUKUA NA KUREKODI USHAHIDI KATIKA UCHUNGUZI NA USIKILIZAJI WA KESI

**Masharti ya Jumla**

Ushahidi utachukuliwa mbele ya mshtakiwa.

**200.** Isipokuwa kama imeelezwa vyenginevyo wazi wazi, ushahidi wote unaochukuliwa katika uchunguzi wowote au usikilizaji wa kesi chini ya Sheria hii utachukuliwa mbele ya mshtakiwa, au, pale uhudhuriaji wake umesamehewa, mbele ya Wakili wake.

**Mahakama za Chini**

Namna ya kurekodi ushahidi mbele ya hakimu.

**201.**-(1) Katika uchunguzi na usikilizaji wa kesi, kwa au mbele ya hakimu, ushahidi wa mashahidi utalazimika kurekodiwa katika namna ifuatayo:

(a) ushahidi wa kila shahidi utalazimika kuchukuliwa kwa maandishi katika lugha ya mahakama na hakimu, au mbele yake na akiwa anasikia na chini ya maelekezo yake yeye mwenyewe na usimamizi wake, na utalazimika kusainiwa na hakimu, na utakuwa ni sehemu ya kumbukumbu;

(b) ushahidi huo kwa kawaida hautachukuliwa katika muundo wa maswali na majibu, lakini katika muundo wa maelezo, isipokuwa kwamba hakimu anaweza, kwa uwezo wake, kuandika au kuwezesha kuandikwa swali lolote mahsusi na jawabu.

(2) Hakimu atamuarifu kila shahidi kwamba ana haki ya kusomewa ushahidi wake alioutoa.

(3) Ikiwa shahidi ataomba asomewe ushahidi wake hakimu atawezesha ushahidi huo kusomwa kwa shahidi huyo kwa lugha ambayo anaifahamu.

(4) Mahakama inaweza kurekodi ushahidi kwa kutumia kifaa chochote cha kielektroniki.

Tafsiri ya ushahidi kwa mshtakiwa au wakili wake.

**202.**-(1) Wakati wowote ushahidi wowote unapotolewa katika lugha ambayo mshtakiwa haifahamu, na yupo yeye mwenyewe binafsi, utatafsiriwa kwake yeye katika mahakama ya wazi kwa lugha ambayo mshtakiwa anaifahamu.

(2) Ikiwa amewakilishwa na wakili na ushahidi unatolewa katika lugha isiyokuwa lugha ya mahakama, na wakili haifahamu lugha hiyo, utatafsiriwa kwa ajili ya wakili huyo katika lugha ya Kiingereza au Kiswahili.

(3) Ikiwa nyaraka zinaletwa kwa madhumuni ya ithibati rasmi itakuwa ni katika uwezo wa mahakama kutafsiri kwa kiasi ambacho kama itakavyoonekana ni lazima.

Maelezo kuhusu muonekano wa shahidi.

**203.** Pale hakimu amerekodi ushahidi wa shahidi atarekodi pia maelezo ambayo, kama yapo, anayaona ni muhimu kuhusiana na muonekano wa shahidi huyo wakati anahojiwa.

Ushahidi utakaorekodiwa sehemu ya ushahidi huo na hakimu mmoja na sehemu nyengine na hakimu mwengine.

**204.**-(1) Pale ambapo hakimu yeyote, baada ya kusikilizwa na kurekodiwa ushahidi wote au sehemu ya ushahidi huo katika uchunguzi wowote au usikilizaji wa kesi yoyote iliyoendeshwa yote kwa sababu yoyote hawezi kumaliza uchunguzi au usikilizwaji wa kesi ndani ya muda unaofaa, hakimu mwengine ambaye ana mamlaka na anatekeleza mamlaka hayo atachukua na kuendelea na uchunguzi au usikilizaji huo wa kesi, kama hali itakavyokuwa, na hakimu huyo anayechukua na kuendeleza atatumia ushahidi huo au mwenendo wa kesi uliorekodiwa na mtangulizi wake.

(2) Hakuna chochote katika kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, kitakachotafsiriwa kuwa kinamzuia hakimu ambaye amerekodi ushahidi wote katika usikilizaji wa kesi yoyote na ambaye, kabla ya kutoa hukumu hawezi kumaliza usikilizaji wa kesi, asiandike hukumu na kupeleka kumbukumbu za mwenendo wa kesi pamoja na hukumu hiyo kwa hakimu aliyechukua kesi baada yake kwa ajili ya hukumu hiyo kusomwa na, ikiwa mshtakiwa anatiwa hatiani, kwa ajili ya adhabu kutolewa na huyo hakimu mwengine.

### Mahakama Kuu

Kumbukumbu za ushahidi katika Mahakama Kuu.

**205.** Kwa kuzingatia maelezo yanayotolewa na Jaji Mkuu mara kwa mara, utaratibu wa kurekodi ushahidi katika Mahakama Kuu, kwa kadri iwezekanavyo, utakuwa ule ule kama utaratibu wa kurekodi ushahidi katika Mahakama za chini.

## SEHEMU YA TISA
## UTARATIBU KATIKA USIKILIZAJI KESI MBELE YA MAHAKAMA ZA CHINI

### Masharti yanayohusiana na Usikilizaji na Uamuzi wa Kesi

Kutokuhudhuria kwa mlalamikaji.

**206.** Ikiwa, katika kesi yoyote ambayo mahakama ya chini ina mamlaka ya kuisikiliza na kuiamua, mshtakiwa anafika katika kutii wito aliopelekewa katika wakati na pahala palipotajwa katika wito huo kwa ajili ya usikilizaji wa kesi hiyo, au analetwa mbele ya mahakama baada ya kukamatwa, baadae, ikiwa mlalamikaji, akiwa na taarifa ya muda na pahala palipotajwa kwa ajili ya usikilizaji wa shtaka, hajahudhuria, mahakama inaweza kuondosha shtaka, isipokuwa kama kuna sababu mahakama itaona inafaa kuakhirisha usikilizaji wa kesi hiyo mpaka tarehe nyengine, kwa masharti itakayoona yanafaa, katika hali hiyo mahakama inaweza, kwa kusubiri usikilizaji ulioakhirishwa, ama kumpa mshtakiwa dhamana au kumuweka mahabusu katika Chuo cha Mafunzo, au kuchukua ahadi ya dhamana kwa ajili ya kufika mahakamani kama mahakama itakavyoona inafaa.

Kufika kwa wahusika wote wa kesi.

**207.** Iwapo katika muda uliotajwa kwa ajili ya usikilizaji wa kesi hiyo mlalamikaji na mshtakiwa wote wamefika mbele ya mahakama ambayo itasikiliza na kuamua shtaka, mahakama itaendelea kuisikiliza kesi hiyo.

Kuondosha malalamiko.

**208.** Iwapo mwendesha mashtaka binafsi, wakati wowote kabla ya kutolewa kwa amri ya mwisho katika kesi yoyote chini ya Sehemu hii, anairidhisha mahakama kwamba kuna sababu za kutosha kumruhusu mlalamikaji kuondosha malalamiko yake, mahakama inaweza kumruhusu mlalamikaji kuondoa malalamiko hayo na baadae itamuachia huru mshtakiwa.

Kuakhirisha.

**209.**-(1) Kabla au wakati wa usikilizaji wa kesi yoyote, itakuwa ni halali kwa mahakama katika uwezo wake kuakhirisha usikilizaji wa kesi kwa muda fulani na pahala

ambapo baadae patatajwa na pataelezwa mbele ya mhusika au wahusika au mawakili wao watakaokuwepo wakati huo, na katika wakati huo mahakama inaweza kumruhusu mshtakiwa kuwa huru, inaweza kumpeleka mshtakiwa Chuo cha Mafunzo, au inaweza kumuachia kwa ahadi ya dhamana akiwa na wadhamini au bila ya wadhamini katika uwezo wa mahakama, au kwa kuweka masharti yanayomtaka kufika katika wakati na pahala ambapo usikilizaji huo na au usikilizaji mwengine zaidi umeakhirishwa.

(2) Uakhirishaji huo hautokuwa kwa zaidi ya siku thelathini, au ikiwa mshtakiwa amepelekwa Chuo cha Mafunzo, hautozidi siku kumi na tano, siku inayofuata ile siku ambayo kesi imeakhirishwa itahesabiwa kuwa ndiyo siku ya kwanza.

(3) Pale mashahidi wanapohudhuria, uakhirishaji wa kesi hautofanywa bila ya kuwahoji mashahidi hao, isipokuwa kwa sababu za msingi zitakazorekodiwa kwa maandishi.

Kuanza usikilizaji wa kesi kwa makosa yenye dhamana.

**210.**-(1) Usikilizaji wa kesi katika kosa lenye dhamana utaanza ndani ya miezi mitatu.

(2) Iwapo usikilizaji haujaanza ndani ya miezi mitatu, mahakama inaweza kumuachia mshtakiwa lakini kumuachia huko hakutokuwa kizuizi kwa usikilizaji wa baadae kwa mambo hayo hayo.

(3) Katika kuhesabu muda ulioelezwa chini ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki, kipindi ambacho mshtakiwa alitoroka au hakuwepo Zanzibar na kutokuwepo huko kumeathiri au kumecheleweshа upelelezi, hakitahesabiwa.

(4) Iwapo usikilizaji kwa kosa lolote haujaanza ndani ya miaka mitatu baada ya mshtakiwa kuachiliwa na mahakama chini ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki, au kuondoshwa na mwendesha mashtaka chini ya kifungu cha 103(a) cha Sheria hii, au kutokuwepo nia ya kuendelea kushtaki *(nolle prosequi),* hakuna shtaka litakaloletwa mbele ya mahkama kwa mambo hayo hayo isipokuwa baada ya kupata kwanza ruhusa ya mahakama iliyotolewa baada ya ombi la mwendesha mashtaka.

(5) Kwa madhumuni ya kuondoa shaka inaelezwa wazi kwamba masharti ya kifungu hiki hayatatumika katika upelelezi wowote wa jinai kwa shtaka ambalo halijafunguliwa katika mahakama yoyote.

Kutokuhudhuria kwa wahusika wa kesi baada ya kuakhirishwa.

**211.**-(1) Iwapo katika wakati na pahala ambapo usikilizaji wa kesi au usikilizaji zaidi utakuwa umeakhirishwa, mshtakiwa hakufika mbele ya mahakama ambayo imetoa amri ya kuakhirisha itakuwa ni halali kwa mahakama hiyo kuendelea na usikilizaji wa kesi au kusikiliza zaidi kama kwamba mshtakiwa yupo mahakamani, na ikiwa mlalamikaji hajafika mahakama italifuta shtaka na itamuachia mshtakiwa kwa gharama au bila ya gharama kama mahakama itakavyoona inafaa.

(2) Ikiwa mahakama inamtia hatiani mshtakiwa pasi na kuwepo mahakamani, inaweza kutengua hatia hiyo baada ya kuridhika kwamba kutokuwepo mahakamni kwa mshtakiwa kumesababishwa na sababu zilizo nje ya uwezo wake, na kwamba alikuwa ana utetezi wa msingi.

(3) Adhabu iliyotolewa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, itachukuliwa kuwa imeanza kuanzia tarehe alipokamatwa, na mtu aliyetekeleza ukamataji huo atathibitisha kwa kuweka tarehe nyuma ya hati ya kupelekwa Chuo cha Mafunzo.

Gharama za uakhirishaji.

**212.** Ikiwa katika wakati na pahala ambapo usikilizaji wa kesi au usikilizaji zaidi wa kesi utakuwa umeakhirishwa, wakili wa mshtakiwa hajafika au amefika na anaomba kesi iakhirishwe, mahakama, isipokuwa kama sababu za msingi za kuakhirisha usikilizaji wa kesi zinatolewa, inaweza kumuamuru wakili kulipa gharama zisizopungua Shilingi Laki Moja lakini zisizozidi Shilingi Laki Tano.

Kumwita mshtakiwa kujibu shtaka.

**213.**-(1) Mahakama itamuelezea mshtakiwa maudhui ya shtaka au malalamiko, na mshtakiwa ataulizwa ama anakubali au anakataa ukweli wa shtaka hilo.

(2) Ikiwa mshtakiwa anakubali ukweli wa shtaka hilo, kukiri kwake kutarekodiwa kama iwezekanavyo kwa maneno yale yale aliyoyatumia mshtakiwa, na mahakama itamtia hatiani mshtakiwa huyo na itatoa adhabu au amri dhidi ya mshtakiwa, isipokuwa kama mahakama itaona kuna sababu ya msingi kinyume na hivyo.

(3) Ikiwa mshtakiwa hajakubali ukweli wa shtaka, Mahakama itaendelea kuisikiliza kesi hiyo kama itakavyoelezwa baadae.

(4) Ikiwa mshtakiwa anakataa kujibu shtaka, Mahakama itarekodi jawabu la “kutokuwa na hatia”.

Utaratibu kwa jawabu la “kutokuwa na hatia”.

**214.**-(1) Ikiwa mshtakiwa hakubali ukweli wa shtaka, Mahakama itaendelea kumsikiliza mlalamikaji na mashahidi wake na ushahidi mwengine, kama upo.

(2) Mwendesha mashtaka hahitaji kumwita daktari au shahidi mtaalamu ambaye amewasilisha ripoti yake mahakamani ikiwa mshtakiwa au wakili wake hahitaji kumfanyia mahojiano kinzani shahidi huyo.

(3) Mshtakiwa au Wakili wake anaweza kumuuliza maswali kila shahidi anayeletwa dhidi yake.

(4) Ikiwa mshtakiwa hajaajiri Wakili, Mahakama, baada ya kumalizika kwa mahojiano ya kila shahidi wa upande wa mashtaka, itamuuliza mshtakiwa kama anapenda kumuuliza maswali yoyote shahidi huyo na itarekodi jibu lake.

(5) Ikiwa mshtakiwa, anapotakiwa kumfanyia mahojiano kinzani shahidi yeyote huyo, anatoa maelezo ambayo hayahitaji kurekodiwa lakini mahakama, kwa niaba ya mshtakiwa itamuuliza shahidi huyo swali lolote linalotokana na maelezo hayo.

Kumuachia mshtakiwa anapokuwa hana kesi ya kujibu.

**215.** Ikiwa wakati wa kufunga ushahidi unaounga mkono shtaka mahakama inaona kwamba hakuna kesi iliyojitokeza dhidi ya mshtakiwa inayofaa kumtaka mshtakiwa kujitetea, mahakama itafuta shtaka na itamuachia mshtakiwa huyo.

Utetezi.

**216.**-(1) Wakati wa kufunga ushahidi unaounga mkono shtaka, ikiwa mahakama inaona kwamba kuna kesi dhidi ya mshtakiwa inayofaa kumtaka mshtakiwa kutoa utetezi wake, mahakama inamuelezea mshtakiwa maudhui ya shtaka na itamuarifu haki zake:

(a) kutoa ushahidi ama kwa kiapo au bila ya kiapo au kwa uthibitisho au bila ya uthibitisho, kwa niaba yake mwenyewe; na

(b) kuwaita mashahidi katika utetezi wake,

na baadae itamuuliza mshtakiwa au wakili wake kama ana nia ya kutumia moja kati ya haki zilizotajwa chini ya aya ya (a) au (b) za kifungu hiki, na itarekodi jawabu hilo; na mahakama baadae itamuita mshtakiwa kujitetea isipokuwa pale mshtakiwa hataki kutumia haki yoyote kati ya hizo.

(2) Bila ya kujali kwamba mshtakiwa anachagua kutoa ushahidi bila ya kiapo au kwa kiapo au kwa uthibitisho au bila ya uthibitisho, atawajibika kufanyiwa mahojiano kinzani na upande wa mashtaka.

(3) Ikiwa mshtakiwa anaeleza kwamba ana mashahidi wa kuwaita lakini mashahidi hao hawapo mahakamani, na mahakama inaridhika kwamba kutokuwepo kwa mashahidi hao hakutokani na kosa lolote au kudharau kulikofanywa na mshtakiwa, na kwamba kuna uwezekano kwamba wanaweza mashahidi hao, ikiwa wapo, kutoa ushahidi muhimu kwa niaba ya mshtakiwa, mahakama inaweza kuakhirisha usikilizaji wa kesi hiyo na kutoa wito, au kuchukua hatua nyengine, kulazimisha uhudhuriaji wa mashahidi hao.

Ushahidi katika majibu.

**217.** Ikiwa mshtakiwa ameshawahoji mashahidi wowote au ameshatoa ushahidi wowote usiokuwa ushahidi unaohusu tabia yake kwa ujumla mahakama inaweza kutoa ruhusa kwa mwendesha mashtaka kutoa au kuwasilisha ushahidi katika majibu.

Ufunguaji na ufungaji wa kesi kwa upande wa mashtaka na upande wa utetezi.

**218.**-(1) Mwendesha mashtaka au wakili wake atakuwa na haki kuihutubia mahakama wakati wa kuanza kwa kesi yake na mshtakiwa au wakili wake atakuwa na haki ya kuihutubia mahakama wakati wa kuanza au wakati wa ufungaji wa kesi yake kama atakavyoona inafaa.

(2) Isipokuwa kwa ruhusa ya mahakama, mwendesha mashtaka au wakili wake hatoruhusiwa katika hali yoyote kuihutubia mahakama baada ya kufungwa kwa kesi ya upande wa mshtakiwa wala mshtakiwa au wakili wake bila ya ruhusa hiyo kama ilivyoelezwa awali hatakuwa na haki ya kuihutubia mahakama juu ya ushahidi uliotolewa na mwendesha mashtaka katika majibu.

Tofauti baina ya hati ya mashtaka na ushahidi na marekebisho ya hati ya mashtaka.

**219.**-(1) Pale ambapo, katika hatua yoyote ya usikilizaji wa kesi kabla ya ufungaji wa kesi kwa upande wa mashtaka, mahakama inaona kwamba hati ya mashtaka ina kasoro, ama katika maudhui au katika muundo, mahakama inaweza kutoa amri kwa ajili ya mabadiliko ya hati ya mashtaka ama kwa njia ya marekebisho ya shtaka au kwa njia ya kubadilisha shtaka au kwa njia ya kuongeza shtaka jipya kama mahakama inavyoona ni lazima kuendana na mazingira ya kesi hiyo.

(2) Pale ambapo, katika hatua yoyote ya usikilizaji wa kesi kabla ya ufungaji wa kesi kwa upande wa mashtaka, mwendesha mashtaka anaona kwamba hati ya mashtaka ina kasoro, ama katika maudhui au muundo, mwendesha mashtaka anaweza kuomba ruhusa ya mahakama kubadilisha hati ya mashtaka.

(3) Pale hati ya mashtaka inabadilishwa kama ilivyoelezwa awali, mahakama itamuita wakati huo mshtakiwa kuja kujibu shtaka jipya lililobadilishwa.

(4) Pale ambapo hati ya mashtaka imebadilishwa chini ya kifungu hiki mshtakiwa anaweza kutaka kwamba mashahidi au yeyote miongoni mwao aitwe tena na watoe ushahidi wao upya au wafanyiwe mahojiano kinzani zaidi na mshtakiwa au wakili wake na, katika tukio lililotajwa mwisho, upande wa mashtaka utakuwa na haki ya kumhoji tena shahidi yeyote yule kuhusiana na jambo lililojitokeza katika mahojiano kinzani zaidi.

(5) Tofauti baina ya shtaka na ushahidi uliotolewa katika kuunga mkono shtaka hilo kuhusiana na wakati ambapo kosa linalodaiwa kutendwa limetendwa siyo muhimu na shtaka hilo halihitaji kufanyiwa marekebisho kutokana na tofauti hiyo ikiwa inathibitika kwamba mwenendo wa kesi ulikuwa umeanzishwa kwa hakika ndani ya muda, kama upo, endapo kuna sheria iliyoweka ukomo wa muda wa uanzishaji wa shtaka hilo.

Uamuzi.

**220.** Mahakama, baada ya kuwasikiliza mlalamikaji na mshtakiwa na mashahidi wao na ushahidi, ama itamtia hatiani mshtakiwa na kutoa adhabu, au itatoa amri dhidi ya mshtakiwa kwa mujibu wa sheria au itamuachia huru mshtakiwa, au itafuta shtaka chini ya kifungu cha 330 cha Sheria hii.

Kuandika hatia au amri.

**221.** Hatia au amri inaweza, ikiwa inahitajika, baadae kuandikwa na itasainiwa na mahakama iliyomtia hatiani mshtakiwa au iliyotoa amri dhidi ya mshtakiwa, au itasainiwa na Mrajis.

Amri ya kufuta shtaka itazuia utaratibu zaidi.

**222.** Uwasilishaji wa nakala ya amri ya kufuta, iliyothibitishwa na Mrajis, bila ya uthibitisho mwengine itakuwa ni kizuizi kwa taarifa ya mashtaka au malalamiko mengine yoyote ya baadae kwa ajili ya jambo hilo hilo dhidi ya mshtakiwa huyo huyo.

**Ukomo wa Muda na Udhuru Kuhusiana na usikilizaji wa Kesi mbele ya Mahakama za Chini**

Ukomo wa muda kwa ajili ya usikilizaji wa kesi moja kwa moja.

**223.** Isipokuwa pale ambapo muda mrefu zaidi unaruhusiwa na sheria, hakuna kosa ambalo adhabu kubwa kabisa ya kosa hilo haizidi kifungo cha miezi sita au faini isiyozidi Shilingi Laki Tano, au adhabu hizo zote mbili kifungo na faini, litasikilizwa na mahakama ya chini, isipokuwa shtaka au malalamiko kuhusina na kosa hilo liwe limepelekwa ndani ya miezi kumi na mbili kuanzia muda ambapo jambo la shtaka hilo au lalamiko hilo limetokea.

Utaratibu katika kesi ya kosa linalothibitika halifai kusikilizwa kwa utaratibu wa usikilizaji kesi moja kwa moja.

**224.** Ikiwa wakati wa usikilizaji wa kesi mbele ya mahakama ya chini inaonekana na hakimu katika hatua yoyote ya mwenendo wa shauri kwamba kesi hiyo ni moja inayopaswa kusikilizwa na Mahakama Kuu, hakimu atasimamisha mwenendo zaidi wa shauri hilo na atampeleka mshtakiwa kwa ajili ya kusikilizwa kupitia taarifa ya mashtaka mbele ya Mahakama Kuu, na katika kesi hiyo atafuata utaratibu utakaoelezwa humu baadae kuhusu makosa yanayosikilizwa na Mahakama Kuu.

## SEHEMU YA KUMI
## UTARATIBU KATIKA USIKILIZAJI WA KESI MBELE YA MAHAKAMA KUU

Ufanyaji kazi wa Mahakama Kuu katika mamlaka yake ya jinai.

**225.-**(1) Ufanyaji kazi wa Mahakama Kuu ya Zanzibar katika mamlaka yake ya jinai utakuwa, kwa mambo ambayo hayajaelezwa wazi wazi katika Sheria hii, unafanana kwa kadiri ya mazingira yatakavyoruhusu na ufanyaji kazi wa mahakama za nchi za Jumuiya ya Madola katika mamlaka yao ya jinai.

(2) Mambo yote ya awali kuhusu kesi ya jinai katika Mahakama Kuu yatafanywa mbele ya Jaji.

Mashtaka kuendeshwa na Mkurugenzi wa Mashtaka.

**226.** Katika usikilizaji wowote wa kesi mbele ya Mahakama Kuu, uendeshaji mashtaka utafanywa na Mkurugenzi wa Mashtaka, Wakili wa Serikali au mtu mwengine yeyote aliyeidhinishwa na Mkurugenzi wa Mashtaka.

Upande wa Mashtaka kutoa rekodi za ushahidi.

**227.-**(1) Katika siku ya mwanzo iliyopangwa kwa ajili ya usikilizaji wa kesi, upande wa mashtaka utatoa jalada kamili la rekodi ya ushahidi ambao inakusudia kuutegemea kwa mshtakiwa au kwa kila mmoja miongoni mwa washtakiwa au mawakili wao kama hali itakavyokuwa.

(2) Mahakama baada ya hapo itaakhirisha kesi mpaka tarehe ya baadae ambayo si zaidi ya mwezi mmoja kama itakavyoona inafaa ili kuupa wakati wa kutosha upande wa utetezi kujiandaa kwa ajili ya usikilizaji wa kesi.

### Namna ya Usikilizaji Kesi

Usikilizaji kesi utakuwa pamoja na washauri wa mahakama watatu.

**228.**-(1) Katika Mahakama Kuu, usikilizaji wa kesi za makosa yote ambayo adhabu yake ni kifo utakuwa ni kwa msaada wa washauri wa mahakama ambao idadi yao itakuwa ni watatu.

(2) Usikilizaji wa kesi nyengine za makosa ambayo adhabu yake siyo kifo, hautakuwa kwa msaada wa washauri wa mahakama.

### Orodha ya Washauri wa Mahakama

Utayarishaji wa Orodha.

**229.** Mrajis wa Mahakama Kuu kabla ya siku ya kwanza ya mwezi wa Machi ya kila mwaka, na kwa kuzingatia Kanuni ambazo Jaji Mkuu wa Zanzibar anaweza kila baada ya muda kuziandaa, atatayarisha orodha ya watu wanaofaa katika Zanzibar wenye sifa za kuwa washauri wa mahakama.

Wajibu wa kuhudumu kama washauri.

**230.** Isipokuwa kama ilivyoelezwa chini ya kifungu cha 231 cha Sheria hii, watu wote wenye umri kuanzia miaka arubaini wanafaa kuhudumu kama washauri wa Mahakama katika usikilizaji wa kesi yoyote unaofanywa na Mahakama Kuu ndani ya Zanzibar kwa msaada wa washauri wa mahakama.

Kutoruhusiwa kuhudumu kama washauri wa mahakama.

**231.**-(1) Watu waliotajwa katika Jadweli la Nne la Sheria hii hawaruhusiwi kuhudumu kama washauri wa mahakama.

(2) Jaji Mkuu wa Zanzibar anaweza kwa kutoa taarifa kwenye Gazeti kuongeza maafisa wengine wowote wa Zanzibar au watu wengine wowote kwenye orodha hiyo ya watu waliotajwa katika Jadweli la Nne la Shera hii.

Uchapishaji wa orodha.

**232.**-(1) Nakala ya orodha iliyotayarishwa na Mrajis ya watu wanaowajibika kuhudumu kama washauri kwa Mahakama itachapishwa katika Gazeti katika toleo la kwanza la Gazeti hilo katika mwezi wa Machi, na sehemu za Gazeti hilo zenye majina ya watu wanaofaa kuhudumu kama washauri wa mahakama wanaoishi katika kila Wilaya yatabandikwa ili watu wayakague majina hayo katika Ofisi za Mkuu wa Wilaya wa kila Wilaya.

(2) Kwa kila nakala hiyo au sehemu hiyo ya majina hayo kutaunganishwa chini yake notisi inayoeleza kwamba pingamizi kwa orodha hiyo zitasikilizwa na kuamuliwa na Jaji wa Mahakama Kuu pamoja na Hakimu ambaye atateuliwa na Mahakama Kuu katika wakati na pahala patakapotajwa katika notisi hiyo.

Mapitio ya orodha.

**233.**-(1) Kwa ajili ya usikilizaji wa pingamizi za orodha hiyo Jaji wa Mahakama Kuu atakaa na hakimu, na katika muda na pahala palipotajwa katika notisi, watafanya mapitio na watasikiliza pingamizi, kama zipo, za watu wanaopenda kufanywe mabadiliko katika orodha hiyo, na wataondoa jina la mtu yeyote ambaye hafai kwa maoni yao kuhudumu kama mshauri wa mahakama, au anayeweza kuthibitisha haki yake ya kusamehewa kuhudumu kama ilivyowekwa chini ya kifungu cha 231 cha Sheria hii, na wataingiza jina la mtu ambaye lilikuwa halijaingizwa katika orodha ambaye wao wanamuona anafaa kuhudumu kama mshauri wa mahakama.

(2) Ikitokezea tofauti ya maoni baina ya Jaji huyo na hakimu huyo, jina la mshauri wa mahakama linalopendekezwa litaondolewa kwenye orodha.

(3) Nakala ya orodha iliyokwishafanyiwa mapitio itasainiwa na Jaji huyo pamoja na hakimu huyo na itapelekwa kwa Mrajis wa Mahakama Kuu.

(4) Amri ya Jaji huyo na hakimu huyo kama ilivyoelezwa awali katika utayarishaji na kuifanyia mapitio orodha hiyo itakuwa ni ya mwisho.

(5) Udhuru wowote wa kutokuwajibika kuhudumu kama mshauri wa mahakama ambao haukudaiwa chini ya kifungu hiki utachukuliwa kuwa umesamehewa mpaka pale orodha hiyo itapopitiwa tena.

(6) Orodha iliyotayarishwa kwa utaratibu huo na kupitiwa itapitiwa tena mara moja katika kila mwaka.

Washauri wa mahakama kula kiapo.

**234.**-(1) Kabla hawajaanza majukumu yao, washauri wa mahakama watakula kiapo mbele ya Jaji wa Mahakama Kuu.

(2) Kiapo chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, kitakuwa katika muundo na namna iliyoainishwa katika Jadweli la Saba la Sheria hii.

**Mahudhurio ya Washauri wa Mahakama**

Kuwaita washauri wa mahakama.

**235.**-(1) Mrajis wa Mahakama Kuu kwa kawaida, angalau siku saba kabla ya siku ambayo kila baada ya muda inaweza kupangwa kwa ajili ya kufanyika kwa kikao cha Mahakama Kuu, kupeleka barua kwa hakimu mwenye dhamana ya kuendesha mahakama ya chini, mwenye mamlaka katika Wilaya ambayo vikao hivyo vitafanywa, kumtaka hakimu huyo kuwaita watu wengi kama itakavyoonekana watahitajika katika vikao hivyo na Jaji ambaye ataongoza vikao hivyo.

(2) Kuhusu watu waliotajwa katika orodha, majina hayo ya watu watakaoitwa yatateuliwa kwa kura na hakimu katika mahakama ya wazi, wakiachwa wale waliokwishahudumu ndani ya miezi sita isipokuwa kama idadi haitotimia bila ya wao.

Aina ya wito.

**236.** Wito wa kumwita mshauri wa mahakama utakuwa kwa maandishi, na utamtaka ahudhurie kama mshauri, katika muda na pahala patapoainishwa ndani ya wito huo.

Dharura kwa kutohudhuria.

**237.** Mahakama Kuu inaweza kwa sababu ya msingi kumruhusu mshauri wa mahakama yeyote asihudhurie katika vikao vyovyote, na inaweza, ikiwa itaona inafaa, utakapomalizika usikilizaji wa kesi yoyote, kuelekeza kwamba washauri wa mahakama ambao wameshahudumu katika usikilizaji huo wa kesi hawatoitwa kuhudumu tena kwa kipindi cha miezi kumi na mbili.

Orodha ya washauri wa mahakama wanaohu-dhuria.

**238.**-(1) Katika kila kikao cha Mahakama Kuu, Jaji Mkuu wa Zanzibar atawezesha kutayarishwa orodha ya majina ya wale ambao wamehudhuria kama washauri wa mahakama katika vikao hivyo, na orodha hiyo itawekwa pamoja na orodha ya washauri wa mahakama kama ilivyofanyiwa mapitio chini ya kifungu cha 233 cha Sheria hii.

(2) Kumbukumbu itawekwa upande wa pembeni ya orodha hiyo iliyofanyiwa mapitio kwa kila jina miongoni mwa majina ambayo yametajwa katika orodha hiyo iliyotaarishwa chini ya kifungu hiki.

Adhabu kwa kutohudhuria.

**239.**-(1) Mtu aliyeitwa kuhudhuria kama mshauri wa mahakama ambaye, bila ya sababu ya msingi, anashindwa kuhudhuria kama alivyotakiwa na wito huo, au ambaye, baada ya kuhudhuria, anaondoka bila ya kupata ruhusa ya Mahakama Kuu, au anashindwa kuhudhuria baada ya mahakama kuakhirishwa baada ya kuamriwa ahudhurie, atawajibika kwa amri ya Mahakama Kuu kutozwa faini isiyozidi Shilingi Laki Moja.

(2) Faini hiyo isipokuwa kama italipwa itatozwa na hakimu wa Mahakama ya chini kwa njia ya ukamataji na uuzaji wa mali yoyote inayohamishika inayomilikiwa na mshauri huyo wa mahakama ndani ya eneo la mipaka ya mamlaka ya hakimu huyo.

(3) Kwa sababu ya msingi itakayotolewa, Mahakama Kuu inaweza kuondoa au kupunguza faini yoyote iliyotozwa.

(4) Ikiwa itashindikana kupatikana faini hiyo kwa njia ya ukamataji na uuzaji mshauri wa mahakama anaweza, kwa amri ya Mahakama Kuu, kupelekwa Chuo cha Mafunzo kama mwanafunzi wa madai kwa kipindi cha siku kumi na tano isipokuwa kama faini hiyo inalipwa kabla ya kumalizika kipindi hicho.

**Kusomewa shtaka**

Kujibu taarifa ya Shtaka.

**240.** Mtuhumiwa atakayeshtakiwa mbele ya Mahakama Kuu kwa taarifa ya shtaka atawekwa katika kizimba cha mshtakiwa bila ya kufungwa pingu, isipokuwa kama mahakama itaona kuwa kuna sababu ya kuamuru vyenginevyo, na taarifa hiyo ya shtaka atasomewa na Mrajis au afisa mwengine wa mahakama, na kufafanuliwa

ikihitajika hivyo, na afisa huyo au kutafsiriwa na mkalimani wa mahakama, na mtu huyo anayeshtakiwa atatakiwa ajibu wakati huo huo hapo hapo, isipokuwa pale ambapo mtu anayeshtakiwa ana haki ya kupewa nakala ya taarifa ya shtaka, atapinga kuwa hajapewa nakala hiyo, na mahakama itaamua kwamba mshtakiwa huyo hajapewa nakala hiyo ya taarifa ya shtaka kama ilivyotakiwa.

Marekebisho ya taarifa ya shtaka, usikilizaji wa kesi tofauti na uakhirishaji wa usikilizaji wa kesi.

**241.**-(1) Pingamizi kwa taarifa ya kesi kuhusu kasoro yoyote inayoonekana wazi wazi itawasilishwa mara moja baada ya taarifa ya shtaka kusomwa kwa mshtakiwa na siyo baadae.

(2) Pale, kabla ya usikilizaji wa kesi inayotokana na taarifa ya kesi au katika hatua yoyote ya usikilizaji huo wa kesi, mahakama inaona kwamba taarifa hiyo ya kesi ina kasoro, mahakama itatoa amri kwa ajili ya marekebisho ya taarifa hiyo ya kesi kama mahakama itaona ni muhimu katika mazingira ya kesi hiyo, isipokuwa kama, kwa kuzingatia misingi ya kesi hiyo, marekebisho yanayohitajika hayataweza kufanywa bila ya kuharibu utoaji wa haki.

(3) Marekebisho hayo yatafanywa kwa mujibu wa masharti kama mahakama itakavyoona inafaa.

(4) Endapo taarifa ya shtaka inarekebishwa kwa utaratibu huo, maelezo ya amri ya marekebisho yataingizwa kwenye taarifa hiyo ya shtaka, na taarifa hiyo ya shtaka itachukuliwa kwa madhumuni ya mwenendo wa kesi inayohusiana na taarifa hiyo ya shtaka kama ilifunguliwa kwa namna ilivyorekebishwa

(5) Pale, kabla ya usikilizaji wa kesi inayotokana na taarifa ya shtaka au katika hatua yoyote ya usikilizaji huo wa kesi, mahakama ina maoni kwamba mshtakiwa anaweza kuathirika au anaweza kutokuwa na utulivu katika utetezi wake kwa sababu ya kushtakiwa pamoja kwa kosa zaidi ya moja katika taarifa hiyo ya shtaka, au kwamba kwa sababu nyengine yoyote inaona inafaa kuelekeza kwamba mshtakiwa ashtakiwe tofauti kwa kosa lolote moja au makosa zaidi ya moja anayoshtakiwa nayo katika taarifa ya shtaka, mahakama inaweza kuamuru usikilizaji tofauti wa kosa lolote moja au makosa zaidi ya moja ya taarifa hiyo ya kosa.

(6) Pale, kabla ya usikilizaji wa kesi inayotokana na taarifa ya shtaka au katika hatua yoyote ya usikilizaji huo wa kesi, mahakama ina maoni kwamba uakhirishaji wa usikilizaji wa kesi hiyo ya mshtakiwa ni muhimu kutokana na utumiaji wa mamlaka yoyote ya mahakama hiyo chini ya Sheria hii, mahakama itatoa amri hiyo kuhusu uakhirishaji huo wa usikilizaji kesi kama inavyoona inafaa.

(7) Pale amri ya mahakama inapotolewa chini ya kifungu hiki kwa ajili ya usikilizaji tofauti wa kesi au kwa ajili ya uakhirishaji wa usikilizaji wa kesi:

(a) mahakama inaweza kuamrisha kwamba washauri wa mahakama wataruhusiwa wasitoe maoni kuhusu shtaka au mashtaka ambayo usikilizaji wake unaoakhirishwa, au kuhusiana na taarifa hiyo ya shtaka kama hali itakavyokuwa;

(b) utaratibu katika usikilizaji tofauti wa shtaka lolote utakuwa ni ule ule kwa namna zote kama kwamba shtaka hilo lilianzishwa katika taarifa tofauti ya shtaka, na utaratibu katika usikilizaji wa kesi ulioakhirishwa utakuwa ni ule ule kwa namna zote, isipokuwa kwamba washauri wa mahakama, kama wapo, watakuwa wameachiwa, kama kwamba usikilizaji wa kesi ulikuwa haujaanza; na

(c) mahakama inaweza kutoa amri kuhusu kumruhusu mshtakiwa kwa dhamana, na kuhusu kuongeza masharti ya ahadi ya dhamana na vyenginevyo kama mahakama inavyoona inafaa.

(8) Uwezo wa mahakama chini ya kifungu hiki utakuwa ni kuweka nyongeza katika jambo liliopo na si kupunguza uwezo wowote mwengine wa mahakama kwa jambo kama hilo au kwa madhumuni yanayolingana na hayo.

Kuondoshwa kwa taarifa ya shtaka.

**242.**-(1) Iwapo taarifa ya shtaka haielezi, na haiwezi, kwa marekebisho yoyote yanayoruhusiwa chini ya kifungu cha 241 cha Sheria hii, kueleza, kosa lolote ambalo mshtakiwa alishaarifiwa, taarifa ya shtaka itaondoshwa ama kwa ombi lililofanywa kabla mshtakiwa hajajibu shtaka au kwa hoja itakayotolewa katika kuzuia hukumu.

(2) Taarifa ya maandishi ya kila ombi au hoja hiyo itapelekwa kwa Mrajis au afisa mwengine wa mahakama kwa niaba ya mshtakiwa na itaingizwa katika kumbukumbu.

Utaratibu katika hatia za awali.

**243.**-(1) Endapo taarifa ya shtaka inajumuisha shtaka linalomshtaki mshtakiwa ambaye awali alishawahi kutiwa hatiani kwa kosa lolote, utaratibu utakuwa kama ufuatao:

(a) sehemu ya taarifa ya shtaka inayoeleza utiwaji hatiani wa awali haitasomwa katika mahakama, wala mshtakiwa hataulizwa ama ameshatiwa hatiani awali kama inavyodaiwa katika taarifa ya shtaka, isipokuwa kama na hadi pale ama mshtakiwa ameshajibu shtaka au ameshatiwa hatiani kwa kosa linalofuatia;

(b) iwapo anakiri kosa au anatiwa hatiani kwa kosa linalofuatia, ataulizwa baadae ama ameshatiwa hatiani kabla kama inavyodaiwa katika taarifa ya shtaka;

(c) ikiwa anajibu kwamba ameshatiwa hatiani awali, mahakama inaweza kuendelea kutoa adhabu kwake yeye ipasavyo;

(d) ikiwa anakataa kwamba alishatiwa hatiani awali, au anakataa au hajibu swali hilo, mahakama baadae itasikiliza ushahidi kuhusu utiwaji hatiani huo wa awali.

(2) Endapo usikilizaji wa kesi ya mtu kwa ajili ya kosa hilo lolote linalofuatia mtu huyo atatoa ushahidi wa tabia yake njema, itakuwa halali kwa wakili wa upande wa mashtaka, katika kujibu jambo hilo, kutoa ushahidi wa kutiwa hatiani huko kwa mtu huyo kwa kosa hilo la awali au makosa kabla hajatiwa hatiani kwa kosa hilo linalofuatia, na mahakama itafanya uchunguzi kuhusiana na kutiwa hatiani huko kwa awali au kutiwa hatiani katika wakati huo huo ambao inachunguza kuhusu kosa hilo linalofuatia.

Mapatano ya kukubali kosa.

**244.**-(1) Katika hatua yoyote wakati wa upelelezi wa kosa au wakati wa usikilizaji wa kesi, Mkurugenzi wa Mashtaka au mtu aliyeidhinishwa kwa maandishi kwa niaba yake, kwa kushauriana na muathirika wa jinai au jamaa yake wa karibu, anaweza kuingia katika hatua ya mapatano ya kukubali kosa na mshtakiwa yeye mwenyewe au wakili wake.

(2) Wakili wa mshtakiwa anaweza kuanzisha mapatano ya kukubali kosa na Mkurugenzi wa Mashtaka kuhusiana na jambo lolote ambalo linamhusisha mteja wake.

Matokeo ya mapatano ya kukubali kosa.

**245.** Mapatano ya kukubali kosa yanaweza kupelekea makubaliano na Mkurugenzi wa Mashtaka kuwa asimshtaki mshtakiwa, au mshtakiwa kukubali kosa lililopunguzwa au kosa dogo zaidi, au mshtakiwa kukubali shtaka mahsusi ili aondoshewe mashtaka mengine.

Taarifa ya makubaliano kwa mahakama.

**246.**-(1) Makubaliano yaliyoingiwa kwa mujibu wa masharti ya vifungu vya 244 na 245 vya Sheria hii, yatasajiliwa na Mahakama Kuu.

(2) Mahakama Kuu, kabla ya kusajili makubaliano yoyote, itajiridhisha kwamba makubaliano hayo hayakupatikana kwa vitisho au kwa kulazimishwa, au yalitokana na ahadi zisizotekelezwa, au kwamba mshtakiwa hakuwa na akili timamu katika kuingia makubaliano hayo.

(3) Mahakama inaweza kutoa uamuzi kutokana na makubaliano ya mapatano ya kukubali kosa au kutoa amri hizo nyengine zozote kama inavyoona ni muhimu ikijumuisha amri ya kubatilisha makubaliano hayo na kuwataka wahusika wa kesi kwenda katika usikilizaji wa kesi.

Utaratibu unaofanana kwa Mahakama ya Mkoa.

**247.** Utaratibu ulioelezwa katika vifungu vya 244, 245 na 246 vya Sheria hii, utatumika kwa kesi mbali mbali katika Mahakama za Hakimu wa Mkoa.

Matokeo ya kutokukubali kosa.

**248.** Mshtakiwa, baada ya kusomewa shtaka linalotokana na taarifa ya shtaka, kwa kujibu kwa ujumla kuwa "siyo mkosa", bila ya utaratibu wa ziada, atachukuliwa kuwa ameingia kwenye usikilizaji wa kesi yake.

Kujibu kuwa alishaachiliwa huru na alishatiwa hatiani.

**249.**-(1) Mshtakiwa ambaye dhidi yake taarifa ya shtaka ilifunguliwa anaweza kujibu:

(a) kwamba alishawahi awali kutiwa hatiani au kuachiwa huru, kama hali itakavyokuwa kwa kosa hilo; au

(b) kwamba alishapewa msamaha na Rais wa Zanzibar kwa kosa hilo.

(2) Iwapo yoyote ya majibu hayo yamejibiwa katika kesi yoyote na yakakataliwa kuwa ni kweli kwa uhakika, mahakama itasikiliza kama jibu hilo ni kweli kwa uhakika au siyo kweli.

(3) Iwapo mahakama inaona kwamba majibu yanayodaiwa na mshtakiwa hayathibitishi jibu hilo au ikiwa inaona kwamba ni uongo kwa hakika, mshtakiwa atatakiwa kujibu taarifa ya shtaka.

Kukataa kujibu.

**250.**-(1) Ikiwa mshtakiwa anasomewa shtaka kuhusiana na taarifa ya shtaka anakaa kimya kwa makusudi, au hajibu moja kwa moja kuhusu taarifa ya shtaka, au kutokana na sababu ya ulemavu hawezi kujibu moja kwa moja kuhusu taarifa ya shtaka, mahakama, ikiwa inaona inafaa:

(a) itaingiza majibu ya "siyo mkosa" na majibu hayo yatakayoingizwa yatakuwa na uzito ule ule na matokeo yale yale kama kwamba mshtakiwa huyo kwa uhakika amejibu majibu hayo; **au**

(b) itaendelea kusikiliza ama mshtakiwa ana akili timamu au hana akili timamu kama ifuatavyo;

(i) iwapo atagundulika kuwa ana akili timamu, mahakama itaendelea na usikilizaji wa kesi; au

(ii) iwapo atagundulika kuwa hana akili timamu, na kutokana na hali hiyo hawezi kujitetea, mahakama itaamrisha usikilizaji wa kesi uakhirishwe, na mshtakiwa apelekwe kwa wakati huo

katika hifadhi salama katika pahala na namna kama mahakama inavyoona inafaa, na itatoa taarifa ya kesi hiyo kwa ajili ya kupata amri ya Rais.

(2) Kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (1) (b) (ii) cha kifungu hiki, Rais anaweza kutoa amri kuwa mshtakiwa azuiwe katika hospitali ya akili, Chuo cha Mafunzo au pahala pengine panapofaa pa hifadhi salama.

Utaratibu wa kukubali kosa.

**251.** Ikiwa mshtakiwa anajibu kuwa "ni mkosa" jibu hilo litarekodiwa na anaweza kutiwa hatiani kwa jibu hilo.

Utaratibu unaohusiana na kujibu "siyo mkosa".

**252.**-(1) Ikiwa mshtakiwa anajibu kuwa "siyo mkosa", au ikiwa jibu la "siyo mkosa" limeingizwa kwa mujibu wa masharti ya kifungu cha 250 cha Sheria hii, mahakama itaendelea kuchagua washauri wa mahakama ikiwa inahitajika, kama itakavyoelekezwa baadae na, kusikiliza kesi hiyo.

(2) Kwa kuzingatia haki ya kuweka pingamizi itakayotajwa baadae, washauri wa mahakama wale wale wanaweza kusaidia katika usikilizaji wa kesi za washtakiwa wengi mfululizo kama mahakama inavyoona inafaa.

Uwezo wa kupeleka mbele au kuakhirisha mwenendo wa kesi.

**253.**-(1) Ikiwa, kutokana na kutokuwepo mashahidi au sababu nyengine yoyote ya msingi itakayorekodiwa katika mwenendo wa kesi, mahakama inaona ni muhimu au vyema kusogeza mbele kuanza au kuakhirisha usikilizaji wowote wa kesi, mahakama mara kwa mara itasogeza mbele au itaakhirisha usikilizwaji huo kwa masharti kama inavyoona inafaa kwa wakati huo kama inavyoona ni muafaka, na inaweza kwa hati kumpeleka mahabusu mshtakiwa katika Chuo cha Mafunzo au pahala pengine pa usalama.

(2) Mwenendo wa kesi hautasimamishwa na usikilizaji mpya hautofanywa kutokana na sababu kwamba mmoja kati ya washauri wa mahakama, kwa sababu yoyote ile, amezuilika asihudhurie au amejiondoa katika mwenendo wa kesi.

(3) Wakati yupo mahabusu, mahakama inaweza, wakati wowote, kuamuru mshtakiwa aletwe mbele yake.

(4) Mahakama inaweza kumpa dhamana mshtakiwa aliye mahabusu.

## Uteuzi wa Washauri wa Mahakama

Uteuzi wa washauri wa mahakama.

**254.** Wakati usikilizaji wa kesi utakapofanywa kwa msaada wa washauri wa mahakama, mahakama itateua watatu kutoka katika orodha ya walioitwa kuhudumu kama washauri wa mahakama katika vikao.

Kutokuwepo kwa mshauri wa mahakama.

**255.**-(1) Iwapo, wakati wa usikilizaji wa kesi kwa msaada wa washauri wa mahakama, wakati wowote kabla ya uamuzi, mshauri yeyote wa mahakama kutokana na sababu yoyote ya msingi amezuilika kuhudhuria wakati wote wa usikilizaji wa kesi, au anajiondoa yeye mwenyewe, na haiwezekani kwa haraka kulazimisha uhudhuriaji wake, usikilizaji wa kesi utaendelea kwa msaada wa washauri wa mahakama wengine waliobaki.

(2) Ikiwa washauri wa mahakama wawili au zaidi wanazuilika kuhudhuria, au wanajiondoa wenyewe, mwenendo wa kesi utasimamishwa na usikilizaji mwengine utafanywa pamoja na washauri wa mahakama wapya.

Mshauri wa mahakama kuhudhuria katika vikao vilivyoakhirishwa.

**256.** Ikiwa usikilizaji wa kesi umeakhirishwa, washauri wa mahakama watatakiwa kuhudhuria katika kikao kilichoakhirishwa, na katika kikao chochote cha baadae hadi kumalizika kwa usikilizaji wa kesi.

**Maswali kutoka kwa Washauri wa Mahakama**

Uwezo wa washauri wa mahakama kuuliza maswali.

**257.** Washauri wa mahakama wanaweza kuwauliza mashahidi maswali yoyote, kwa kupitia au kwa ruhusa ya Jaji, ambayo Jaji mwenyewe angeweza kuuliza na ambayo anayaona yanafaa.

**Kesi ya Upande wa Mashtaka**

Kuanza usikilizaji wa kesi kwa upande wa mashtaka.

**258.** Katika usikilizaji wa kesi inayosikilizwa kwa msaada wa washauri wa Mahakama, wakati washauri wa mahakama wameshachaguliwa, upande wa mashtaka utaanza kuendesha kesi dhidi ya mshtakiwa, na utawaita mashahidi na kutoa ushahidi kwa ajili ya kuunga mkono shtaka.

Mashahidi wa upande wa mashtaka.

**259.**-(1) Upande wa mashtaka utakuwa na haki ya kuwaita mashahidi wote au idadi yoyote ya mashahidi ambayo wanaiona inafaa kwa madhumuni ya kuthibitisha kosa au makosa ambayo mshtakiwa anashtakiwa nayo.

(2) Upande wa mashtaka hauhitaji kumuita daktari au shahidi mwengine mtaalamu ambaye ameshawasilisha ripoti yake mahakamani, ikiwa mshtakiwa au wakili wake hahitaji kufanya mahojiano kinzani kwa shahidi huyo.

Kutokufika kwa wahusika wa kesi baada ya kuakhirishwa.

**260.**-(1) Ikiwa katika muda na pahala ambapo usikilizwaji au usikilizaji zaidi utakuwa umeakhirishwa, mshtakiwa hakufika mbele ya mahakama ambayo ilitoa amri ya kuakhirisha kesi, itakuwa ni halali kwa mahakama hiyo, kuendelea na usikilizaji au usikilizaji zaidi kama kwamba alikuwepo, na ikiwa mlalamikaji hakufika, mahakama inaweza, kuondosha shtaka kwa kulipa gharama au bila ya kulipa gharama kama mahakama itakavyoona inafaa.

(2) Ikiwa mahakama inamtia hatiani mshtakiwa bila ya mshtakiwa huyo kuwepo mahakamani, mahakama inaweza kutengua hatia hiyo baada ya kuridhika kwamba kutokuwepo kwake mshtakiwa kulisababishwa na sababu zilizo nje ya uwezo wake, na kwamba mshtakiwa alikuwa na utetezi wa maana.

(3) Adhabu iliyotolewa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, itachukuliwa kuwa imeanza kuanzia tarehe ya kukamatwa, na mtu aliyetekeleza ukamataji huo atathibitisha tarehe hiyo nyuma ya hati ya kumpeleka Chuo cha Mafunzo.

Shahidi anaweza kutoa ushahidi kwa njia ya kielektroniki.

**261.**-(1) Mahakama inaweza katika hali inayofaa kuruhusu ushahidi kutolewa na shahidi kwa njia ya kielektroniki.

(2) Mahakama inaweza kumruhusu shahidi kutoa ushahidi kwa njia ya kielektroniki katika mazingira yafuatayo tu:

(a) pale ambapo utambulisho wa shahidi unaweza kuhakikishwa; au

(b) pale ambapo mahojiano au mahojiano kinzani yanaweza kufanywa pasi na kizuizi.

Mahojiano kinzani kwa mashahidi.

**262.** Mashahidi wanaoitwa kwa ajili ya upande wa mashtaka watalazimika kufanyiwa mahojiano kinzani na mshtakiwa au wakili wake, na kufanyiwa mahojiano ya mara ya pili na wakili wa upande wa mashtaka.

Ufungaji wa kesi kwa upande wa mashtaka.

**263.**-(1) Endapo ushahidi wa mashahidi kwa ajili ya upande wa mashtaka umekamilika, mahakama ikiwa inaona, baada ya kuwasikiliza mawakili wa upande wa mashtaka na wa upande wa utetezi, kwamba hakuna ushahidi kuwa mshtakiwa au yeyote miongoni mwa washtakiwa wengi ametenda kosa, itarekodi uamuzi wa kutokuwa mkosa.

(2) Pale ushahidi wa mashahidi wa upande wa mashtaka umekamilika, na mahakama ikiwa inaona kwamba kuna ushahidi kuwa mshtakiwa au yeyote miongoni mwa washtakiwa wengi ametenda kosa, itamuarifu kila mshtakiwa haki zifuatazo:

(a) kutoa ushahidi kwa ajili yake yeye mwenyewe, au kutoa maelezo bila ya kiapo; na

(b) kuwaita mashahidi katika utetezi wake.

(3) Mahakama baadae itamuuliza mshtakiwa, au wakili wake, ikiwa inakusudiwa kutumiwa yoyote miongoni mwa haki zilizotajwa chini ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki na itarekodi majibu.

(4) Mahakama baadae itamuita mshtakiwa kwa ajili ya kutoa utetezi wake isipokuwa kama mshtakiwa hataki kutumia yoyote kati ya haki hizo chini ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki.

### Kesi kwa Upande wa Utetezi

Kuanza kwa kesi kwa ajili ya utetezi.

**264.**-(1) Mshtakiwa au Wakili wake anaweza wakati huo kuanza kesi yake, kueleza maelezo ya kesi au sheria ambayo anakusudia kuegemea, na kutoa maoni ambayo kama anavyoona ni muhimu kuhusiana na ushahidi wa upande wa mashtaka.

(2) Mshtakiwa anaweza wakati huo kutoa ushahidi wake mwenyewe na wakili wake anaweza kuwafanyia mahojiano mashahidi wake, kama wapo, na baada ya mahojiano kinzani na mahojiano ya mara ya pili, kama yapo, anaweza kufanya muhtasari wa kesi yake.

Mashahidi kwa ajili ya utetezi.

**265.** Mshtakiwa ataruhusiwa kuwaita mashahidi kwa ajili ya utetezi wake na kuwahoji mashahidi hao.

Majibu ya mwendesha mashtaka.

**266.** Ikiwa mshtakiwa, au yeyote kati ya washtakiwa, anatoa ushahidi wowote kuhusu tabia nzuri, wakili wa upande wa mashtaka atakuwa na haki ya kujibu.

Pale mshtakiwa hatoi ushahidi wowote.

**267.** Ikiwa mshtakiwa anasema kwamba hakusudii kutoa au kuwasilisha ushahidi na mahakama inaona kwamba kuna ushahidi kwamba alitenda kosa, Wakili wa upande wa mashtaka atafanya muhtasari wa kesi dhidi ya mshtakiwa na baadae mahakama itamuita mshtakiwa binafsi au kwa kupitia Wakili wake kuzungumza mbele ya mahakama kwa niaba ya mshtakiwa huyo.

### Ufungaji wa Usikilizaji Kesi

Utoaji wa maoni ya washauri wa mahakama.

**268.**-(1) Pale usikilizaji wa kesi wa pande zote mbili umefungwa, Jaji atafanya muhtasari wa ushahidi wa upande wa mashtaka na wa upande wa utetezi, na baadae atawataka washauri wa Mahakama kila mmoja kutoa maoni yake kwa njia ya mdomo, na atarekodi maoni hayo.

(2) Jaji baadae atatoa hukumu, lakini katika kufanya hivyo hatowajibika kufuata maoni ya Washauri wa Mahakama.

(3) Ikiwa mshtakiwa anatiwa hatiani, Jaji atatoa adhabu kwa mshtakiwa huyo kwa mujibu wa sheria.

(4) Hakuna chochote katika kifungu hiki kitakachosomeka kuwazuia washauri wa mahakama, au yeyote miongoni mwao, kwenda kwenye mapumziko kwa ajili

ya kutafakari maoni yao ikiwa wanahitaji kufanya hivyo; au wakati wowote huo wa mapumziko, au wakati wowote wa usikilizaji wa kesi, kushauriana miongoni mwao.

(5) Ikiwa kesi ilisikilizwa bila ya msaada wa washauri wa mahakama, Jaji ataendelea kutoa hukumu.

## Utoaji wa Adhabu

Kumuita mshtakiwa.

**269.** Ikiwa Jaji anamtia hatiani mshtakiwa au ikiwa mshtakiwa anakiri kosa, itakuwa ni wajibu wa mahakama kumuuliza mshtakiwa kama ana chochote cha kusema kwa nini adhabu isitolewe kwake yeye kwa mujibu wa sheria, lakini kuacha kumuuliza mshtakiwa hakutakuwa na athari katika uhalali wa mwenendo wa kesi.

Hoja ya kuzuia hukumu.

**270.**-(1) Mshtakiwa anaweza, wakati wowote kabla ya adhabu, ama kwa kukiri au vyenginevyo, kutoa hoja ya kuzuia hukumu kwa sababu kwamba taarifa ya shtaka, baada ya marekebisho yoyote ambayo mahakama iliyafanya na ilikuwa na uwezo wa kuyafanya, haielezi kosa lolote ambalo mahakama ina mamlaka ya kulisikiliza.

(2) Mahakama inaweza, kwa uwezo wake, ama kusikiliza na kuamua jambo hilo katika kikao hicho, au kuakhirisha usikilizaji wa jambo hilo hadi wakati mwengine utakaopangwa kwa madhumuni hayo.

(3) Ikiwa mahakama inaamua kwa manufaa ya mshtakiwa ataachiwa huru kutokana na taarifa hiyo ya shtaka.

Adhabu.

**271.** Ikiwa hakuna hoja ya kuzuia hukumu iliyotolewa, au kama mahakama inaamua dhidi ya mshtakiwa kuhusu hoja hiyo, mahakama inaweza kumpa adhabu mshtakiwa wakati wowote wa vikao vya mahakama.

Uwezo wa kuzuia uamuzi.

**272.**-(1) Mahakama ambayo mbele yake mtu yeyote kesi yake inasikilizwa kwa kosa inaweza kuzuia utoaji wa uamuzi wake wa mwisho juu ya hoja zilizoibuliwa wakati wa usikilizaji, na uamuzi wake wakati wowote utakapotolewa utachukuliwa kuwa umetolewa wakati wa usikilizaji.

(2) Katika mazingira yoyote hakuna uamuzi utakaozuiliwa kwa zaidi ya siku sitini ambapo utamuathiri mshtakiwa.

Pingamizi zilizosawazishwa na uamuzi wa mahakama.

**273.** Hukumu haitosimamishwa au kuzuiliwa kutokana na hoja ya pingamizi yoyote, ambayo kama ingeelezwa baada ya taarifa ya shtaka kusomwa kwa mshtakiwa, au wakati usikilizaji wa kesi unaendelea, ingeweza kurekebishwa na mahakama, na siyo kwa ajili ya kasoro yoyote katika kuwaapisha mashahidi au yeyote miongoni mwa mashahidi.

Ushahidi kwa ajili ya kufikia adhabu inayofaa.

**274.** Mahakama inaweza, kabla ya kutoa adhabu, kupokea ushahidi huo kama inavyoona inafaa, ili kujiridhisha yenyewe kuhusu adhabu inayofaa kutolewa.

## SEHEMU YA KUMI NA MOJA
## HATIA NA HUKUMU

### Kutiwa hatiani kwa makosa ambayo siyo aliyoshtakiwa nayo mshtakiwa

Iwapo kosa limethibitishwa linajumuishwa na kosa lililoshtakiwa.

**275.**-(1) Pale mtu anashtakiwa kwa kosa linalokusanya maelezo tofauti, mkusanyiko wa baadhi ya maelezo hayo tu yanaweza kutengeneza kosa dogo lililokamilika, na mkusanyiko huo unathibitishwa lakini maelezo yaliyobakia hayakuthibitishwa, anaweza kutiwa hatiani kwa kosa dogo ingawa mtu huyo hakushtakiwa kwa kosa hilo.

(2) Pale mtu anashtakiwa kwa kosa na maelezo yanathibitika ambayo yanalishusha kuwa kosa dogo, anaweza kutiwa hatiani kwa kosa dogo ingawa mtu huyo hakushtakiwa kwa kosa hilo.

Mtu anayeshtakiwa kwa kosa lolote anaweza kutiwa hatiani kwa kujaribu kutenda kosa.

**276.** Pale mtu anashtakiwa kwa kosa, anaweza kutiwa hatiani kwa kosa la kujaribu kutenda kosa hilo ingawa mtu huyo hakushtakiwa kwa kujaribu kutenda kosa.

Mwanamke anayeshtakiwa kwa kosa la kuua kwa makusudi mtoto wake anaweza kutiwa hatiani kwa kosa la kuua mtoto mchanga.

**277.** Wakati mwanamke anashtakiwa kwa kosa la kuua kwa makusudi mtoto wake, akiwa mtoto wa chini ya miezi kumi na mbili, na mahakama inaona kwamba:

(a) mwanamke huyo kwa kutenda kitendo chochote cha makusudi au kuacha kutenda kitendo chochote anasababisha kifo cha mtoto huyo lakini wakati wa kutenda huko au kuacha kutenda huko mwanamke huyo bado hajapona vizuri kutoka katika athari ya uzazi wa mtoto huyo; na

(b) kwa sababu hiyo au kwa sababu ya athari ya kunyonyesha kufuatia kuzaliwa kwa mtoto huyo, usawa wa akili yake uliathiriwa,

anaweza, bila ya kujali kwamba mazingira yalikuwa kiasi hicho lakini kwa mujibu wa masharti ya kifungu cha 187 cha Sheria ya Adhabu, angeweza kutiwa hatiani kwa kosa la kuua kwa kukusudia, kutiwa hatiani kwa kosa la kuua mtoto mchanga ingawa mtu huyo hakushtakiwa kwa kosa hilo.

Mtu anayeshtakiwa kwa kosa la kuharibu mtoto anaweza kutiwa hatiani kwa kosa dogo.

**278.** Pale mtu anashtakiwa kwa kosa la kuharibu mtoto na mahakama inaona kwamba mtu huyo siyo mkosa wa kosa hilo lakini mtu huyo ni mkosa wa kosa linalohusiana na kujaribu kuwezesha kutoa mimba au kutoa mimba kwa mwanamke mwenye mtoto, mtu huyo anaweza kutiwa hatiani kwa kosa la kujaribu kuwezesha kutoa mimba au kutoa mimba kwa mwanamke mwenye mtoto, ingawa mtu huyo hakushtakiwa kwa kosa hilo.

Mtu anashtakiwa kwa kosa la kuua kwa makusudi au kuua mtoto mchanga au kuua mtoto aliyekuwa hajazaliwa anaweza kutiwa hatiani kwa kosa la kuficha kuzaa.

**279.** Pale mtu anashtakiwa kwa kosa la kuua kwa makusudi au kuua mtoto yeyote mchanga au kuua mtoto ambaye hajazaliwa na mahakama inaona kwamba mtu huyo siyo mkosa wa makosa yoyote yaliyotajwa lakini ikiwa inaonekana kwenye ushahidi kwamba mtoto huyo muda mfupi tu ameshazaliwa na kwamba mtu huyo, kwa njia za siri amezika mwili wa mtoto huyo aliyekufa, amefanya juhudi kuficha kuzaliwa kwa mtoto huyo, anaweza kutiwa hatiani kwa kosa la kuficha kuzaliwa kwa mtoto huyo ingawa mtu huyo hakushtakiwa kwa kosa hilo.

Uwezo wa kutia hatiani kwa kosa la uzembe au uendeshaji wa hatari katika usikilizaji wa kesi kwa kuua bila ya kukusudia.

**280.** Kufuatia usikilizaji wa kesi ya mtu ambaye anashtakiwa kwa kosa la kuua bila ya kukusudia inayohusiana na kuendesha kwake chombo cha moto, ikiwa mahakama inaridhika kwamba mtu huyo ni mkosa wa kosa la uzembe au la uendeshaji wa hatari chini ya Sheria ya Usafiri Barabarani, mtu huyo anaweza kuonekana ni mkosa wa kosa hilo ama kwa masharti ya Sheria hiyo iliyotajwa mwisho, au bila ya masharti ya Sheria hiyo, ambayo yanahusu notisi ya upande wa mashtaka, yametekelezwa kuhusu kosa hilo.

Mtu anashtakiwa kwa kosa la kubaka anaweza kutiwa hatiani kwa kosa lolote chini ya masharti ya Sheria ya Adhabu.

**281.** Pale mtu anashtakiwa kwa kosa la kubaka na mahakama inaona kwamba mtu huyo siyo mkosa wa kosa hilo lakini mtu huyo ni mkosa wa kosa chini ya masharti ya Sheria ya Adhabu yanayohusu makosa yanayohusisha shambulio la aibu au kumkashifu mwanamke, kuwezesha ngono haramu na kuingilia maharimu, anaweza kutiwa hatiani kwa kosa hilo, ingawa mtu huyo hakushtakiwa kwa kosa hilo.

Mtu anayeshtakiwa kwa kosa la kuingilia maharimu anaweza kutiwa hatiani kwa kosa la kuingilia bila ya halali.

**282.** Pale mtu anashtakiwa kwa kosa la kuingilia maharimu chini ya Sheria ya Adhabu na mahakama inaona kwamba mtu huyo siyo mkosa wa kosa hilo, lakini kwamba mtu huyo ni mkosa wa kosa la kunajisi mtu mwenye ulemavu wa akili au shambulio la aibu chini ya Sheria iliyotajwa, anaweza kutiwa hatiani kwa kosa hilo, ingawa mtu huyo hakushtakiwa kwa kosa hilo.

Mtu anayeshtakiwa kwa kosa la kunajisi mtoto wa kiume anaweza kutiwa hatiani kwa kosa chini ya masharti mengine ya Sheria ya Adhabu.

**283.** Pale mtu anashtakiwa kwa kosa la kunajisi mtoto wa kiume na mahakama inaona kwamba mtu huyo siyo mkosa wa kosa hilo lakini ni mkosa wa kosa la shambulio la aibu au kukashifu au kuwezesha ngono haramu chini ya Sheria ya Adhabu, anaweza kutiwa hatiani kwa kosa hilo, ingawa mtu huyo hakushtakiwa kwa kosa hilo.

Mtu anayeshtakiwa kwa kosa la kuvunja nyumba usiku anaweza kutiwa hatiani kwa kosa linalofanana na hilo.

**284.** Pale mtu anashtakiwa kwa kosa lolote chini ya Sheria ya Adhabu linalohusu kuvunja jengo usiku, kuvunja nyumba mchana au makosa yanayofanana na hayo, na mahakama inaona kwamba mtu huyo siyo mkosa wa kosa hilo lakini kwamba mtu huyo ni mkosa wa kosa jengine lolote linalofanana na hayo, anaweza kutiwa hatiani kwa kosa hilo jengine, ingawa mtu huyo hajashtakiwa kwa kosa hilo.

Mtu anayeshtakiwa kwa kosa la kuiba anaweza kutiwa hatiani kwa kosa la kupokea mali ya wizi au kupata mali kwa njia ya kujisingizia.

**285.**-(1) Pale mtu anaposhtakiwa kwa kosa la kuiba kitu chochote na:

(a) inathibitika kwamba mtu huyo amepokea au amezuia kitu kwa kujua au akiwa na sababu ya kuamini kuwa kitu hicho kimeibiwa, mtu huyo anaweza kutiwa hatiani kwa kosa la kupokea au kuzuia kitu kama hali itakavyokuwa, ingawa mtu huyo hakushtakiwa kwa kosa hilo; au

(b) inathibitika kwamba mtu huyo amepata kitu hicho kwa namna yoyote ambayo angeweza, chini ya masharti ya Sheria ya Adhabu, kukipata kitu hicho kwa njia ya kujisingizia kwa nia ya kuhadaa, anaweza kutiwa hatiani kwa kosa la kujipatia kitu kwa njia ya kujisingizia ingawa mtu huyo hakushtakiwa kwa kosa hilo.

(2) Pale mtu anashtakiwa kwa kosa la kupokea kitu chochote akijua kitu hicho kuwa kimeibiwa, na inathibitika kwamba amekizuia kitu hicho akijua kitu hicho kuwa kimeibiwa, anaweza kutiwa hatiani kwa kosa la kuzuia kitu hicho ingawa mtu huyo hakushtakiwa kwa kosa hilo.

(3) Pale mtu anashtakiwa kwa kosa la kuzuia kitu chochote akijua kitu hicho kuwa kimeibiwa, na inathibitika kwamba mtu huyo amepokea kitu hicho akijua kitu hicho kuwa kimeibiwa, anaweza kutiwa hatiani kwa kosa la kupokea kitu hicho ingawa mtu huyo hakushtakiwa kwa kosa hilo.

Hukumu mbadala katika mashtaka ya kupatikana na mali inayotuhumiwa kuwa imepatikana kwa njia ya rushwa.

**286.** Pale mtu anashtakiwa kwa kosa lolote chini ya masharti na Sheria ya Kupambana na Rushwa na Makosa ya Kuhujumu Uchumi Zanzibar yanayohusu kupata au kupokea mali kwa njia ya rushwa, na mahakama inaona kwamba mtu huyo hakupata au kupokea mali hiyo kwa njia ya rushwa, lakini kwamba mtu huyo ni mkosa wa kosa chini ya masharti ya Sheria ya Adhabu kuhusiana na matumizi mabaya ya mali bila ya uaminifu, mahakama inaweza kumtia hatiani mtu huyo kwa kosa hilo ingawa mtu huyo hakushtakiwa kwa kosa hilo.

Mtu anayeshtakiwa kwa kujipatia mali kwa njia ya kujisingizia anaweza kutiwa hatiani kwa kosa la kuiba.

**287.** Pale mtu anashtakiwa kwa kosa la kujipatia kitu chochote kinachoweza kuibiwa kwa njia ya kujisingizia kwa nia ya hadaa, na ikathibitika kwamba amekiiba kitu hicho mtu huyo anaweza kutiwa hatiani kwa kosa la kuiba ingawa mtu huyo hakushtakiwa kwa kosa hilo.

Tafsiri ya vifungu vya 275 hadi 287.

**288.** Masharti ya vifungu vya 275 hadi 287 vya Sheria hii, vyote kwa pamoja, vitatafsiriwa kama nyongeza ya, na siyo kuondoa masharti ya sheria nyengine yoyote na masharti mengine ya Sheria hii, na masharti ya vifungu vya 277 hadi 285 vya Sheria hii, vyote kwa pamoja, vitatafsiriwa bila kuathiri ujumla wa masharti ya kifungu cha 276 cha Sheria hii.

## Hukumu

Utaratibu wa kutoa Hukumu.

**289.**-(1) Hukumu, katika usikilizaji wa kesi yoyote katika mahakama yoyote ya jinai, katika utekelezaji wa mamlaka yake ya awali, itasomwa, au maudhui ya hukumu hiyo yataelezwa, katika mahakama ya wazi mara tu baada ya kukamilika kwa usikilizaji wa kesi au katika wakati ujao, katika hali yoyote, usizidi siku sitini ambazo notisi itatolewa kwa wahusika wa kesi au mawakili wao, ikiwa wapo.

(2) Hukumu yote itasomwa na Jaji anayeongoza mahakama inayosikiliza kesi au hakimu ikiwa anatakiwa kufanya hivyo ama na upande wa mashtaka au upande wa utetezi.

(3) Mshtakiwa, ikiwa yupo katika kizuizi, ataletwa, au, ikiwa hayupo katika kizuizi, atatakiwa na mahakama kufika mbele ya mahakama hiyo, kusikiliza hukumu inayotolewa, isipokuwa pale uhudhuriaji wake binafsi wakati wa usikilizaji wa kesi haukuhitajika au mshtakiwa huyo anaachiwa huru.

(4) Hukumu iliyotolewa na mahakama yoyote haitachukuliwa kuwa siyo halali kwa sababu tu ya kutokuwepo upande wowote au wakili wake katika siku au pahala

ambapo pametajwa kwa ajili ya kutolewa hukumu hiyo, au kwa kutokupeleka hati ya wito, au kuwepo kwa makosa katika kupeleka hati, kwa wahusika wa kesi au mawakili wao, au mmoja kati ya hao, notisi ya siku hiyo na pahali.

(5) Hakuna chochote katika kifungu hiki kitakachotafsiriwa kuwa katika hali yoyote kinaweka ukomo kwa masharti ya kifungu cha 381 cha Sheria hii.

Yaliyomo kwenye hukumu.

**290.**-(1) Kila hukumu hiyo, isipokuwa kama itaelezwa vyenginevyo katika Sheria hii, itaandikwa na Jaji au hakimu wa mahakama anayesikiliza kesi hiyo katika lugha ya mahakama, na itajumuisha hoja kwa ajili ya maamuzi, uamuzi na sababu za uamuzi huo, na itawekwa tarehe na kutiwa saini na Jaji au hakimu aliyesikiliza kesi hiyo katika mahakama ya wazi wakati wa kusomwa hukumu hiyo.

(2) Katika kesi ya kutiwa hatiani, hukumu itaainisha kosa ambalo na kifungu ambacho, Sheria ya Adhabu au sheria nyengine ambayo mshtakiwa anatiwa hatiani, na adhabu ambayo mshtakiwa huyo anaadhibiwa nayo.

(3) Katika kesi ambayo mshtakiwa anaachiwa huru, hukumu itaeleza kosa ambalo mshtakiwa anaachiwa huru kwa kosa hilo na itaelekeza kwamba mshtakiwa huyo aachiwe huru.

Haki ya mshtakiwa kupatiwa nakala ya hukumu.

**291.**-(1) Kufuatia ombi la mshtakiwa nakala ya hukumu, au, pale anapohitaji, tafsiri katika lugha yake, kama inawezekana, atapewa bila kuchelewa.

(2) Kufuatia ombi la Mkurugenzi wa Mashtaka, nakala ya hukumu, atapewa bila kuchelewa.

(3) Nakala ya hukumu hiyo au tafsiri ya hukumu hiyo itatolewa bila ya gharama.

## SEHEMU YA KUMI NA MBILI
## ADHABU NA UTEKELEZAJI WAKE

### Aina tofauti za adhabu.

Aina Tofauti za Adhabu

**292.** Adhabu zifuatazo zinaweza kutolewa na mahakama:

(a) kifo;

(b) kifungo;

(c) kutumikia jamii;

(d) faini;

(e) kutaifisha;

(f) malipo ya gharama;

(g) malipo ya fidia;

(h) kuweka dhamana kwa ajili ya kutunza amani na kuwa na tabia njema, au kufika mahakamani kwa ajili ya hukumu;

(i) uangalizi;

(j) kufuta au kusimamisha leseni ya udereva chini ya Sheria ya Usafiri Barabarani;

(k) kuachiwa kwa masharti chini ya Sheria ya Uangalizi wa Wahalifu;

(l) amri kuhusu skuli zilizoidhinishwa chini ya Sheria ya Watoto;

(m) adhabu nyengine yoyote inayotolewa na Sheria ya Adhabu au sheria nyengine yoyote.

**Adhabu ya Kifo**

Adhabu ya kifo.

**293.**-(1) Endapo mtu yeyote anahukumiwa adhabu ya kifo, adhabu hiyo itaelekeza kwamba mtu huyo atanyongwa shingoni mpaka afe.

(2) Adhabu ya kifo haitotamkwa au kurekodiwa dhidi ya:

(a) mwanamke ambaye ni mja mzito kwa mujibu wa masharti ya kifungu cha 294 cha Sheria hii, lakini badala yake mahakama itamhukumu mwanamke huyo kifungo cha maisha;

(b) mtu ambaye mahakama inaona alikuwa, wakati kosa linatendwa, chini ya umri wa miaka kumi na nane, lakini badala yake mahakama itamhukumu mtu huyo awekwe kizuizini kama Rais atakavyoona inafaa, na ikiwa amehukumiwa hivyo atawajibika kuwekwa kizuizini katika pahala ambapo na katika masharti ambayo kama Rais atakavyoelekeza, na wakati akiwa kizuizini itachukuliwa kuwa yupo katika kizuizi halali.

(3) Pale mtu ameshahukumiwa adhabu ya kuwa kizuizini kama apendavyo Rais chini ya aya ya (b) ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki, Jaji anayesikiliza kesi atapeleka kwa Rais nakala ya maelezo ya ushahidi yaliyochukuliwa wakati wa usikilizaji wa kesi, pamoja na ripoti ya maandishi iliyosainiwa na Jaji huyo inayojumuisha mapendekezo na maoni juu ya kesi kama anavyoona inafaa kuyatoa.

Utaratibu pale mwanamke aliyetiwa hatiani kwa kosa lenye adhabu ya kifo anapodai kuwa yeye ni mja mzito.

**294.**-(1) Pale mwanamke aliyetiwa hatiani kwa kosa lenye adhabu ya kifo anadai kwamba yeye ni mja mzito, au pale mahakama ambayo mbele yake mwanamke anatiwa hatiani inaona kuwa inafaa kuamrisha hivyo, suala ama mwanamke huyo ni mja mzito au siyo mjamzito, kabla hukumu haijatolewa kwake, litaamuliwa na mahakama.

(2) Suala ama mwanamke ni mja mzito au siyo mja zito litaamuliwa na mahakama kwa ushahidi ambao unaweza kuletwa mbele yake ama na upande wa mwanamke huyo au na upande wa Mkurugenzi wa Mashtaka, na mahakama, kama hali itakavyokuwa, itaamua kwamba mwanamke huyo hana uja uzito isipokuwa kama itathibitika kwa uhakika wa kujiridhisha kwake kwamba mwanamke huyo ni mja mzito.

Rufaa ya uamuzi kwamba mwanamke siyo mja mzito.

**295.** Pale mwenendo wa kesi chini ya kifungu cha 294 cha Sheria hii, mahakama inaona kwamba mwanamke husika siyo mja mzito, mwanamke huyo anaweza kukata rufaa katika Mahakama ya Rufaa na mahakama hiyo, ikiwa itaridhika kwamba kwa sababu yoyote uamuzi unapaswa kutenguliwa, itaifuta adhabu iliyotolewa kwa mwanamke huyo na badala ya adhabu hiyo itatoa kwa mwanamke huyo adhabu ya kifungo cha maisha.

Mshtakiwa kujulishwa haki ya kukata rufaa.

**296.** Endapo mshtakiwa anahukumiwa adhabu ya kifo, mahakama itamjulisha mtu huyo haki yake ya kukata rufaa na kipindi ambacho, ikiwa atapenda kukata rufaa, rufaa yake itapaswa kuwasilishwa.

Uthibitisho kwa ajili ya kuweka kizuizini.

**297.** Hati iliyotolewa na Jaji au Mrajis kwamba adhabu ya kifo imetolewa, na kumtaja mtu aliyehukumiwa kifo, itakuwa ni uthibitisho wa kutosha kwa ajili ya kumuweka mtu huyo kizuizini.

Kumbukumbu na taarifa kupelekwa kwa Rais.

**298.**-(1) Mapema iwezekanavyo baada ya adhabu ya kifo kutolewa, ikiwa hakuna rufaa kuhusiana na adhabu hiyo imewasilishwa, au ikiwa rufaa hiyo imewasilishwa na adhabu hiyo imethibitishwa, baadae mapema iwezekanavyo baada ya uthibitisho huo, Jaji anayesikiliza kesi hiyo atawasilisha kwa Rais nakala ya maelezo ya ushahidi uliochukuliwa katika usikilizaji wa kesi, pamoja na taarifa ya maandishi iliyosainiwa na Jaji huyo inayojumuisha mapendekezo yoyote au maoni kuhusu kesi hiyo kama anavyoona inafaa kuyatoa.

(2) Mahakama, baada ya kupokea amri ya uthibitisho wa **adhabu** au amri nyengine kutoka kwa Rais, kama hali itakavyokuwa, itatoa hati au itachukua hatua nyengine kama itakavyokuwa ni lazima kwa ajili ya utekelezaji wa amri hiyo au amri hizo.

## Adhabu ya Kifungo

Kifungo.

**299.** Mtu anayewajibika kupewa adhabu ya kifungo cha maisha au kipindi chengine chochote cha kifungo anaweza kuhukumiwa kwa kipindi chochote kifupi zaidi.

Hati kwa adhabu ya kifungo.

**300.**-(1) Hati inayotolewa na Jaji au hakimu kwamba mshtakiwa ataadhibiwa kwa kifungo, inayoamrisha kuwa adhabu itatekelezwa katika Chuo cha Mafunzo chochote ndani ya Zanzibar, itatolewa na Jaji au hakimu anayetoa adhabu, na itakuwa ushahidi wa kutosha kwa afisa dhamana wa Chuo cha Mafunzo hicho na kwa watu wengine wowote kwa ajili ya utekelezaji wa adhabu iliyoelezwa katika hati hiyo.

(2) Isipokuwa endapo imeelezwa vyenginevyo katika Sheria hii, kila adhabu itachukuliwa kuanza kutoka, na kujumuisha siku yote nzima na tarehe ambayo adhabu hiyo ilitolewa.

Kutumika kizuizi cha polisi kwa ajili ya kifungo kidogo.

**301.**-(1) Bila ya kuathiri chochote kilichomo katika kifungu cha 300 cha Sheria hii, hakuna adhabu ya kifungo kwa kipindi kilicho chini ya siku tano, ama kilichotolewa kama adhabu kamili au kwa sababu ya kutokulipa fedha ambapo kutokupatikana kwa fedha hizo kifungo kinaweza kutolewa, itakayotekelezwa katika Chuo cha Mafunzo chochote ndani ya Zanzibar.

(2) Mahakama inaweza, ikiwa pahala popote panapofaa pameelezwa na pamethibitishwa katika namna itakayoelezwa baadae panapatikana kwa madhumuni hayo, itaamrisha mtu huyo kuwekwa kizuizini hapo kwa kipindi hicho kisichozidi siku nne kama mahakama inavyoona inafaa, na amri hiyo itapelekwa pamoja na mkosaji kwa mtu mwenye dhamana ya pahala ambapo mkosaji atawekwa kizuizini, na itakuwa ni uthibitisho wa kutosha kwa kuweka kwake kizuizini katika pahala hapo kwa mujibu wa masharti hayo.

(3) Gharama za kuwakimu watu kwenye kizuizi chini ya kifungu hiki italipwa katika utaratibu kama ule wa gharama za kuwakimu wanafunzi katika vyuo vya mafunzo ambavyo Sheria ya Vyuo vya Mafunzo inatumika.

(4) Rais anaweza, kwa ombi la Kamishna wa Polisi, kuthibitisha jengo lolote kuwa pahala panapofaa kwa ajili ya kuwaweka kizuizini watu walioadhibiwa kuwekwa kizuizini chini ya kifungu hiki, na anaweza kutunga kanuni kwa ajili ya ukaguzi wa pahala hapo palipoelezwa, huduma za watu wanaowekwa kizuizini pahala hapo, na kwa ujumla kwa ajili ya utekelezaji wa kifungu hiki ipasavyo.

(5) Pahala palipothibitishwa hapatatumika kwa ajili ya kuwaweka kizuizini wanawake isipokuwa kama masharti yanawekwa **kuwa wanawake hao wataangaliwa na mwanamke mwenzao.**

Adhabu kuchanganywa isipokuwa pale itakapoamuliwa vyenginevyo.

**302.**-(1) Endapo mtu baada ya kutiwa hatiani kwa kosa anatiwa hatiani kwa kosa jengine, ama kabla ya adhabu kutolewa kwa mtu huyo chini ya hatia ya awali au kabla ya kumalizika kwa adhabu hiyo, adhabu yoyote, isipokuwa adhabu ya kifo ambayo inatolewa kwa mtu huyo kwa hatia inayofuata, itatekelezwa baada ya kumalizika kwa adhabu ya awali, isipokuwa kama mahakama inaeleza kwamba itatekelezwa pamoja na adhabu ya awali au sehemu yoyote ya adhabu hiyo.

(2) Haitokuwa halali kwa mahakama kuelekeza kwamba adhabu ya kifungo kwa sababu ya kutokulipa faini itatekelezwa pamoja na adhabu ya awali chini ya kifungu cha 320 cha Sheria hii.

Adhabu katika hali ya hatia kwa makosa tofauti katika usikilizaji mmoja wa kesi.

**303.**-(1) Pale mtu anatiwa hatiani katika usikilizaji mmoja wa kesi wa makosa mawili tofauti au zaidi mahakama inaweza kumpa adhabu mtu huyo, kwa makosa hayo, kwa adhabu tofauti zilizoelezwa kuhusu makosa hayo ambayo Mahakama hiyo ina uwezo wa kutoa; adhabu hizo, pale inapojumuisha kifungo, itaanza moja baada ya kumalizika nyengine katika utaratibu ambao Mahakama inaweza kuelekeza, isipokuwa pale mahakama inapoelekeza kwamba adhabu hizo zitatekelezwa kwa pamoja.

(2) Katika hali ya adhabu zinazotolewa kutekelezwa moja baada ya nyengine haitokuwa lazima kwa Mahakama, kwa sababu tu mjumuiko wa adhabu kwa makosa tofauti unazidi adhabu ambayo Mahakama ina mamlaka ya kutoa kwa hatia ya kosa moja, kumpeleka mkosaji kwa ajili ya usikilizaji wa kesi mbele ya Mahakama ya juu, kama inavyoelezwa ifuatavyo:

(a) katika mazingira yoyote yale isipokuwa pale mtu anatiwa hatiani kwa kosa ambalo anaadhibiwa kwa kifungo cha maisha, mtu huyo hataadhibiwa kwa kifungo kikubwa cha zaidi ya miaka kumi na nne;

(b) ikiwa kesi inasikilizwa na mahakama ya chini adhabu mjumuiko haitozidi mara mbili ya kiwango cha adhabu ambacho mahakama, katika kutumia mamlaka yake ya awali, ina uwezo wa kutoa.

(3) Kwa madhumuni ya rufaa, mjumuiko wa adhabu mbali mbali zinazotolewa chini ya kifungu hiki katika hali ya hatia ya makosa mawili au zaidi katika usikilizaji mmoja wa kesi utachukuliwa kuwa ni adhabu moja.

Adhabu kwa mkosaji ambaye tayari ameshaadhibiwa kwa kosa jengine.

**304.**-(1) Endapo mtu tayari anatumikia adhabu ya kifungo anapewa adhabu kwa hatia inayofuata ya kifungo au kifungo cha maisha, kifungo hicho au kifungo cha maisha kitaanza baada ya kumalizika kwa kifungo ambacho mtu huyo awali alitiwa hatiani, isipokuwa kama pale mahakama inaelekeza kwamba adhabu inayofuata itatekelezwa pamoja na adhabu ya awali.

(2) Endapo mtu tayari anatumikia adhabu ya kifungo cha maisha anapewa adhabu kwa hatia inayofuata ya kifungo kwa kipindi au kifungo cha maisha adhabu inayofuata itatekelezwa na adhabu hiyo ya awali.

Wanafunzi wanaotoroka kutumikia kifungo kilichokuwa hakijamaliza pale anapokamatwa.

**305.** Pale adhabu inatolewa kwa mwanafunzi aliyetoroka, adhabu hiyo, ikiwa ya kifo au faini, kwa kuzingatia masharti ya Sheria hii, itaanza kutekelezwa mara tu, na ikiwa ni adhabu ya kifungo itaanza kutekelezwa kwa mujibu wa kanuni zifuatazo:

(a) ikiwa adhabu mpya ni kali katika uhalisia wake kuliko adhabu ambayo mwanafunzi huyo alikuwa anaitumikia wakati alipotoroka, adhabu mpya itaanza mara tu; au

(b) pale adhabu mpya siyo kali katika uhalisia wake kuliko adhabu ambayo mwanafunzi huyo alikuwa anaitumikia wakati alipotoroka, adhabu mpya itaanza baada ya kutumikia kifungo kwa kipindi cha ziada sawa na kile ambacho wakati wa utorokaji wake, kilichokuwa hakijamalizika katika adhabu yake ya awali.

Kufutwa kwa adhabu ya viboko.

**306.** Mahakama ya kisheria au Baraza la Maamuzi lililoanzishwa kwa sheria halitotoa adhabu ya viboko kwa mtu yeyote ndani ya Zanzibar.

**Faini**

Faini badala ya au ziada ya kifungo.

**307.**-(1) Mtu yeyote anayewajibika kupewa adhabu ya kifungo kwa kosa dhidi ya sheria yoyote anaweza kuadhibiwa:

(a) kwa kutozwa faini pamoja na kifungo; au

(b) kwa kulipa faini badala ya kifungo kwa makosa yenye adhabu ya kifungo kisichozidi miaka miwili.

(2) Katika hali yoyote endapo faini inaainishwa kama mbadala wa kifungo mtu huyo hatowajibika kwa adhabu zote mbili faini na kifungo isipokuwa kama kuwajibika huko kumeelezwa bayana.

Uwezo wa Mahakama.

**308.** Pale faini inatozwa chini ya sheria yoyote, baadae kwa kukosekana masharti ya wazi kuhusu faini hiyo katika sheria hiyo, masharti yafuatayo yatatumika:

(a) endapo hakuna kiwango kilichotajwa ambacho faini inaweza kuongezeka, kiwango cha faini hiyo ambacho kinaweza kuongezwa huwa hakina ukomo, lakini hakitakuwa kikubwa;

(b) katika hali ya kosa ambalo adhabu yake ni faini au kifungo kwa kipindi utozaji wa faini au utoaji wa adhabu ya kifungo utakuwa ni jambo litakalokuwa chini ya uwezo wa maamuzi ya mahakama;

(c) katika hali ya kosa ambalo adhabu yake ni kifungo pamoja na faini ambalo mkosaji ataadhibiwa kulipa faini na kifungo au bila ya kifungo, na katika hali yoyote ya kosa adhabu yake ni faini pekee ambalo mkosaji anaadhibiwa kulipa faini, mahakama inayotoa adhabu inaweza, katika uwezo wake:

(i) kutoa maelekezo kwa adhabu yake kwamba katika kushindwa kulipa faini mkosaji atatumikia kifungo kwa kipindi maalum, kifungo ambacho kitakuwa ni pamoja na kifungo chengine chochote ambacho ameweza kuadhibiwa au anaweza kuwajibika kwa kubadilishiwa adhabu; au

(ii) kutoa hati kwa ajili ya malipo ya kiwango kuhusu mali isiyohamishika au inayohamishika ya mkosaji kwa ajili ya ukamataji au kuuza chini ya hati.

Kutaifisha.

**309.**-(1) Mahakama inaweza, baada ya kutiwa hatiani mtu kwa kosa chini ya Sheria ya Adhabu kuamuru kwamba kitu chochote kilichobebwa au kutumiwa na mtu huyo kuhusiana na utendekaji wa kosa kutaifishwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

(2) Pale mtu yeyote anatiwa hatiani kwa moja ya makosa yafuatayo chini ya Sheria ya Adhabu yaani:

(a) kufifilisha kosa chini ya kifungu cha 84; au

(b) kufifilisha shtaka chini ya kifungu cha 85,

mahakama inaweza, pamoja na, au badala ya, adhabu yoyote ambayo inaweza kutolewa, kuamuru Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kutaifisha mali yoyote ambayo imetumika kuhusiana na utendwaji wa kosa hilo, au, ikiwa mali hiyo haiwezi kutaifishwa au haiwezi kupatikana,itatoza kiwango ambacho mahakama itatathmini kama thamani ya mali hiyo.

(3) Malipo ya kiwango chochote kilichoamriwa kutaifishwa yanaweza kutekelezwa katika namna ile ile na katika mazingira yale yale kama katika ulipaji wa faini.

**Gharama**

Uwezo wa kutoza gharama dhidi ya mshtakiwa au mwendesha mashtaka binafsi.

**310.**-(1) Itakuwa ni halali kwa Jaji wa Mahakama Kuu au hakimu wa mahakama ya chini kuamuru mtu aliyetiwa hatiani mbele yake kwa kosa lolote kumlipa mwendesha mashtaka binafsi kiwango cha gharama kinachostahili kama Jaji au hakimu huyo atakavyoona inafaa, ikiwa ni pamoja na adhabu nyengine yoyote iliyotolewa.

(2) Ikiwa mashtaka yanaendeshwa na mwendesha mashtaka binafsi, itakuwa ni halali kwa Jaji wa Mahakama Kuu au hakimu wa mahakama ya chini ambaye anamuachia huru au anamuachia mshtakiwa kwa kosa lolote, kumuamuru mwendesha mashtaka huyo binafsi kumlipa mshtakiwa gharama inayofaa kama Jaji au hakimu huyo anavyoweza kuona inafaa.

(3) Amri hiyo chini ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki, haitatolewa kama Jaji au hakimu anaona kwamba mwendesha mashtaka binafsi alikuwa na sababu za msingi za kuleta malalamiko yake.

(4) Gharama zinazotozwa chini ya kifungu hiki zinaweza kutozwa pamoja na fidia yoyote inayotozwa chini ya kifungu cha 314 cha Sheria hii.

Haki ya rufaa kutokana na amri ya gharama.

**311.**-(1) Rufaa itakuwepo kutoka katika amri yoyote ya kutoza gharama chini ya kifungu cha 310 cha Sheria hii, ikiwa amri ilitolewa na hakimu rufaa itapelekwa Mahakama Kuu na ikiwa amri ilitolewa na Jaji rufaa itapelekwa Mahakama ya Rufaa.

(2) Mahakama yenye kusikiliza rufaa itakuwa na uwezo wa kutoza gharama za rufaa kama itakavyoona inafaa.

Kurejesha gharama.

**312.** Kiwango kilichoruhusiwa kwa ajili ya gharama katika kesi zote kitaainishwa katika hatia au amri, na kiwango hicho kitarejeshwa katika utaratibu unaofanana kama ule wa adhabu yoyote inavyoweza kurejeshwa chini ya Sheria hii.

**Fidia**

Mahakama inaweza kuamuru fidia.

**313.**-(1) Mahakama iliyomtia hatiani mshtakiwa inaweza au kwa maombi ya upande wa mashtaka, kuamuru mtu huyo aliyetiwa hatiani kumlipa fidia muathirika wa jinai.

(2) Fidia hiyo inaweza kuwa pamoja na adhabu nyengine yoyote inayotolewa chini ya sheria yoyote.

Fidia katika kesi za makosa ya kingono.

**314.** Pale mahakama inapomtia hatiani mshtakiwa wa kosa la kingono, pamoja na adhabu yoyote ambayo inaitoa, itaamuru kumtaka mshtakiwa kulipa fidia inayofaa kama inavyoweza kuamua kuwa inalingana na fidia ambayo inapatikana kwenye kesi ya madai kwa muathirika wa kosa la kingono kwa madhara ama ya kimwili au kiakili aliyoyapata muathirika wa jinai kutokana na kosa hilo kuwa limetendwa dhidi yake.

Uwezo wa kuagiza ulipwaji wa gharama au fidia kutoka katika faini.

**315.**-(1) Wakati wowote mahakama yoyote inapotoza faini, au inapothibitisha katika rufaa, mapitio au vyenginevyo adhabu ya faini, au adhabu ambayo faini ni sehemu ya adhabu hiyo, mahakama inaweza, wakati wa kutoa hukumu, kuamuru faini yote au sehemu yoyote ya faini iliyopatikana itumike:

(a) katika kulipa gharama sahihi zilizopatikana katika uendeshaji wa kesi;

(b) katika malipo ya fidia kwa mtu yeyote kwa hasara au madhara yaliyosababishwa na kosa pale fidia halisi kwa maoni ya mahakama inaweza kupatikana katika kesi ya madai.

(2) ikiwa faini imetolewa katika kesi ambayo inaweza kukatiwa rufaa hakuna malipo hayo yatakayofanywa kabla ya kumalizika kwa kipindi kinachoruhusika kuwasilisha rufaa, au, ikiwa rufaa imeshawasilishwa, kabla ya uamuzi wa rufaa hiyo.

(3) Wakati wa kuamuru ulipaji wa fidia katika kesi yoyote ya baadae ya madai inayohusiana na jambo hilo hilo, mahakama itatilia maanani kiwango chochote kilicholipwa au kilichopatikana kama fidia chini ya kifungu hiki.

Uainishaji na upatikanaji wa fidia.

**316.** Kiwango kinachoruhusiwa kwa ajili ya fidia, katika kesi zote, kitaainishwa katika adhabu au amri, na fidia hiyo itapatikana katika namna ile ile kama adhabu yoyote inavyoweza kupatikana chini ya Sheria hii.

## Utekelezaji wa Amri kwa ajili ya Malipo ya Faini, Gharama, au Fidia kwa kukamata Mali

Hati kwa ajili ya kutoza faini.

**317.**-(1) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (5) cha kifungu hiki, pale mahakama inapoamuru fedha kulipwa na mshtakiwa au mwendesha mashtaka binafsi kwa ajili ya faini, adhabu, fidia, gharama, matumizi au vyenginevyo, fedha zinaweza kutozwa katika mali inayohamishika na mali isiyohamishika ya mtu aliyeamriwa kulipa fedha hizo kwa kukamata mali na kuuza chini ya hati.

(2) Ikiwa mshtakiwa au mwendesha mashtaka binafsi anaonesha mali inayohamishika ya kutosha utekelezaji wa amri hiyo, mali yake isiyohamishika haitauzwa.

(3) Mtu huyo anaweza kulipa au kuwasilisha kwa afisa mwenye dhamana ya utekelezaji wa hati hiyo kiwango ambacho kimetajwa katika hati hiyo, pamoja na kiwango cha gharama za ukamataji hadi wakati wa malipo au uwasilishaji, na baada ya hapo afisa huyo atasitisha utekelezaji wa hati hiyo.

(4) Hati chini ya kifungu hiki inaweza kutekelelezwa ndani ya eneo la mipaka ya mamlaka ya mahakama iliyotoa hati hiyo, na itaidhinisha ukamataji na uuzaji wa mali yoyote inayomilikiwa na mtu huyo nje ya mipaka hiyo pale itapothibitishwa na hakimu mwenye mamlaka ya kuendesha mahakama ya chini ndani ya eneo la mipaka ya mamlaka ambapo mali hiyo ilipatikana.

(5) Ikiwa adhabu inaelekeza kwamba ikishindikana kulipwa faini mkosaji apelekwe Chuo cha Mafunzo, na ikiwa mkosaji huyo ameshatumikia kifungo hicho chote kwa kushindwa kulipa faini, hakuna mahakama yoyote itakayotoa hati ya ukamataji mali isipokuwa kwa sababu maalum zitakazorekodiwa kwa maandishi mahakama itakapoona ni lazima.

Pingamizi kwa ukamataji mali.

**318.**-(1) Mtu anayedai kuwa ana haki au ana maslahi ya kisheria au maslahi ya haki katika mali yote au sehemu ya mali yoyote iliyokamatwa katika utekelezaji wa hati iliyotolewa chini ya kifungu cha 317 cha Sheria hii anaweza, wakati wowote kabla ya malipo kutoka mahakamani ya mapato ya mauzo ya mali hiyo, kutoa notisi kwa maandishi kwa Mahakama kuhusu pingamizi yake ya kukamatwa mali hiyo.

(2) Notisi hiyo itaeleza kwa ufupi msingi wa dai ambalo mtu huyo, katika kifungu hiki baadae atajulikana kuwa "mleta pingamizi", analitoa kuhusu mali yote au sehemu ya mali iliyokamatwa, na atathibitisha thamani ya mali hiyo anayoidai mtu huyo, na thamani hiyo itaelezwa kwa hati ya kiapo, ambayo itawasilishwa mahakamani pamoja na notisi hiyo.

(3) baada ya kupokea notisi inayojumuisha thamani iliyotolewa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, mahakama itaelekeza kusimamishwa kwa mwenendo wa utekelezaji, na, ikiwa mapato ya mauzo ya mali hayajapokelewa na mahakama, itatoa notisi kwa maandishi kuhusu mapato hayo kwa afisa mwenye dhamana ya utekelezaji wa hati hiyo.

(4) Pale usimamishwaji wa utekelezaji wa mwenendo umeelekezwa chini ya kifungu kidogo cha (3) cha kifungu hiki, Mahakama, kwa notisi ya maandishi, itamuelekeza mleta pingamizi kufika mbele ya Mahakama hiyo na kuwasilisha dai lake katika tarehe itayoainishwa katika notisi hiyo.

(5) Notisi itapelekwa kwa mtu ambaye mali yake, kwa hati iliyotoewa chini ya kifungu 317 cha Sheria hii, ilielekezwa ikamatwe na, isipokuwa kama mali hiyo itatumika kulipa faini, kwa mtu mwenye haki ya mapato hayo ya mauzo ya mali hiyo.

(6) Notisi hiyo itaainisha muda na pahala palipopangwa kwa ajili ya kufika mleta pingamizi na itamuelekeza mtu ambaye amepelekewa notisi hiyo kufika mbele ya mahakama katika wakati huo na pahala hapo ikiwa atapenda kusikilizwa wakati wa usikilizaji wa pingamizi hiyo.

(7) Katika siku iliyopangwa kwa ajili ya usikilizwaji wa pingamizi mahakama itachunguza dai hilo na, kwa madhumuni hayo, inaweza kusikiliza ushahidi wowote ambao mleta pingamizi anaweza kuutoa au kuuwasilisha na ushahidi wowote unaotolewa au unaowasilishwa na mtu aliyepelekewa notisi kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (5) cha kifungu hiki.

(8) Ikiwa, katika uchunguzi wa dai hilo, mahakama inaridhika kwamba mali iliyokamatwa, wakati wa kukamatwa, haikuwa mikononi mwa mtu aliyeamriwa kulipa fedha au mtu mwengine aliyepewa dhamana kwa niaba ya mtu huyo, au katika ukaazi wa mpangaji au mtu mwengine anayelipa kodi kwa mtu huyo, au kwamba, ipo mikononi

mwa mtu aliyeamriwa kulipa fedha katika wakati huo ilikuwa ipo mikononi mwake siyo kwa sababu ya manufaa yake mwenyewe au kama mali yake mwenyewe lakini kwa manufaa ya au katika dhamana kwa ajili ya mtu mwengine au sehemu ni kwa manufaa yake mwenyewe na sehemu ni kwa manufaa ya mtu mwengine, mahakama itatoa amri inayoiachia mali hiyo kutoka katika ukamataji, yote au kwa kiasi ambacho inaona inafaa.

(9) Ikiwa, katika siku iliyopangwa kwa ajili ya kufika kwake, mleta pingamizi anashindwa kufika, au ikiwa, baada ya uchunguzi wa dai hilo kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (7) cha kifungu hiki, mahakama inaona kwamba mleta pingamizi ameshindwa kuthibitisha dai lake, mahakama itaamuru ukamataji mali na utekelezaji uendelee, na itatoa amri kuhusu gharama kama inavyoona inafaa.

(10) Hakuna chochote katika kifungu hiki kitakachochukuliwa kumnyima mtu aliyeshindwa kutimiza matakwa ya vifungu vidogo vya (1) na (2) vya kifungu hiki haki ya kuchukua hatua nyengine ambazo, mbali ya masharti ya kifungu hiki, zinaweza kisheria kuchukuliwa na mtu anayedai kuwa ana maslahi katika mali iliyokamatwa chini ya hati.

Kasoro au kukosekana muundo katika mwenendo wa kesi hakuwezi kubatilisha ukamataji.

**319.** Hakuna ukamataji unaofanywa chini ya Sheria hii utakaochukuliwa kuwa batili, wala hakuna mtu yeyote anayefanya ukamataji huo wa mali atakayechukuliwa kuwa mvamizi, kutokana na kasoro yoyote au kukosekana muundo katika wito, hatia, hati ya ukamataji mali au mwenendo mwengine unaohusiana na hayo.

## Kifungo Kwa Kushindwa Kulipa Faini, Gharama au Fidia

Kifungo kwa kushindwa kulipa faini.

**320.** Katika hali ya kosa ambalo adhabu yake ni kifungo na pia faini ambalo mkosaji anaadhibiwa kwa kutozwa faini pamoja na kifungo au bila ya kifungo, na katika kila kesi ya kosa ambalo adhabu yake ni faini tu katika kosa hilo mkosaji anaadhibiwa kulipa faini, mahakama katika kutoa adhabu inaweza, katika uwezo wake, kuelekeza katika adhabu yake kwamba anaposhindwa kulipa faini mkosaji atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi fulani, kifungo ambacho kitakuwa ni pamoja na kifungo chengine chochote ambacho anaweza kuwa angeadhibiwa au ambacho anaweza kuwa anawajibika chini ya ubadilishaji wa adhabu.

Uakhirishaji wa adhabu ya kifungo kwa kushindwa kulipa faini.

**321.**-(1) Katika kesi yoyote ambayo amri kwa ajili ya malipo ya fedha inatolewa kwa kutokupatikana fedha hizo ambapo adhabu ya kifungo inaweza kutolewa, na fedha hazijalipwa mara moja, mahakama, bila ya kujali kitu chochote kilichomo katika aya ya (c) ya kifungu cha 308 cha Sheria hii, haitatoa kwa kitendo hicho kwa mtu aliyeamriwa kufanya malipo hayo adhabu ya kifungo kwa kushindwa kulipa kiwango hicho isipokuwa:

(a) mahakama inaridhika kwamba ana uwezo wa kutosha kumuwezesha kulipa malipo hayo mara moja;

(b) baada ya kuulizwa na mahakama ama anahitaji kwamba apewe muda kwa ajili ya kulipa, haelezi kwamba anahitaji hivyo, au anashindwa kuiridhisha mahakama kwamba ana makaazi ya kudumu ndani ya eneo la mipaka ya mamlaka ya mahakama hiyo; au

(c) mahakama inaamua kwamba kwa sababu maalum, ama kwa kuzingatia uzito wa kosa, kwa kuzingatia tabia ya mtu aliyeamriwa kufanya malipo hayo, au kwa kuzingatia mazingira mengine maalum,

inafaa kwamba mkosaji apelekwe Chuo cha Mafunzo bila ya uchunguzi wa ziada kwa kushindwa kulipa.

(2) Endapo mtu yeyote huyo anahitaji kupewa muda kwa ajili ya kufanya malipo mahakama katika kuamua muda gani apewe itazingatia maelezo yoyoye yaliyotolewa na mtu huyo, lakini muda utakaoruhusiwa hautapungua siku saba kamili.

(3) Ikiwa kabla ya kumalizika kwa muda uliotolewa mtu huyo anajisalimisha mwenyewe mahakamani na anaeleza kwamba anapenda apelekwe kizuizini mara moja kuliko kusubiri kumalizika kwa muda alioruhusiwa, mahakama inaweza ikiwa inaona inafaa kutoa mara moja hati ya kupelekwa mtu huyo Chuo cha Mafunzo.

(4) Endapo muda umetolewa kwa ajili ya malipo ya kiwango chochote ambacho kifungu hiki kinatumika, mahakama inaweza kumtaka mtu aliyeamriwa kufanya malipo hayo kuingia katika ahadi ya dhamana akiwa na wadhamini au bila ya wadhamini kama Mahakama inavyoona inafaa, kuweka masharti ya kufika kwake mbele ya mahakama hiyo katika tarehe ambayo siyo zaidi ya siku thelathini kutoka muda wa utekelezaji wa ahadi ya dhamana, na akishindwa kufanya hivyo mahakama inaweza mara moja kutoa adhabu ya kifungo kama kwamba muda haukutolewa kwa malipo hayo.

(5) Endapo muda umetolewa kwa ajili ya malipo kama ilivyoelezwa, muda wa ziada, kwa kuzingatia sharti lolote ambalo mahakama inaweza kuona inafaa kuliweka, unaweza kutolewa na mahakama, au, mahakama hiyo inaweza, kwa kuzingatia yaliyoelezwa, kuelekeza kwamba fedha yoyote ambayo kifungu hiki kinatumika zinaweza kulipwa kwa awamu kwa muda ambao mahakama inaweza kuona inafaa.

(6) Katika kesi zote endapo muda kwa ajili ya malipo haujatolewa, mahakama itarekodi sababu kwa ajili ya kupelekwa kizuizini mara moja.

(7) Masharti ya kifungu hiki hayatatumika katika kesi ya mtu yeyote aliyetiwa hatiani kwa kosa lolote na aliyepewa adhabu kwa kosa hilo zote mbili kifungo na faini, au kwa mtu aliyepo katika Chuo cha Mafunzo.

Kupelekwa Chuo cha Mafunzo kwa kushindikana ukamataji mali.

**322.** Ikiwa afisa mwenye dhamana ya kutekeleza hati ya ukamataji mali anatoa taarifa kwamba hakupata mali yoyote au amepata mali isiyotosha kutozwa fedha zilizotajwa katika hati ya ukamataji mali pamoja na gharama, mahakama inaweza kwa hati hiyo hiyo au kwa hati nyengine inayofuata kumpeleka Chuo cha Mafunzo mtu huyo aliyeamriwa kulipa kwa muda uliotajwa ndani ya hati, isipokuwa kama fedha na gharama zote za ukamataji, upelekaji na usafirishaji wa mtu huyo kwenda Chuo cha Mafunzo kilichoainishwa katika hati unalipwa haraka zaidi.

Kupelekwa Chuo cha Mafunzo badala ya ukamataji mali.

**323.** Pale mahakama inapoona kwamba ukamataji na uuzaji wa mali ungekuwa na madhara kwa mtu aliyeamriwa kulipa fedha au familia yake, au kwa kukiri kwake au vyenginevyo, kwamba hana mali ambayo katika mali hiyo fedha zinaweza kutozwa, au sababu nyengine ya msingi inayodhihirika kwa mahakama, mahakama inaweza ikiwa inaona inafaa, badala ya au baada ya kutoa hati ya ukamataji mali, kumpeleka katika Chuo cha Mafunzo kwa kipindi kilichoainishwa katika hati, isipokuwa kama fedha na gharama zote za ukamataji, upelekaji na usafirishaji wa mtu huyo kwenda Chuo cha Mafunzo kilichoainishwa katika hati unalipwa haraka zaidi.

Kiwango cha kifungo kwa kushindwa kulipa faini.

**324.**-(1) Kipindi cha kifungo kilichoamriwa na mahakama kuhusiana na kutokulipwa kwa kiwango chochote cha fedha kilichoamuliwa kulipwa kutokana na hatia au kutokana na kushindwa ukamataji wa mali ya kutosha kuridhisha kiwango chochote hicho kitakuwa kipindi ambacho kwa maoni ya mahakama kitatosheleza kutoa haki katika kesi hiyo, lakini hakitazidi katika kesi yoyote kiwango cha juu kabisa kilichopangwa na kiwango chini ya Jadweli la Tatu la Sheria hii.

(2) Kwa kushindwa kulipa gharama au fidia au ukamataji wa mali kuhusiana na gharama hizo au fidia mtu aliyeshindwa atawajibika kupewa kifungo kwa kipindi kisichozidi miezi mitatu isipokuwa kama gharama hizo au fidia zitalipwa haraka zaidi.

(3) Kupelekwa Chuo cha Mafunzo kwa kutokulipwa fedha hakutakuwa kwa kipindi kirefu zaidi kuliko miezi sita, isipokuwa kama sheria ambayo chini yake hatia imepatikana inaelekeza au inaruhusu kipindi kirefu zaidi.

Malipo yote baada ya mtu kupelekwa Chuo cha Mafunzo.

**325.** Mtu aliyepelekwa Chuo cha Mafunzo kwa kutokulipa fedha anaweza kulipa kiwango kilichotajwa katika hati, pamoja na gharama zilizoidhinishwa ndani ya hati hiyo, kama zipo, mahakamani, na mahakama baada ya hapo itamuachia mtu huyo ikiwa yupo kizuizini siyo kwa jambo jengine lolote.

Sehemu ya malipo baada ya kupelekwa Chuo cha Mafunzo.

**326.**-(1) Ikiwa mtu amepelekwa Chuo cha Mafunzo kwa kutokulipa fedha atalipa kiwango chochote cha sehemu ya fedha kwa ajili ya kulipa kiwango kilichoamuliwa kulipwa, kipindi cha kifungo chake kitapunguzwa kwa idadi ya siku zinazolingana kwa kadiri inavyowezekana kwa uwiyano ule ule wa idadi ya siku ambazo mtu huyo anawekwa kizuizini, na kiwango kilicholipwa kinalingana na kiwango ambacho yeye anawajibika.

(2) Afisa mwenye dhamana ya Chuo cha Mafunzo ambacho mtu huyo amezuiwa ambaye anapenda kutumia fursa ya masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, kwa maombi yanayofanywa kwake na mwanafunzi huyo, atampeleka mara moja mtu huyo mbele ya mahakama, na mahakama hiyo itathibitisha kiwango ambacho kipindi cha kifungo ambacho mwanzo kilitolewa kinapunguzwa kutokana na malipo hayo kwa kulipa sehemu, na itatoa amri kama inavyohitajika katika mazingira hayo.

## Dhamana kwa Ajili ya Kutunza Amani au Kufika kwa ajili ya Hukumu

Dhamana kwa ajili ya kutunza amani.

**327.**-(1) Mtu aliyetiwa hatiani kwa kosa ambalo adhabu yake siyo kifo au lenye adhabu ya kifungo kisichozidi miaka mitatu, anaweza, badala ya, au pamoja na, adhabu yoyote ambayo anawajibika kupewa, ataamriwa kuchukua ahadi ya dhamana yake mwenyewe akiwa na wadhamini au bila ya wadhamini, kwa kiwango ambacho mahakama inaona inafaa, itampa masharti, kwamba mtu huyo atatunza amani na atakuwa na tabia njema kwa muda utakaopangwa na mahakama.

(2) Mahakama inaweza kuamuru mshtakiwa kupelekwa Chuo cha Mafunzo mpaka pale ahadi ya dhamana, pamoja na wadhamini itakapochukuliwa.

(3) Kifungo kwa kutokuchukua ahadi ya dhamana hakitaongezeka kwa kipindi kirefu zaidi ya mwaka mmoja na, pamoja na muda uliopangwa wa kifungo, kama upo, hakitaongezeka kwa kipindi kirefu zaidi kuliko kipindi kirefu kabisa ambacho angeweza kuadhibiwa kwa kupewa kifungo bila ya faini.

Dhamana kwa ajili ya kufika kupokea hukumu.

**328.**-(1) Pale mtu anatiwa hatiani kwa kosa lolote ambalo adhabu yake siyo kifo au lenye adhabu ya kifungo kisichozidi miaka mitatu, mahakama inaweza, badala ya kutoa adhabu, kumuachia mtu aliyetiwa hatiani baada ya kuchukua ahadi ya dhamana yake mwenyewe, akiwa na wadhamini au bila ya wadhamini, katika kiwango ambacho mahakama inaweza kuona inafaa, itampa masharti kwamba mtu huyo atafika kupokea hukumu katika kikao cha baadae cha mahakama au wakati atakapoitwa.

(2) Hakuna chochote katika kifungu hiki kitakachochukuliwa kuathiri uwezo wa mahakama yoyote wa kumuachia mkosaji baada ya kutiwa hatiani kwa uangalizi chini ya masharti ya sheria inayohusiana na uangalizi wa wakosaji.

Masharti yanayotumika kwa, na ahadi ya dhamana chini ya vifungu vya 327 na 328.

**329.**-(1) Masharti ya vifungu vya 158, 159 na 161 vya Sheria hii yatatumika kama yalivyo kwa ahadi zote za dhamana zinazochukuliwa chini ya kifungu cha 327 au 328 cha Sheria hii.

(2) Masharti ya sheria inayohusiana na uangalizi wa wakosaji kuhusu kushindwa kutimiza masharti ya kuachiwa yatatumika kama yalivyo kwa mtu anayeshindwa kutimiza sharti lolote katika masharti ya ahadi ya dhamana iliyochukuliwa na mtu huyo chini ya kifungu cha 325 au 326 cha Sheria hii.

## Kuachiwa Mkosaji Bila ya Kutiwa Hatiani au Kuwekwa kwenye Uangalizi

Kuachiwa mkosaji bila ya kutiwa hatiani au kuwekwa kwenye uangalizi.

**330.**-(1) Endapo, katika usikilizaji wa kesi yoyote mahakama inaona kwamba shtaka dhidi ya mshtakiwa limethibitishwa lakini ina maoni kwamba, kwa kuzingatia tabia, historia, umri, afya, au hali ya kiakili ya mshtakiwa, au kwa udogo wa kosa lenyewe, au hali ya mazingira ambayo kosa limetendeka, siyo vyema kutoa adhabu yoyote, mahakama inaweza, bila ya kuendelea kumtia hatiani, kutoa amri ya kufuta shtaka.

(2) Endapo amri imetolewa na mahakama chini ya kifungu hiki, amri kwa madhumuni ya kurudisha tena umiliki au kukirejesha kitu kilichoibiwa, na kwa kuiwezesha mahakama kutoa amri yoyote chini ya masharti ya kifungu cha 337 cha Sheria hii, itakuwa na matokeo sawa sawa kama ya kutiwa hatiani.

(3) Endapo shtaka lolote limefutwa chini ya kifungu hiki, mahakama inaweza kumuamuru mshtakiwa kulipa gharama zote au sehemu ya gharama za mashtaka na gharama zinazoambatana na mashtaka.

(4) Hakuna chochote katika kifungu hiki kitakachochukuliwa kuathiri uwezo wa mahakama wa kumuachia mkosaji baada ya kutiwa kwake hatiani kumpeleka kwenye uangalizi chini ya masharti ya sheria inayohusu uangalizi wa wakosaji.

## Usimamizi

Uwezo wa kumuweka mtu kwenye usimamizi.

**331.**-(1) Endapo mtu:

(a) atatiwa hatiani kwa kosa lenye adhabu ya kifungo kwa kipindi cha miaka miwili au zaidi; na

(b) ameshatiwa hatiani kwa angalau mara tatu zilizopita kwa makosa yenye adhabu hiyo na, katika angalau mara mbili kati ya hizo, alipewa adhabu ya kifungo,

mahakama inaweza, ikiwa inaona inafaa, wakati wa kutoa adhabu ya kifungo kwa mtu huyo, kuamuru kwamba mtu huyo awekwe chini ya usimamizi kama itakavyoelezwa baadae kwa kipindi kisichozidi miaka mitano kutoka tarehe ya kumalizika kwa adhabu hiyo.

(2) Amri iliyotolewa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, ikiwa hatia inatenguliwa kwenye rufaa au vyenginevyo, itakuwa batili.

Masharti yanayoweza kuwekwa kwa mtu anayewekwa kwenye usimamizi.

**332.**-(1) Mahakama inaweza, katika kutoa amri chini ya kifungu cha 331 cha Sheria hii, kuelekeza kwamba mtu huyo, wakati anawekwa kwenye usimamizi na yupo huru ndani ya Zanzibar, kutekeleza yote au lolote katika masharti yafuatayo:

(a) kuishi ndani ya Shehia iliyoainishwa;

(b) kutokuhamisha makaazi yake kwenda sehemu yoyote nje ya Shehia hiyo iliyoainishwa bila ya ruhusa ya maandishi kutoka kwa Mkuu wa Wilaya wa Wilaya ambayo Shehia hiyo ipo;

(c) kwa wakati wote kumjulisha Sheha wa Shehia anayoishi kuhusu nyumba au pahala ambapo mtu huyo anaishi; au

(d) kufika yeye mwenyewe, wakati wowote anapotakiwa kufanya hivyo na Sheha wa Shehia ambayo yeye anakaa au na afisa wa polisi mwenye dhamana ya Wilaya ambayo yeye anaishi, katika pahala popote ndani ya Shehia hiyo au pahala popote ndani ya Wilaya hiyo kama itakavyokuwa,

na mahakama inaweza, wakati wowote, kubadilisha maelekezo hayo.

(2) Jaji Mkuu wa Zanzibar anaweza kutengeneza Kanuni kwa ajili ya utekelezaji wa masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki na, bila ya kuathiri ujumla wa yaliyotangulia, kueleza utaratibu ambao watu wanaweza kuletwa mbele ya mahakama kwa madhumuni ya kifungu hicho kidogo.

Kosa la kushindwa kutekeleza masharti yaliyowekwa kwa mtu aliyepo kwenye usimamizi.

**333.**-(1) Ikiwa mtu yupo katika usimamizi kutokana na amri iliyotolewa chini ya kifungu cha 331 cha Sheria hii, ambaye yupo huru ndani ya Zanzibar, anakataa au anadharau kutekeleza sharti lolote lililowekwa kwake yeye chini ya kifungu cha 332 cha Sheria hii au masharti ya Kanuni yoyote iliyotengenezwa chini kifungu cha 332, isipokuwa kama atathibitisha kwa kuiridhisha mahakama kwamba ametekeleza au amejaribu kutekeleza matakwa na masharti yote hayo, atakuwa ni mkosa na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miezi sita.

(2) Afisa wa polisi au Sheha anaweza kumkamata bila ya hati ya ukamataji mtu ambaye afisa wa polisi au Sheha kwa sababu za msingi anamtuhumu kuwa ametenda kosa chini ya kifungu hiki.

### Hati na Amri

Nani anaweza kutoa hati.

**334.** Hati yoyote kwa ajili ya utekelezaji wa adhabu yoyote inaweza kutolewa ama na Jaji au hakimu aliyetoa adhabu au mrithi wake katika ofisi.

Marekebisho ya makosa na kasoro.

**335.** Mahakama inaweza wakati wowote kurekebisha kasoro yoyote katika maudhui au katika muundo wa amri au hati yoyote, na hakuna kasoro au kosa kuhusiana na muda na pahala, na hakuna kasoro katika muundo wa amri yoyote au hati yoyote iliyotolewa chini ya Sheria hii, itakayokifanya kuwa ni batili au kinyume cha sheria kitendo chochote kilichofanywa au kilichokusudiwa kufanywa kutokana na amri hiyo au hati hiyo, isipokuwa kwamba ikiwa inaelezwa katika hati hiyo au amri hiyo, au inaweza kuhusishwa kutoka katika hati hiyo au amri hiyo, kwamba inatokana na hatia au hukumu, na kuna hatia halali au hukumu halali inayounga mkono amri hiyo au hati hiyo.

## SEHEMU YA KUMI NA TATU
## KUREJESHA MALI

### Mali Aliyokutwa nayo Mshtakiwa

Mali aliyokutwa nayo mshtakiwa.

**336.** Endapo, baada ya kukamatwa mtu aliyeshtakiwa kwa kosa lolote, mali yoyote inachukuliwa kutoka kwa mtu huyo, mahakama ambayo mbele yake mtu huyo anashtakiwa inaweza kuamuru:

(a) kwamba mali hiyo au sehemu ya mali hiyo irejeshwe kwa mtu ambaye mahakama inaona kuwa ana haki kwenye mali hiyo, na, ikiwa yeye ni mtu anayeshtakiwa, kwamba irejeshwe ama kwake yeye au kwa mtu mwengine ambaye mshtakiwa anaweza kuelekeza; au

(b) kwamba mali hiyo au sehemu ya mali hiyo itumike kulipia faini yoyote au gharama zozote au fidia iliyoelekezwa kulipwa na mshtakiwa.

### Kurejeshwa Mali Iliyoibiwa

Mali iliyoibiwa.

**337.**-(1) Ikiwa mtu ni mkosa wa kosa lililotajwa katika Sheria ya Adhabu kuhusiana na kuiba, kuchukua, kujipatia, kunyang'anya, kubadilisha au kuhaulisha, au kwa kujua anapokea mali yoyote, anashtakiwa na kutiwa hatiani na, au kwa niaba ya mmiliki wa mali hiyo, mali hiyo itarejeshwa kwa mmiliki au kwa mwakilishi wake.

(2) Katika hali yoyote iliyotajwa kwenye kifungu hiki, mahakama ambayo mbele yake mkosaji huyo anatiwa hatiani itakuwa na uwezo wa kutoa muda baada ya muda amri kwa ajili ya kurejeshwa mali hiyo au kuamuru kurejeshwa mali hiyo katika utaratibu wa haraka.

(3) Pale ambapo vitu vimepatikana kwa njia ya hadaa au kwa njia nyengine zozote zisizo halali ambazo siyo kuiba, mali katika vitu hivyo haitorudi kwa mtu ambaye alikuwa ni mmiliki wa vitu hivyo, au mwakilishi wake binafsi, kwa sababu tu ya kutiwa hatiani kwa mkosaji.

(4) Hakuna chochote katika kifungu hiki kitakachotumika katika hali yoyote ya thamani ya dhamana yoyote ambayo kwa nia njema ililipwa au imetekelezwa na mtu mwengine anayewajibika kwa malipo hayo, au, ikiwa ni hati ya kuamuru malipo ya fedha, imechukuliwa kwa nia njema au kupokelewa kwa njia ya uhaulishaji au kupokelewa na mtu yeyote kwa haki na thamani ya malipo bila ya notisi yoyote au bila ya sababu ya msingi kutuhumu kwamba hati hiyo ya kuamuru malipo ya fedha imeibiwa.

(5) Kwa madhumuni ya kifungu kidogo cha (3) cha kifungu hiki,"bidhaa" inajumuisha vitu vyote binafsi vinavyohamishika visivyokuwa vitu visivyoshikika na fedha, na pia inajumuisha vifaa, mazao ya biashara ya viwanda, na vitu vilivyoambatanishwa kwenye au vilivyo sehemu ya ardhi, ambavyo vinakubaliwa kutenganishwa kabla ya kuuzwa au chini ya mkataba wa mauziano.

(6) Katika urejeshaji wa mali yoyote iliyoibiwa ikiwa inaonekana na mahakama kutokana na ushahidi kwamba mkosaji ameshauza mali iliyoibiwa kwa mtu, kwamba mtu huyo aliyeuziwa hakuwa akijua kwamba mali hiyo iliibiwa, na kwamba fedha zozote zilichukuliwa kutoka kwa mkosaji wakati wa kukamatwa kwake, mahakama inaweza, kwa maombi ya mnunuzi huyo, kuamuru kwamba kutoka kwenye fedha hizo kiasi kisichozidi kiwango cha mapato ya uuzaji huo kipelekwe kwa mnunuzi huyo.

(7) Utekelezaji wowote wa amri chini ya kifungu hiki, isipokuwa kama mahakama ambayo mbele yake hatia imepatikana inaelekeza vyenginevyo katika hali yoyote ambayo umiliki wa mali hiyo haukubishaniwa, utasimamishwa:

(a) katika hali yoyote mpaka kumalizika kwa muda wa rufaa; na

(b) katika hali yoyote endapo rufaa imefunguliwa, mpaka kutolewa uamuzi wa rufaa.

amri haitafanya kazi kuhusiana na mali husika ikiwa hatia inatenguliwa kwenye rufaa.

(8) Jaji Mkuu wa Zanzibar anaweza kuweka masharti kwa Kanuni kwa ajili ya uwekaji katika uhifadhi salama wa mali yoyote, kufuatia usimamishaji wa utekelezaji wa amri hiyo yoyote.

(9) Mtu yeyote aliyeathirika na amri iliyotolewa chini ya kifungu hiki anaweza kukata rufaa kwa mahakama ya juu zaidi, na baada ya usikilizaji wa rufaa hiyo Mahakama inaweza kwa amri kubatilisha au kubadilisha amri yoyote iliyotolewa wakati wa usikilizaji wa kesi kwa ajili ya urejeshaji wa mali yoyote kwa mtu yeyote, ingawa hatia haijatenguliwa; na amri hiyo, ikiwa itabatilishwa, haitafanya kazi, na, ikibadilishwa, itafanya kazi kama ilivyobadilishwa.

(10) Bila ya kujali chochote kilicho kinyume na yaliyomo ndani ya kifungu hiki, ikiwa mali ambayo amri inaweza kutolewa ni ile ambayo inaweza kuharibika au kuoza kwa haraka au kama mahakama ambayo mbele yake mkosaji anatiwa hatiani inaona kwamba uuzwaji wake wa haraka utakuwa ni kwa manufaa ya mmiliki, mahakama inaweza, wakati wowote, kuelekeza mali hiyo kuuzwa na kuelekeza kwamba mapato ya mauzo hayo yalipwe kwa mmiliki wa mali iliyouzwa.

(11) Masharti ya kifungu kidogo cha (7) cha kifungu hiki, kwa kadiri inavyowezekana kutekelezwa, yatatumika kwa mapato halisi ya mauzo hayo.

## SEHEMU YA KUMI NA NNE
## RUFAA KWA UJUMLA

Tafsiri.

**338.** Katika Sehemu hii:

"Mahakama inayosikiliza rufaa" maana yake ni Mahakama Kuu, Mahakama ya Hakimu wa Mkoa au Mahakama ya Hakimu wa Wilaya kama hali itakavyokuwa;

"Muomba rufaa" isipokuwa kama itaelezwa vyenginevyo maana yake ni Mkurugenzi wa Mashtaka au mtu mwengine yeyote mwenye haki chini ya Sheria hii kukata rufaa.

Haki za asili za rufaa.

**339.** Mtu ambaye hakuridhika na uamuzi wa mahakama yoyote atakuwa na haki ya kukata rufaa kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii.

Kukata rufaa Mahakama Kuu.

**340.**-(1) Bila ya kuathiri chochote kitakachoelezwa baadae, mtu asiyeridhika na uamuzi wa Mahakama ya Mahakimu wa Mkoa anaweza kukata rufaa Mahakama Kuu na atataarifiwa hivyo na hakimu wa mahakama hiyo katika wakati ambao adhabu inatolewa.

(2) Kukata rufaa katika Mahakama Kuu kunaweza kuwa juu ya jambo linalohusu maelezo ya kesi na pia juu ya jambo linalohusu sheria.

Kukata rufaa Mahakama ya Hakimu wa Mkoa.

**341.**-(1) Mtu ambaye hakuridhika na uamuzi wa Mahakama ya Hakimu wa Wilaya anaweza kukata rufaa katika Mahakama ya Hakimu wa Mkoa na atataarifiwa hivyo na Hakimu wa mahakama hiyo.

(2) Kukata rufaa Mahakama ya Hakimu wa Mkoa inaweza kuwa juu ya jambo linalohusu maelezo ya kesi na pia juu ya jambo linalohusu sheria.

Kukata rufaa Mahakama ya Hakimu wa Wilaya.

**342.**-(1) Bila ya kuathiri chochote kitakachoelezwa baadae, mtu asiyeridhika na uamuzi wa mahakama ya mwanzo anaweza kukata rufaa katika Mahakama ya Hakimu wa Wilaya na atataarifiwa hivyo na hakimu wa mahakama ya mwanzo.

(2) Kukata rufaa Mahakama ya Hakimu wa Wilaya inaweza kuwa juu ya jambo linalohusu maelezo ya kesi na pia juu ya jambo linalohusu sheria.

Kukatwa rufaa na Mkurugenzi wa Mashtaka.

**343.**-(1) Kwa kuzingatia ukomo wa rufaa ulioelezwa katika Sehemu hii, Mkurugenzi wa Mashtaka anaweza, katika hali yoyote ya kutiwa hatiani kunakotokana na usikilizaji wa kesi iliyosikilizwa na mahakama yoyote ya jinai, kumuelekeza wakili yeyote wa Serikali au afisa mwengine kuwasilisha rufaa katika mahakama inayostahiki dhidi ya adhabu kuhusu udogo wa adhabu hiyo.

(2) Pale rufaa imeshafunguliwa dhidi ya udogo wa adhabu, mahakama inayosikiliza rufaa haitaongeza adhabu isipokuwa baada ya kumpa mshtakiwa nafasi ya kutosha kutoa sababu dhidi ya kuongezwa adhabu hiyo na wakati anatoa sababu hiyo, anaweza kuomba kuachiwa huru au kupunguzwa kwa adhabu hiyo.

Kukata rufaa endapo mtu ameachiwa huru.

**344.** Mkurugenzi wa Mashtaka anaweza, katika hali yoyote kumuelekeza Wakili wa Serikali, au afisa mwengine yeyote kwa ajili hiyo, kuwasilisha rufaa katika mahakama yoyote kutokana na amri ya awali au amri ya rufaa ya kuachiwa huru iliyotolewa na mahakama yoyote ya chini.

Notisi ya nia ya kukata rufaa.

**345.** Pale mshtakiwa anapoachiwa huru au anapoachiwa katika kesi yoyote au usikilizaji wa kesi na mwendesha mashtaka hakuridhika na uamuzi huo, anaweza kuwasilisha notisi ya nia ya kukata rufaa kwa njia ya mdomo au maandishi mara tu baada ya kusomwa kwa hukumu au uamuzi na pale notisi hiyo inapowasilishwa mahakama itarekodi kuwasilishwa huko.

Ukomo.

**346.**-(1) Rufaa kutokana na uamuzi wowote, adhabu au amri haitosikilizwa isipokuwa kama muomba rufaa:

(a) ameshatoa notisi ya rufaa kwa Mrajis ndani ya siku kumi na tano kutoka tarehe ya uamuzi, adhabu au amri;

(b) ameshawasilisha ombi lake la rufaa ndani ya siku arobaini na tano kutoka terehe ya uamuzi, adhabu au amri.

(2) Katika kuhesabu muda huo wa siku arobaini na tano, muda unaotakiwa kupata nakala za hukumu au amri inayokatiwa rufaa hautahesabiwa.

(3) Mahakama Kuu au Mahakama ya Hakimu wa Mkoa inaweza, kwa sababu ya msingi, kukubali rufaa yoyote bila ya kujali kwamba kipindi chochote cha ukomo kilichoainishwa katika kifungu hiki kimeshamalizika.

Ombi la rufaa.

**347.**-(1) Rufaa itafanywa kwa njia ya ombi la maandishi linalowasilishwa na muombaji au wakili wake, na ombi lolote hilo isipokuwa kama Mahakama Kuu itaelekeza vyenginevyo, litaambatana na nakala ya hukumu au amri inayokatiwa rufaa.

(2) Endapo muomba rufaa anawakilishwa na wakili ombi la rufaa litajumuisha maelezo kuhusu mambo ya sheria au maelezo ya kesi ambayo Mahakama ya chini inayokatiwa rufaa inadaiwa kuwa imekosea.

Muomba rufaa katika Chuo cha Mafunzo.

**348.**-(1) Ikiwa muomba rufaa yupo katika Chuo cha Mafunzo, anaweza kuwasilisha ombi lake la rufaa na nakala zinazoambatana na ombi hilo kwa afisa dhamana wa Chuo cha Mafunzo, ambaye baadae atapeleka ombi hilo na nakala hizo kwa Mrajis wa Mahakama Kuu.

(2) Baada ya kupokea ombi lolote la rufaa Mrajis atapeleka ombi hilo na kumbukumbu zinazoambatana na ombi hilo kwa:

(a) Jaji Mkuu kwa ajili ya kupangwa katika rufaa za Mahakama Kuu; na

(b) Hakimu husika kwa rufaa zisizokuwa za Mahakama Kuu.

Ukataaji wa rufaa mara moja.

**349.**-(1) Baada ya kupokea ombi la rufaa na nakala chini ya kifungu cha 347 cha Sheria hii, mahakama inayosikiliza rufaa itapitia ombi hilo la rufaa, na, ikiwa inaona kwamba hakuna sababu ya msingi ya kuingilia, inaweza kufuta rufaa hiyo mara moja.

(2) Rufaa haitafutwa mara moja isipokuwa katika mazingira yaliyotajwa katika kifungu kidogo cha (3) cha kifungu hiki, isipokuwa kama muomba rufaa au wakili wake amepewa fursa ya kusikilizwa kwa ajili ya kuunga mkono rufaa hiyo.

(3) Endapo rufaa inaletwa kwa sababu kwamba hatia iko kinyume na uzito wa ushahidi, au kwamba adhabu ni kubwa, na inaonekana na mahakama kwamba ushahidi unatosha kuunga mkono hatia na kwamba hakuna kitu chochote muhimu

katika mazingira ya kesi hiyo ambacho kingeweza kuibua shaka ya maana ama hatia ilikuwa sahihi au imepelekea kuonekana kwamba adhabu ingeweza kupunguzwa, rufaa inaweza, bila ya kupangwa kwa ajili ya kusikilizwa, kufutwa mara moja kwa amri ya mahakama inayothibitisha kwamba imepitia kumbukumbu na imejiridhisha kwamba rufaa hiyo imefunguliwa bila ya kuwepo sababu yoyote ya msingi ya madai.

(4) Pale ambapo rufaa imefutwa mara moja taarifa ya kufutwa huko itapelekwa haraka iwezekanavyo kwa Mkurugenzi wa Mashtaka.

Taarifa ya muda, pahala na usikilizaji.

**350.**-(1) Ikiwa mahakama inayosikiliza rufaa haijaifuta rufaa mara moja, itawezesha taarifa kupelekwa kwa muomba rufaa au wakili wake, na kwa Mkurugenzi wa Mashtaka, kuhusu muda na pahala ambapo rufaa hiyo itasikilizwa na itampelekea mjibu rufaa nakala ya mwenendo wa kesi na nakala ya sababu za rufaa;

(2) Taarifa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, haihitaji kupelekwa kwa muomba rufaa au wakili wake ikiwa imeelezwa hatika ombi la rufaa kwamba muomba rufaa hatopenda kuwepo na hana nia ya kuweka wakili kwa ajili ya kumuwakilisha katika usikilizaji wa rufaa hiyo.

Uwezo wa mahakama inayosikiliza rufaa.

**351.**-(1) Baada ya kupitia kumbukumbu hizo na kumsikiliza muomba rufaa au wakili wake, ikiwa atafika, na Mkurugenzi wa Mashtaka ikiwa atafika, mahakama inayosikiza rufaa ikiwa inaona kwamba hakuna sababu ya msingi kuingilia, itaifuta rufaa, au inaweza:

(a) katika rufaa inayotokana na amri ya kuachiwa huru, itaibadilisha amri hiyo na itaelekeza kwamba uchunguzi zaidi ufanywe, au kwamba mshtakiwa ashtakiwe upya au apelekwe kwa ajili ya usikilizaji wa kesi, kama hali itakavyokuwa, au itamuona kuwa ni mkosa na kumpa adhabu kwa mujibu wa sheria;

(b) katika rufaa dhidi ya hatia:

(i) itabadilisha uamuzi na adhabu na itamuachia huru au kumuachia mshtakiwa, au kuamuru mshtakiwa kesi yake isikilizwe upya na mahakama yenye mamlaka ya kusikiliza kesi hiyo iliyo chini ya mahakama hiyo inayosikiliza rufaa hiyo au kumpeleka kwa ajili ya usikilizaji wa kesi; au

(ii) itabadilisha uamuzi, itabakisha adhabu, au

(iii) pamoja na au bila ya kubadilisha uamuzi, itabadilisha aina au kiwango, au itabadilisha aina na kiwango, cha adhabu hiyo;

(c) katika rufaa kwa ajili ya kuongeza adhabu:

(i) itageuza uamuzi na adhabu na kumuachia huru au kumuachia mshtakiwa, au kuamrisha kesi ya mshtakiwa kusikilizwa upya na mahakama yenye mamlaka ya kusikiliza kosa hilo; au

(ii) itabadilisha uamuzi, itabakisha adhabu, au

(iii) pamoja na au bila ya kubadilisha uamuzi, itabadilisha aina au kiwango, au itabadilisha aina na kiwango, cha adhabu kwa ajili ya kuongeza au kupunguza adhabu hiyo;

(d) katika rufaa kuhusu amri yoyote nyengine, itabadilisha au itageuza amri hiyo;

(e) itafanya marekebisho yoyote au itatoa amri inayotokana na matokeo ya marekebisho hayo au amri inayoendana sambamba na marekebisho hayo inayoweza kuwa sawa au inafaa.

(2) Hakuna chochote katika kifungu hiki kitakachotafsiriwa kuizuia mahakama inayosikiliza rufaa kutoa adhabu kubwa zaidi kuliko adhabu ambayo ingeweza kutolewa na mahakama ambayo ilitoa adhabu hiyo.

(3) Adhabu haitaongezwa isipokuwa kama mshtakiwa amepewa fursa ya kuonesha sababu ya kupinga dhidi ya kuongezwa kwa adhabu hiyo.

Amri ya mahakama inayosikiliza rufaa itathibitishwa kwa mahakama ya chini.

**352.**-(1) Pale ambapo kesi inaamuliwa na mahakama inayosikiliza rufaa chini ya Sehemu hii, itathibitisha hukumu yake au amri kwa mahakama ambayo uamuzi uliokatiwa rufaa, adhabu au amri iliokatiwa rufaa dhidi yake ilirekodiwa au ilitolewa.

(2) Mahakama iliyotoa uamuzi, adhabu au amri iliyokatiwa rufaa, ambayo kwa mahakama hiyo mahakama inayosikiliza rufaa inathibitisha hukumu yake au amri, baadae itatoa amri hizo ambazo zinalingana na hukumu au amri iliyotolewa na mahakama inayosikiliza rufaa, na, ikiwa ni muhimu kumbukumbu zitarekebishwa kwa mujibu wa hukumu au amri hiyo.

Kupewa dhamana muomba rufaa na kuwa kizuizini kusubiri rufaa.

**353.**-(1) Muomba rufaa aliyetiwa hatiani ambaye hajapewa dhamana, wakati akisubiri uamuzi wa rufaa yake, atachukuliwa kama mwanafunzi ambaye hajatiwa hatiani.

(2) Mahakama Kuu au mahakama ya chini ambayo imemtia hatiani muomba rufaa inaweza, ikiwa inaona inafaa, kumpa muomba rufaa dhamana kusubiri uamuzi wa rufaa yake.

(3) Endapo mahakama ya chini inakataa kumuachia mtu huyo kwa dhamana, mtu huyo anaweza kuomba dhamana Mahakama Kuu.

(4) Kipindi cha muda ambacho muomba rufaa, anasubiri uamuzi wa rufaa yake, anapewa dhamana, na kwa mujibu wa maelekezo yoyote ambayo Mahakama Kuu inaweza kutoa kinyume na rufaa hiyo, kipindi cha muda ambao muomba rufaa, ikiwa yupo kizuizini, anashughulikiwa kama mwanafunzi aliyekuwa hajatiwa hatiani chini ya kifungu hiki, hakitahesabiwa kama ni sehemu ya kipindi chochote cha kifungo chini ya adhabu yake.

(5) Adhabu ya muomba rufaa ama ni adhabu iliyotolewa na mahakama ya chini au adhabu iliyotolewa na Mahakama Kuu katika rufaa, kwa mujibu wa maelekezo yoyote ambayo yanaweza kutolewa na mahakama hiyo iliyotajwa, itachukuliwa kuwa imeanza upya au inaanza kama mazingira yatakavyolazimu ikiwa:

(a) muomba rufaa yupo kizuizini, kutoka siku ambayo rufaa imeamuliwa; au

(b) muomba rufaa huyo hayupo kizuizini, kutoka siku ambayo amepokelewa katika Chuo cha Mafunzo chini ya adhabu hiyo.

(6) Bila ya kujali masharti ya kifungu kidogo cha (5) (a) cha kifungu hiki, endapo muomba rufaa yupo kizuizini kusubiri uamuzi wa rufaa yake kwa kipindi kirefu zaidi ya wiki sita baadae isipokuwa kama Mahakama Kuu itaamuru vyenginevyo adhabu yake itaanza kutekelezwa mara tu pale alipokuwa kizuizini kwa jumla ya kipindi cha wiki sita.

(7) Pale muomba rufaa kwenye hatia ameamuliwa kulipa kiasi cha fedha kama faini, adhabu, fidia, gharama, matumizi au vyenginevyo, Mahakama Kuu au mahakama ya chini, ambayo imemtia hatiani muomba rufaa, inaweza kusitisha utekelezaji wa amri hiyo kwa ajili ya malipo hayo baada ya kuchukua ahadi ya dhamana, akiwa na wadhamini au bila ya wadhamini, au kwa kuweka fedha au mali nyengine yoyote, au vyenginevyo, kwa ajili ya malipo ya kiwango hicho kwa muomba rufaa wakati atakapoamriwa na Mahakama Kuu kwa ajili ya utekelezaji huo kusimamishwa.

Uwezo wa kuchukua ushahidi wa ziada.

**354.**-(1) Katika kushughulikia rufaa, mahakama inayosikiliza rufaa, ikiwa inaona kuwa ushahidi wa ziada ni muhimu, itarekodi sababu zake, na inaweza ama kuchukua ushahidi huo wa ziada yenyewe au kuelekeza ushahidi huo uchukuliwe na mahakama iliyo chini yake.

(2) Wakati ushahidi wa ziada unachukuliwa na mahakama ya chini, mahakama hiyo itathibitisha ushahidi huo kwa mahakama inayosikiliza rufaa ambayo baadae itaendelea na umalizaji wa rufaa hiyo.

(3) Isipokuwa kama mahakama inayosikiliza rufaa inaelekeza vyenginevyo, muomba rufaa na mjibu rufaa au mawakili wao, pale inapofaa, lazima wawepo wakati wa uchukuaji huo wa ushahidi wa ziada.

(4) Ushahidi uliochukuliwa kwa mujibu wa kifungu hiki, utachukuliwa kama vile ulikuwa ushahidi uliochukuliwa wakati wa usikilizaji wa kesi mbele ya mahakama ya chini.

Idadi ya majaji katika rufaa.

**355.-**(1) Isipokuwa kama inahitajika na sheria nyengine yoyote inayotumika kwa wakati huo au kwa maelekezo ya Jaji Mkuu, rufaa zote chini ya Sheria hii zitasikilizwa na jaji mmoja.

(2) Pale ambapo rufaa imeanza kusikilizwa mbele ya jaji mmoja, Jaji Mkuu anaweza kuelekeza kwamba rufaa isikilizwe na majaji watatu na maelekezo hayo yanaweza kutolewa wakati wowote kabla ya kusomwa kwa hukumu

(3) Ikiwa, baada ya usikilizaji wa rufaa, mahakama imegawika katika maoni, uamuzi utakuwa ni wa wengi.

Kuondoshwa kwa rufaa.

**356.-**(1) Rufaa iliyofunguliwa na Mkurugenzi wa Mashtaka itaondoshwa kufuatia kifo cha mshtakiwa.

(2) Rufaa nyengine yoyote chini ya Sehemu hii, isipokuwa rufaa kuhusu adhabu ya faini, mwisho itaondoshwa kufuatia kifo cha muomba rufaa.

(3) Endapo rufaa ni dhidi ya hatia na adhabu ya kifo au adhabu ya kifungo, na muomba rufaa anafariki wakati akisubiri rufaa hiyo, mtu yeyote kutoka katika familia ya muomba rufaa anaweza, ndani ya siku thelathini kutoka siku ya kifo cha muomba rufaa, kuomba katika mahakama inayosikiliza rufaa ruhusa ya kuendelea na rufaa hiyo na ikiwa ruhusa inatolewa, rufaa haitaondoshwa.

Rufaa katika Mahakama ya Rufaa.

**357.** Upande wowote kwenye rufaa kutoka mahakama ya chini unaweza kukata rufaa dhidi ya uamuzi wa Mahakama Kuu katika mamlaka yake ya rufaa kwenye Mahakama ya Rufaa kwa mujibu wa Kanuni za Mahakama ya Rufaa.

Kupewa dhamana kusubiri rufaa katika Mahakama ya Rufaa.

**358.-**(1) Jaji wa Mahakama Kuu anaweza, katika mamlaka yake, katika kesi yoyote ambayo rufaa kutoka uamuzi wa Mahakama Kuu katika mamlaka yake ya rufaa kwenda Mahakama ya Rufaa imefunguliwa, kutoa dhamana kusubiri usikilizaji wa rufaa hiyo.

(2) Masharti ya vifungu vidogo vya (1), (2) na (3) vya kifungu cha 353 cha Sheria hii, yatatumika kwa waomba rufaa waliotiwa hatiani wanaokata rufaa chini ya masharti ya kifungu cha 357 cha Sheria hii, kama vile maneno "Mahakama Kuu" yamebadilishwa kuwa maneno "Mahakama ya Rufaa" na maneno "Mahakama ya Chini' yamebadilishwa kuwa maneno "Mahakama Kuu".

## Mapitio

Uwezo wa Mahakama Kuu kuita kumbukumbu.

**359.** Mahakama Kuu inaweza kuita na kuzipitia kumbukumbu za mwenendo wowote wa jinai mbele ya Mahakama yoyote ya chini kwa madhumuni ya kujiridhisha kuhusu usahihi, uhalali au umakini wa uamuzi wowote, adhabu au amri iliyorekodiwa au iliyotolewa, na pia kuhusu utaratibu wa mwenendo wowote wa kesi wa Mahakama ya chini hiyo yoyote.

Uwezo wa Mahakimu kuita kumbukumbu kwa mahakama ya chini.

**360.**-(1) Hakimu yeyote anaweza kuitisha kwa kupitia kumbukumbu za mwenendo wowote wa kesi ya jinai iliyopo mbele ya Mahakama ya chini zaidi kuliko mahakama ambayo yeye ana dhamana ya kuisikiliza kesi, na ipo ndani ya eneo la mipaka ya mamlaka yake, kwa madhumuni ya kujiridhisha kuhusu usahihi, uhalali au umakini wa uamuzi wowote, adhabu au amri iliyowekewa kumbukumbu au iliyotolewa, na pia kuhusu utaratibu wa mwenendo wowote wa kesi wa mahakama hiyo ya chini yoyote.

(2) Ikiwa hakimu anatekeleza chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, anaona kwamba uamuzi, adhabu au amri ya Mahakama hiyo ya chini ni batili au siyo sahihi, au kwamba mwenendo wowote huo ni kinyume na utaratibu, atazipeleka kumbukumbu hizo pamoja na maelezo hayo kama anavyoona inafaa, kwa Mahakama Kuu, na kusubiri uamuzi wa Mahakama Kuu, hakimu huyo anaweza kwa sababu atakazozirekodi kwa maandishi kuamuru kwamba utekelezaji wa adhabu au amri ya mahakama hiyo ya chini usimamishwe na pia, ikiwa mtu aliyetiwa hatiani yupo katika kizuizi kwamba aachiwe kwa dhamana au kwa ahadi ya dhamana yake mwenyewe.

(3) Katika hali yoyote adhabu au amri iliyoshughulikiwa chini ya kifungu hiki inathibitishwa na Mahakama Kuu, muda ambao mtu aliyetiwa hatiani ameachiwa hautahesabiwa katika kuhesabu muda wa adhabu aliyopewa.

Uwezo wa Mahakama Kuu katika mapitio.

**361.**-(1) Katika hali ya mwenendo wa kesi wowote katika Mahakama ya chini, kumbukumbu ambazo zimeitwa au zimeripotiwa kwa ajili ya amri, au vyenginevyo Mahakama Kuu imepata taarifa au kwa maombi, Mahakama Kuu inaweza:

(a) katika mazingira ya kutiwa hatiani, kutumia uwezo wake wowote iliyopewa kama mahakama inayosikiliza rufaa chini ya vifungu vya 351, 353 na 354 vya Sheria hii na inaweza kuongeza adhabu; na

(b) katika mazingira ya amri yoyote isiyokuwa amri ya kuachiwa huru, kubadilisha au kugeuza amri hiyo.

(2) Amri chini ya kifungu hiki haitofanywa kwa kumuathiri mshtakiwa au kumuathiri Mkurugenzi wa Mashtaka isipokuwa mshtakiwa au Mkurugenzi wa Mashtaka kama hali itakavyokuwa amepewa fursa ya kusikilizwa binafsi au kupitia wakili wake.

(3) Pale adhabu husika chini ya kifungu hiki imeshatolewa na Mahakama ya chini, isipokuwa kama jambo linahusu kosa la kingono; Mahakama Kuu haitatoa adhabu kubwa zaidi kwa kosa hilo, ambalo kwa maoni ya Mahakama Kuu mshtakiwa amelitenda, kuliko ile ambayo ingeweza kutolewa na Mahakama ambayo imetoa adhabu hiyo.

(4) Hakuna chochote katika kifungu hiki kitakachochukuliwa kuwa kinaizuia Mahakama Kuu kubadilisha uamuzi wa kumuachia huru mshtakiwa na badala yake kumtia hatiani pale ambapo Mahakama Kuu inaona ni muhimu kufanya hivyo kwa maslahi ya kutenda haki.

(5) Hakuna mwenendo wa kesi wowote kwa njia ya mapitio utakaosikilizwa ikiwa tayari kuna rufaa iliyokwishafunguliwa.

(6) Endapo Mahakama Kuu inageuza kumbukumbu za mwenendo wa kesi katika Mahakama ya chini inayohusiana na kosa la kingono, inaweza ikiwa inaona kwamba ili kutenda haki jambo hilo linahitajika, kutoa adhabu kubwa kuliko ile ambayo Mahakama iliyomtia hatiani ingeweza kuitoa kama vile jambo hilo kiuhalisia limekuja kwa rufaa, lakini adhabu hiyo Mahakama Kuu ingeweza kuitoa ikiwa jambo hilo lingekuja mbele yake kwa rufaa.

Uwezo wa mahakama katika kuwasikiliza wahusika wa kesi.

**362.**-(1) Mhusika wa kesi hana haki yoyote ya kusikilizwa ama binafsi au kupitia wakili wake mbele ya Mahakama Kuu inapotekeleza mamlaka yake ya kufanya mapitio.

(2) Mahakama inaweza, ikiwa inaona inafaa, inapotekeleza mamlaka hayo, kumsikiliza mhusika yeyote wa kesi ama yeye binafisi au kupitia wakili wake, na kwamba hakuna chochote katika kifungu hiki kitakachochukuliwa kuathiri kifungu kidogo cha (2) cha kifungu cha 361 cha Sheria hii.

Idadi ya majaji katika mapitio.

**363.**-(1) Kesi mbele ya Mahakama Kuu wakati wa kutekeleza mamlaka yake katika kufanya mapitio inaweza kusikilizwa na hukumu yoyote au amri ya kesi hiyo inaweza kutolewa na Jaji mmoja.

(2) Wakati mahakama inajumuisha Jaji zaidi ya mmoja na inagawika sawa sawa katika maoni, adhabu au amri ya Mahakama ya chini itaungwa mkono.

Amri ya mapitio itathibitishwa na mahakama ya chini.

**364.** Wakati kesi inafanyiwa mapitio na Mahakama Kuu, Mahakama hiyo itathibisha uamuzi wake au amri katika mahakama ambayo adhabu au amri hiyo iliyofanyiwa mapitio imerikodiwa au yametolewa, na Mahakama ambayo uamuzi au amri inathibitishwa hivyo baadae itatoa amri hizo kama zinavyolingana na uamuzi huo uliothibitishwa, na, ikiwa ni lazima, kumbukumbu zitarekebishwa kwa mujibu wa uamuzi huo.

## Kupeleka Kesi Mahakama Kuu

Kupeleka kesi Mahakama Kuu.

**365.**-(1) Endapo mahakama yoyote inaridhika kwamba kesi iliyo mbele yake inahusisha suala la uhalali wa sheria yoyote, Sheria, Kanuni au Taratibu, au sharti lolote lililomo katika sheria, Sheria, Kanuni au Taratibu, uamuzi wa suala hilo ni muhimu kwa ajili ya kuimaliza kesi hiyo, na ina maoni kwamba sheria yoyote hiyo, Sheria, Kanuni au Taratibu au sharti siyo halali au halitekelezeki, lakini haijatamkwa hivyo na Mahakama Kuu, Mahakama itatoa maelezo ya kesi hiyo kuainisha maoni yake na sababu za maoni hayo na itaiwasilisha kesi hiyo Mahakama Kuu kwa ajili ya kutolewa uamuzi.

(2) Mahakama yoyote iliyowasilisha kesi Mahakama Kuu chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, inaweza wakati wa kusubiri uamuzi wa Mahakama Kuu kuhusu kesi hiyo, ama kumpeleka mshtakiwa Chuo cha Mafunzo au kumuachia mshtakiwa kwa dhamana kufika mbele ya mahakama atakapoitwa.

Kuimaliza kesi kwa mujibu wa uamuzi wa Mahakama Kuu.

**366.**-(1) Pale ambapo suala limepelekwa kwa mujibu wa kifungu cha 365 cha Sheria hii, Mahakama Kuu itatoa amri kuhusu suala hilo kama inavyoona inafaa, na itawezesha nakala ya amri hiyo kupelekwa katika Mahakama iliyolipeleka suala hilo Mahakama Kuu, ambayo itaimaliza kesi hiyo kulingana na amri hiyo ya Mahakama Kuu.

(2) Mahakama Kuu inaweza kuelekeza nani atalipa gharama za upelekaji huo wa kesi.

Uwezo wa kuirejesha kesi katika mahakama ya chini.

**367.** Mahakama Kuu itakuwa na uwezo, ikiwa inaona inafaa:

(a) kuwezesha kesi kurejeshwa kwa ajili ya marekebisho au kutolewa maelezo upya, na kesi hiyo itarekebishwa au itaelezwa upya ipasavyo, na hukumu itatolewa baada ya kufanyiwa marekebisho hayo au kutolewa upya maelezo; au

(b) kuirejesha kesi katika mahakama ya chini kwa ajili ya kusikilizwa tena na kuamuliwa pamoja na maelekezo kama inavyoweza kuona ni lazima.

Idadi ya majaji kwa kesi iliyopelekwa Mahakama Kuu.

**368.**-(1) Kesi iliyopelekwa kwa ajili ya maoni ya Mahakama Kuu inaweza kusikilizwa kama Jaji Mkuu atakavyoamua isikilizwe na Jaji mmoja au wawili wa Mahakama Kuu.

(2) Pale usikilizaji wa kesi iliyopelekwa Mahakama Kuu umeshaanza mbele ya Jaji mmoja, Jaji Mkuu anaweza kuelekeza kwamba isikilizwe na majaji wawili, kama wapo, maelekezo hayo yanaweza kutolewa wakati wowote kabla ya hukumu kutolewa.

(3) Ikiwa baada ya usikilizaji mahakama inagawika sawa sawa katika maoni, uamuzi wa Mahakama ya chini utathibitishwa.

## Rufaa Kutoka Mahakama Kuu

Rufaa kwa Mahakama ya Rufaa kuhusiana na hatia iliyopatikana katika Mahakama Kuu.

**369.**-(1) Mtu aliyetiwa hatiani katika usikilizaji wa kesi uliofanywa na Mahakama Kuu anaweza kukata rufaa katika Mahakama ya Rufaa dhidi ya hatia au adhabu au vyote viwili hatia na adhabu isipokuwa hatia ya kosa la uhaini.

(2) Hakutakuwa na haki ya kukata rufaa dhidi ya adhabu pale ambapo adhabu hiyo imewekwa na sheria.

(3) Kila rufaa hiyo itakuwa kwa mujibu wa masharti kama yanavyoweza kuainishwa na Kanuni zilizotengenezwa na Mahakama ya Rufani ya Tanzania.

(4) Rufaa dhidi ya uamuzi wa Mahakama Kuu kuhusu hatia ya kosa la uhaini itasikilizwa na jopo la Majaji watatu wa Mahakama Kuu.

# SEHEMU YA KUMI NA TANO
# UPELELEZI WA VIFO VYA GHAFLA NA UCHUNGUZI WA VIFO

## Jukumu la Kutoa Taarifa ya Uhalifu au Ajali au Kifo katika Mazingira Fulani

Wajibu wa kutoa taarifa ya uhalifu.

**370.** Kila mtu ambaye ikiwa anajua au atajua utendwaji wa kosa au nia ya mtu mwengine yeyote ya kutenda kosa lenye adhabu kisheria atatoa mara moja taarifa kwa afisa wa polisi au kwa mtu yeyote mwenye mamlaka katika eneo ambaye mtu huyo atapeleka taarifa hiyo kwa mkuu wa kituo cha polisi kilicho karibu.

Wajibu wa kutoa taarifa kuhusu kukutwa maiti.

**371.** Pale ambapo maiti inakutwa au mtu amejiua au ameuliwa na mtu mwengine au kwa ajali au amefariki katika mazingira yanayoibua shaka kwamba mtu mwengine ametenda kosa, itakuwa ni wajibu wa mtu yeyote anayeikuta maiti au atakayejua kuhusu kifo mara moja kutoa taarifa kuhusu kifo hicho kwa Mkuu wa Wilaya aliye karibu naye, Sheha au afisa wa polisi.

## Upelelezi Kuhusiana na Vifo vya Ghafla

Upelelezi na taarifa ya polisi.

**372.**-(1) Mkuu wa Kituo cha Polisi, au afisa mwengine yeyote aliyepewa mamlaka mahsusi na Rais kwa ajili hiyo, baada ya kupokea taarifa kwamba mtu:

(a) amejiua;

(b) ameuliwa na mtu mwengine au kwa ajali; au

(c) amekufa katika mazingira yanayoibua shaka kwamba mtu mwengine ametenda kosa,

atatoa mara moja taarifa ya kifo hicho kwa hakimu aliyepo karibu mwenye mamlaka ya kufanya uchunguzi wa vifo, na, isipokuwa kama inaelekezwa

vyenginevyo na Kanuni zilizotolewa na Jaji Mkuu wa Zanzibar, atakwenda katika pahala ambapo mwili wa mtu aliyekufa upo, na hapo atafanya upelelezi na ataandaa taarifa ya sababu inayoonekana kuwa imesababisha kifo, inayoelezea majeraha, kuvunjika, michubuko na alama nyengine za majeraha kama yatakavyoonekana katika mwili, na itaeleza kwa namna gani au kwa silaha gani au kifaa gani, kama kipo, alama hizo zinaonekana kuwepo.

(2) Taarifa itapelekwa mara moja kwa hakimu aliyopo karibu mwenye mamlaka ya kufanya uchunguzi wa vifo.

(3) Endapo kuna shaka yoyote kuhusu sababu ya kifo, au kwa sababu nyengine yoyote afisa wa polisi anaona ni vyema kufanya hivyo, afisa wa polisi huyo, kwa mujibu wa Kanuni zilizotolewa na Jaji Mkuu wa Zanzibar, ataupeleka mwili, kwa madhumuni ya kufanyiwa uchunguzi wa kitabibu, kwa daktari aliyopo karibu au mtu mwengine aliyeteuliwa na Jaji Mkuu wa Zanzibar kwa ajili hiyo, ikiwa hali ya hewa na masafa yanaruhusu mwili huo kupelekwa bila ya athari ya kuharibika njiani ambako kutafanya uchunguzi huo wa kitabibu kuwa hauna maana.

### Uchunguzi wa Vifo

Wajibu wa kumjulisha Jaji Mkuu.

**373.-**(1) Jaji Mkuu atateua Hakimu yeyote wa Mkoa au Hakimu wa Wilaya kuchunguza kifo ama kwa ujumla au kwa uchunguzi maalum wa kifo.

(2) Endapo mtu anakufa wakati yupo katika kizuizi cha polisi, au yupo katika kizuizi cha Chuo cha Mafunzo, au yupo katika Chuo cha Mafunzo, itakuwa ni wajibu wa Kamishna wa Polisi au Kamishna wa Chuo cha Mafunzo kama hali itakavyokuwa, mara moja kumtaarifu Jaji Mkuu kuhusu kifo hicho.

(3) Endapo hakimu mwenye dhamana ya kufanya uchunguzi wa kifo tayari ameteuliwa na anajulikana, itakuwa ni wajibu wa mkuu wa kituo cha polisi au afisa mwengine yeyote aliyepewa mamlaka mahsusi na Rais, mara moja kumtaarifu hakimu huyo kuhusiana na kifo hicho na hakimu huyo ataendelea kwa mujibu wa kifungu cha 374 cha Sheria hii.

Uchunguzi wa kifo unaofanywa na hakimu.

**374.-**(1) Pale ambapo mtu anafariki katika mazingira yaliyotajwa katika kifungu cha 371, 372 au 373(2) cha Sheria hii, Hakimu aliyepewa mamlaka na Jaji Mkuu, anaweza kufanya uchunguzi wa sababu ya kifo, ama badala ya au pamoja na upelelezi uliofanywa na polisi au afisa mwengine, na katika kufanya uchunguzi chini ya kifungu hiki, Hakimu atakuwa na mamlaka yote ambayo Hakimu huyo angekuwa nayo katika kufanya uchunguzi wa kosa.

(2) Wakati wowote Hakimu huyo anapoona inafaa kufanywa uchunguzi wa maiti ya mtu aliyekwishazikwa, ili kugundua sababu ya kifo chake, Hakimu huyo au afisa wa umma anaweza kuwezesha mwili ufukuliwe na uchunguzwe.

(3) Ikiwa kabla au wakati wa kumalizika kwa uchunguzi, Hakimu anaona kwamba utendwaji kosa na mtu anayejulikana au watu umegundulika, atatoa wito au hati kwa ajili ya kumkamata au kuwakamata, kama hali itakavyokuwa, au atachukua hatua nyengine kama itakavyokuwa ni lazima ili ahudhurie au wahudhurie kujibu shtaka hilo.

(4) Baada ya kuhudhuria mtu huyo au watu hao, Hakimu ataanza uchunguzi upya na ataendelea kama kwamba alishapewa taarifa ya kosa.

(5) Ikiwa baada ya kumalizika kwa uchunguzi Hakimu ana maoni kwamba kosa limetendwa na mtu fulani au watu wasiojulikana, atarekodi maoni yake na atapeleka mara moja nakala ya maoni hayo kwa Mkurugenzi wa Mashtaka.

(6) Ikiwa baada ya kumalizika kwa uchunguzi Hakimu ana maoni kwamba hakuna kosa lililotendwa, atarekodi maoni yake ipasavyo.

## SEHEMU YA KUMI NA SITA
## MAELEKEZO YA HABEAS CORPUS NA AMRI NYENGINE ZA KIPEKEE

### Maelekezo ya Aina ya Habeas Corpus

Uwezo wa kutoa maelekezo ya aina ya *habeas corpus.*

**375.** Mahakama Kuu inaweza wakati wowote inapoona inafaa kuelekeza:

(a) kwamba mtu aliyepo ndani ya mipaka ya Zanzibar aletwe mbele ya Mahakama ili ashughulikiwe kwa mujibu wa sheria;

(b) kwamba mtu aliyewekwa kizuizini kinyume na sheria au kinyume na utaratibu katika kizuizi cha umma au binafsi ndani ya mipaka hiyo aachiliwe huru;

(c) kwamba mwanafunzi aliyewekwa kizuizini katika Chuo cha Mafunzo chochote kilichopo ndani ya mipaka hiyo aletwe mbele ya Mahakama ili hapo ahojiwe kama shahidi katika jambo lolote lililopo mahakamani au litakalochunguzwa katika mahakama hiyo;

(d) kwamba mwanafunzi aliyewekwa kizuizini kama ilivyoelezwa awali aletwe mbele ya mahakama ya kijeshi au mbele ya makamishna wowote wanaotekeleza kazi chini ya mamlaka ya kamisheni yoyote iliyoundwa na Rais kwa ajili ya usikilizaji wa kesi au kwa ajili ya kuhojiwa kuhusiana na jambo lolote lililopo mbele ya mahakama hiyo ya kijeshi au makamishna hao kama itakavyokuwa;

(e) kwamba mwanafunzi aliyepo ndani ya mipaka hiyo aondolewe kutoka kwenye kizuizi kimoja na kupelekwa kwenye kizuizi chengine kwa ajili ya usikilizaji wa kesi; au

(f) kwamba mshtakiwa aliyepo ndani ya mipaka hiyo aletwe mahakamani katika utekelezaji wa hati ya ukamataji.

Uwezo wa kutoa baadhi ya amri.

**376.** Mahakama Kuu inaweza katika utekelezaji wa mamlaka yake ya jinai kutoa amri yoyote ambayo inaweza kutolewa na Mahakama za Uingereza.

Uwezo wa kutunga kanuni.

**377.** Jaji Mkuu anaweza kutunga kanuni zinazosimamia utaratibu katika kesi chini ya vifungu vya 375 na 376 vya Sheria hii, kila baada ya muda.

## SEHEMU YA KUMI NA SABA
## MWENENDO WA KESI USIOFUATA UTARATIBU

Mwenendo wa kesi pahala pasipo sahihi.

**378.** Hakuna uamuzi, adhabu au amri ya mahakama yoyote ya jinai itakayotenguliwa kwa sababu tu kwamba uchunguzi, usikilizaji wa kesi au mwenendo mwengine wa kesi, wakati wa kufikiwa kwake ulipatikana au ulitolewa, katika wilaya au eneo jengine kimakosa, isipokuwa kama inaonekana kwamba kosa hilo limesababisha kimsingi ukosefu wa kutenda haki.

Kupokelewa au kukataliwa ushahidi kimakosa.

**379.** Kukataliwa au kukubaliwa kwa ushahidi kimakosa hakutokuwa ni sababu pekee kwa ajili ya usikilizaji mpya wa kesi au kugeuza uamuzi wowote katika kesi yoyote, ikiwa itaonekana na mahakama ambayo mbele yake pingamizi hiyo imetolewa kwamba, bila ya kutegemea ushahidi unaopingwa na ambao umepokelewa, kulikuwa na ushahidi wa kutosha kuhalalisha uamuzi, au kwamba, ikiwa ushahidi uliokataliwa ungepokelewa, usingeweza kubadilisha uamuzi.

Kuacha kula kiapo.

**380.** Hakuna kuacha kula kiapo chochote au kuthibitisha kokote, hakuna ubadilishaji wa kimoja kwa ajili ya chengine miongoni mwao, na hakuna upungufu wowote katika aina ambayo chochote katika hivyo kinatekelezwa, kitabatilisha mwenendo wowote wa kesi au kupelekea kutokupokelewa ushahidi wowote ule, au unaohusiana na, kuacha huko, kubadilisha au upungufu uliotokea, au kitakachoathiri wajibu wa shahidi kueleza ukweli.

Kuacha na makosa katika mwenendo wa kesi.

**381.-**(1) Kwa kuzingatia masharti yaliyoelezwa kabla ndani ya Sheria hii, hakuna uamuzi, adhabu au amri iliyotolewa na mahakama yenye mamlaka itakayogeuzwa au kubadilishwa katika rufaa au mapitio kwa sababu ya:

(a) kosa lolote, kuacha au upungufu katika malalamiko, wito, hati, shtaka, tamko, amri, hukumu au mwenendo mwengine mbele ya au wakati

wa usikilizaji wa kesi au katika uchunguzi wowote au mwenendo mwengine chini ya Sheria hii; au

(b) kuacha kufanya mapitio ya orodha yoyote ya washauri wa mahakama kwa mujibu wa kifungu cha 233 cha Sheria hii, isipokuwa kama kosa hilo, kuacha huko au upungufu huo kimsingi kumepelekea kukosekana kwa haki.

(2) Katika kuamua ama kosa lolote, kuacha au upungufu kumepelekea kukosekana kwa haki, mahakama itazingatia suala ama pingamizi ingeweza na ilipaswa kutolewa katika hatua za awali katika mwenendo wa kesi.

## SEHEMU YA KUMI NA NANE
## MENGINEYO

Watu ambao viapo vinaweza kuapwa mbele yao.

**382.** Viapo na uthibitisho vitakavyotumika mbele ya Mahakama Kuu vinaweza kuapwa au kuthibitishwa mbele ya Jaji wa Mahakama Kuu au Hakimu yeyote au Mrajis au Naibu Mrajis wa Mahakama Kuu au Kamishna yeyote wa viapo.

Hatimkato za mwenendo wa kesi.

**383.** Hatimkato zinaweza kuchukuliwa katika mwenendo wa kesi wakati wa usikilizaji wa mtu mbele ya Mahakama Kuu, na maandishi ya hati hizo yataandaliwa kama mahakama itaelekeza hivyo, na maandishi hayo kwa madhumuni yote yatachukuliwa kuwa ni kumbukumbu rasmi za mwenendo wa kesi katika usikilizaji huo wa kesi.

Kumbukumbu za kielektroniki.

**384.** Mahakama yoyote inaweza kuchukua kumbukumbu za mwenendo wa kesi kupitia vifaa vya kielektroniki.

Haki ya kupata nakala za mwenendo ya kesi.

**385.** Iwapo mtu yeyote ameathirika na hukumu yoyote au amri iliyotolewa katika mwenendo wowote chini ya Sheria hii anapenda kuwa na nakala ya hukumu au amri au maelezo ya shahidi au sehemu nyengine ya kumbukumbu, atapewa nakala hiyo baada ya kufanya maombi, iwapo analipa kwa ajili ya nakala hiyo, isipokuwa kama mahakama kwa sababu maalum inaona inafaa kumpa nakala hiyo bila ya gharama.

Fomu zitakazotumika.

**386.** Fomu hizo kama Mahakama Kuu mara kwa mara itakavyoidhinisha, pamoja na mabadiliko kama mazingira ya kila kesi yatakavyohitaji, zinaweza kutumika kwa madhumuni husika yaliyotajwa katika fomu hizo, na kama zimetumika zitakuwa zimetosheleza.

Gharama za washauri wa mahakama na mashahidi.

**387.** Kwa kuzingatia kanuni zozote za mahakama ambazo zinaweza kutungwa na Jaji Mkuu, mahakama yoyote inaweza kuamuru malipo kwa upande wa Serikali kwa matumizi ya msingi ya mshauri yeyote wa mahakama au shahidi anayehudhiria

mbele ya mahakama hiyo kwa madhumuni ya uchunguzi wowote, usikilizaji wa kesi au mwenendo mwengine wa kesi chini ya Sheria hii.

Kanuni za jumla.

**388.** Jaji Mkuu anaweza, kila baada ya muda, kutunga kanuni kwa ajili ya utekelezaji mzuri wa masharti ya Sheria hii.

Marekebisho ya Sheria ya Mahakama za Mahakimu.

**389.** Masharti ya Sheria ya Mahakama za Mahakimu yanayohusiana na mamlaka ya jinai ya Mahakama za Mahakimu yanafutwa na kuweka badala yake masharti ya Sheria hii yanayohusiana na mamlaka ya jinai ya Mahakama za Mahakimu.

Kufuta Sheria ya Mwenendo wa Jinai, Nam. 7 ya 2004.

**390.** Sheria ya Mwenendo wa Jinai, Nam.7 ya 2004 inafutwa.

Masharti ya Mpito.

**391.**(1) Bila ya kujali kufutwa kwa Sheria ya Mwenendo wa Jinai, Nam.7 ya 2004, jambo lolote lililopo katika Mahakama yoyote kabla ya kuanza kutumika kwa Sheria hii, umalizikaji wa jambo hilo unaathirika kwa kufutwa Sheria hii, litashughulikiwa na kumalizwa chini ya Sheria iliyofutwa.

(2) Sheria zote ndogo zilizotungwa chini ya Sheria iliyofutwa zitaendelea kuwa na nguvu za kisheria kama kwamba zimetungwa chini ya Sheria hii, isipokuwa kama baadae zitafutwa.

(3) Kitendo chochote cha jinai kilichotendwa au kuacha kutendwa, kabla ya kufutwa kwa Sheria ya Adhabu Nam.6 ya 2004 na ambacho bado hakijapelekwa katika mahakama yoyote, kinaweza kupelelezwa, kuchunguzwa au kusikilizwa katika kesi chini ya masharti ya Sheria hii.

## JADWELI YA KWANZA

**Makosa chini ya Sheria ya Adhabu**

[Chini ya Vifungu vya 4 (1) na 5 (2)]

## MAELEZO YA UFAFANUZI

1. Yaliyomo katika kolamu ya pili na ya nne ya Jadweli hili, yenye vichwa vya habari "Kosa" na "Adhabu chini ya Sheria ya Adhabu" hayakusudiwi kuwa tafsiri ya makosa na adhabu zilizoelezwa katika vifungu husika mbalimbali vya Sheria ya Adhabu au wala siyo ufupisho wa vifungu hivyo, lakini tu ni marejeo kuhusu maudhui ya kifungu hicho, ambacho namba yake imewekwa katika kolamu ya kwanza.

2. Chini ya kifungu cha 307 cha Sheria hii mtu anaewajibika kupewa adhabu ya kifungo anaweza kupewa adhabu ya kulipa faini pamoja na kifungo au badala ya kifungo:

Isipokuwa kwamba endapo faini inayoainishwa ni mbadala wa kifungo mtu huyo hatowajibika kutumikia adhabu zote mbili isipokuwa kama imeelezwa hivyo.

Makosa yote yanayosikilizwa na Mahakama Kuu na maneno "Mahakama Kuu" yanaonekana tu katika kolamu ya nne katika kesi pekee zinazosikilizwa na mahakama hiyo.

| (1) | (2) | (3) | (4) | (5) |
|---|---|---|---|---|
| *Kifungu* | *Kosa* | *Iwapo afisa wa polisi anaweza au hawezi kukamata bila ya halali.* | *Adhabu chini ya Sheria Adhabu.* | *Mahakama ambayo kosa linaweza kusikilizwa.* |

## SEHEMU YA NNE
## WAHUSIKA KATIKA MAKOSA

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 24 | Kumshawishi mwengine kutenda kosa. | Anaweza kukamata bila hati ya ukamataji ikiwa ukamataji kwa kosa la kusaidia, kuwezesha, kushauri au kusaidia kuwezesha kutendwa kosa kunaweza kufanywa bila ya hati ya ukamataji lakini siyo vyenginevyo. | Adhabu ile ile kwa kosa la kusaidia, kuwezesha, kushauri au kuwezesha kutendwa. | Mahakama yoyote ambayo kosa la kusaidia, kuwezesha, kushauri au kuwezesha kutendwa linaweza kusikilizwa. |

## SEHEMU YA SITA

## UHAINI NA MAKOSA MENGINE DHIDI YA SERIKALI

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 27 | Uhaini | Anaweza kukamata bila hati | Kifo | Mahakama Kuu |
| 28 | Kuingia Zanzibar kwa nia ya kupanga dhidi ya Mapinduzi | Anaweza kukamata bila hati | Kifo | Mahakama Kuu |
| 29 | Kuchochea uvamizi | Anaweza kukamata bila hati | Kifo | Mahakama Kuu |
| 30 | Kuficha uhaini. | Anaweza kukamata bila hati | Kifungo cha maisha | Mahakama Kuu |
| 31 | Makosa yanayohusiana na uhaini. | Anaweza kukamata bila hati | Kifungo cha maisha | Mahakama Kuu |
| 33 | Kuchochea uasi. | Anaweza kukamata bila hati | Kifungo cha maisha | Mahakama Kuu |
| 34 | Kuwasaidia Wanajeshi au maafisa wa polisi katika vitendo vya uasi. | Hawezi kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka mitano | Mahakama ya Wilaya |
| 35 | Kuwashawishi wanajeshi au maofisa wa polisi kutoroka | Hawezi kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka mitano lakini kisichozidi miaka kumi | Mahakama ya Mkoa |
| 36 | Kusaidia kwa kujua mateka wa vita kutoroka | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo cha maisha | Mahakama Kuu |
| 37 | Kuruhusu kwa uzembe mateka wa vita kutoroka | Hawezi kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka miwili | Mahakama ya mwanzo au Mahakama ya Mkoa |
| 39 | Viapo visivyo halali ili kutenda makosa makubwa | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo cha maisha | Mahakama Kuu |
| 40(b) | Viapo vyengine visivyo halali ili kutenda makosa | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka saba. | Mahakama ya Wilaya au Mahakama ya Mkoa |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 42(1) | Mafunzo ya kijeshi yasiyo halali. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka saba. | Mahakama ya Wilaya au Mahakama ya Mkoa |
| 42(2) | Kufundishwa mafunzo ya kijeshi yasiyo halali | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka miwili | Mahakama ya Mwanzo au Mahakama ya Wilaya |
| 43 | Kuchapisha taarifa za uongo | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kisichopungua miezi sita lakini kisichozidi miaka miwili | Mahakama ya Mwanzo au Mahakama ya Wilaya |
| 44 | Kuchochea kufanya ghasia | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka miwili | Mahakama ya Mwanzo au Mahakama ya Wilaya |

## SEHEMU YA SABA

## MAKOSA YANAYOATHIRI MAHUSIANO NA NCHI ZA NJE NA UTULIVU WA NJE

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 45 | Kukashifu. | Hawezi kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka miwili | Mahakama ya Mwanzo au Mahakama ya Wilaya |
| 46 | Uandikishaji wa wanajeshi wa kigeni | Hawezi kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka miwili | Mahakama ya Mwanzo au Mahakama ya Wilaya |
| 47 | Uharamia. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo cha maisha | Mahakama Kuu |

**SEHEMU YA NANE**

**MIKUSANYIKO ISIYO HALALI, GHASIA NA MAKOSA MENGINE DHIDI YA UTULIVU WA JAMII**

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 49(1) | Kuongoza jumuiya isiyo halali. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka saba | Mahakama ya Mkoa |
| 49(2) | Kuwa mwanachama wa jumuiya isiyo halali | Anaweza kukamata bila ya hati | Faini Shilingi Laki Tatu au kifungo kwa kipindi cha miezi mitatu | Mahakama ya Mkoa |
| 55 | Mkusanyiko usio halali. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi kisichozidi mwaka mmoja | Mahakama ya Mwanzo au Mahakama ya Wilaya |
| 56 | Adhabu ya kushiriki katika ghasia. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka miwili | Mahakama ya Mwanzo au Mahakama ya Wilaya |
| 59 | Ghasia baada ya tangazo. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka mitano | Mahakama ya Wilaya |
| 60 | Kuzuia au kupinga utoaji wa tangazo. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka kumi au mitano | Mahakama ya Mkoa |
| 61 | Wafanya ghasia kubomoa majengo. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo cha maisha | Mahakama Kuu |
| 62 | Wafanya ghasia kuharibu majengo. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka saba | Mahakama ya Mkoa |
| 63 | Kuingilia kwa ghasia gari au chombo cha baharini. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka miwili | Mahakama ya Mwanzo au Mahakama ya Wilaya |
| 64(1) | Kutembea na silaha hadharani | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka miwili | Mahakama ya Mwanzo au Mahakama ya Wilaya |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 64(2) | Kumiliki silaha bila halali. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka mitano lakini kisichozidi miaka kumi na nne. | Mahakama ya Mkoa |
| 65 | Kuingia kwa nguvu. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka miwili | Mahakama ya Mwanzo au Mahakama ya Wilaya |
| 66 | Kuzuia kwa nguvu. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka miwili | Mahakama ya Mwanzo au Mahakama ya Wilaya |
| 67 | Kupigana hadharani. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miezi sita au faini ya Shilingi Laki Tano | Mahakama ya Mwanzo |
| 68 | Kuchochea mapigano ya watu wawili. | Hawezi kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka miwili | Mahakama ya Mwanzo au Mahakama ya Wilaya |
| 69(1) | Kutishia kwa kutumia nguvu. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha mwaka mmoja | Mahakama ya Mwanzo au Mahakama ya Wilaya |
| 69(2) | Iwapo kosa limetendwa wakati wa usiku. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka miwili | Mahakama ya Mwanzo au Mahakama ya Wilaya |
| 70 | Kusumbua na kuzonga. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miezi sita au faini isiyozidi Shilingi Laki Tano | Mahakama ya Mwanzo |
| 71 | Kutisha. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha mwaka mmoja au faini isiyozidi Shilingi Milioni Moja | Mahakama ya Mwanzo au Mahakama ya Wilaya |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 72 | Mkusanyiko kwa madhumuni ya kufanya magendo. | Anaweza kukamata bila ya hati | Faini isiyozidi Shilingi Laki Tano au kifungo kwa kipindi cha miezi sita | Mahakama ya Mwanzo au Mahakama ya Wilaya |
| 73(1) (a) | Silaha za hatari katika mikutano ya hadhara. | Anaweza kukamata bila ya hati | Faini isiyozidi Shilingi Laki Mbili na Elfu Hamsini au kifungo kwa kipindi cha miezi mitatu | Mahakama ya Mwanzo |
| 73(1) (b) | Kitendo cha uvunjifu wa amani katika mikutano ya hadhara. | Anaweza kukamata bila ya hati | Faini isiyozidi Shilingi Laki Mbili na Elfu Hamsini au kifungo kwa kipindi cha miezi mitatu | Mahakama ya Mwanzo |
| 74 | Kuwa na silaha za hatari bila ya mamlaka ya kisheria. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka miwili | Mahakama ya Mwanzo au Mahakama ya Wilaya |

## SEHEMU YA TISA

## MAKOSA YANAYOHUSU USIMAMIZI WA HAKI

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 76 | Maelezo ya uwongo ya wakalimani. | Hawezi kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka saba | Mahakama ya Mkoa |
| 77 | Adhabu ya kutoa ushahidi wa uongo na kushawishi kutoa ushahidi wa uongo. | Hawezi kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka saba | Mahakama ya Mkoa |
| 79 | Kutunga ushahidi. | Hawezi kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka saba | Mahakama ya Mkoa |
| 80 | Kiapo cha uongo. | Hawezi kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka miwili | Mahakama ya Wilaya |
| 81 | Kudanganya mashahidi. | Hawezi kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka miwili | Mahakama ya Wilaya |
| 82 | Kuharibu ushahidi. | Hawezi kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka miwili | Mahakama ya Wilaya |
| 83 | Njama za kuzuia haki na kuingilia mashahidi. | Hawezi kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka miwili | Mahakama ya Wilaya |
| 84 | Kufifilisha makosa. | Hawezi kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka miwili | Mahakama ya Wilaya |
| 85 | Kufifilisha mashtaka. | Hawezi kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka miwili | Mahakama ya Wilaya |
| 86 | Matangazo kwa mali iliyoibiwa. | Hawezi kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka miwili | Mahakama ya Wilaya |
| 87(1) | Kudharau Mahakama. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miezi mitatu | Mahakama yoyote |
| 87(2) | Kudharau Mahakama mbele ya mahakama. | Anaweza kukamata bila ya hati | Faini ya Shilingi Laki Moja au kifungo kwa kipindi cha mwezi mmoja akishindwa kulipa faini. | Mahakama ambayo mbele yake kosa limetendwa |

## SEHEMU YA KUMI
## KUOKOA, KUTOROKA NA KUWAZUIA WATUMISHI WA MAHAKAMA

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 88(a) | Kuokoa. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo cha maisha | Mahakama Kuu |
| 88(b) | Kuokoa. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kisichozidi miaka saba | Mahakama ya Mkoa. |
| 88(c) | Kuokoa. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kisichozidi miaka miwili | Mahakama ya Wilaya. |
| 89(1) | Kutoroka kwenye kizuizi halali. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi mara mbili zaidi ya kifungo alichokuwa akikitumikia kwenye kizuizi halali | Mahakama yoyote |
| 89(3) | Kutoroka kwenye kizuizi halali. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka miwili | Mahakama ya Wilaya. |
| 90 | Kusaidia wafungwa kutoroka | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka saba | Mahakama ya Mkoa |
| 91 | Kutoroka kwenye kizuizi halali. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka miwili au faini isiyozidi Shilingi Milioni Mbili au zote Mbili | Mahakama ya Wilaya. |
| 92 | Uondoshaji wa mali iliyokamatwa kihalali. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka miwili | Mahakama ya Wilaya |
| 93 | Kuwazuia maafisa wa Mahakama. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha mwaka mmoja | Mahakama ya Wilaya |

## SEHEMU YA KUMI NA MOJA
## MAKOSA MCHANGANYIKO DHIDI YA MAMLAKA YA UMMA

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 94 | Udanganyifu na uvunjaji uaminifu kwa watumishi wa umma | Hawezi kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka miwili | Mahakama ya Wilaya |
| 95 | Kuupuza wajibu wa kikazi | Hawezi kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka miwili | Mahakama ya Wilaya |
| 96 | Kusababisha hasara kwa Serikali au Taasisi za Umma | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi kinachozidi miaka mitatu lakini kisichozidi miaka kumi au faini inayozidi Milioni Tatu lakini isiyozidi Shilingi Milioni Kumi au adhabu zote mbili | Mahakama ya Wilaya au Mahakama ya Mkoa |
| 97 | Kutoa taarifa za uongo kwa mtumishi wa umma. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miezi sita au faini ya Shilingi Laki Tano au adhabu zote mbili | Mahakama ya Mwanzo au Mahakama ya Wilaya |
| 98 | Kutokutii wajibu wa kisheria. | Hawezi kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha mwaka mmoja au faini ya Shilingi Milioni Moja | Mahakama ya Wilaya |
| 99 | Kutokutii amri za halali. | Hawezi kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka miwili au faini ya Shilingi Milioni Mbili au adhabu zote mbili | Mahakama ya Wilaya |

## SEHEMU YA KUMI NA MBILI
## MAKOSA YANAYOHUSIANA NA DINI

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 100 | Kukashifu dini yoyote. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka miwili | Mahakama ya Wilaya |
| 101 | Kufanya ghasia kwenye mikusanyiko ya dini. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka miwili | Mahakama ya Wilaya |
| 102 | Kuingia sehemu ya makaburi bila halali. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka miwili | Mahakama ya Wilaya |
| 103 | Kuzuia mazishi ya mwili wa mtu aliyekufa. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka miwili | Mahakama ya Wilaya |
| 104 | Kuandika au kutamka maneno kwa nia ya kuumiza imani ya dini. | Hawezi kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka miwili | Mahakama ya Wilaya |
| 105 | Kukashifu dini. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka saba | Mahakama ya Mkoa |
| 106(1) | Kuhamasisha uadui baina ya makundi tofauti. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka mitatu | Mahakama ya Wilaya |
| 106(2) | Kuhamasisha uadui baina ya makundi tofauti | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka mitano | Mahakama ya Wilaya |

**SEHEMU YA KUMI NA TATU**

**MAKOSA DHIDI YA MAADILI**

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 109(1) | Adhabu ya kubaka. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo cha maisha, au kifungo kisichopungua miaka thelathini na faini na fidia | Mahakama ya Mkoa |
| 109(2)(a) | Adhabu ya kubaka. | Anaweza kukamata bila ya hati | Mwaka mmoja katika nyumba ya watoto, skuli zilizoidhinishwa au kuitumikia jamii | Mahakama ya Mkoa |
| 109(2)(b) | Adhabu ya kubaka. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miezi kumi na mbili | Mahakama ya Mkoa |
| 109(2)(c) | Adhabu ya kubaka. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo cha maisha, au kifungo kisichopungua miaka thelathini na faini na fidia | Mahakama ya Mkoa |
| 110 | Adhabu ya kubaka kwa kundi | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo cha maisha | Mahakama ya Mkoa |
| 111(1) | Kujaribu kubaka | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka ishirini | Mahakama ya Mkoa |
| 111(3) | Kujaribu kubaka | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo cha miezi sita kwenye nyumba ya watoto, skuli iliyoidhinishwa au kuitumikia jamii | Mahakama ya Mkoa |
| 112 | Kutorosha mwanamke | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka saba | Mahakama ya Mkoa |
| 113 | Kutorosha watoto wa kike na wa kiume | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka kumi | Mahakama ya Mkoa |
| 114(1) | Shambulio la aibu | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka kumi na nne na fidia | Mahakama ya Mkoa |
| 114(3) | Shambulio la aibu | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka mitatu na fidia | Mahakama ya Mkoa |
| 115(1) | Kunajisi mtoto wa kiume. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo cha maisha | Mahakama ya Mkoa |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 115(2) | Kujaribu kunajisi mtoto wa kiume | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka thelathini | Mahakama ya Mkoa |
| 116(1) | Kunajisi mtu mwenye ulemavu wa akili | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo cha maisha | Mahakama ya Mkoa |
| 116(2) | Kujaribu kunajisi mtu mwenye ulemavu wa akili | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka thelathini | Mahakama ya Mkoa |
| 117 | Kuwezesha ukahaba | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka mitano na kisichozidi miaka kumi au faini isiyopungua Shilingi Milioni Tano lakini isiyozidi Shilingi Milioni Kumi au adhabu zote mbili | Mahakama ya Mkoa |
| 118 | Kuwezesha ngono haramu | Anaweza kukamata bila ya hati | Faini isiyopungua Shilingi Milioni Moja lakini isiyozidi Shilingi Milioni Kumi au kifungo kisichopungua mwaka mmoja lakini kisichozidi miaka kumi au adhabu zote mbili | Mahakama ya Mkoa |
| 119 | Mwenye nyumba kuruhusu mtoto wa kiume kunajisiwa | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka kumi | Mahakama ya Wilaya |
| 120 | Mwenye nyumba kuruhusu mtoto wa kike kuingiliwa | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka kumi | Mahakama ya Wilaya |
| 121 | Kumzuia mwanamke, mtoto wa kike au mtoto wa kiume katika danguro au penginepo | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka saba | Mahakama ya Mkoa |
| 123 | Kosa la ukahaba. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka mitatu | Mahakama ya Wilaya |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 124 | Mtu mwanamme anayeishi kwa kipato cha ukahaba. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka miwili | Mahakama ya Wilaya |
| 125 | Mtu mwanamke anayeishi kwa kipato cha ukahaba au kusaida ukahaba. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka miwili | Mahakama ya Wilaya |
| 127 | Danguro. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka miwili | Mahakama ya Wilaya |
| 128 | Njama ya kubaka. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka mitatu | Mahakama ya Wilaya |
| 129 | Kujaribu kuwezesha kutoa mimba. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka kumi na nne | Mahakama ya Mkoa |
| 130 | Kutoa mimba kwa mwanamke au mtoto wa kike | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka saba | Mahakama ya Mkoa |
| 131 | Kutoa dawa au vifaa vya kuwezesha kutoa mimba. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka mitatu | Mahakama ya Wilaya |
| 133 | Makosa ya kuingilia kinyume na maumbile. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka thelathini | Mahakama ya Mkoa |
| 134 | Kujaribu kutenda kosa la kuingilia kinyume na maumbile. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka kumi | Mahakama ya Mkoa |
| 135 | Shambulio la aibu kwa mtoto wa kiume. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka ishirini na tano | Mahakama ya Mkoa |
| 136 | Matendo ya usagaji. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka kumi | Mahakama ya Mkoa |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 137(1) | Matendo ya aibu kubwa baina ya watu. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka mitatu lakini kisichozidi miaka mitano au faini isiyopungua Shilingi Milioni Tatu na isiyozidi Milioni Tano | Mahakama ya Mkoa |
| 137(2) | Endapo kosa limetendwa na mtu mwenye umri wa miaka kumi na nane au zaidi | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka mitano lakini kisichozidi miaka kumi na fidia itakayoamuliwa na Mahakama | Mahakama ya Mkoa |
| 138 | Utumiaji wa watoto kingono. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka mitano na kisichozidi miaka ishirini | Mahakama ya Mkoa |
| 139(2)(a) | Udhalilishaji mkubwa wa kingono. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo si chini ya miaka kumi na tano lakini kisichozidi miaka thelathini na fidia | Mahakama ya Mkoa |
| 139(2)(b) | Udhalilishaji mkubwa wa kingono. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo si chini ya miaka ishirini na tano lakini kisichozidi miaka thelathini na fidia | Mahakama ya Mkoa |
| 140 | Muungano wa watu wa jinsia moja. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka saba | Mahakama ya Mkoa |
| 141(1) | Usumbufu wa kingono. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka mitano au faini isiyozidi Shilingi Milioni Tano au adhabu zote mbili | Mahakama ya Wilaya |
| 142 | Uzinifu. | Hawezi kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka miwili | Mahakama ya Wilaya |
| 143(2) | Kufanya maingiliano ya kingono na maharimu. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka ishirini na tano | Mahakama ya Mkoa |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 143(3) | Kufanya maingiliano ya kingono na maharimu. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka mitano | Mahakama ya Mkoa |
| 143(4) | Kufanya maingiliano ya kingono na maharimu. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo cha maisha | Mahakama ya Mkoa |
| 143(5) | Kufanya maingiliano ya kingono na maharimu. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kisichopungua miaka ishirini | Mahakama ya Mkoa |
| 143(6) | Kufanya maingiliano ya kingono na maharimu. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kisichopungua miaka kumi | Mahakama ya Mkoa |
| 143(7) | Kufanya maingiliano ya kingono na maharimu. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kisichopungua miaka mitatu | Mahakama ya Mkoa |
| 145 | Kuweka wazi utambulisho wa muathirika. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka miwili na fidia | Mahakama ya Wilaya |

SEHEMU YA KUMI NA NNE

**MAKOSA YANAYOHUSIANA NA NDOA NA MAHUSIANO YA KIFAMILIA**

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 146 | Ndoa ya hadaa | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka kumi | Mahakama ya Mkoa |
| 147 | Kufunga ndoa kinyume na sheria. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka mitano | Mahakama ya Wilaya |
| 148 | Sherehe ya ndoa iliyofanyika kihadaa bila ya ndoa halali. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka mitano | Mahakama ya Wilaya |
| 149 | Ukatili kwa watoto. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kisichopungua miaka mitano lakini kisichozidi miaka kumi na tano au faini isiyozidi Milioni Kumi na Tano au adhabu zote mbili na fidia | Mahakama ya Mkoa |
| 150 | Kutelekeza mtoto au mtu mwenye ulemavu. | Hawezi kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka miwili | Mahakama ya Wilaya |
| 151 | Kupuuza kutoa chakula kwa mtoto au mtu mwenye na ulemavu. | Hawezi kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka miwili | Mahakama ya Wilaya |
| 152 | Mwajiri kutompatia mwanafunzi au mwajiriwa wake mahitaji. | Hawezi kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka miwili | Mahakama ya Wilaya |
| 153 | Usafirishaji wa binaadamu. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kisichopungua miaka mitano lakini kisichozidi miaka ishirini au faini isiyopungua Shilingi Milioni Tano lakini isiyozidi Shilingi Milioni Ishirini au adhabu zote mbili | Mahakama Kuu |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 154 | Kuiba mtoto. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kisichopungua miaka mitano lakini kisichozidi miaka kumi | Mahakama ya Wilaya |

**SEHEMU YA KUMI NA TANO**

**MAUDHI NA MAKOSA DHIDI YA AFYA NA UTULIVU**

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 155 | Maudhi kwa jamii. | Hawezi kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha mwaka mmoja | Mahakama ya Mwanzo au Mahakama ya Wilaya |
| 156(3) | Nyumba ya kamari. | Hawezi kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka mitatu | Mahakama ya Wilaya |
| 156(4) | Kukutwa katika nyumba maarufu ya kamari | Hawezi kukamata bila ya hati | Faini isiyopungua Shilingi Milioni Mbili kwa kosa la kwanza; na kwa kila kosa linalofuata atatozwa faini isiyopungua Shilingi Milioni Tatu au kifungo kisichopungua miaka miwili au adhabu zote mbili | Mahakama ya Wilaya |
| 157 | Mashine za kamari | Hawezi kukamata bila ya hati | Faini isiyopungua Shilingi Milioni Nne au kifungo kisichopungua miaka minne au adhabu zote mbili. | Mahakama ya Wilaya |
| 158 | Nyumba ya kuweka dau. | Hawezi kukamata bila ya hati | Kifungo kisichozidi miaka minne au faini isiyozidi Shilingi Milioni Nne au adhabu zote mbili | Mahakama ya Wilaya |
| 159(1) | Bahati nasibu | Hawezi kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka miwili | Mahakama ya Wilaya |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 159(2) | Kuchapisha au kutangaza-tangazo au linalohusiana na bahati nasibu | Hawezi kukamata bila ya hati | Faini isiyozidi Shilingi Laki Tano | Mahakama ya Wilaya |
| 161 | Kusafirisha machapisho machafu. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka mitatu lakini kisichozidi miaka sita au faini isiyopungua Shilingi Milioni Tatu na isiyozidi Shilingi Milioni Sita | Mahakama ya Wilaya au Mahakama ya Mkoa |
| 162 | Matendo machafu. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miezi mitatu au faini ya Shilingi Laki Mbili na Elfu Hamsini au adhabu zote mbili | Mahakama ya Mwanzo |
| 163 | Watu wavivu na wenye tabia mbaya. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi kisichopungua mwaka mmoja na kisichozidi miaka miwili au faini isiyopungua Shilingi Milioni Moja na isiyozidi Shilingi Milioni Mbili | Mahakama ya Wilaya |
| 164 | Wakorofi na wazururaji. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi kisichopungua miezi mitatu lakini kisichozidi miaka miwili au faini isiyozidi Shilingi Milioni Mbili | Mahakama ya Mwanzo |
| 165(1) | Makosa dhidi ya sare za kijeshi. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha mwezi mmoja au faini isiyozidi Shilingi Laki Moja | Mahakama ya Mwanzo |
| 165(3) | Kuleta dharau kwa sare | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miezi mitatu au faini isiyozidi Shilingi Laki Mbili na Elfu Hamsini | Mahakama ya Mwanzo |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 165(4) | Kuingiza au kuuza sare bila ya ruhusa | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miezi sita au faini isiyozidi Shilingi Laki Tano | Mahakama ya Mwanzo |
| 166 | Kitendo cha uzembe kinachoweza kueneza maambukizo. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka miwili | Mahakama ya Wilaya |
| 167 | Kuchafua maji. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka miwili | Mahakama ya Wilaya |
| 168 | Kuchafua hewa. | Hawezi kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka miwili | Mahakama ya Wilaya |
| 169 | Biashara mbaya. | Hawezi kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha mwaka mmoja | Mahakama ya Wilaya |
| 170 | Kutotii amri ya karantini. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi kisichozidi miezi sita au faini isiyozidi Shilingi Laki Tano au adhabu zote mbili | Mahakama ya Wilaya |
| 171 | Adhabu ya maudhi kwa jamii. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi kisichozidi mwaka mmoja | Mahakama ya Wilaya |
| 172 | Kuendelea kwa maudhi. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka miwili au faini isiyozidi Shilingi Milioni Mbili au adhabu zote mbili | Mahakama ya Wilaya |
| 173 | Kuchanganya chakula na kitu kingine. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka miwili | Mahakama ya Wilaya |
| 174 | Kuuza chakula chenye madhara. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka miwili | Mahakama ya Wilaya |
| 175 | Kuchanganya dawa. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka miwili | Mahakama ya Wilaya |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 176 | Kuuza dawa zilizochanga-nywa. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka miwili | Mahakama ya Wilaya |

**SEHEMU YA KUMI NA SITA**
**KUUA, KUUA BILA YA KUKUSUDIA NA KUUA MTOTO MCHANGA**

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 178 | Adhabu ya kuua bila kukusudia. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo cha maisha | Mahakama Kuu |
| 180 | Adhabu ya kuua kwa kukusudia. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifo | Mahakama Kuu |
| 182 | Kuua kwa kukasirishwa. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo cha maisha | Mahakama Kuu |
| 187 | Kuua mtoto mchanga. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka saba | Mahakama Kuu |

**SEHEMU YA KUMI NA SABA**
**WAJIBU KUHUSIANA NA HIFADHI YA MAISHA NA AFYA**

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 192 | Adhabu kwa kushindwa kutimiza wajibu. | Hawezi kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi kisichozidi mwaka mmoja au faini isiyozidi Shilingi Milioni Moja au adhabu zote mbili | Mahakama ya Wilaya |

## SEHEMU YA KUMI NA NANE
## MAKOSA YANAYOHUSIANA NA KUUA KWA KUKUSUDIA NA KUJIUA

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 193 | Kujaribu bila halali kusababisha kifo. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo cha maisha | Mahakama Kuu |
| 194 | Kusaidia baada ya kutendeka kosa la kuua kwa kukusudia. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka saba | Mahakama Kuu |
| 195 | Kutishia kwa maandishi kuua kwa kukusudia. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka saba | Mahakama Kuu |
| 196 | Kula njama ya kuua kwa makusudi. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka kumi na nne | Mahakama Kuu |
| 197 | Kusaidia kujiua. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo cha maisha | Mahakama Kuu |
| 198 | Kujaribu kujiua. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka miwili | Mahakama ya Wilaya |
| 199 | Kuficha kuzaliwa kwa mtoto. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka miwili | Mahakama ya Wilaya |
| 200 | Kuharibu mtoto. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo cha maisha | Mahakama Kuu |
| 201(1) | Kuficha mpango wa kutenda kosa. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka saba au miaka mitatu | Mahakama ya Mkoa |
| 201(2) | Kuficha mpango wa kutenda kosa. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha mwaka mmoja au miezi sita | Mahakama ya Mkoa |

## SEHEMU YA KUMI NA TISA

## MAKOSA YA KUHATARISHA MAISHA AU AFYA

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 202 | Kumzuia mtu kujihami ili kosa litendeke. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo cha maisha | Mahakama ya Mkoa |
| 203 | Kumpumbaza mtu kwa nia ya kutenda kosa. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo cha maisha | Mahakama ya Mkoa |
| 204 | Vitendo vinavyokusudia kusababisha madhara makubwa au kuzuia ukamataji | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo cha maisha | Mahakama ya Mkoa |
| 205 | Kumzuia mtu kujiokoa katika chombo. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo cha maisha | Mahakama ya Mkoa |
| 206 | Kwa makusudi kuhatarisha usalama wa watu wanaosafiri kwa reli. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo cha maisha | Mahakama ya Mkoa |
| 207 | Kuhatarisha usalama wa chombo. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo cha maisha | Mahakama ya Mkoa |
| 208 | Madhara makubwa. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka saba | Mahakama ya Mkoa |
| 209 | Kujaribu kujeruhi kwa kitu kinachoripuka. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka kumi na nne | Mahakama Kuu |
| 210 | Kuweka sumu kwa nia mbaya kwa lengo la kudhuru. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka kumi na nne | Mahakama Kuu |
| 211 | Kujeruhi na matendo yanayofanana na hayo. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka mitatu | Mahakama ya Wilaya |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 212 | Kushindwa kutoa mahitaji ya muhimu. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka mitatu | Mahakama ya Wilaya |

**SEHEMU YA ISHIRINI**

**MAKOSA YANAYOHUSIANA NA SHUGHULI ZA MAKUNDI YA KIJINAI**

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 216&217<br><br>216(1) | Makosa yanayohusiana na makundi. | Anaweza kukamata bila ya hati | Faini isiyozidi Shilingi Milioni Sita au kifungo kwa kipindi cha miaka sita | Mahakama ya Mkoa |
| 216(2)(a) | Kusababisha au kuchangia kwenye mpango wa shughuli za kundi la kihalifu | Anaweza kukamata bila ya hati | Faini isiyozidi Shilingi Milioni Sita au kifungo kwa kipindi cha miaka sita | Mahakama ya Mkoa |
| 216(2)(b) | Kushawishi na kuchochea katika mpango wa shughuli za kundi la kihalifu | Anaweza kukamata bila ya hati | Faini isiyozidi Shilingi Milioni Tatu au kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka mitatu | Mahakama ya Mkoa |
| 216(2)(c) | Kusababisha, kuhamasisha, kufundisha kujiunga na kundi la kihalifu. | Anaweza kukamata bila ya hati | Faini isiyozidi Shilingi Milioni Tatu au kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka mitatu | Mahakama ya Mkoa |

## SEHEMU YA ISHIRINI NA MOJA
## JINAI KWA KUTOJALI NA KUPUUZA

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 219 | Tendo la kuharakisha au la kizembe linalosababisha kifo. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka kumi au faini isiyozidi Shilingi Milioni Kumi au adhabu zote mbili | Mahakama Kuu |
| 220 | Vitendo vya kuharakisha na vya kizembe. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka miwili | Mahakama ya Wilaya |
| 221(1) | Kuondosha matonsisi. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka mitano | Mahakama ya Wilaya |
| 221(2) | Kuondosha matonsisi. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo cha maisha | Mahakama Kuu |
| 222(1) | Uondoshaji wa viungo vya binaadamu. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka ishirini | Mahakama Kuu |
| 222(2) | Uondoshaji wa viungo vya binaadamu. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifo | Mahakama Kuu |
| 223 | Vitendo vyengine vya uzembe vinavyosababisha madhara. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miezi sita au faini isiyozidi Shilingi Laki Tano | Mahakama ya Wilaya |
| 224 | Ushughulikiaji vitu vya sumu kwa uzembe. | Hawezi kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miezi sita au faini isiyozidi Shilingi Laki Tano | Mahakama ya Wilaya |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 225 | Kuhatarisha usalama wa watu wanaosafiri kwa njia ya reli. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka miwili | Mahakama ya Wilaya |
| 226 | Kuonesha taa za uongo, alama au boya. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka saba | Mahakama ya Mkoa |
| 227 | Kusafirisha mtu kwa njia ya maji kwa malipo katika chombo kisichokuwa salama au kilichojaza sana. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka miwili | Mahakama ya Wilaya |
| 228 | Hatari au kizuwizi kwenye njia ya umma au njia ya usafiri. | Hawezi kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi kisichozidi mwaka mmoja au faini isiyozidi Shilingi Milioni Moja au adhabu zote mbili | Mahakama ya Wilaya |

## SEHEMU YA ISHIRINI NA MBILI
## MASHAMBULIO

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 229 | Shambulio la kawaida. | Hawezi kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha mwaka mmoja | Hakimu yeyote |
| 230 | Shambulio linalosababisha madhara ya mwili. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka mitano | Mahakama ya Wilaya |
| 231 | Mashambulio kwa watu wanaolinda vyombo. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka saba | Mahakama ya Mkoa |
| 232 | Mashambulio mbali mbali | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka mitano | Mahakama ya Wilaya |

## SEHEMU YA ISHIRINI NA TATU
## MAKOSA DHIDI YA UHURU WA MTU

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 233, 234 & 235 | Adhabu ya kuteka nyara. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka kumi | Mahakama Kuu |
| 237 | Kuteka nyara au kutorosha kwa ajili ya kuua kwa kukusudia. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo cha maisha | Mahakama Kuu |
| 238 | Kuteka nyara au kutorosha kwa nia ya kumfungia mtu. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka kumi na nne | Mahakama Kuu |
| 239 | Kuteka nyara au kutorosha kwa nia ya kumsababishia mtu madhara makubwa au kumfanya mtumwa. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka kumi | Mahakama Kuu |
| 240 | Kuficha mtu aliyetekwa au kutoroshwa kinyume na sheria. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka kumi | Mahakama Kuu |
| 241 | Kumteka nyara au kumtorosha mtoto kwa nia ya kumuibia. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka saba | Mahakama ya Mkoa |
| 242 | Kuteka nyara au kutorosha mtoto kwa nia ya kudai fedha. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka kumi na tano | Mahakama Kuu |
| 243& 245 | Adhabu ya kuzuia bila halali. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi kisichozidi mwezi mmoja au faini isiyozidi Shilingi Laki Moja | Mahakama ya mwanzo |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 244 & 246 | Adhabu ya kuweka kizuizini bila halali. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha mwaka mmoja au faini isiyozidi Shilingi Milioni Moja | Mahakama ya Wilaya |
| 247 | Kumnunua au kumuuza mtu yeyote kama mtumwa. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka saba | Mahakama ya Mkoa |
| 248 | Mazoea ya kujihusisha na watumwa. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka kumi | Mahakama Kuu |
| 249 | Kumlazimisha mtu kufanya kazi. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka mitatu na kisichozidi miaka mitano | Mahakama ya Wilaya |

## SEHEMU YA ISHIRINI NA NNE
## WIZI

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 258 | Adhabu ya jumla ya wizi. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka mitatu | Hakimu yeyote |
| 259 | Kuiba wasia | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka kumi | Mahakama ya Mkoa |
| 260 | Kuiba kutoka maungoni au kuiba bidhaa zinazosafirishwa. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka saba | Mahakama ya Mkoa |
| 261(1) | Kuibia Serikali. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi kisichopungua mwaka mmoja lakini kisichozidi miaka minne | Mahakama ya Wilaya |
| 261(2) | Kuibia Serikali. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka mitano na fidia | Mahakama ya Wilaya |
| 262 | Wizi wa makarani na watumishi. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka saba | Mahakama ya Mkoa |
| 263 | Wizi wa wakurugenzi au maafisa wa makampuni. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka saba | Mahakama ya Mkoa |
| 264 | Wizi wa mawakala. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka saba | Mahakama ya Mkoa |
| 265 | Wizi wa wapangaji au wageni. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka saba | Mahakama ya Mkoa |
| 266 | Kuiba baada ya kutiwa hatiani awali. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka saba | Mahakama ya Mkoa |
| 267 | Wizi wa karafuu. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka kumi na kupanda na kulea mikarafuu mia moja | Mahakama Kuu |
| 268 | Wizi wa mazao. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka mitano pamoja na kulipa mara mbili ya thamani ya soko la mazao yaliyoibiwa | Mahakama ya Wilaya |

**SEHEMU YA ISHIRINI NA TANO**
**MAKOSA YANAYOFANANA NA WIZI**

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 270 | Kuficha madaftari ya kumbukumbu. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kisichopungua mwaka mmoja lakini kisichozidi miaka kumi | Mahakama Kuu |
| 271 | Kuficha wasia. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka kumi | Mahakama Kuu |
| 272 | Kuficha nyaraka. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka mitatu | Mahakama ya Wilaya |
| 273 | Kuua mnyama kwa nia ya kumuiba. | Anaweza kukamata bila ya hati | Adhabu ile ile kama kwamba amemuiba mnyama | Mahakama yoyote ambayo kosa la wizi wa mnyama lingeweza kusikilizwa. |
| 274 | Kuhamisha kwa nia ya kuiba | Anaweza kukamata bila ya hati | Adhabu ile ile kama kwamba ameiba kitu hicho | Mahakama yoyote ambayo kosa la wizi wa kitu hicho lingeweza kusikilizwa. |
| 275 | Kuhaulisha kwa udanganyifu bidhaa zilizowekwa rehani. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka miwili | Mahakama ya Wilaya |
| 276 | Udanganyifu unaohusiana na madini katika migodi. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka mitano | Mahakama ya Wilaya |
| 277 | Kuchukua umeme kwa udanganyifu. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka mitano | Mahakama ya Wilaya |
| 278 | Kubadilisha kusikokuwa wizi. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miezi sita au faini isiyozidi Shilingi Laki Tano au adhabu zote mbili | Mahakama ya Wilaya |

## SEHEMU YA ISHIRINI NA SITA
## UNYANG'ANYI NA KUPORA KWA NGUVU

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 279 | Tafsiri na adhabu ya unyang'anyi. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka ishirini na tano | Mahakama ya Mkoa |
| 280 | Unyang'anyi wa kutumia silaha. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo cha maisha | Mahakama ya Mkoa |
| 281(1) | Adhabu ya kujaribu kufanya unyang'anyi | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka kumi | Mahakama ya Mkoa |
| 281(2) | Kujaribu kufanya unyang'anyi wa kutumia silaha. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo cha maisha | Mahakama ya Mkoa |
| 282 | Shambulio kwa nia ya kuiba. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka saba | Mahakama ya Mkoa |
| 283 | Kudai mali kwa vitisho vya maandishi. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka kumi na nne | Mahakama ya Mkoa |
| 284(1) | Kujaribu kuchukua kwa vitisho. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka mitano | Mahakama ya Mkoa |
| 284(2) | Kujaribu kuchukua kwa vitisho. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka kumi na nne | Mahakama ya Mkoa |
| 284(3) | Kujaribu kuchukua kwa vitisho. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka mitatu | Mahakama ya Mkoa |
| 285 | Kuwezesha utekelezaji wa nyaraka kwa vitisho. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka kumi na nne | Mahakama ya Mkoa |
| 286 | Kudai mali kwa kutishia kwa nia ya kuiba. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka mitano | Mahakama ya Wilaya |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 287 | Matumizi mabaya ya mali bila ya uaminifu. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka miwili au faini isiyozidi Shilingi Milioni mbili au adhabu zote mbili | Mahakama ya Wilaya |
| 288 | Matumizi mabaya ya mali bila ya uaminifu ya mtu aliyekufa. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka mitatu au faini isiyodizi Shilingi Milioni Tatu au kifungo kwa kipindi cha miaka saba | Mahakama ya Wilaya |
| 289 | Kuvunja uaminifu kijinai. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka mitatu au faini isiyozidi Shiling Milioni Tatu au adhabu zote mbili | Mahakama ya Wilaya |

## SEHEMU YA ISHIRINI NA SABA
## UVUNJAJI WA NYUMBA USIKU, UVUNJAJI WA NYUMBA MCHANA NA MAKOSA YANAYOFANANA NA HAYO

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 291(1) | Uvunjaji nyumba mchana | Anaweza kukamata bila hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka kumi | Mahakama ya Mkoa |
| 291(2) | Uvunjaji nyumba usiku | Anaweza kukamata bila hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka kumi na tano | Mahakama ya Mkoa |
| 292(1) | Kuingia katika nyumba ya makaazi kwa nia ya kutenda kosa. | Anaweza kukamata bila hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka kumi | Mahakama ya Mkoa |
| 292(2) | Ikiwa kosa limetendeka usiku | Anaweza kukamata bila hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka kumi na mbili | Mahakama ya Mkoa |
| 293 | Kuvunja jengo kwa ajili ya kuingia na kutenda kosa. | Anaweza kukamata bila hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka kumi na mbili | Mahakama ya Mkoa |
| 294 | Kuvunja jengo kwa ajili ya kuingia kwa nia ya kutenda kosa. | Anaweza kukamata bila hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka kumi | Mahakama ya Mkoa |
| 295(1) | Kukutwa na silaha kwa nia ya kutenda kosa. | Anaweza kukamata bila hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka saba | Mahakama ya Mkoa |
| 295(2) | Ikiwa mkosa alishatiwa hatiani awali kwa kosa linalohusiana na mali | Anaweza kukamata bila hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka kumi | Mahakama ya Mkoa |
| 296(1) | Kuingia kijinai. | Anaweza kukamata bila hati | Kifungo kwa kipindi cha miezi mitatu au faini ya Shilimgi Laki Mbili na Elfu Hamsini au adhabu zote mbili | Mahakama ya mwanzo |
| 296(2) | Ikiwa mali ambayo kosa limetendeka ni chombo kinachotumika kama makaazi ya binaadamu au sehemu ya ibada au sehemu ya kuhifadhia mali | Anaweza kukamata bila hati | Kifungo kwa kipindi cha mwaka mmoja | Hakimu yeyote |

## SEHEMU YA ISHIRINI NA NANE
## UDANGANYIFU

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 299 | Kujipatia mali kwa njia ya udangayifu. | Anaweza kukamata bila hati | Kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka mitatu lakini kisichozidi miaka mitano | Mahakama ya Wilaya |
| 300 | Kujipatia utekelezaji wa dhamana kwa njia ya udanganyifu. | Anaweza kukamata bila hati | Kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka mitatu lakini kisichozidi miaka mitano | Mahakama ya Wilaya |
| 301 | Kuhadaa. | Anaweza kukamata bila hati | Kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka mitatu lakini kisichozidi miaka mitano | Mahakama ya Wilaya |
| 302 | Kujipatia mkopo kwa njia ya udanganyifu. | Anaweza kukamata bila hati | Kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka mitatu | Mahakama ya Wilaya |
| 303 | Kula njama ya kudanganya. | Anaweza kukamata bila hati | Kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka mitatu | Mahakama ya Wilaya |
| 304 | Udanganyifu katika kuuza au kuweka rehani mali. | Anaweza kukamata bila hati | Kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka miwili | Mahakama ya Wilaya |
| 305 | Kujifanya kupiga ramli. | Anaweza kukamata bila hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka miwili | Mahakama ya Wilaya |
| 306 | Kujipatia usajili kwa udanganyifu | Anaweza kukamata bila hati | Kifungo kwa kipindi kisichozidi mwaka mmoja | Mahakama ya Wilaya |
| 307 | Tamko la uongo ili kupata hati ya kusafiria | Anaweza kukamata bila hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka miwili | Mahakama ya Wilaya |
| 308 | Kujifanya afisa wa umma. | Anaweza kukamata bila hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka miwili | Mahakama ya Wilaya |

## SEHEMU YA ISHIRINI NA TISA
## KUPOKEA MALI ILIYOIBWA AU ILIYOPATIKANA ISIVYO HALALI NA MAKOSA YANAYOFANANA NA HAYO

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 309(1) | Kupokea mali iliyoibiwa au iliyopatikana isivyo halali. | Anaweza kukamata bila hati | Kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka kumi | Mahakama ya Wilaya |
| 309(2) | Kupokea mali iliyoibiwa au iliyopatikana isivyo halali. | Anaweza kukamata bila hati | Kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka mitatu | Mahakama ya Wilaya |
| 310 | Watu wanaotuhumiwa kuwa na, au kusafirisha mali ya wizi. | Anaweza kukamata bila hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka miwili | Mahakama ya Wilaya |
| 311 | Kupatikana na mali ya wizi. | Anaweza kukamata bila hati | Kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka mitatu lakini kisichozidi miaka kumi au faini isiyopungua Shilingi Milioni Tatu lakini isiyozidi Shilingi Milioni Kumi na kutaifishwa na Serikali mali inayohusiana na utendwaji kosa | Mahakama ya Wilaya |
| 312 | Kuficha bidhaa. | Anaweza kukamata bila hati | Kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka saba au faini isiyopungua Shilingi Milioni Saba au adhabu zote mbili na kutaifishwa na Serikali bidhaa zote zilizohusika katika shtaka | Mahakama ya Wilaya |
| 313 | Kukutwa na mali iliyoibiwa nje ya Zanzibar. | Anaweza kukamata bila hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka saba | Mahakama ya Mkoa |

**SEHEMU YA THELATHINI**
**UDANGANYIFU WA WADHAMINI NA WATU WALIO KATIKA NAFASI ZA DHAMANA NA HESABU ZA UONGO**

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 314 | Wadhamini kuharibu au kubadilisha mali za muamana kwa udanganyifu. | Anaweza kukamata bila hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka saba | Mahakama ya Mkoa |
| 315 | Ubadhirifu na udanganyifu wa wakurugenzi na maafisa wa mashirika. | Anaweza kukamata bila hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka kumi na nne | Mahakama ya Mkoa |
| 316 | Maelezo ya uongo ya maafisa wa kampuni. | Anaweza kukamata bila hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka saba | Mahakama ya Mkoa |
| 317 | Hesabu za uongo. | Anaweza kukamata bila hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka saba | Mahakama ya Mkoa |
| 318 | Hesabu za uongo kwa Afisa wa umma. | Anaweza kukamata bila hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka saba | Mahakama ya Mkoa |

## SEHEMU YA THELATHINI NA MOJA
## MAKOSA YANAYOSABABISHA UHARIBIFU WA MALI

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 319 | Uchomaji wa mali kwa makusudi. | Anaweza kukamata bila hati | Kifungo cha maisha | Mahakama Kuu |
| 320 | Kujaribu kuchoma mali. | Anaweza kukamata bila hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka kumi na nne | Mahakama ya Mkoa |
| 321 | Kuchoma moto mazao na mimea. | Anaweza kukamata bila hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka kumi na nne | Mahakama ya Mkoa |
| 322 | Kujaribu kuchoma moto mazao. | Anaweza kukamata bila hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka saba | Mahakama ya Mkoa |
| 323 | Kupeleka chombo mrama. | Anaweza kukamata bila hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka kumi na nne | Mahakama Kuu |
| 324 | Kujaribu kupeleka mrama chombo. | Anaweza kukamata bila hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka saba | Mahakama Kuu |
| 325 | Kujeruhi wanyama. | Anaweza kukamata bila hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka miwili | Mahakama ya Wilaya |
| 326(1) | Kuharibu mali kwa makusudi | Anaweza kukamata bila hati | Kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka mitano | Mahakama ya Wilaya |
| 326(2) | Kuharibu nyumba ya makaazi au chombo kwa miripuko | Anaweza kukamata bila hati | Kifungo cha maisha | Mahakama Kuu |
| 326(3) | Kuharibu ukingo au ukuta wa mto, mfereji, msingi wa kupita majiau daraja | Anaweza kukamata bila hati | Kifungo cha maisha | Mahakama Kuu |
| 326(4) | Kuharibu au kuathiri wasia au madaftari ya kumbukumbu. | Anaweza kukamata bila hati | Kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka kumi na nne | Mahakama Kuu |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 326(5) | Kuharibu chombo kilicho hatarini au kilichozama, au kilichokwama. | Anaweza kukamata bila hati | Kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka saba | Mahakama ya Mkoa |
| 326(6) | Kuharibu au kuathiri njia za reli au barabara. | Anaweza kukamata bila hati | Kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka kumi na nne | Mahakama ya Mkoa |
| 326(7) | Kuharibu au kuathiri mali yenye thamani maalum | Anaweza kukamata bila hati | Kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka saba | Mahakama ya Mkoa |
| 326(8) | Kuharibu au kuathiri hati au kumbukumbu | Anaweza kukamata bila hati | Kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka saba | Mahakama ya Mkoa |
| 326(9)(a) | Kuharibu mali inayotumika au inayokusudiwa kutumika kwa madhumuni ya utoaji huduma muhimu | Anaweza kukamata bila hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka ishirini | Mahakama Kuu |
| 326(9)(b) | Kuharibu mali inayotumika au inayokusudiwa kutumika kwa madhumuni ya utoaji huduma muhimu | Anaweza kukamata bila hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka kumi na tano | Mahakama Kuu |
| 327 | Kujaribu kuharibu mali kwa miripuko | Anaweza kukamata bila hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka kumi na nne | Mahakama ya Mkoa |
| 328 | Kusambaza maradhi ya kuambukiza kwa wanyama. | Anaweza kukamata bila hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka saba | Mahakama ya Mkoa |
| 329 | Kuondosha alama za mipaka kwa nia ya kudanganya | Anaweza kukamata bila hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka mitatu | Mahakama ya Wilaya |
| 330 | Kuharibu kwa makusudi alama za upimaji na alama za mipaka | Anaweza kukamata bila hati | Kifungo kwa kipindi kisichozidi miezi mitatu au faini isiyozidi Shilingi Laki Mbili na Elfu Hamsini | Hakimu yeyote |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 331 | Adhabu kwa kuharibu ujenzi wa reli au barabara | Anaweza kukamata bila hati | Kifungo kwa kipindi kisichozidi miezi mitatu au faini isiyozidi Shilingi Laki Mbili na Elfu Hamsini | Hakimu yeyote |
| 332 | Vitisho vya kuchoma au kuharibu | Anaweza kukamata bila hati | Kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka saba | Mahakama ya Mkoa |

## SEHEMU YA THELATHINI NA MBILI
## KUGHUSHI, UTENGENEZAJI WA SARAFU, UTENGENEZAJI FEDHA BANDIA NA MAKOSA YANAYOFANANA NA HAYO

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 337 | Adhabu ya jumla ya kughushi | Anaweza kukamata bila hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka saba | Mahakama ya Wilaya |
| 338 | Kughushi kunakoadhibiwa kwa kifungo cha maisha | Anaweza kukamata bila hati | Kifungo cha maisha na waraka kutaifishwa na Serikali | Mahakama Kuu |
| 339 | Kughushi hati ya mahakama au waraka rasmi | Anaweza kukamata bila hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka saba | Mahakama ya Mkoa |
| 340 | Kughushi na makosa mengine yanayohusiana na stempu | Anaweza kukamata bila hati | Kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka saba | Mahakama ya Mkoa |
| 341 | Kutengeneza au kumiliki karatasi au zana za kughushi | Anaweza kukamata bila hati | Kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka saba | Mahakama ya Mkoa |
| 342 | Kuwasilisha nyaraka za uongo | Anaweza kukamata bila hati | Adhabu ile ile kama kwamba ameghushi kitu kinachohusika | Mahakama yoyote ambayo kesi ya waraka ulioghushiwa ingeweza kusikilizwa |
| 343 | Kuwasilisha nyaraka zilizofutwa au zilizomaliza muda | Anaweza kukamata bila hati | Adhabu ile ile kama kwamba ameghushi kitu kinachohusika | Mahakama yoyote ambayo kesi ya waraka ulioghushiwa ingeweza kusikilizwa |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 344 | Kuwezesha utekelezaji wa waraka kwa njia ya udanganyifu | Anaweza kukamata bila hati | Adhabu ile ile kama kwamba ameghushi kitu kinachohusika | Mahakama yoyote ambayo kesi ya waraka ulioghushiwa ingeweza kusikilizwa |
| 345 | Kufuta mistari katika hundi | Anaweza kukamata bila hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka saba | Mahakama ya Mkoa |
| 346 | Kutengeneza nyaraka bila ya mamlaka | Anaweza kukamata bila hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka saba | Mahakama ya Mkoa |
| 347 | Kudai mali kwa nyaraka za wasia zilizoghushiwa | Anaweza kukamata bila hati | Adhabu ile ile kama kwamba alighushi waraka huo | Mahakama yoyote ambayo kesi ya waraka ulioghushiwa ingeweza kusikilizwa |
| 348 | Kununua noti zilizoghushiwa | Anaweza kukamata bila hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka saba | Mahakama ya Mkoa |
| 349 | Kughushi hati za fedha zinazolipwa chini ya mamlaka ya umma | Anaweza kukamata bila hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka saba | Mahakama ya Mkoa |
| 350 | Kughushi daftari la kumbukumbu | Anaweza kukamata bila hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka saba | Mahakama ya Mkoa |
| 351 | Kupeleka cheti cha uongo cha ndoa kwa Mrajis | Anaweza kukamata bila hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka saba | Mahakama ya Mkoa |
| 352 | Maelezo ya uongo kwa ajili ya daftari la uandikishaji wa vizazi, vifo au ndoa | Anaweza kukamata bila hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka mitatu | Mahakama ya Wilaya |

## SEHEMU YA THELATHINI NA TATU
## MAKOSA YANAYOHUSIANA NA SARAFU NA NOTI

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 355 | Kughushi sarafu. | Anaweza kukamata bila hati | Kifungo cha maisha | Mahakama Kuu |
| 356 | Matayarisho ya kutengeneza sarafu bandia. | Anaweza kukamata bila hati | Kifungo cha maisha | Mahakama Kuu |
| 357 | Kupunguza sarafu. | Anaweza kukamata bila hati | Kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka saba | Mahakama ya Mkoa |
| 358 | Kumiliki vipande vya sarafu zilizokatwa. | Anaweza kukamata bila hati | Kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka saba | Mahakama ya Mkoa |
| 359 | Kutoa sarafu bandia. | Anaweza kukamata bila hati | Kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka mitatu | Mahakama ya Wilaya |
| 360 | Kurudia kutoa sarafu bandia. | Anaweza kukamata bila hati | Kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka mitano | Mahakama ya Wilaya |
| 361 | Kuwasilisha chuma au sarafu isiyotumika kama sarafu kwa wakati huo. | Anaweza kukamata bila hati | Kifungo kwa kipindi kisichozidi mwaka mmoja | Mahakama ya Wilaya |
| 362 | Kuingiza ndani ya nchi au kusafirisha nje ya nchi sarafu bandia. | Anaweza kukamata bila hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka miwili | Mahakama ya Wilaya |
| 364 | Kubadilisha noti ya kibenki na kuyayusha sarafu. | Anaweza kukamata bila hati | Kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka miwili au faini isiyozidi Shilingi Milioni Mbili kwa kila noti au sarafu | Mahakama ya Wilaya |
| 365 | Utoaji wa noti usio halali. | Anaweza kukamata bila hati | Kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka mitano | Mahakama ya Wilaya |

## SEHEMU YA THELATHINI NA NNE
## STEMPU BANDIA

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 366 | Kumiliki muhuri wa moto kwa madhumuni ya Kutengeneza stempu. | Anaweza kukamata bila hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka saba | Mahakama ya Wilaya |
| 367 | Karatasi na muhuri wa moto kwa ajili ya kutengeneza stempu za posta. | Anaweza kukamata bila hati | Kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka mitatu au faini isiyozidi Shilingi Milioni Tatu | Mahakama ya Wilaya |

## SEHEMU YA THELATHINI NA TANO
## MAKOSA YANAYOHUSIANA NA KOMPYUTA

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 369(4)(a) | Makosa dhidi ya mali ya ubunifu. | Anaweza kukamata bila hati | Kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka mitano | Mahakama ya Mkoa |
| 369(4)(b) | Makosa dhidi ya mali ya ubunifu. | Anaweza kukamata bila hati | Kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka kumi | Mahakama ya Mkoa |
| 370(1) | Makosa dhidi ya vifaa au vitu vya kompyuta. | Anaweza kukamata bila hati | Kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka mitano | Mahakama ya Mkoa |
| 370(2) | Makosa dhidi ya vifaa au vitu vya kompyuta. | Anaweza kukamata bila hati | Kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka kumi | Mahakama ya Mkoa |
| 371(1) | Kuharibu vifaa vya kompyuta. | Anaweza kukamata bila hati | Kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka mitatu lakini kisichozidi miaka kumi | Mahakama ya Mkoa |
| 371(2) | Kuharibu vifaa vya kompyuta. | Anaweza kukamata bila hati | Kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka mitano lakini kisichozidi miaka kumi na tano | Mahakama ya Mkoa |
| 372 | Kuingilia taarifa. | Anaweza kukamata bila hati | Kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka mitano au faini isiyozidi Shilingi Milioni Tano au adhabu zote mbili | Mahakama ya Wilaya |
| 373 | Kuingilia mfumo wa kompyuta. | Anaweza kukamata bila hati | Kifungo kwa kipindi kisichopungua mwaka mmoja lakini kisichozidi miaka mitano au faini isiyopungua Shilingi Milioni Moja lakini isiyozidi Shilingi Milioni Tano au adhabu zote mbili | Mahakama ya Wilaya |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 374 | Kuingilia kati taarifa kinyume na sheria. | Anaweza kukamata bila hati | Kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka mitano au faini isiyozidi Shilingi Milioni Tano au adhabu zote mbili | Mahakama ya Wilaya |
| 375 | Vifaa visivyo halali. | Anaweza kukamata bila hati | Kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka mitano au faini isiyozidi Shilingi Milioni Tano au adhabu zote mbili | Mahakama ya Wilaya |
| 376(1) | Kosa dhidi ya watumiaji wa kompyuta. | Anaweza kukamata bila hati | Kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka mitano au faini isiyozidi Shilingi Milioni Tano | Mahakama ya Wilaya |
| 376(2) | Kosa dhidi ya watumiaji wa kompyuta. | Anaweza kukamata bila hati | Kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka kumi au faini isiyozidi Shilingi Milioni Kumi | Mahakama ya Wilaya |
| 377 | Udanganyifu na kitendo kinachohusiana na kompyuta za Serikali. | Anaweza kukamata bila hati | Kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka kumi na tano au faini isiyozidi Shilingi Milioni Kumi na Tano | Mahakama ya Mkoa |

## SEHEMU YA THELATHINI NA SITA
## KUGHUSHI ALAMA ZA BIASHARA

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 380 | Kughushi alama za biashara. | Hawezi kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka miwili | Mahakama ya Wilaya |

## SEHEMU YA THELATHINI NA SABA
## KUJIFANYA MTU MWENGINE

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 381(1) | Kujifanya mtu mwengine kwa ujumla. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka miwili | Mahakama ya Wilaya |
| 381(2) | Iwapo kujifanya huko ni kwamba mkosaji ni mtu anayestahiki kwa wasia au kwa utekelezaji wa sheria mali yoyote maalum na anatenda kosa la kujipatia mali hiyo au mali hiyo kuwa katika milki yake | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka saba | Mahakama ya Wilaya |
| 382 | Kwa udanganyifu anatoa maelezo ya kukiri dhima. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka miwili | Mahakama ya Wilaya |
| 383 | Kujifanya mtu aliyeandikwa katika cheti. | Anaweza kukamata bila ya hati | Adhabu ile ile kama kwamba ameghushi cheti hicho | Mahakama yoyote ambayo ingeweza kusikiliza kesi ya kughushi cheti hicho |
| 384 | Kuazimisha, waraka au cheti kwa kujifanya mtu mwengine. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka miwili | Mahakama ya Wilaya |
| 385 | Kujifanya mtu aliyetajwa kwenye uthibitisho wa tabia. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi kisichozidi mwaka mmoja | Mahakama ya Wilaya |
| 386 | Kuazimisha uthibitisho kwa ajili ya kujifanya mtu mwengine. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka miwili | Mahakama ya Wilaya |

## SEHEMU YA THELATHINI NA NANE
**KUJARIBU**

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 388 | Kujaribu kutenda makosa. | Inategemea ama kosa hilo polisi anaweza kukamata bila ya hati au kwa hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka miwili | Mahakama yoyote ambayo kosa lililojaribiwa kutendwa lingeweza kusikilizwa |
| 389 | Adhabu kwa kujaribu kutenda baadhi ya makosa. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka saba | Mahakama yoyote ambayo kosa lililojaribiwa kutendwa lingeweza kusikilizwa |
| 390 | Kushawishi au kuchochea wengine kutenda kosa ndani ya Zanzibar au kwengine. | Anaweza kukamata bila ya hati ikiwa kosa alilochochea au aliloshawishi mtu anaweza kukamatwa bila ya hati na siyo vyenginevyo | Adhabu ile ile kama kwamba amejaribu kutenda kosa alilolishawishi au alilolichochea | Mahakama yoyote ambayo kosa alilolishawishi au alilolichochea lingeweza kusikilizwa |
| 391 | Kupuuza kuzuia kosa. | Hawezi kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka miwili | Mahakama yoyote ya chini |

## SEHEMU YA THELATHINI NA TISA
## KULA NJAMA

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 392(2) | Kula njama ya kutenda kosa. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka miwili | Mahakama yoyote ambayo kosa alilokula njama lingeweza kusikilizwa |
| 392(3) | Kula njama ya kutenda kosa. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka saba | Mahakama yoyote ambayo kosa alilokula njama lingeweza kusikilizwa |
| 393 | Njama nyenginezo. | Inategemea ama kosa hilo polisi anaweza kukamata bila ya hati au kwa hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka miwili | Mahakama yoyote ambayo kosa lingeweza kusikilizwa |

## SEHEMU YA AROBAINI
## WASHIRIKI WA UHALIFU BAADA YA KUTENDEKA KOSA

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 395 | Adhabu ya mshiriki wa uhalifu baada ya kosa kutendeka. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka mitatu | Mahakama yoyote ya chini |
| 396 | Adhabu ya kumshawishi au kumchochea mtu mwengine kutenda kosa. | Anaweza kukamata bila ya hati | Kifungo kwa kipindi cha miaka miwili | Mahakama yoyote ya chini |

## MAKOSA CHINI YA SHERIA NYENGINE

| | | | |
|---|---|---|---|
| Ikiwa ni kosa lenye adhabu ya kifo au adhabu ya kifungo cha miaka kumi na tano au zaidi | Anaweza kukamata bila ya hati | - | Mahakama Kuu |
| Ikiwa ni kosa lenye adhabu ya kifungo cha miaka saba au zaidi, lakini lenye adhabu ya kifungo chini ya miaka kumi na tano | Anaweza kukamata bila ya hati | - | Mahakama ya Mkoa |
| Ikiwa ni kosa lenye adhabu ya kifungo cha miaka miwili au zaidi, lakini lenye adhabu ya kifungo chini ya miaka saba | Anaweza kukamata bila ya hati | - | Mahakama ya Wilaya |
| Ikiwa ni kosa lenye adhabu ya kifungo chini ya mwaka mmoja au adhabu ya faini pekee | Anaweza kukamata bila ya hati | - | Hakimu yeyote |

**JADWELI IA PILI**

**Fomu zinazoelezea Makosa katika Hati za Mashtaka**

*[Chini ya kifungu cha 167(2)(e)]*

## 1. KUUA KWA MAKUSUDI

Kuua kwa makusudi, kinyume na kifungu cha 176 cha Sheria ya Adhabu.

**MAELEZO YA KOSA**

A B, katika siku ya ……. ya ……………,…………… katika wilaya ya ……….. bila ya halali na kwa makusudi ulimuua J.S.

----------------------

## 2. KUSHIRIKI KATIKA UHALIFU BAADA YA KUTENDEKA KOSA LA KUUA KWA MAKUSUDI

Kushiriki katika uhalifu baada ya kutendeka kosa la kuua kwa makusudi, kinyume na kifungu cha 194 cha Sheria ya Adhabu.

**MAELEZO YA KOSA**

A.B., kwa kujua kwamba, H.C., katika siku ya ,…………., katika Wilaya ya ……………., ulimuua C.C., umefanya katika siku ya ………………….., katika wilaya ya ………… na katika siku nyengine za baadae ulimpokea, ulimhifadhi, ulimficha, ulimsaidia na ulimtunza H.C.

--------------------

## 3. KUUA BILA KUKUSUDIA

Kuua bila ya kukusudia, kinyume na kifungu cha 177 cha Sheria ya Adhabu.

**MAELEZO YA KOSA**

A.B. katika siku ya ……………, katika Wilaya ya ………….. bila halali ulimuua J.S.

## 4. KUBAKA

Kubaka, kinyume na kifungu cha 108 cha Sheria ya Adhabu.

**MAELEZO YA KOSA**

A.B., katika siku ya…….., …….., katika Wilaya ya ……… ulimuingilia E.F bila ya ridhaa yake

------------------------

## 5. KUJERUHI

**Kosa la kwanza**

Kujeruhi kwa nia ya, kinyume na kifungu cha 204 cha Sheria ya Adhabu.

**MAELEZO YA KOSA**

A.B., katika siku ya …….. katika Wilaya ya …………, ulimjeruhi C.D., kwa nia ya kumtia kilema, kumvunja au kumsababishia ulemavu, au kusababisha madhara makubwa, au kuzuia ukamataji halali uliofanywa na A.B.

**Kosa la Pili**

Kujeruhi, kinyume na kifungu cha 211 cha Sheria ya Adhabu.

**MAELEZO YA KOSA**

A.B., katika siku ya ……….., ……… , katika Wilaya ya ………… bila halali ulimjeruhi C.D

-------------

## 6. WIZI

**Kosa la kwanza**

Wizi, kinyume na kifungu cha 258 cha Sheria ya Adhabu

**MAELEZO YA KOSA**

A.B., katika siku ya ………..,………, katika Wilaya ya ……., uliiba mkoba, mali ya C.D.

**Kosa la Pili**

Kupokea bidhaa zilizoibiwa, kinyume na kifungu cha 309 cha Sheria ya Adhabu.

**MAELEZO YA KOSA**

A.B., katika siku …….. ,……… , katika Wilaya ya ……….. ulipokea mkoba, mali ya C.D., ukijuwa kuwa mkoba huo umeibiwa.

----------------

## 7. WIZI UNAOFANYWA NA MAKARANI

Wizi, unaofanywa na karani au mtumishi, kinyume na kifungu cha 262 cha Sheria ya Adhabu.

**MAELEZO YA KOSA**

A.B., katika siku ya ……………., katika Wilaya ya ……… ukiwa ni karani au mtumishi wa M.N., uliiba kutoka kwa M.N., yadi kumi za kitambaa.

---------------

## 8. UNYANG'ANYI WA KUTUMIA NGUVU

Unyang'anyi wa kutumia nguvu, kinyume na kifungu cha 279 cha Sheria ya Adhabu.

## MAELEZO YA KOSA

A.B., Katika siku ya ………, ………, katika Wilaya ya …......, ulimnyang'anya kwa kutumia nguvu C.D. Saa, na katika au mara baada ya au mara tu kabla ya, wakati unyanga'anyi huo umefanyika umetumia nguvu binafsi kwa C.D.

-----------------

## 9. KUVUNJA JENGO USIKU

Kuvunja jengo usiku, kinyume na kifungu cha 291, na kuiba katika nyumba ya makaazi, kinyume na kifungu cha 258, cha Sheria ya Adhabu.

## MAELEZO YA KOSA

A.B., katika usiku wa siku ya……., katika Wilaya ya …… ulivunja na kuingia katika nyumba ya makaazi ya C.D., kwa nia ya kuiba ndani humo, na uliiba ndani humo saa moja, mali ya S.T., saa ambayo ina thamani ya Shilingi Mia na Hamsini.

---------------

## 10. VITISHO

Kudai mali kwa njia ya vitisho vya maandishi, kinyume na kifungu cha 283 cha Sheria ya Adhabu.

## MAELEZO YA KOSA

A.B.,katika siku ya ………….. , katika Wilaya ya …….., kwa nia ya kujipatia fedha kutoka kwa C.D., ulisababisha C.D., kupokea barua yenye vitisho vya kudhuru au kusababisha hasara kwa E.F.

--------------------

## 11. KUJARIBU KUCHUKUA KWA VITISHO

Kujaribu kuchukua kwa njia ya vitisho, kinyume na kifungu cha 284 cha Sheria ya Adhabu.

## MAELEZO YA KOSA

A.B., Katika siku ya ……..…, katika Wilaya ya…….., kwa nia ya kuchukua fedha kutoka kwa C.D., ulimtuhumu au ulitishia kumtuhumu C.D., kuwa ametenda kosa la kuingilia kinyume na maumbile

----------------

## 12. KUJIPATIA MALI KWA NJIA YA UDANGANYIFU

Kujipatia bidhaa kwa njia ya udanganyifu, kinyume na kifungu cha 299 cha Sheria ya Adhabu.

**MAELEZO YA KOSA**

A.B., katika siku ya……., ………, katika Wilaya ya …, kwa nia ya hadaa, ulijipatia kutoka kwa S.P. yadi 5 za kitambaa kwa njia ya udanganyifu kwamba A.B.,ulikuwa ni mtumishi wa J.S., na kwamba wewe A.B., ulitumwa na J.S., kwenda kwa S.P. kwa ajili ya kitambaa hicho, na kwamba ulikuwa wewe A.B., tayari umeshaidhinishwa na J.S. kupokea kitambaa hicho kwa niaba ya J.S.

## 13. KULA NJAMA YA KUDANGANYA

Kula njama ya kudanganya, kinyume na kifungu cha 303 cha Sheria ya Adhabu.

**MAELEZO YA KOSA**

A.B., na C.D., katika siku ya ………….,na katika siku tofauti baina ya siku hiyo na siku ya …, ……., katika Wilaya ya ……, kwa pamoja na kwa nia ya kudaganya mlikula njama kwa njia ya tangazo lilowekwa na nyinyi, A.B na C.D., katika gazeti la H.S, kwa udanganyifu mlieleza kwamba A.B. na C.D. mlikuwa wakati huo mkifanya biashara halali kama masonara……... katika Wilaya ya ……… na kwamba mlikuwa wakati huo na uwezo wa kumpatia baadhi ya mapambo ya kisonara mtu yeyote ambae angewatumia kiasi cha Shilingi Sitini.

----------------

## 14. KUCHOMA MOTO

Kuchoma moto, kinyume na kifungu cha 319 cha Sheria ya Adhabu

**MAELEZO YA KOSA**

A.B., katika siku ya …….., …… , katika Wilaya ya………. , kwa makusudi na bila halali ulichoma moto nyumba.

----------------

## 15. KUCHOMA MOTO NA WALIOSAIDIA KABLA YA KUCHOMA MOTO

Kuchoma moto, kinyume na kifungu cha 319 cha Sheria ya Adhabu.,C.D.,mshiriki kabla ya kutendwa kosa hilo la kuchoma moto

**MAELEZO YA KOSA**

A.B., katika siku ya ........, ...... , katika Wilaya ya........ , kwa makusudi na bila halali ulichoma moto nyumba. C.D., katika siku hiyo hiyo ........, ...... , katika Wilaya ya ......., ulimshauri au ulimuwezesha A.B., kutenda kosa hilo.

-----------------

## 16. KUHARIBU KWA MAKUSUDI ALAMA ZA UPIMAJI NA ALAMA ZA MIPAKA

Kuharibu alama za upimaji na za mipaka, kinyume na kifungu cha 330 cha Sheria ya Adhabu.

**MAELEZO YA KOSA**

A.B., katika siku ya ........, ...... , katika Wilaya ya....... , kwa makusudi na bila halali uliharibu alama za upimaji na alama za mipaka.

------------------

## 17. KUGHUSHI

**Kosa la kwanza**

Kughushi, kinyume na kifungu cha 337 cha Sheria ya Adhabu.

**MAELEZO YA KOSA**

A.B., katika siku ya ........, ...... , katika Wilaya ya.......... , ulighushi wasia unaodaiwa kuwa ni wasia wa C.D.

**Kosa la Pili**

Kuwasilisha waraka wa uongo, kinyume na kifungu cha 342 cha Sheria ya Adhabu.

## MAELEZO YA KOSA

A.B., katika siku ya ……., …… , katika Wilaya ya……., kwa kujua na kwa njia ya udanganyifu uliwasilisha wasia ulioghushiwa unaodaiwa kuwa ni wasia wa C.D.

-------------------

## 18. SARAFU BANDIA

Kuwasilisha sarafu bandia, kinyume na kifungu cha 359 cha Sheria ya Adhabu

## MAELEZO YA KOSA

A.B., katika siku ya ……., …… , katika soko la …….. , katika Wilaya ya…… ……., uliwasilisha sarafu bandia ukijua kuwa sarafu hiyo ni bandia.

----------------

## 19. KUTOA USHAHIDI WA UONGO

Kutoa ushahidi wa uongo, kinyume na kifungu cha 75 cha Sheria ya Adhabu.

## MAELEZO YA KOSA

A.B katika siku ya …………..,katika Wilaya ya…………………, ukiwa shahidi katika usikilizaji wa kesi katika mahakama ya ……………,iliyopo ……………, ambapo mshtaki alikuwa ……………., na mshtakiwa alikuwa………….., kwa kujua ulitoa ushahidi wa uongo kwamba ulimuona M.W, katika mtaa unaoitwa ……………., katika siku ya………..

---------------

## 20. HESABU ZA UONGO

### Kosa la Kwanza

Hesabu za uongo kwa udanganyifu, kinyume na kifungu cha 317 cha Sheria ya Adhabu.

## MAELEZO YA KOSA

A.B., katika siku ya……………, katika Wilaya ya ……………….., ukiwa karani au mtumishi wa C.D., kwa nia ya kudanganya, ulifanya au ulishiriki katika kufanya maingizo ya uongo katika kitabu

cha hesabu cha C.D., muajiri wako yanayokusudia kuonesha kwamba siku hiyo Shilingi Elfu Tatu zimelipwa kwa L.M.

**Kosa la Pili**

Lile lile kama kosa la kwanza.

**MAELEZO YA KOSA**

A.B., katika siku ya..............., katika Wilaya ya ..............., ukiwa karani au mtumishi wa C.D., kwa nia ya kudanganya, uliacha au ulishiriki katika kuacha kuingiza mambo muhimu katika kitabu cha hesabu cha C.D., muajiri wako, yaani, upokeaji katika siku hiyo wa Shilingi Elfu Moja na Mia Tano kutoka kwa H.S.

------------------

## 21. WIZI ULIOFANYWA NA WAKALA

**Kosa la Kwanza**

Wizi uliofanywa na mawakala na watu wengine, kinyume na kifungu cha 264 cha Sheria ya Adhabu.

**MAELEZO YA KOSA**

A.B. katika siku ya ............, ......, katika Wilaya ya ........., uliiba Shilingi Elfu Tatu ambazo uliaminiwa na H.S. kwa niaba yake, wewe A.B., uziweke katika hifadhi salama.

**Kosa la Pili**

Wizi wa mawakala na wengine, kinyume na kifungu cha 264 cha Sheria ya Adhabu.

**MAELEZO YA KOSA**

A.B. katika siku ya ............, ......, katika Wilaya ya ........., uliiba Shilingi Elfu Tatu ambazo zilipokelewa na wewe kwa niaba ya na kwa manufaa ya L.M.,

---------------

## 22. HATIA YA AWALI

Kabla ya kufanyika kwa kosa lililotajwa, mshtakiwa A.B. ulishawahi kutiwa hatiani kwa kosa la ........................ katika siku ya .......... 19..... au 20......, katika.. ....... iliyokaa .........

## JADWELI LA TATU

**Kiwango cha Kifungo kwa Kushindwa Kulipa Faini au Kushindwa Kupata Mali ya Kutosha ya Kuikamata**

*[Chini ya kifungu cha 324(1)]*

| *Kiwango* | | *Kipindi cha Juu kabisa* |
|---|---|---|
| Kisichozidi Shs. 50,000 | | Siku 15 |
| Kinachozidi ... Shs. 50,000 | Lakini kisichozidi ... Shs. 100,000 | siku 30 |
| Shs. 100,000 | Shs. 200,000 | siku 60 |
| Shs. 200,000 | Shs. 300,000 | siku 90 |
| Shs. 300,000 | Shs. 500,000 | siku 120 |
| Shs. 500,000 | Shs. 700,000 | siku 150 |
| Shs. 700,000 | Na kuendelea | siku 180 |

## JADWELI YA NNE

**Watu Waliosamehewa Kuwajibika Kuhudumu kama Washauri wa Mahakama**

*[Chini ya kifungu cha 231]*

(1) Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi.

(2) Wajumbe wa Baraza la Mapinduzi.

(3) Majaji na Mahakimu.

(4) Watu wanaotekeleza majukumu ya viongozi wa dini au viongozi wa dini zao husika.

(5) Madaktari wa kawaida, madaktari wa upasuaji, madaktari wa meno na wafamasia waliopo kazini.

(6) Mawakili wa Serikali.

(7) Mawakili wanaofanya kazi ya uwakili. .

(8) Maafisa wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania, Usalama wa Taifa na Maafisa wa Idara Maalum.

(9) Askari Polisi na Askari wa Chuo cha Mafunzo.

(10) Katibu wa Rais, Katibu wa Makamo wa Kwanza wa Rais, Katibu wa Makamo wa Pili wa Rais na Makatibu wa Mawaziri wote wengine.

(11) Makatibu Wakuu wote, Makamishna na Wakurugenzi katika Utumishi wa Serikali.

(12) Maafisa uangalizi walioteuliwa chini ya sheria inayohusiana na uangalizi wa wahalifu.

(13) Watu wenye ulemavu wa akili.

(14) Wafanyakazi wanaofanya kazi za ukarani katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, Mahakama, Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka na Wizara inayohusika na mambo ya sheria.

## JADWELI YA TANO

### Mamlaka ya Mahakama

(Chini ya kifungu cha 21 cha Sheria Nambari 9 ya 2009 kama ilivyorekebishwa na Sheria Nambari 12 ya 2011

| NAM. | KIFUNGU | KOSA | ADHABU | MAHAKAMA INAYOWEZA KUSIKILIZA KOSA |
|---|---|---|---|---|
| 1. | 13 | Kilimo cha baadhi ya mimea na dawa | Kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka kumi na tano au faini isiyopungua Skilingi Milioni Arobaini (40, 000,000/=)au adhabu zote mbili. | Mahakama ya Mkoa |
| 2. | 14 | Utengenezaji wa dawa za nakotiki na saikotropiki. | Kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka thelathini na pamoja na faini ya Shilingi Milioni Thelathini (30,000,000/=). | Mahakama ya Mkoa. |
| 3. | 15(1)(a) | Kukutwa na kununua koka au dawa za nakotiki. | Kifungo kwa kipindi cha miaka kumi na tano au faini isiyopungua Shilingi Milioni Arobaini (40,000,000/=) au adhabu zote mbili. | Mahakama ya Mkoa. |
| 4. | 15(1)(b)(i) | Usafirishaji wa dawa za nakotiki au dawa za saikotropiki. | Kifungo kwa kipindi cha miaka kumi na tano na faini ya Shilingi Milioni Arobaini (40,000,000/=). | Mahakama ya Mkoa. |
| 5. | 15(1)(b)(ii) | Usafirishaji wa dawa nyengine yoyote isiyokuwa dawa ya nakotiki au saikotropiki ambayo inafanana au inaonekana kuwa ni dawa ya nakotiki au dawa ya saikotropiki. | Faini isiyopungua Shilingi Milioni Mbili (2,000,000/=) na pamoja na kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka kumi. | Mahakama ya Wilaya. |
| 6. | 15(1)(c), | Kuvuta kwa mdomo, kuvuta kwa pua, kunusa au vyenginevyo kutumia dawa yoyote ya nakotiki au dawa ya saikotropiki. | Kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka saba au faini isiyopungua Shilingi Milioni Tano (5,000,000/=) au adhabu zote mbili. | Mahakama ya Wilaya |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | 15(1)(d), | Kukutwa katika nyumba yoyote, chumba au pahala palipokodiwa kwa madhumuni ya kuuza, kuvuta kwa mdomo, kuvuta kwa pua, kunusa nakadhalika dawa yoyote ya nakotiki au dawa ya saikotropiki. | Kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka saba au faini isiyopungua Shilingi Milioni Tano (5,000,000/=) au adhabu zote mbili. | Mahakama ya Wilaya |
| | 15(1)(e) | Kuruhusu majengo kutumika kwa ajili ya utayarishaji wa kasumba kwa ajili ya kuvuta, kuuza nakadhalika au kwa ajili ya kutengeneza, kuuza au kusambaza dawa za nakotiki au dawa za saikotropiki | Kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka saba au faini isiyopungua Shilingi Milioni Tano (5,000,000/=) au adhabu zote mbili. | Mahakama ya Wilaya |
| | 15(1)(f) | Kukutwa na kiko au kifaa chengine kwa ajili ya matumizi yanayohusiana na uvutaji au unusaji nakadhalika. | Kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka saba au faini isiyopungua Shilingi Milioni Tano (5,000,000/=) au adhabu zote mbili. | Mahakama ya Wilaya |
| 7. | 16(1). | Kukutwa, kutumia kiwango kidogo cha dawa za nakotiki na dawa za saikotropiki. | | Mahakama ya Wilaya |
| | (a) | Ikiwa kokeni, mofini, mchanganyiko wa mofini au dawa nyengine kama zitakavyotangazwa katika Gazeti. | Kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka saba au faini isiyopungua Shilingi Milioni Tano (5,000,000/=). | Mahakama ya Wilaya |
| | (b) | Nyengine ambazo hazikuainishwa katika aya ya (a) | Faini isiyopungua Shilingi Milioni Tano (5,000,000/=) au kifungo kwa kipindi cha miaka saba. | Mahakama ya Wilaya |
| | (c) | | Kifungo kwa kipindi cha miezi sita. | Mahakama ya Wilaya |
| 8. | 17(c) | Kukutwa unatumia dawa za nakotiki au dawa za saikotropiki. | Faini ya Shilingi Milioni Kumi na Tano (15,000,000/=) au kifungo kwa kipindi cha miaka kumi na tano au adhabu zote mbili. | Mahakama ya Wilaya |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 9. | 18. | Kumpatia mtu dawa za nakotiki au dawa za saikotropiki. | Kifungo kwa kipindi cha miaka thelathini na faini ya Shilingi Milioni Thelathini (30,000,000/=) | Mahakama ya Mkoa |
| 10. | 19. | Kukiuka masharti, leseni au ruhusa. | Kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka thelathini na faini isiyopungua Shilingi Milioni Thelathini (30,000,000/=). | Mahakama ya Mkoa |
| 11. | 20. | Kugharamia shughuli zisizo halali. | Adhabu iliyo sawa na ile ya mkosaji mkuu. | Mahakama ya Mkoa Au Mahakama ya Wilaya kutegemea na kosa. |
| 12. | 21 | Kusaidia kutenda kosa. | Adhabu iliyo sawa na ile ya mkosaji mkuu. | Mahakama ya Mkoa Au Mahakama ya Wilaya kutegemea na kosa. |
| 13. | 22. | Kujaribu kutenda kosa. | | |
| | | Kutenda kosa baada ya hatia ya awali. | Adhabu mara mbili. | Mahakama ya Mkoa |
| | (a) | Kwa makosa chini ya kifungu cha 16. | Kifungo kwa kipindi cha miaka 35 au faini ya Shilingi Milioni Sitini(60,000,000/=). | Mahakama ya Mkoa |
| 14. | 23. (b) | Makosa chini ya vifungu vya 17, 19, 20 na 21. | Kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka saba na kisichozidi miaka kumi na tano. | Mahakama ya Wilaya |
| 15. | 32(2). | Makosa yoyote ambayo hayajawekewa adhabu.<br><br>Kushindwa kumlinda mtoa habari. | Kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka mitano au faini isiyozidi Shilingi Milioni Kumi (10,000,000/=) au adhabu zote mbili. | Mahakama ya Wilaya |

## JADWELI LA SITA

**Maudhui na Muundo wa Hati ya Upekuzi**

*[Chini ya kifungu cha 145(2)]*

---

## HATI YA UPEKUZI

**(Ijazwe wakati Hakimu au Jaji wakati anataka upekuzi ufanywe)**

Mimi ninakutaka wewe....................................... Cheo/Wadhifa/Nam. ............................ ufanye upekuzi kwa ajili ya kitu au vitu vilivyoainishwa katika pahala palipoelezwa hapa chini:

.......................................................................................................................................

.......................................................................................................................................

.......................................................................................................................................

.......................................................................................................................................

.......................................................................................................................................

**Jina la Mahakama:** ..............................................

**Tarehe:** ........................................................

**Muda:** ..........................................................

..........................................

**Hakimu/Jaji**

**JADWELI LA SABA**

**Kiapo kitakachoapwa na Mshauri wa Mahakama**

*(Chini ya kifungu cha 234(2))*

Mimi..........................................ninaapa/ninathibitisha kwamba, nitatekeleza kwa uwezo wangu wote na kwa uaminifu wajibu wangu kama mshauri wa mahakama katika kesi za jinai, na ninaahidi kulinda na kutunza uadilifu, kutokupendelea na haki kama inavyohitajika kwa mshauri wa mahakama katika kutekeleza majukumu yake.

**IMESAINIWA** leo ........................ Siku ya ............................ 20 ....................................

..........................................

MSHAURI WA MAHAKAMA

**Mbele ya:**

JINA LA JAJI: ..................................................

SAINI: ..........................................................

**UMEPITISHWA** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar, tarehe 13 Februari, 2018.

..........................................

(RAYA ISSA MSELLEM)

***Katibu wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar.***